**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

# OFISI YA WAZIRI MKUU

# BARAZA LA TAIFA LA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI

# TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SERA YA TAIFA YA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI MEI 2018 MPAKA APRILI 2019

**JUNI, 2019**

## VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| **AfDB** | African Development Bank |
| **AGITF** | Agricultural Inputs Trust Fund |
| **AMCOS** | Agricultural Marketing Cooperative Society |
| **AMEDA** | Africa and Middle East Depository Association |
| **ASDP** | Agricultural Sector Development Programme |
| **ASCAs** | Accumulating Savings and CreditAssociations |
| **BOT** | Bank of Tanzania |
| **CAF** | Contractors Assistance Fund |
| **CAG** | Controler Auditor General |
| **CFGs** | Community Financial Groups |
| **COSTECH** | Commission for Science and Technology |
| **COCOBA** | Community Conservation Banks |
| **CSDR** | Central Securities Depository and Registry Services |
| **DCB** | Dar es Salaam Commercial Bank |
| **DIT** | Dar es Salaam Institute of Technology |
| **DSE** | Dar es Salaam Stock Exchange |
| **DTBi** | Dar Teknohama Business Incubator |
| **EACOP** | East Africa Crude Oil Pipeline |
| **EPZA** | Export Processing Zone Authority |
| **EWURA** | Energy and Water Utilities Regulatory Authority |
| **GDP** | Gross Domestic Product |
| **GePG** | Government electronic Payment Gateway |
| **GMS** | Government Mailing System |
| **HIDF** | Human Innovation and Development Fund |
| **IFMIS** | Intergrated Financial Management Information System |
| **ILO** | International Labour Organisation |
| **IR VICOBA** | Inter Religious VICOBA |
| **JOSACA** | Jozan Saving and Credit Association |
| **KKCF** | Kilimo Kwanza Fund |
| **MEF** | Mwananchi Empowerment Fund |
| **MGOV** | Mfumo wa Huduma za Serikali kupitia Simu za Mikononi |
| **MIVARF** | Programu ya Miundo Mbinu ya Masoko na Huduma za Kifedha Vijijini |
| **MKURABITA** | Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania |
| **MSCL** | Mfumo huu unaotumiwa na Kampuni ya Huduma za Meli |
| **NBC** | National Bank of Commerce |
| **NEDC** | National Entrepreneurship Development Committee |
| **NEDF** | National Entrepreneurship Development Fund |

| | |
|---|---|
| **NEEC** | National Economic Empowerment Council |
| **NICOL** | National Investment Company Limited |
| **NMB** | National Microfinance Bank |
| **OWM** | Ofisi ya Waziri Mkuu |
| **PASS** | Trust Private Agricultural Sector Support Trust |
| **PPRA** | Public Procurement Regulatory Authority |
| **REF** | Rural Energy Fund |
| **RFB** | Road Fund Board |
| **PSC** | Programme Steering Committee |
| **SACCOS** | Savings and Credit Cooperative Societies |
| **SAGCOT** | Southern Agriculture Growth Coridor of Tanzania |
| **SCTF** | SAGCOT Catalytic Trust Fund |
| **SIDO** | Small Industries Development Organisation |
| **SILC** | Savings for Internal and Lending Community |
| **SMEs** | Small and Medium Enterprises |
| **SUA** | Sokoine University of Agriculture |
| **TAA** | Tanzania Airport Authority |
| **TaFF** | Tanzania Forest Fund |
| **TAMISEMI** | Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa |
| **TANePS** | Tanzania National eProcurement System |
| **TANROADS** | Tanzania National Roads Agency |
| **TASAF** | Tanzania Social Action Fund |
| **TCC** | Tanzania Cigarette Company |
| **TCCIA** | Tanzania Chamber of Commerce, Industry and Agriculture |
| **TCDC** | Tanzania Cooperative Development Commission |
| **TDL** | Tourism Development Levy |
| **TECC** | Tanzania Entrepreneurship Competitive Center |
| **TEDAP** | Tanzania Energy Development and Expansion |
| **TEF** | Tanzania Education Fund |
| **TEHAMA** | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| **TIB** | Tanzania Investment Bank |
| **TIMAP** | Tanzania Informal Microfinance Association of Practioners |
| **TIRDO** | Tanzania Investment and Research Development Organisation |
| **TPB** | Tanzania Postal Bank |
| **TPDC** | Tanzania Petroleum Development Cooperation |
| **TPSF** | Tanzania Private Sector Foundation |
| **TRC** | Tanzania Railway Cooperation |
| **TWCC** | Tanzania Women Chamber of Commerce |
| **TWPF** | Tanzania Wildlife Protection Fund |
| **TYC** | Tanzania Youth Coalition |

| | |
|---|---|
| **UNCTAD** | United Nations Conference on Trade and Development |
| **UNDP** | United Nations Development Program |
| **USSD** | Unstructured Supplementary Service Data |
| **VETA** | Vocational Education and Training Authority |
| **VICOBA** | Village Community Banks |
| **VICOBA-FETA** | VICOBA Federation Tanzania |
| **VITOVU** | Vituo vya Maendeleo ya Jamii vya Kuondoa Umaskini |
| **VSO** | Voluntary Service Overseas |
| **WDF** | Women Development Fund |
| **WFE** | World Federation of Exchanges |
| **YBI** | Youth Business International |
| **YDF** | Youth Development Fund |

## YALIYOMO


VIFUPISHO ... 2
1.0. BARAZA LA TAIFA LA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI ... 9
1.1. UTANGULIZI ... 9
1.2. DIRA ... 9
1.3. DHAMIRA ... 9
1.4. AMALI ZA BARAZA ... 10
1.5. MAJUKUMU ... 10
1.6. WAJUMBE WA BARAZA ... 10
1.7. UONGOZI WA SEKRETARIATI YA BARAZA ... 14
1.8. MUUNDO NA WAFANYAKAZI WA SEKRETARIATI ... 15
1.9. MAPITIO YA MPANGO MKAKATI WA BARAZA ... 16
1.10. SHUGHULI ZA UTAFITI ... 17
1.11. UKAGUZI WA HESABU ZA BARAZA ... 17
2.0. UTEKELEZAJI SERIKALI MTANDAO ... 18
2.1. HATUA ZILIZOCHUKULIWA ... 18
2.2. UTEKELEZAJI WA SERIKALI MTANDAO KATIKA BARAZA LA UWEZESHAJI ... 24
2.3. MIPANGO YA BAADAE ... 25
3.0. HALI YA UCHUMI ... 27
3.1. UTANGULIZI ... 27
3.2. PATO LA TAIFA ... 27
3.3. HALI YA MAISHA YA WANANCHI ... 29
3.4. SEKTA YA FEDHA ... 31
3.5. MFUMUKO WA BEI ... 32
3.6. UTENDAJI WA KIUCHUMI KWA UJUMLA (MACROECONOMIC PERFORMANCE) ... 33
3.7. CHANGAMOTO ... 33
4.0. SERA NA SHERIA ... 34
4.1. UTANGULIZI ... 34
4.2. SHERIA ZILIZOTUNGWA AU KUFANYIWA MAREKEBISHO ... 34
4.3. MAZINGIRA YA BIASHARA ... 37
5.0. SEKTA YA ARDHI ... 41
5.1. UTANGULIZI ... 41
5.2. UWEZESHAJI WANANCHI ... 41
5.3. MAFANIKIO ... 42

5.4. MABORESHO YA SERA, SHERIA NA KANUNI ........................................................ 43
6.0. USHIRIKA ........................................................ 45
6.1. UTANGULIZI ........................................................ 45
6.2. IDADI NA AINA YA VYAMA VYA USHIRIKA ........................................................ 45
6.3. HALI YA VYAMA VYA USHIRIKA ........................................................ 46
6.4. USIMAMIZI NA UHAMASISHAJI WA MAENDELEO YA USHIRIKA NCHINI ........................................................ 47
6.5. MIPANGO YA BAADAYE ........................................................ 49
6.6. CHANGAMOTO ........................................................ 49
7.0. SOKO LA MITAJI NA HISA LA DAR ES SALAAM ........................................................ 51
7.1. UTANGULIZI ........................................................ 51
7.2. HATIFUNGANI ZA SERIKALI ........................................................ 52
7.3. HATIFUNGANI ZA MAKAMPUNI BINAFASI (CORPORATE BONDS) ........................................................ 52
7.4. DHAMANA ........................................................ 53
7.5. IDADI YA WAWEKEZAJI ........................................................ 53
7.6. MIPANGO NA MALENGO YA MWAKA 2019 ........................................................ 56
8.0. MIFUKO NA PROGRAMU ZA SERIKALI ZA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI ........................................................ 57
8.1. UTANGULIZI ........................................................ 57
8.2. MAKUNDI YA MIFUKO NA MATOKEO UTEKEZAJI WA SHUGHULI ZAKE ........................................................ 58
8.3. MIFUKO INAYOTOA MIKOPO MOJA KWA MOJA KWA WALENGWA ........................................................ 59
8.4. MIFUKO INAYOTOA DHAMANA ........................................................ 63
8.5. MIFUKO INAYOTOA RUZUKU ........................................................ 69
8.6. PROGRAMU ZA UWEZESHAJI ........................................................ 76
9.0. VIKUNDI VYA KIFEDHA VYA KIJAMII ........................................................ 81
9.1. UTANGULIZI ........................................................ 82
9.2. UHAKIKI WA TAASISI NA VIKUNDI ........................................................ 83
9.3. MATOKEO YA UHAKIKI ........................................................ 84
9.4. HATUA ZA MABORESHO ........................................................ 89
9.5. SERA YA TAIFA YA HUDUMA NDOGO ZA FEDHA YA MWAKA 2017 ........................................................ 89
10.0. USHIRIKI WA WATANZANIA KATIKA UWEKEZAJI NA MIRADI YA KIMKAKATI ........................................................ 91
10.1. UTANGULIZI ........................................................ 91
10.2. UTEKELEZAJI WA MIRADI YA KIMKAKATI ........................................................ 91
10.3. SEKTA NDOGO YA MAFUTA NA GESI ........................................................ 98
10.4. KANZI DATA YA WATOA HUDUMA SEKTA YA MAFUTA NA GESI NA YA NGUVU KAZI 101
11.0. SERA, SHERIA NA MIONGOZO ........................................................ 103
11.1. UTANGULIZI ........................................................ 103

11.2. CHANGAMOTO ..... 104
11.3. MAPENDEKEZO ..... 104
12.0. UJASIRIAMALI ..... 106
12.1. UTANGULIZI ..... 107
12.2. KAMATI YA TAIFA YA MAENDELEO YA UJASIRIAMALI ..... 107
12.3. MATUMIZI YA TEKNOLOJIA NA UBUNIFU KATIKA BIASHARA ..... 108
12.4. KUPANUA WIGO WA MITAJI KWA WAFANYABIASHARA NA WAJASIRIAMALI NCHINI 108
12.5. HALI YA UTEKELEZAJI WA MKAKATI WA TAIFA WA UJASIRIAMALI ..... 109
12.6. UBORESHAJI WA MAZINGIRA YA BIASHARA ..... 109
12.7. KUIMARISHA UJUZI NA ELIMU YA UJASIRIAMALI ..... 110
12.8. KUWEZESHA MATUMIZI YA TEKNOLOJIA NA UBUNIFU ..... 110
12.9. KUBORESHA UPATIKANAJI WA MITAJI ..... 112
12.10. KUIMARISHA UHAMASISHAJI NA MATUMIZI YA MITANDAO YA KIBIASHARA ..... 112
12.11. MAENDELEO YA BIASHARA YA SEKTA NDOGO NA KATI ..... 112
12.12. MCHANGO WA PROGRAM YA FURSA KWA WAJASIRIAMALI NCHINI ..... 117
13.0. UBUNIFU NCHINI ..... 119
13.1. UTANGULIZI ..... 120
13.2. MNYORORO WA THAMANI KATIKA UBUNIFU ..... 121
13.3. ATAMIZI ZA UBUNIFU NCHINI ..... 122
13.4. CHANGAMOTO KATIKA TASNIA YA UBUNIFU NCHINI ..... 128
13.5. MAPENDEKEZO ..... 130
14.0. UWEZESHAJI KWA VIJANA ..... 132
14.1. UTANGULIZI ..... 132
14.2. MCHANGO WA ASASI ZA KIRAIA KWA VIJANA ..... 137
15.0. UWEZESHAJI WA WANAWAKE KIUCHUMI ..... 139
15.1. UTANGULIZI ..... 139
15.2. UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA UWEZESHAJI WANAWAKE KIUCHUMI ..... 139
15.3. MAREKEBISHO YA SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA YA MWAKA 2018 ..... 141
15.4. USHIRIKI WA WAJASIRIAMALI WANAWAKE KATIKA MANUNUZI YA SERIKALI ..... 141
15.5. HITIMISHO ..... 142
16.0. MANUNUZI YA UMMA ..... 143
16.1. UTANGULIZI ..... 143
16.2. MWONGOZO WA USHIRIKI WA MAKUNDI MAALUM KATIKA MANUNUZI YA UMMA 143
16.3. MADHUMUNI NA MALENGO YA MWONGOZO ..... 144

16.4. UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA UWEZESHAJI KWENYE MANUNUZI YA UMMA....144
16.5. MFUMO WA MANUNUZI KWA NJIA YA MTANDAO "TANePS"....145
17.0. UWEZESHAJI KATIKA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA....146
17.1. MKAKATI WA TAIFA WA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI....147
17.2. PROGRAMU ZA UWEZESHAJI NA UBUNIFU....148
17.3. VIWANDA NA UWEKEZAJI....152
17.4. URASIMISHAJI WA BIASHARA NDOGO KWA VITAMBULISHO....155
17.5. MIKUTANO YA BIASHARA NA MAONESHO YA WAZI....158
18.0. MAMBO YA KUJIFUNZA KUTOKA MIKOANI (BEST PRACTICES)....160
18.1. MKOA WA TANGA (Utatuzi wa changamoto ya Masoko na Uchakataji wa Muhogo Wilaya ya Handeni)....161
18.2. MKOA WA GEITA (Soko la Madini)....162
18.3. MKOA WA KIGOMA (Utekelezaji wa Mradi wa LIC na KJP)....163
18.4. MKOA WA SIMIYU (Uvutiaji wa Biashara na Uwekezaji)....164
18.5. MKOA WA MBEYA (Uanzishaji wa Mtandao wa Biashara na Nchi Jirani)....165
18.6. MKOA WA SHINYANGA (Kutenga eneo kwa ajili ya Kituo cha Uwezeshaji)....166

# 1.0. BARAZA LA TAIFA LA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI

## 1.1. UTANGULIZI

Taarifa hii ni mwendelezo wa taarifa za utekelezaji wa sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi zinazotolewa kila mwaka na Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi. Baraza limekuwa likiandaa taarifa hizi ili kuleta mrejesho kwa wadau na wananchi kwa ujumla jinsi utekelezaji wa sera ulivyofanyika kwa mwaka husika. Tangu Tanzania ipate uhuru mwaka 1961, Serikali imekuwa ikifanya juhudi mbalimbali ili wananchi waweze kushiriki kikamilifu katika kujenga uchumi wa nchi yao. Jitihada hizo ni pamoja na Azimio la Arusha ambalo liliweka njia kuu za uchumi mikononi mwa wananchi, Vijiji vya ujamaa, Kilimo cha kufa na kupona na nyingine nyingi. Dira ya Taifa ya mwaka 2025 inalenga kuwa ifikapo mwaka 2025 sehemu kubwa ya uchumi wa nchi iwe inamilikiwa na watanzania wenyewe. Ili kufikia malengo hayo serikali ilibuni na kutekeleza Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ya mwaka 2004. Utekelezaji wa Sera ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi unasimamiwa na Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ambalo ni chombo cha juu Kitaifa cha kusimamia, kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa shughuli zilizoanishwa katika sera hiyo.

Baraza ni Taasisi ambayo ipo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu limeundwa kwa mujibu wa sheria ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ya mwaka 2004. Lengo la Sera hii ni kuwawezesha watanzania kushiriki kikamilifu katika kujenga na kumiliki uchumi wa nchi yao.

Baraza lilizinduliwa rasmi mwezi Novemba, 2005, na lilianza rasmi utekelezaji wa majukumu yake mwezi Mei 2007 baada ya kuundwa kwa Sekretarieti ya Baraza ambayo ni nyenzo ya utekelezaji wa majukumu ya Baraza.

## 1.2. DIRA

Dira ya Baraza ni kuongoza kimkakati katika kuwezesha, kuratibu, kusimamia, kufuatilia na kutathmini shughuli zote zinazolenga kuwawezesha Wananchi wa Tanzania Kiuchumi.

## 1.3. DHAMIRA

Kuwaongoza watanzania kuelekea uchumi imara kupitia uimarishaji wa mazingira ambayo ni rafiki kwa wafanyabiashara kwa ujumla na kuhamasisha ushiriki wa jamii kwenye shughuli halali za kiuchumi.

### 1.4. AMALI ZA BARAZA

Katika kutekeleza majukumu yake Baraza linaamini katika:-

| | | |
|---|---|---|
| **Uwazi** | **Umahiri** | **Uwajibikaji** |
| **Usawa** | **Uadilifu** | **Umoja** |

### 1.5. MAJUKUMU

Majukumu ya Baraza yametokana na maudhui yaliyoainishwa katika Sera ya Uwezeshaji na Sheria ya Uwezeshaji ya mwaka 2004. Majukumu makuu ya Baraza ni:

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Kuwapatia watanzania fursa za kushiriki kikamilifu katika shughuli za kiuchumi; | 2. | Kuandaa Mpango Mkakati wa kisekta na wa Sekta mbalimbali wa upatikanaji na matumizi ya raslimali kwa shughuli za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi; |
| **3.** | Kuhamasisha na kuhimiza uwekaji wa Akiba, Uwekezaji na Ushirikishwaji makini wa Wananchi kwenye shughuli za kiuchumi; | 4. | Kuandaa Mkakati wa kitaifa wa Uraghibishi wa sekta mbalimbali wa shughuli za uwezeshaji wananchi kiuchumi; |
| **5.** | Kuendeleza na kuwezesha shughuli za kibiashara zinazoanzishwa na kuendeshwa na watanzania; | 6. | Kuainisha fursa za mafunzo ya kiuchumi na uwekezaji na kuratibu programu za mafunzo hayo; |
| **7.** | Kusimamia, kuongoza na kutafuta vyanzo vya fedha na michango kwa ajili ya Mfuko wa Uwezeshaji; | 8. | Kuhamasisha Utafiti wa shughuli za kiuchumi na kuhimiza ushirikiano na Taasisi za Utafiti; |
| **9.** | Kufanya mapitio ya sheria mbalimbali kwa lengo la kutoa mapendekezo ambayo yatalenga kuboresha mazingira ya uwezeshaji wananchi kiuchumi. | 10. | Kuandaa Mfumo wa kufuatilia maendeleo ya shughuli za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na kutathmini matokeo; na Mfumo wa Menejimenti ya Habari za Uwezeshaji; |
| **11** | Kushauri kwenye shughuli zote za uanzishaji wa vikundi, ushirika, ushirikiano na ushirikiano wa biashara wa muda mfupi. | 12. | Kuanzisha mfumo wa utoaji taarifa za uwezeshaji wa wananchi kiuchumi kutoka sekta zote; |

### 1.6. WAJUMBE WA BARAZA

Hili ni Baraza la nne (4) tangu kuanzishwa kwa Taasisi hii. Wajumbe wa Baraza waliteuliwa mnamo tarehe 17 Desemba, 2016. Mwenyekiti aliteuliwa tarehe 9 Septemba, 2018 kuchukuwa nafasi iliyoachwa wazi na Dkt. John Jingu aliyeteuliwa kuwa Katibu Mkuu wa wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Wanawake, Jinsia, Wazee na Watoto. Baraza la sasa lina wajumbe tisa (9) ikiwa ni pamoja na mwenyekiti. Baraza limeundwa na wajumbe wenye uzoefu wa fani mbalimbali kama vile Viongozi wa

Serikali Wastaafu, Wanataaluma, Watafiti, Wafanyabiashara na Taasisi Zisizokuwa za Serikali za maendeleo ya wananchi. Wajumbe hao wa Baraza pamoja na picha zao ni:-



**Dkt. Festus B. Limbu, *Mwenyekiti wa Baraza***

Ni Mhadhiri Mstaafu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam katika masuala ya Uchumi. Vilevile ni Mtafiti mwandamizi na Mshauri mwelekezi wa masuala ya uchumi chini ya Taasisi ya Utafiti (Economic and Social Research Foundation - ESRF). Mbunge Mstaafu wa jimbo la uchaguzi la Magu mkoani Mwanza (2000-2015). Naibu Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo na Naibu waziri wa fedha katika serikali ya awamu ya tatu. Aliwahi kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Pamba Tanzania (Tanzania Cotton Board) na kuwa mjumbe katika bodi mbalimbali hapa nchini, Afrika Mashariki na Dunia kwa ujumla. Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, alimteua Dkt. Festus Limbu, kuwa Mwenyekiti wa Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, Septemba 2018.

**Profesa Samuel M. Wangwe, *Mjumbe***

Mwenyekiti wa DAIMA Ltd (Daima Associates Limited). Profesa wa uchumi mstaafu wa Chuo Kikuu cha dar es Salaam. Alikuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya ESRF na REPOA. Sasa ni Mtafiti mshiriki katika taasisi hizo. Alikiwa Mwenyekiti wa Bodi ya Tume ya Ushindani wa Biashara (FCC). Mshauri wa sera katika ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma.





**Profesa Lucian A. Msambichaka, *Mjumbe***

Ni Profesa Mstaafu wa Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam katika masuala ya Uchumi wa kilimo. Mwenyekiti wa Bodi ya Taasisi ya Ustawi wa Jamii (ISW) na ni Mwenyekiti wa Bodi ya Benki ya Biashara DCB. Alikuwa Mwenyekiti Mwanzilishi wa Bodi ya Bima ya Afya (NHIF), Mwenyekiti Mwanzilishi wa Bodi ya Chuo Kikuu Kishiriki cha Usihirika na Biashara (MUCCoBS), Moshi na Mkurugenzi Mwanzilishi wa Kituo cha Ushauri cha Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam.
Pia aliwahi kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), Mwenyekiti wa Bodi ya Kituo cha Uwekezaji (TIC) na Kaimu Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (TAA). Alikuwa Mshauri Mkuu na Mwezeshaji Kiongozi wa "Majadiliano ya Ushirikiano kwa Manufaa ya Wote (Global Smart Partnership Dialogue)" na Mshauri Mkuu na Mwezeshaji Kiongozi wa "Majadiliano ya Kitaifa Kuhusu Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Tanzania".

**Bw. Ladislaus J. Mwamanga, *Mjumbe***

Ni Mkurugenzi Mtendaji wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) uliopo chini ya Ofisi ya Rais Ikulu. Lengo kuu la TASAF ni kusaidiana na vyombo vingine vya Serkali katika kupunguza Umasikini kwa kuzingatia ushirikishwaji wa Jamii ngazi zote. Kabla ya kujiunga TASAF alifanya kazi na Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (Tanzania Petroleum Development Corporation – TPDC 1982 - 1984), Benki ya Taifa ya Biashara (National Bank of Commerce – NBC 1987 – 1994 ) na Shirika la Uuzaji na Usambazaji wa Mafuta Tanzania (Total Tanzania Limited 1994 – 1999).





**Dkt. Frederick S. Ringo, *Mjumbe***

Ni Wakili wa Mahakama Kuu ya Tanzania na ni Mhadhiri Mwandamizi wa Shule ya Sheria katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam katika masuala ya sheria ya biashara na fedha. Aliwahi kuwa Afisa Sheria Mkuu (PSRC), Mkuu wa kitengo cha Huduma za Kisheria (Africa Export-Import Bank -Cairo) na Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Ushindani wa Biashara (Fair Competition Commission). Ni mwanachama wa Taasisi ya Wasuruhishi wa Migogoro (UK na Tanzania).

**Bibi Anna T. Maembe, *Mjumbe***

Ni Katibu Mkuu mstaafu kutoka Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto, akiwa hapo alifanya mambo mengi ya kimkakati kwa ajili ya wanawake na watoto. Cheo hiki alidumu nacho kati ya mwaka 2011 mpaka 2015. Amekuwa mtumishi wa umma kwa kipindi cha miaka 34. Amekuwa Mkurugenzi wa Elimu na Usambazaji wa Taarifa za Mazingira ktk Baraza la Mazingira kuanzia 2001 mpk 2010. Pia amehudumu katika Bodi mbalimbali za masuala ya Mazingira, wanawake na watoto nchini, SADC na Kimataifa. Amebobea katika masuala ya Utafiti wa Ikolojia, Elimu and na Tathmini ya Athari ya Mazingira.
Ameshiriki kuongoza masuala mengi ya Serikali ikiwamo kuongoza Bodi mbalimbali za Taasisi za Umma. Pia ametoa machapisho mbalimbali katika masuala ya utunzaji wa mazingira na kutoa ushauri kwa Taasisi mbalimbali za ndani na nje ya nchi. Yeye ni mbobezi katika masuala ya mazingira.





**Dkt. Augustine Y. Hangi, *Mjumbe***

Ni Mwenyekiti Mtendaji wa kampuni ya Madini (Mineral Resources Company Limited). Ametoa shauri mbalimbali zinazohusiana na masuala ya madini. Kabla ya kushika nafasi yake ya sasa, Dkt. Augustine Y. Hangi alikuwa kaimu Mkurugenzi wa London-based Diamond Sorting Organization (TANSORT). Aliwahi pia kuwa Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Madini Tanzania (STAMICO) kwa miaka 13 mpaka mwaka 2004. Tangu mwaka 2009 mpaka sasa amekuwa akifanya kazi na chuo kikuu huria (Open University of Tanzania) kama msimamizi wa wanafunzi wanaosomea shahada ya uzamili. Kabla ya hapo alikuwa mhadhiri wa chuo hicho kati ya mwaka 2007 na 2009. Kwa hivi sasa pia ni Mwenyekiti wa Bodi ya Mineral Resources Company Limited, Aliwahi kuwa Mjumbe wa bodi ya Tanzania Minerals Audit Agency na pia mjumbe wa bodi ya Williamson Diamonds Limited.

**Dkt. Astronaut Bagile, *Mjumbe***

Ni Mkurugenzi Mtendaji na mwanzilishi wa shirika lisilo la kiserikali la Women In Social Entrereneurship (WISE). Amefanya kazi katika mashirika yasiyo ya kiserikali ya kitaifa na kimataifa kwa miaka 25 akichangia kuinua hali za uchumi za wananchi husan makundi yaliyo na hali duni zaidi kama wakulima, wanawake, vijana na watoto. Aliwahi kuwa mwenyekiti wa bodi ya FEMINA. Ni mjumbe wa bodi wa shirika la kimataifa linalojihusisha na utafiti wa masuala ya kijinsia na wanawake Afrika (AAWORD) lililo na makao yake Senegal. Pia ni Mjumbe wa bodi wa shirika lisilo la kiserikali lijulikanalo kama SCODIA.





**Bibi Neema M. Kiure, *Mjumbe***

Ni Mkaguzi Mshiriki Mwenza wa Ernst & Young (EY). Aliungana na Ernst & Young (EY) tangu mwaka 2005. Kabla ya hapo alifanyakazi na Diamond Trust Bank (T) Limited kama Meneja wa Fedha na Utawala mnamo mwaka 2004. Pia aliwahi kufanya kazi na PriceWaterhouseCoopers (PwC) kama Mkaguzi manmo mwaka 2004 na pia alifanyakazi na ULC (Tanzania) Limited kama Mhasibu Mkuu mnamo mwaka 2000.

Pia hufundisha masomo ya Utawala Bora wa wakurugenzi wa makampuni uliothibitishwa na Jumuiya ya Madola, amewahi kufundisha masomo ya muda maalum kwa ajili ya kujiandaa na mitihani ya Uhasibu. Ni mjumbe wa bodi ya Wahasibu na Wakaguzi wa (NBAA) na ni mjumbe wa bodi wa Shirikisho la Kimataifa la Wahasibu (IFAC). Alikuwa kiongozi wa Mradi wa kuhakikisha Serikali inaweza kuingia kwenye mfumo wa Kanuni za Kimataifa za Uaandaji wa hesabu katika taasisi za umma (IPSAS).

## 1.7. UONGOZI WA SEKRETARIATI YA BARAZA

Kazi za kila siku za Baraza hufanywa na Sekretariati ya Baraza. Kwa mujibu kifungu cha 14 cha Sheria ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ya Mwaka 2004, Menejimenti ya Sekretariati ya Baraza inaongozwa na Katibu Mtendaji ambaye huteuliwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Baraza huajiri Wakurugenzi na Mameneja. Kwa sasa timu ya Menejimenti ina watumishi wafuatao:-



**Bibi Beng'i M. Issa,** ***Katibu Mtendaji***

Aliteuliwa kushika nafasi hiyo na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 4 Desemba, 2014. Pia ni Katibu wa Baraza. Kabla ya uteuzi huo alifanya kazi Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (Tanzania Commission For AIDS - TACAIDS) kama Mkurugenzi wa Fedha, Utawala na Utafutaji Rasilimali kwa miaka 12. Pia alikuwa Mdhibiti wa fedha wa Taasisi ya CARE International Tanzania kwa miaka 3. Aliwahi kuwa mhadhiri wa masuala ya fedha na uhasibu katika kilichokuwa Chuo cha Uongozi wa Maendeleo (IDM Mzumbe) sasa Chuo kikuu cha Mzumbe kwa kipindi cha miaka 9 (1992 -2000). Alikuwa Mwenyekiti wa Bodi za Benki ya Wanawake (TWB). Mwenyekiti wa Taasisi ya Ushindani ya Ujasiriamali Tanzania (TECC). Vilevile ni makamu mwenyekiti wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Mafuta na Gesi (PURA). Aliwahi kuwa Mjumbe wa Bodi wa ya Benki ya DCB na ni mjumbe wa bodi ya Tanzania Legal Service Facility.

**Bw.Suleiman M. Malela*****, Kaimu Mkurugenzi wa Huduma za Taasisi***

Aliteuliwa kushika nafasi hiyo mwezi Octoba, 2016. Kabla ya uteuzi huo Bw.Suleiman M. Malela alikuwa mkuu wa kitengo cha Ukaguzi wa Ndani kutoka mwezi Octoba, 2008 alipoajiriwa na Baraza mpaka mwezi Octoba, 2016. Kabla ya kujiunga na Baraza, Bw. Malela alifanya kazi Shirika la Bima la Taifa Tanzania (National Insurance Corporation - NIC) katika nafasi mbalimbali kuanzia mwaka 1993 mpaka 2008.



**Bi Esther B. Mmbaga*****, Kaimu Mkurugenzi wa Uwezeshaji na Ushiriki wa Watanzania kwenye uwekezaji***


Aliteuliwa kushika nafasi hiyo mwaka, 2015. Pamoja na uteuzi huo Bi Esther pia ni Mkuu wa Kitengo cha Huduma za Sheria kutoka mwaka 2007 alipoajiriwa na Baraza. Ni mjumbe wa bodi ya Taasisi ya watoa huduma kwenye tasnia ya mafuta na gesi (ATOGS). Kabla ya kujiunga na Baraza, Bi Esther alifanya kazi katika idara ya mahakama kama Hakimu Mkazi toka mwezi Mei, 2003 mpaka mwezi Aprili, 2007.



### 1.8. MUUNDO NA WAFANYAKAZI WA SEKRETARIATI

Katika kipindi cha mwezi Mei 2018 mpaka Aprili, 2019 Sekretariati iliidhinishiwa muundo mpya. Katika Muundo huo mpya utakuwa na wafanyakazi 57 ambao wanaongozwa na Katibu Mtendaji. Katibu Mtendaji anasaidiwa na Wakurugenzi 2 na Wakuu wa Vitengo 4. Hivi sasa Baraza kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Sekretariati ya Ajira lipo katika jitihada za kuajiri ili kujaza nafasi mbalimbali kwa mujibu wa Muundo huo mpya. Sekretariati kwa hivi sasa ina watumishi 29, kati yao wanaume ni 20 na wanawake ni 9. Watumishi 26 ni wa ajira ya kudumu na malipo ya uzeeni, mtumishi 1 ni wa ajira ya mkataba, na watumishi 2 ni wa ajira ya muda maalum. Muundo mpya ulioidhinishwa ni kama unavyooneshwa kwenye ***mchoro Na. 1***

***Mchoro Na. 1: Muundo wa wafanyakazi wa Sekretariati***



## 1.9. MAPITIO YA MPANGO MKAKATI WA BARAZA

Mpango Mkakati wa Baraza (*NEEC Strategic Plan*) ni moja ya nyenzo inayotumika katika kuhakikisha kwamba adhima ya serikali ya kuwawezesha wananchi wake kiuchumi inafikiwa. Nyenzo zingine ni kama Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ya mwaka 2004, Sheria ya Uwezeshaji Namba 16 ya mwaka 2004, Mkakati wa Utekelezaji wa Sera katika sekta mbalimbali na miongozo mingine. Baraza limeandaa Mpango Mkakati wake wa tatu kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka 2018/2019 mpaka mwaka 2022/2023. Mpango Mkakati huo mpya wa Baraza umeandaliwa baada ya kumalizika kwa Mpango Mkakati wake wa pili ambao ulikuwa ni wa miaka mitano kuanzia mwaka 2013/2014 mpaka mwaka 2017/2018. Misingi mikuu ya kuandaliwa kwa Mpango huu mpya ni kuangalia mahitaji ya sera; kupima mafanikio na udhaifu katika utekelezaji wa mpango mkakati uliopita; Miongozo ya serikali na maoni ya wadau. Wadau mbalimbali walishiriki kutoa maoni yao kuhusu utekelezaji wa mpango uliopita na matarajio yao katika Mpango mpya. Moja ya matarajio makubwa ya Mpango huu ni kuona kiwango cha ukuaji wa uchumi kwa nchi kinakwenda sambamba na ukuaji wa uchumi wa mwananchi na uwepo kwa mazingira ya uwezeshaji, hivyo kuwa na ukuaji wa uchumi jumuishi *(Inclusive Economic Growth and Enabling Investments Environment).* Mpango umeainisha malengo makuu manne na malengo mengine ishirini na tatu. Malengo makuu yaliyomo kwenye Mpango ambayo yanalenga kuwa na matokeo makubwa na ya haraka. Malengo makuu hayo ni pamoja na:-

i. Baraza kutafuta rasilimali (fedha, watumishi wenye sifa, vitendea kazi na technolojia ya kisasa) za kutosha ili liwe endelevu na lenye uwezo liweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo ifikapo mwaka 2023;

ii. Baraza kuwajengea uwezo kuhusu dhana ya uwezeshaji wadau wake wakuu. Wadau watajengewa uwezo ili kuongeza ujuzi katika uzalishaji wa bidhaa bora zinakokidhi vigezo vya soko la ndani na nje na kupewa elimu ya ujasiriamali ifikapo mwaka 2023;

iii. Baraza kutekeleza jukumu lake la kusimamia na kuratibu shughuli zote za uwezeshaji wananchi kiuchumi ambazo zinafanywa na wadau mbalimbali ili shughuli hizo zifanywe kwa ufanisi mkubwa na kutoa matokeo makubwa ifikapo mwaka 2023; na

iv. Baraza kutumia njia mbalimbali za kujitangaza kwa wadau na wananchi ili litambulike. Huduma zinazotolewa na Baraza ziwafikie wananchi wengi zaidi ifikapo mwaka 2023.

Baraza na watumishi wote wamejipanga kwa ari kubwa kutekeleeza Mpango Mkakati huu kwa ufanisi mkubwa na kuona kwamba matarajio ya serikali ya kuwawezesha watanzania kiuchumi na kuwaondolea umaskini yanafikiwa.

### 1.10. SHUGHULI ZA UTAFITI

Katika kuwawezesha Wananchi kiuchumi, Baraza linashirikiana na wadau mbalimbali kufikia adhima yake hiyo. Mingoni mwa wadau ambao Baraza inashirikiana nao ni watafiti. Watafiti ni watu muhimu sana katika maendeleo ya wanadamu. Nchi zilizoendelea zinatumia zaidi ya asilimia moja ya pato lake kwa ajili ya kufanyia utafiti. Kuna tafiti mbalimbali zinafanywa kila siku lakini lengo kuu la tafiti zote hizo ni kuboresha maisha ya mwanadamu. Imeelezwa kwamba zaidi ya tafiti mia saba kwa mwaka zinaomba usajili kutoka *COSTECH*.

Baraza limeunda Kamati maalum ya utafiti ambayo wajumbe wake wanatoka katika taasisi serikali na binafsi zinazojihusisha na masuala ya utafiti. Baraza kwa kushirikiana na Kamati inaibua matokeo ya tafiti mbalimbali zilizofanywa zinazolenga kutatua changamaoto kwa wananchi za kupambana na umaskini. Tafiti ambazo zinatoa ufumbuzi wa matatizo mbalimbali ya kiuchumi. Kamati hiyo imeshakutana mara mbili tangu kuanzishwa kwake. Kikao chake cha mwisho kilifanyika tarehe 25/4/2019. Katika mkutano wake huo Kamati imeazimia kuanzisha Kongamano la Utafiti ambalo litawakutanisha watafiti kutoka sehemu mbalimbali kujadili fursa na changamoto wanazokabiliana nazo na kuzipatia ufumbuzi wake kwa pamoja.

### 1.11. UKAGUZI WA HESABU ZA BARAZA

Ripoti za fedha za kila mwaka zimekuwa zikikaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG). Baraza limekuwa likipata hati safi (*Unqualified Audit Opinion*) ya hesabu kwa kipindi chote cha utendaji kazi wake. Ukaguzi wa hesabu za mwaka 2017/18 umekamilika na kupata hati safi kama ilivyo kwa miaka iliyopita.

## 2.0. UTEKELEZAJI SERIKALI MTANDAO

Utekelezaji wa Serikali Mtandao ni moja ya sehemu muhimu ya maboresho yaliyofanyika katika Utumishi wa Umma, ambao umesaidia kurahisisha utoaji wa huduma hiyo muhimu. Utekelezaji wa Serikali Mtandao umejikita katika kuboresha utoaji wa huduma kama ifuatavyo:-

a) Taasisi za umma (Government to Government),
b) Kati ya taasisi za umma na wananchi (Government to Citizens),
c) Kati ya taasisi za umma na sekta ya Biashara (Government to Business), na
d) Serikali kuwahudumia watumishi (Government to Employees).

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwaka 2012 ilianzisha huduma ya ***"Serikali Mtandao***" kwa Sheria ya Wakala za Serikali Na.30 ya Mwaka 1997 Sura ya 245 na Kanuni zake ili kuwezesha wananchi kupitia TEHAMA.




Serikali Mtandao ni matumizi ya TEHAMA katika kuboresha utoaji wa huduma kwa Umma, kwa ufanisi na kwa gharama nafuu wakati wowote na mahali popote.

### 2.1. HATUA ZILIZOCHUKULIWA

Serikali kupitia Wakala wa Serikali Mtandao ambayo ina majukumu na mamlaka ya kuratibu, kusimamia na kukuza jitihada za Serikali Mtandao nchini Tanzania, imechukua hatua zifuatazo kuwawezesha wananchi kupitia TEHAMA.

**i. Ushauri wa Kitaalamu na Msaada wa Kiufundi**

Serikali kupitia Wakala wa Serikali Mtandao (eGovernment Agency), inatoa huduma za ushauri wa kitaalamu na msaada wa kiufundi kuhakikisha kuwa TEHAMA inasimamiwa ipasavyo, inawekezwa, kuendeshwa na kudumishwa ipasavyo kutimiza malengo ya kimkakati ya taasisi.

Huduma zinatolewa katika maeneo ya Uhakiki wa Mifumo ya TEHAMA, Tathmini ya Usalama, Utayarishaji wa Mpango wa Kukabili Majanga, Utayarishaji wa Sera ya TEHAMA, Utayarishaji wa Mkakati wa TEHAMA, Usanifu na Tathmini ya Miradi ya TEHAMA.

**ii. Mifumo Shirikishi ya TEHAMA**

Wakala inaweka mazingira yanayowezesha Taasisi za Umma kushirikiana katika matumizi ya rasimili za TEHAMA ili kuondoa urudufu, kupunguza gharama na kuongeza ubora wa huduma kwa umma. Miongoni mwa mifumo iliyoanzishwa ni pamoja na:-

**a) Mfumo Shirikishi wa Kusimamia Shughuli na Rasilimali za Taasisi (ERMS)**

Wakala ya Serikali Mtandao imebuni, imesanifu na imetengeneza mfumo shirikishi wa Kusimamia Shughuli na Rasilimali za Taasisi (ERMS). Mfumo huu unaunganisha shughuli mbalimbali za Taasisi kuwa katika mfumo mmoja unaowezesha usimamizi, ufuatiliaji, ukaguzi na tathimini ya utekelezaji wa shughuli zote za Taasisi kwa ufanisi.

Akifafanua kuhusu mfumo huu, Mtendaji Mkuu wa Wakala Dkt, Jabiri Bakari amesema, "Tumeamua kutumia utajiri wa utaalamu wetu wa kidigitali kutengeneza Mfumo huu (ERMS) ambao ni dirisha moja linalounganisha shughuli zote ndani ya Taasisi ili kuongeza ufanisi katika utendaji kazi na utoaji wa huduma bora kwa umma."

**b) Tovuti Kuu ya Serikali**

Mfumo huu umetokana na kuhuishwa kwa iliyokuwa Tovuti ya Serikali na kuwa Tovuti Kuu ya Serikali www.tanzania.go.tz, inayosimamiwa na Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, ambayo ni dirisha moja la kutolea taarifa na huduma za Serikali kwa wananchi.

**c) Tovuti Kuu ya Ajira**

Tovuti Kuu ya Ajira http://portal.ajira.go.tz, inayosimamiwa na Sekretariati ya Ajira.

**d) Mfumo wa Barua Pepe Serikalini (GMS)**

Mfumo wa Barua Pepe Serikalini (GMS) unaotumiwa na Taasisi za umma 402 zikiwemo ofisi za Ubalozi nje ya nchi, kwa ajili ya kubadilishana taarifa Serikalini. *Baraza* lilijiunga na mfumo huu mwaka 2014.

**e) Ofisi Mtandao**

Huu ni mfumo ambao unawezesha na kurahisisha shughuli za utawala za kila siku hususani mzunguko wa majalada na nyaraka ndani na miongoni mwa Taasisi za umma, Taasisi za umma 52 zinatumia mfumo huu mpaka sasa.

**f) Mfumo wa Huduma za Serikali kupitia Simu za Mikononi (mGov)**

Mfumo wa huduma za serikali kupitia simu za mkononi (mGov) http://mgov.ega.go.tz ulitengenezwa mwaka 2015 kwa lengo la kujumuisha huduma zote za simu za mkononi serikalini. Mfumo huu unatumia arafa (sms) katika kutoa na kupokea Taarifa. Taarifa hizi zinaweza kutoka Serikalini kwenda kwa wananchi au kutoka kwa wananchi kwenda Serikalini kupitia namba 15200. Pia inatoa orodha ya namba za huduma za Serikali (USSD) * 152*00#. mGOV imeunganishwa na watoa huduma wa simu za mkononi nchini Tanzania na jumla ya Taasisi za Umma 147 zinatumia huduma hiyo na miamala zaidi ya milioni 15 imefanyika mpaka sasa.

**g) Mfumo wa Malipo ya Serikali Kielektroni (GePG)**

Mfumo huu umetengenezwa kwa ushirikiano kati ya Wakala wa Serikali Mtandao na Wizara ya Fedha na Mipango ambao ndio wasimamizi wakuu wa Mfumo huu ni Mfumo wa Malipo ya Serikali Kielektroni (GePG). Mfumo huu unalenga kuongeza udhibiti katika usimamizi wa ukusanyaji wa mapato Serikalini. Mfumo huu unatumiwa na Taasisi za umma 385, watoa huduma za malipo 17 ambao ni Benki Kubwa 12 (NMB, STANBIC, NBC, CRDB, EXIM, TIB, BOT, ECOBANK, PBZ, DCB, DTB na TPB), Mifumo ya Fedha ya Simu za Mkononi 5 (Tpesa, TigoPesa HaloPesa, Mpesa na Airtel Money), mpaka sasa.

**h) Mfumo wa Vibali vya kusafiria nje ya nchi (e-Vibali)**

Mfumo wa e-Vibali (https://safari.gov.go.tz), unatumiwa na taasisi 389 katika kuomba na kupata vibali vya kusafiri nje ya nchi kwa safari za kikazi na binafsi kwa watumishi wa umma.

*Ndani ya Baraza*, idadi ya maombi ya vibali 12 vimeshafanyika na kati ya hizi 10 zimeidhinishwa na 2 kukataliwa hadi wakati taarifa hii inapotayarishwa.



"Kama mifumo haitazungumza, hakuna Serikali Mtandao. Lazima mifumo ifanye kazi sawasawa na lazima izungumze ili iwe inasababisha kuongeza ufanisi, kupunguza gharama za utendaji ndani ya taasisi na kuhakikisha kuwa huduma inapotoka kwenda kwa mwananchi kupitia TEHAMA inakuwa ni ya haraka", *Dkt. Jabiri Kuwe Bakari (katika picha)* akizungumza wakati wa Kikao Kazi cha Pili cha Serikali Mtandao 2019

**i) Mfumo wa kutoa Taarifa za Rushwa**

Serikali kwa kupitia wakala imetoa msaada wa kiufundi wa kusanifu na kutengeneza mfumo wa kutoa taarifa za rushwa kwa taasisi ya kuzuia na kupambana na rushwa ili kuwawezesha wananchi kutoa taarifa za vitendo vya rushwa kupiga simu na kupeleka arafa kupitia namba 113.

**j) Mfumo wa Ukusanyaji wa Taarifa za Miradi ya TEHAMA Serikalini (GIP)**

Mfumo huu wa GIP unatumiwa na taasisi takribani 77.

**k) Mfumo wa Huduma kwa Mteja**

Mfumo huu unaopatikana kupitia (http://helpdesk.ega.go.tz) au kupitia baruapepe egov.helpdesk@ega.g.tz unaotumika kutoa huduma na msaada wa kiufundi kwa huduma zinazotolewa na Wakala. Taasisi 315 zinatumia Mfumo huu na jumla ya matatizo 5,187 yanayohusu TEHAMA yameshughuliliwa.

**l) Mfumo wa Usimamizi wa Tiketi na Mizigo kielektroni (e-ticket and Cargo System)**

Mfumo huu unaotumiwa na Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) na Shirika la Reli Tanzania (TRC).

### iii. Mafunzo na Utafiti

Serikali kwa kupitia wakala wa Serikali Mtandao imetoa mafunzo mbalimbali ya kuwajengea uwezo Maofisa Tehama na watumishi wengine wa taasisi za Serikali ili kurahisisha utekelezaji na jitihada za Serikali Mtandao nchini Tanzania, miongoni mwa elimu inayotolewa ni kuimarisha matumizi sahihi na salama ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano katika kuendesha mifumo ya Tehama Serikalini.

Vilevile Kituo cha Utafiti, Ubunifu, Uundaji na Usaidizi wa Mifumo ya Serikali Mtandao (e-GovRIDSC) kina lengo la kufanyia utafiti, ubunifu na kuunda mifumo ya TEHAMA ya Serikali Mtandao yenye lengo la kuongeza ufanisi na urahisi kwa huduma pamoja na mifumo mbalimbali ya utoaji huduma zitolewazo na Serikali katika sekta zote.

SERIKALI imetoa wito kwa taasisi za Sekta binafsi wanaojishughulisha na utoaji wa huduma za TEHAMA na ujenzi wa mifumo ya TEHAMA kujenga uelewa wa viwango na miongozo ya TEHAMA ili kuisaidia Serikali.

*Baraza la Uwezeshaji* Wananchi Kiuchumi ikisaidiana na Wakala wa Serikali Mtandao imefanya mafunzo mbali mbali ili kuimarisha utendaji kazi na ufanisi katika matumizi ya vifaa vya TEHAMA.

### iv. Viwango vya Serikali Mtandao

Serikali imeweka msukumo mpya katika kutekeleza Serikali Mtandao kwa kutoa miongozo na viwango mbalimbali vilivyowekwa na serikali ili kuhakikisha wanajenga mifumo inayolinda taarifa za wananchi. Miongozo na viwango vya Serikali Mtandao zilisambazwa katika taasisi zote za Serikali ili kila zinapotaka kutekeleza mifumo ya Serikali Mtandao ziweze kuzingatia viwango na miongozo hiyo. Tatizo la usalama mitandaoni linazidi kukua kadri maendeleo ya Teknolojia yanavyozidi kukua, hivyo ili kuweza kukabiliana na changamoto hiyo ni lazima taasisi za umma kuzingatia ***viwango vyote vya usalama***. Miongoni mwa sababu za kuwekwa Viwango vya serikali mtandao ni:

- Kuimarisha matumizi sahihi na salama ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano katika kuendesha mifumo ya Tehama Serikalini.
- Usalama kwenye mifumo husika katika utekelezaji wa Serikali Mtandaowakati wa kubuni, kusanifu, kujenga, kusanikisha na kuendesha mifumo ya TEHAMA, badala ya kujenga mfumo kwanza na unapokamilika ndipo masuala ya usalama wa mifumo ya TEHAMA yanafikiriwa.

- Kujenga mifumo inayoendana na mahitaji halisi ya taasisi husika na kuepuka mifumo inayojengwa kwa shinikizo la wafanyabiashara, wafadhili au kwa matakwa ya mtu binafsi.
- Serikali itakuwa na uwezo wa kuepuka urudufu wa mifumo na kupunguza gharama kubwa za uendeshaji kwa kuwa na mifumo endelevu yenye gharama halisi inayofuata viwango vya Usalama katika kulinda taarifa na data za Serikali.
- Wafanyabiashara katika kada ya TEHAMA wanatakiwa kufuata miongozo na viwango hivi ili kujua mahitaji halisi ya Serikali na kuweza kujenga mifumo ya TEHAMA endelevu na inayoleta tija kwa umma.
- kuhakikisha kuwa mifumo yote ya TEHAMA ya Serikali inakuwa na mawasiliano na kubadilishana taarifa mbalimbali.
- kupunguza gharama za uendeshaji kwa kuwawezesha wananchi na wadau mbalimbali kupata huduma za Serikali kwa gharama nafuu kwa njia ya Mtandao.
- kuboresha utendaji wa Serikali utakao rahisisha upatikanaji wa huduma kwa wananchi na hivyo kutuwezesha kuufikia uchumi wa viwanda tunaoutarajia.




**Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Dkt. Mary Mwanjelwa (Mb) akifungua rasmi kikao kazi cha pili cha Serikali Mtandao kilichowajumuisha Watendaji Wakuu Serikalini katika ukumbi wa Chuo cha Sayansi ya Kompyuta, Habari na**

### v. Mtandao Unganishi wa Serikali (Government network)

Hadi kufikia Decemba 2018, Serikali imeunganisha taasisi za umma 72 na Mtandao wa Mawasiliano wa Serikali (GovNet) ambao Utawawezesha kutumia mtandao.

Taasisi hizo sasa zinaunganishwa kwenye mtandao wa fiber optic kitaifa, mfumo umerahisisha mchakato wa mawasiliano na kupunguza gharama katika taasisi za umma. Pia mikutano kwa njia ya video inafanywa kwa njia ya mfumo huu.

Dhumuni kuu la Serikali ni kuhakikisha mikoa, wilaya, mamlaka, halmashauri za jiji na Taasisi za Umma zinafikiwa na mfumo huu.

**vi. Huduma mtandao**

Hii ni huduma kwa umma kupitia mtandao (e-services), Serikali Mtandao inarahisisha utendaji kazi na utoaji wa huduma kwa kuimarisha miundombinu ya msingi kwa ajili ya utoaji wa huduma kwa mtandao kwa umma, raia na biashara kwa wakati, uwazi, urahisi na kwa gharama nafuu. Huduma kama Mfumo wa Malipo ya Serikali Kielektroni (GePG) ni mfano mzuri wa huduma mtandao.

## 2.2. UTEKELEZAJI WA SERIKALI MTANDAO KATIKA BARAZA LA UWEZESHAJI

Baraza la Taifa la uwezeshaji limekuwa likitekeleza Serikali Mtandao kwa ushirikiano na Wakala wa Serikali Mtandao katika kufanikisha kazi mbalilmbali zinazohusu mifumo, tovuti na miongozo mbalilmbali ya TEHAMA, maeneo makuu ambayo yametekelezwa ni haya yafuatayo:-

**a) Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano (National ICT Broadband Backbone)**

Baraza lilijiunga na huduma ya intaneti ya Mkongo wa Taifamwaka 2014. Mkongo wa Taifa wa mawasiliano ni huduma ya intaneti inayosimamiwa na Wakala wa Serikali Mtandao ikishirikiana na TTCL ambayo husambaza huduma ya Intaneti.

**b) Data centre ya Serikali Mtandao**

Baraza la Taifa la Uwezeshaji lina mifumo mbalimbali inayotumiwa kwa ajili ya shughuli za kiofisi. Baadhi ya mifumo hiyo ni kama Mfumo wa malipo (IFMIS) ambayo kwa ajili ya tahadhari na dharura zinazoweza kutokea, taarifa za mfumo huu zinahifadhiwa katika "Data Centre" za eGA.

Awali "backup" ya Mfumo wa malipo wa Epicor ulikuwa unachukuliwa katika kompyuta ambayo ipo ndani ya Baraza. Lakini sasa backup inahifadhiwa katika server za Wakala wa Serikali Mtandao na hivyo kupunguza hatari ya kupoteza mfumo mzima na data zake pale maafa yanapotokea.

**c) Miongozo ya TEHAMA ndani ya Baraza**

Baraza kupitia Kitengo cha TEHAMA na Takwimu kimeandaa nyaraka mbalimbali kwa ajili ya matumizi ya Baraza, ambazo ni :-

1. Sera ya TEHAMA,
2. Sera ya Matumizi ya TEHAMA,
3. Sera ya Usalama wa TEHAMA na
4. Mpango wa udhibiti wa Maafa ya TEHAMA.

Sera ya TEHAMA na Sera ya matumizi ya TEHAMA zimekamilika na kupitishiwa na Wakala wa Serikali Mtandao pamoja na wajumbe wa Baraza na zimeanza kutumika. Wakati Sera ya Usalama ya TEHAMA na Mpango wa Udhibiti wa Maafa ya TEHAMA zimekamilika zikingoja kupitishwa na wahusika wote ili zianze kutumika rasmi.

**d) Mapitio ya tovuti ya Uwezeshaji**

Tovuti ya awali ya Uwezeshaji ilitengenezwa miaka minne iliyopita, hivyo kuwepo na haja ya kupitia na kubadilisha ili kuendana na mabadiliko ya teknolojia na pia kukidhi miongozo na viwango vya Serikali Mtandano. Katika kufanikisha kazi hii, Barza limeshirikiana na wataalamu kutoka Wakala wa Serikali Mtandao (eGA).

**e) Kutengeneza Tovuti ya Ushiriki wa Watanzania (Local Content)**

Baraza pia kwa ushirikiano na eGA imetegeneza tovuti ya miradi mikubwa ya kimkakati ambayo inabeba dhima ya ushiriki wa watanzania katika uwekezaji (Local Content) itakayo kuwa na anuani ya Kiswahili www.ushirikiwatanzania.go.tz na anuani ya kiengereza www.localcontent.go.tz. Kuwepo kwa tovuti hii muhimu, ni utekelezaji wa agizo la Waziri wa nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (sera, bunge, kazi, vijana, watu wenye ulemavu), Mh. Jenista Muhagama alilolitoa katika Kongamano la wadau kujadili fursa zinazopatikana katika mradi wa bomba la mafuta kutoka Ohima Uganda mpaka Tanga Tanzania lililofanyika tarehe 23/02/2018 katika ukumbi wa Benki kuu ya Tanzania. Lengo kuu la tovuti hii ni kutangaza na kuonyesha fursa zote zinazopatikana katika miradi mikubwa ya kimkakati nchini na maendeleo ya mradi wenyewe.

## 2.3. MIPANGO YA BAADAE

a) Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2017/18 - sura ya tatu imetilia mkazo kujenga uwezo wa wajasiriamali kupata na kutumia taarifa za masoko kupitia TEHAMA.

b) Utekelezaji wa Mkakati Jumuishi wa Kuendeleza Ujasiriamali Tanzania –Sehemu ya 2.4 –Kuwezesha matumizi ya teknolojia na ubunifu; na pia sehemu 2.5- Kutumia tehama na simu za mikononi kuwezesha biashara ndogo na wakazi wa vijijini kupata huduma za fedha.
c) Kujiunga na mtandao wa Serikali "Government Network" ambayo inaratibiwa na Wakala wa Serikali Mtandao.
d) Kutumia "huduma kwa simu" inayotolewa na Wakala wa Serikali Mtandao ili kuweza kutoa taarifa mbalimbali za Uwezeshaji kwa njia ya simu.
e) Kuendelea kushirikiana na wakala wa Serikali katika mambo mbalimbali yanayohusu TEHAMA hasa katika Nyanja ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi.

# 3.0. HALI YA UCHUMI

## 3.1. UTANGULIZI

Serikali ya Tanzania katika awamu ya tano imeendelea kutekeleza na kusimamia utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ya mwaka 2004. Katika awamu hii pamoja na mambo mengine Serikali imekuwa ikifanya jitihada mbalimbali kwa lengo la kuweka mazingira ya kuwa na uchumi shirikishi ili kuwawezesha watanzania kushiriki kikamilifu na kunufaika na shughuli za kiuchumi ili ifikapo 2025 waweze kumiliki asilimia kubwa ya uchumi wa nchi kama dira ya Taifa ya mwaka 2025 yanavyoazimia.



*Waziri wa Fedha na Mipango, Mhe. Dkt. Philip Mpango akiwasilisha bungeni, Hotuba ya Hali ya Uchumi ya mwaka 2018 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2018/19*

## 3.2. PATO LA TAIFA


Kwa nadharia, ni vigumu kwa nchi kupata maendeleo ya kueleweka bila kukua kwa uchumi. Hii inamaanisha, pindi kutakapokuwa na ongezeko katika uchumi wa nchi ndipo maendeleo ya kiuchumi yatapatikana. Aidha, uchumi unaweza kukua pasipo kuambatana na maendeleo ya kiuchumi. Hali hii huweza tokea pale ukuaji huo unapowanufaisha watu wachache na kuwaacha wengi katika lindi la umaskini au sekta moja kuimarika ambayo haina mchango mkubwa kwa wananchi wengi.

Mojawapo ya viasharia ya ukuaji wa uchumi ni ongezeko la Pato la Taifa (GDP). Pato la Taifa ni kipimo cha thamani ya bidhaa na huduma zilizozalishwa katika nchi kwa kulinganisha ukuaji wa kipindi husika na kipindi sawia. Katika taarifa iliyotolewa na

Waziri wa Fedha ya mwezi Desemba, 2018, takwimu zilionyesha kuwa uchumi wa Taifa umeendelea kuimarika, ambapo ukuaji ulifikia asilimia 7.1% (2017) ukilinganishwa na wastani wa ukuaji wa 7.0% kwa miaka miwili iliyopita (2015-2016).

Pia uchumi wa Tanzania ulikuwa kwa kasi zaidi (7.1%) mwaka 2017 ukilinganisha na nchi za Afrika Mashariki kama Rwanda (6.1%), Uganda (5.1%), Kenya (4.9%) na Burundi (0.0%). Mnamo mwezi Januari hadi Juni 2018, Pato la Taifa lilikuwa kwa 7.0% ikilinganishwa na 6.3% katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2017. Sekta ambazo zilikuwa na mchango mkubwa kwa ongezeko la Pato la Taifa (Januari – Juni 2018) ni pamoja na: Kilimo (34.5%), ujenzi (16.8%), na Biashara (10.1%) ambapo sekta nyingine zilichangia kwa asilimia 38%. Aidha, Tanzania inakadiriwa kuwa miongoni mwa nchi zitakazokuwa na kasi ya ukuaji wa uchumi wa kuridhisha ifikapo mwaka 2026 kama inavyoonyeshwa kwenye jedwali Na.1.

***Mchoro Na. 2: Sekta ambazo zilikuwa na mchango mkubwa kwa ongezeko la Pato la Taifa (Januari – Juni 2018)***




*Chanzo: Taarifa ya Waziri wa Fedha na Mipango kwa Vyombo vya Habari, Desemba 2018*

***Jedwali Na 1: Mataifa 15 ambayo yanayokadiriwa kuongoza kwa kasi ya ukuaji wa uchumi kufikia 2026***

| Na. | Taifa | Ukuaji wa Uchumi kwa % |
|---|---|---|
| 1 | India | 7.89 |
| 2 | Uganda | 7.46 |
| 3 | Misri | 6.63 |
| 4 | Tanzania | 6.15 |
| 5 | Indonesia | 6.13 |
| 6 | Kyrgyzstan | 6.04 |
| 7 | Pakistan | 5.99 |
| 8 | Vietnam | 5.89 |
| 9 | Mali | 5.89 |
| 10 | Kenya | 5.87 |
| 11 | Ufilipino | 5.75 |
| 12 | Madagascar | 5.73 |
| 13 | Senegal | 5.7 |
| 14 | Liberia | 5.7 |
| 15 | Uturuki | 5.57 |

*Chanzo: Ripoti kutoka Kituo cha Kimataifa cha Maendeleo cha Chuo Kikuu cha Havard cha Marekani*

### 3.3. HALI YA MAISHA YA WANANCHI

Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, kwa kiwango kikubwa imekuwa chachu katika kuimarisha hali ya maisha ya wananchi. Kuimarika huko, kumechangiwa na maudhui ya Sera ambayo imelenga haswa katika kumkwamua mwananchi kiuchumi kwa kumfungulia milango ya fursa mbalimbali zitakazomuwezesha kuongeza kipato (kupitia upatikanaji wa ajira) na uwezo wa kumiliki mali na rasilimali zilizopo nchini.

Shughuli za kiuchumi ambazo zimekuwa na mchango mkubwa katika kuwainua wananchi kiuchumi ni pamoja na ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya barabara, reli na upanuzi wa bandari na viwanja vya ndege; mauzo ya mazao ya kilimo; ujenzi wa viwanda; na utoaji wa huduma za fedha na mawasiliano. Kwa mfano, hadi kufikia Februari 2019, jumla ya ajira 221,807 zilizalishwa nchini. Kati ya ajira hizo, ajira 146,414 sawa na asilimia 66 zimetokana na utekelezaji wa miradi ya umma ya ujenzi wa miundombinu ya kiuchumi. Aidha, ajira 75,393 ambazo ni asilimia 34 ya ajira zilizozalishwa zimetokana na uwekezaji katika sekta binafsi (*Hotuba ya Waziri Mkuu kuhusu mapitio na mwelekeo wa kazi za serikali na makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Bunge kwa mwaka 2018/19*).

Pia, ukuaji wa uchumi umekuwa na mchango katika kuiwezesha Serikali kuongeza wigo wa mapato nchini na uwezo wa kuboresha huduma mbalimbali za jamii hususan elimu (elimu ya msingi kuwa na mafunzo ya bure), afya (hospitali, vituo vya afya, zahanati, madawa, vitendanishi), maji na kuimarisha uzalishaji na upatikanaji wa umeme.



Aidha, katika hotuba iliyotolewa na Mh. Kassim M. Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika maadhimisho ya siku ya Umoja wa Mataifa tarehe 24 Oktoba 2018, mojawapo ya mambo aliyoyainisha ni pamoja na mikakati ambayo serikali imeiweka katika kuhakikisha vijana wanaendelezwa kimaisha pasipo kumuacha yoyote nyuma. Baadhi ya mikakati hiyo ni pamoja na: kuwepo na Sera ya Elimu ambayo imelenga kuhakikisha vijana wanapata elimu sambamba na kuwajengea ujuzi katika taaluma mbalimbali (mfano ni mradi wa Kukuza Stadi za Kazi na Ujuzi, unaoendeshwa na TPSF na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia); uanzishwaji wa programu za ujuzi kwa vijana kwa lengo la kuwapa vijana miongozo itakayowasaidia kupata ajira zinazoendana na taaluma zao; kujumuisha miongozo ya ajira na kazi za Umoja wa Mataifa katika sera za ajira na mipango ya maendeleo ya nchi; na uanzishwaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo ya jamii kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF).

Katika mwaka 2018/19, jumla ya vijana 32,563 wamewezeshwa kupata mafunzo ya ujuzi wa kujiajiri na kuajiriwa. Hii inahusisha vijana 18,800 waliopata mafunzo ya ujuzi wa kilimo kwa kutumia teknolojia ya vitalu nyumba pamoja na vijana 2,720 waliopatiwa mafunzo ya ufundi wa fani mbalimbali pamoja na vijana 10,443 waliopatiwa mafunzo ya

kurasimisha ujuzi uliopatikana kwa mfumo usio rasmi kwa fani za ufundi wa magari, useremala, uashi, upishi, huduma za vyakula na vinywaji, ufundi umeme, uchomeleaji, ufundi bomba, uchongaji vipuri na ushonaji nguo (*Hotuba ya Waziri Mkuu kuhusu mapitio na mwelekeo wa kazi za serikali na makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Bunge kwa mwaka 2018/19*).

### 3.4. SEKTA YA FEDHA

Sekta ya kifedha imeendelea kufanya vizuri ukilinganisha na miaka iliyosawia. Kwa mfano katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2018/19, Benki Kuu ya Tanzania ilikuja na mikakati mbalimbali kwa dhumuni la kuongeza ukwasi kwenye uchumi ili kuziwezesha benki za biashara kuongeza utoaji wa mikopo hususani kwa sekta binafsi. Miongoni mwa mikakati iliyoainishwa ni pamoja na: kupunguza kiwango cha riba ya mikopo kwa mabenki kutoka 9.0% hadi 7.0% Agosti 2018; utoaji wa mikopo ya muda mfupi kwa mabenki; na kununua fedha za kigeni kutoka katika benki za biashara na taasisi za Serikali. Hatua hizi zimesaidia katika kuongeza ukwasi katika mabenki ya biashara na punguzo katika riba kwa masoko ya fedha, mfano: Riba ya siku moja katika soko la fedha baina ya mabenki ilishuka kutoka 3.72% Oktoba 2017 hadi wastani wa 2.29% Oktoba 2018; riba za mikopo inayotolewa na mabenki ilipungua kwa kiasi kidogo kutoka wastani wa 18.1% katika ya Julai na Oktoba 2017 hadi 17.3% katika kipindi kama hicho mwaka 2018; na ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi uliongezeka kwa wastani wa 4.6% (Julai hadi Oktoba 2018) ukilinganisha na wastani wa 0.2% kwa kipindi kama hicho mwaka 2017.


Aidha katika kutatua changamoto zinazoikumba sekta ndogo ya kifedha, mfano: viwango vikubwa vya riba na tozo ambazo huanzia asilimia 3 mpaka asilimia 20 kwa mwezi; utoaji holela wa mikopo ambao unasababisha limbikizo la madeni kwa wateja; utaratibu mbovu wa ukusanyaji wa madeni ambao unasababisha wananchi kupoteza mali zao na kudhalilika; na kujitokeza kwa baadhi ya wananchi wasio waaminifu na wanaotumia mwaya wa kutokuwepo kwa sheria mahsusi katika u/toaji wa huduma ndogo za kifedha, Serikali ilipitisha sheria mahsusi ya kusimamia sekta ndogo ya fedha (*Micro finance act, 2018*) ambayo ilikadiriwa kuwa na watumiaji wengi wapatao milioni 15.4 sawa na asilimia 55.3 ya nguvu kazi ya Taifa (kwa mujibu wa utafiti wa Finscope wa mwaka 2017). Lengo kuu ilikuwa ni kutengeneza mazingira wezeshi katika upatikanaji na ulipaji wa mikopo kwa masharti nafuu kwa wananchi katika kujiendeleza kiuchumi.

### 3.5. MFUMUKO WA BEI

Mfumuko wa bei umeendelea kupungua kutoka wastani wa 4.3% mwaka 2017/18 hadi kufikia kiwango cha chini kabisa kuwahi kutokea miaka ya karibuni cha 3.0% mwezi Novemba 2018. Kupungua kwa mfumuko wa bei katika kipindi hicho kulichangiwa na: upatikanaji mzuri wa chakula katika masoko ndani na nchi jirani, ambapo uzalishaji wa chakula nchini ulifika tani 15.9m ikilinganishwa na mahitaji ya tani 13.3m kwa kipindi hicho, hivyo kuwa na utoshelevu wa chakula kwa 120%; kutengamaa kwa bei za mafuta katika soko la dunia; na utekelezaji madhubuti wa sera za fedha na za bajeti.

Kati ya Julai hadi Novemba 2018, Tanzania ilikuwa na kiwango kidogo zaidi cha mfumuko wa bei ikilinganishwa na Uganda (3.3%) na Kenya (4.8%). Pia katika ripoti ya mfumuko wa bei katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki ya Februari 2019, kiwango cha mfumuko wa bei nchini Tanzania (3.0%) kilikuwa chini ya wastani wa kiwango cha mfumuko wa bei kwa nchi hizo (7.6%). Kwa ujumla, nchi kumi na mbili zilizopo katika Jumuiya ya Maendeleo ya nchi za kusini mwa Afrika zilikuwa na viwango vya mfumuko wa bei chini ya wastani huo wakati nchi tatu zilizopo katika Jumuiya hiyo (Malawi, Angola na Zimbabwe) zilikuwa na viwango vya mfumuko wa bei juu ya wastani huo. Mchoro ufuatao umetoa maelezo zaidi.

***Mchoro Na 3 : Kiwango cha mfumuko wa bei (kwa asilimia) kwa nchi zilizopo kwenye Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC) – Februari, 2019***




*Chanzo: Ripoti kutoka tovuti ya Jumuiya ya Maendeleo ya Afrika Kusini ya Mfumuko wa bei ya Februari 2019*

## 3.6. UTENDAJI WA KIUCHUMI KWA UJUMLA (MACROECONOMIC PERFORMANCE)

Kutokana na ripoti ya "*tanzania economic outlook",* sekta ya huduma ilikuwa na mchango mkubwa katika ukuaji wa uchumit5rf nchini (39.3%). Uwekezaji binafsi ulikuwa ndiyo chachu katika ukuaji wa uchumi wa upande wa mahitaji (demand-side) kwa asilimia 63.9. Pia, sekta ya nje ilikuwa na mchango katika ukuaji wa uchumi ambapo  Kwa upande wa mchango katika ukuaji wa jumla halisi ya uzalishwaji wa bidhaa za ndani ya nchi, sekta ya ujenzi inaongoza kwa asilimia 22.7

## 3.7. CHANGAMOTO

Licha ya kuwa na mwenendo mzuri katika ukuaji wa uchumi, Tanzania bado imekuwa ikikabiliwa na changamoto mbalimbali ambazo kwa namna moja ama nyingine zinaweza athiri nchi kuwa na mwenendo mzuri katika ukuaji wa uchumi. Changamoto hizo ni pamoja na: ongezeko kwa gharama za mikopo kwenye masoko ya fedha duniani kutokana na mabadiliko ya sera za fedha kwa nchi zenye uchumi mzuri (hususan Marekani na nchi zilizopo bara la Ulaya) na kupungua kwa misaada ya kibajeti na fedha kutoka wadau wa maendeleo zinazotumika katika kugharamia miradi mbalimbali ya kimaendeleo; uwezekano wa kupanda kwa bei za mafuta kwenye soko la dunia kutokana na Marekani kuweka tena vikwazo kwa nchi ya Iran; na mabadiliko ya hali ya hewa yanaweza kuathiri uzalishaji hususan kwa sekta ya kilimo (ambayo ndiyo sekta tegemezi), ambapo shughuli nyingi za uzalishaji huko zinategemea mvua.


# 4.0. SERA NA SHERIA

## 4.1. UTANGULIZI

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kipindi cha Julai 2018 hadi Machi 2019 imetunga Sheria mbalimbali na kufanya marekebisho ya Sheria au Kanuni kwa lengo la kuhakikisha pamoja na mambo mengine watanzania wanawezeshwa kushiriki kikamilifu katika uchumi wa nchi ili kupunguza umaskini.

Katika kipindi hiki Sheria ambazo zimetungwa au kufanyiwa marekebisho ambazo zina lengo la kuwawezesha wananchi kiuchumi ni kama zifuatazo:-

1. Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha, 2018
2. Mabadiliko ya Sheria ya Bodi ya Utalii (Sura ya 364) kupitia *Written Laws (Miscellaneous Amendment)No.2 Act, 2019*
3. *Public Private Partnership (Amendment) Act, 2018*
4. *Mining (Local Content) (Amendment) Regulations, 2019*
5. Sheria ya Kodi ya Mapato (Sura 332)
6. Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (Sura 148)
7. *Excise (Management and Tarrif) Act (Sura 147)*




Malengo ya kutunga sheria hizo au maeneo yaliyobadilishwa yameainishwa hapa chini.

## 4.2. SHERIA ZILIZOTUNGWA AU KUFANYIWA MAREKEBISHO

### i. Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha

Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lilipitisha Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha ya mwaka 2018 mnamo tarehe 16 Novemba, 2018.Sheria hii ilitungwa ili kutekeleza matakwa ya Sera ya Taifa ya Huduma Ndogo za Fedha ya mwaka 2017. Sheria hii ilitungwa ili kuwalinda wananchi dhidi ya baadhi ya taasisi za kifedha zinazoibuka na kuwa kero kwao kwa kuweka riba kubwa pamoja na kutoa huduma zisizoridhisha.

Kifungu cha 12 cha Sheria hii kinaipa mamlaka Benki Kuu ya Tanzania kusajili, kusimamia na kudhibiti biashara ya huduma ndogo za fedha Tanzania bara.

Kifungu cha 16 cha Sheria hiyo kinatoa katazo kwa mtu au taasisi yoyote kufanya biashara ya kutoa huduma ndogo za fedha bila kuwa na leseni iliyotolewa na Benki Kuu ya Tanzania inayomruhusu kufanya biashara hiyo. Aidha masuala mengine yaliyozingatiwa katika Sheria hii ni pamoja na:

a) Kuipa Benki Kuu mamlaka ya kusimamia sekta na kuweka utaratibu wa kuiwezesha kushirikiana na mamlaka nyingine;
b) Kuweka masharti ya kuwalinda watumiaji wa huduma ndogo za fedha;
c) Kuweka masharti ya usimamizi wa utoaji riba na gawio;
d) Kuweka masharti kwa taasisi ndogo za fedha kushiriki katika mfumo wa ubadilishanaji wa taarifa za mikopo;
e) Kuweka utaratibu wa taasisi kutoa taarifa na kupambana na biashara ya fedha haramu;
f) Taratibu za kutoa takwimu na taarifa za uendeshaji;
g) Utaratibu wa ukusanyaji madeni;
h) Vigezo vya kuhama daraja moja kwenda jingine;
i) Masharti ya mtaji;
j) Makosa na adhabu kwa ukiukwaji wa sheria;
k) Ushirikishwaji wa watanzania katika sekta ikiwemo kwenye maeneo ya mafunzo na ajira;
l) Uhamasishaji wa ukuaji endelevu wa watoa huduma katika daraja la nne;
m) Utaratibu wa utoaji elimu ya fedha kwa watumiaji wa huduma ndogo za fedha n.k.

Benki Kuu inaandaa Kanuni za udhibiti na usimamizi wa huduma ndogo za fedha kulingana na madaraja tofauti yalioainishwa kwenye sheria ambayo ni:-

a) Benki na Taasisi za fedha zinazotoa huduma ndogo za fedha;
b) Vyama vya Ushirika wa Kuweka Akiba na Kukopa;
c) Kampuni za Huduma ndogo za Fedha kama vile Brac, Blue Finance, Tujijenge n.k.;
d) Asasi za fedha zisizo za Serikali, Mifuko na Programu za Serikali na Vikundi vya kifedha vya kijamii kama Benki za Kijamii za Vijiji (VICOBA)

Benki Kuu kwa kushirikiana na Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na wadau mbalimbali wanaandaa mpango wa kutoa elimu kwa wadau mbalimbali kuhusu Sera na Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha. Elimu hiyo ina lengo la kujenga uelewa wa wananchi kuhusu malengo na taratibu zilizoainishwa kwenye Sera na Sheria hiyo.

**ii. Public Private Partnership (Amendment) Act, 2018**

Sheria ya Ushirikiano kati ya Sekta ya Umma na Binafsi ilipitishwa mwaka 2010 kwa lengo la kuweka mfumo wakiutawala kwa ajili ya kusimamia masuala ya makubaliano ya ushirikiano kati ya sekta ya umma na binafsi, kuweka utaratibu na miongozo ya manunuzi na utekelezaji wa miradi hiyo. Sheria hii ilifanyiwa marekebisho mwaka 2014 na imefanyiwa tena marekebisho Septemba mwaka 2018. Marekebisho hayo ya mwaka 2018 pamoja na masuala mengine yameongeza kwenye kifungu cha 15 kifungu kidogo cha (5) ambacho kinalenga kwamba Kanuni zitakazotengenezwa chini ya kifungu hiki zizingatie masuala yafuatayo:-

a) Ushiriki wa kampuni za kitanzania na wataalam kwenye mikataba ya washauri wakitaalam (Consultancy contracts);
b) Utumiaji wa bidhaa za kitanzania na wataalam kwenye ujenzi na huduma zisizo zikitaalam (non consultancy services);
c) Kutoa kipaumbele (preference) kwa bidhaa za kitanzania wakati wa kufanya taratibu za tathmini;
d) Kujengea uwezo kampuni za kitanzania;
e) Na masuala mengine yanayo lenga kuwezesha kampuni za kitanzania na watanzania.

Aidha kifungu cha 28 kimebadilisha kipengele (g) kwa lengo la kumwezesha Waziri kutengeneza Kanuni zinazolenga kumwezesha mtanzania kiuchumi pamoja na ununuzi wa bidhaa na huduma za kitanzania, mafunzo na uhaulishaji wa teknolojia, ajira kwa watanzania na masuala ya uwajibikaji kwa jamii (Corporate Social Responsibility).

**iii. Mining (Local Content) (Amendment) Regulations, 2019**

Wizara ya Madini ilitoa Kanuni hizi tarehe 8 Februari, 2019. Kanuni hizi zimefanya mabadiliko amabayo yamelenga kuwezesha utekelezaji wa Kanuni kama ifuatavyo:-

(a) Tafsiri ya kampuni ya kitanzania imebadilishwa kumaanisha, Kampuni iliyosajiliwa chini ya Sheria za Kampuni (Companies Act No. 12 RE. 2002) na yenye hisa zisizopungua 20% zinazomilikiwa na watanzania na kuajiri wafanyakazi kwenye nafasi za juu za uongozi si chini ya 81% na wafanyakazi wa kitanzania 100% kwa nafasi ambazo si za uongozi na nafasi nyingine. Mabadiliko haya yamepunguza kiwango cha hisa za watanzania kwenye kampuni ya kitanzania (local company) zilizoainishwa kwenye Kanuni za mwaka 2018 ambazo zilikuwa si chini ya asilimia 51%.

(b) Kanuni hizi zimetaka wadau kwenye sekta ya madini kuwa na akaunti na benki za kitanzania ambazo watanzania wanashikilia si chini ya hisa za 20% kwenye benki hiyo.

(c) Kanuni hizi zinampa mamlaka Waziri wa Madini kwakushauriana na Tume ya Madini kutoa maelekezo ya kiwango cha chini cha utekelezaji wa *local content* ambazo ni mbadala kwa zile zilizoainishwa kwenye Jedwali la Kwanza la Kanuni.

**iv. Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 4) Act, 2019**

Sheria hii ilifanyia marekebisho Sheria ya Bodi ya Utalii (Tourist Baord Act, (Cap 364). Kifungu cha 4 cha Sheria hii kimebadilishwa kwa kuongeza majukumu ya Bodi ya Utalii ambapo kati ya majukumu ambayo Bodi imepewa ni pamoja na kuhamasisha na kuwezesha jamii karibu na eneo lenye utalii kunufaika na fursa za utalii. Hili jukumu litawezesha j amii zilizopo karibu na maeneo yenye utalii kunufaika kiuchumi na hivyo kupunguza umaskini.

**v. Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.2) Act, 2019**

Sheria hii imefanya marekebisho kwenye Sheria mbalimbali kama ifuatavyo:-

Sheria ya Kodi ya Mapato kwa kufuta kifungu cha 83 B na aya ya 4(d). Lengo la marekebisho haya ni kuondoa kodi ya zuio ya asilimia tano kwa wachimbaji wadogo wa madini ili kuhamasisha wachimbaji wadogo kuuza madini yao katika masoko ya madini yaliyopo nchini.

Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (Sura 148) imerekebishwa ambapo VAT itatozwa kwa asilimia sifuri kwenye madini ya metali na vito yatakayouzwa na wachimbaji wadogo wa madini kwenye masoko ya madini. Lengo ni kuhamasisha wachimbaji wadogo kuuza madini yao katika masoko ya madini nchini na kudhibiti utoroshaji wa madini.


Sheria ya *Excise (Management and Tarrif) (*Sura ya 147). Ushuru wa bidhaa imebadilishwa kwenye Sheria hii ampabo ushuru umepunguzwa kwenye pombe kali inayotengenezwa kwa kutumia zabibu zinazozalishwa nchini kutoka sh. 3,415 hadi sh. 450 kwa lita moja. Lengo la mabadiliko haya ni kuhamasisha viwanda kutumia zabibu zinazopatikana nchini na kuinua kilimo cha zao la zabibu.

### 4.3. MAZINGIRA YA BIASHARA

Pamoja na hatua mbalimbali za kuboresha mazingira ya biashara zinazochukuliwa na Serikali, nafasi ya Tanzania katika taarifa ya wepesi wa kufanya biashara duniani ambapo nchi 190 duniani hulinganishwa imekuwa ikishuka kinyume na lengo la Serikali


la kufikia nafasi ya tarakimu mbili (*double-digit ranking).* Taarifa hii inachapishwa na Benki ya Dunia kila mwaka baada ya kupima vigezo mbalimbali vya wepesi wa kufanya biashara kila mwaka (*Ease of Doing Business Report*). Taarifa ya wepesi wa kufanya biashara ya mwaka 2019 (Ease of Doing Business Report, 2019), iliyozinduliwa tarehe 31 Oktoba, 2018 inaonesha kuwa Tanzania imeendelea kufanya vizuri kwenye viashria vitatu na kufikia nafasi ya tarakimu mbili *(double digit ranking).* Viashiria hivyo ni upatikanaji wa mikopo (*getting credit)* ambapo Tanzania imeshika nafasi ya 60; kuheshimu utekelezaji wa mikataba na ubora wa utatuzi wa migogoro ya kibiashara *(enforcing cotracts)-* nafasi ya 64; na upatikanaji wa umeme *(getting electricity)-* nafasi ya 83. Hata hivyo, Tanzania kwa ujumla imeshuka kinafasi kutoka 137 mwaka 2018 hadi 144 kati ya nchi 190 duniani. Tanzania imefanya vibaya kwenye vigezo vya wepesi wa kufanya biashara katika viashiria vitatu ambavyo ni wepesi wa kusafirisha bidhaa zinazopitia bandarini kwenda nchi jirani *(trading across borders)* ambapo Tanzania imeshika nafasi ya 183 kati ya nchi 190; taratibu za kulipa kodi *(paying taxes)* imeshika nafasi ya 167 kati ya nchi 190 na taratibu za kuanzisha na kuendesha biashara *(starting a business)* ambapo imeshika nafasi ya 163 kati ya 190.

***Mchoro Na. 4: Viasharia ambayo Tanzania ilifanya vizuri katika wepesi wa kufanya biashara nchini***




*Chanzo: Ripoti ya Wepesi wa kufanya biashara ya Tanzania, 2019*

***Mchoro Na. 5: Viasharia ambayo Tanzania haikufanya vizuri katika wepesi wa kufanya biashara nchini***




*Chanzo: Ripoti ya Wepesi wa kufanya biashara ya Tanzania, 2019*

Uchambuzi wa awali umeonesha kwamba sababu kubwa za kushuka kwa nafasi ya Tanzania ni pamoja na:

i. Ufanisi mdogo kwenye utoaji wa huduma za umma kwa sekta binafsi (*public service delivery to the private sector*). Hali hii inajidhihirisha katika mifumo ya udhibiti wa biashara inayosimamiwa na taasisi za Serikali isiyozingatia matakwa ya kibiashara ya kupunguza muda na gharama za kupata leseni na vibali vya kufanya biashara. Gharama za kufanya biashara pia zinaongezeka kutokana na usimamizi dhaifu wa watendaji kwenye taasisi hizo, kukosekana kwa uwazi kwenye mifumo ya udhibiti wa biashara na taratibu nyingi za kiutawala, kuwepo kwa utitiri wa tozo, ada, vibali, leseni, na taasisi nyingi za udhibiti wa biashara, na mwingiliano wa majukumu miongoni mwa taasisi hizo (*multiplicity of fees and levies and overlapping mandates of regulatory authorities);*

ii. Kukosekana kwa mfumo madhubuti wa ufuatiliaji na tathmini ya maboresho ya mazingira ya biashara yanayotekelezwa na wizara na taasisi za Serikali;

iii. Kutokuwepo kwa mifumo ya kielektroniki kwa ajili ya kupokea na kushughulikia maombi na malipo mbalimbali ya wafanyabiashara kwa njia ya mtandao (*on-line services)*; na

iv. Udhaifu katika utoaji wa taarifa zilizokamilika za maboresho yaliyotekelezwa na taasisi za Serikali kwa wakati zikiwa na ushahidi wa kimaandishi unaokubalika kisheria *(documentary evidence of reforms)* pamoja na kukosekana kwa mkakati wa mawasiliano kati ya wizara na taasisi za Serikali na sekta binafsi (OWM, 2019).

Ili kuondoa changamoto hizo na kuboresha utendaji wa Serikali katika kuboresha mazingira ya biashara nchini Serikali imeziagiza Wizara na taasisi za Serikali kufanya uchambuzi wa kina wa maeneo wanayosimamia na kuandaa mikakati mahsusi ya kukabiliana na kushuka kwa nafasi ya Tanzania katika taarifa ya wepesi wa kufanya biashara. Taarifa na mikakati ya Wizara na Taasisi za serikali imejumuishwa kwenye Mpangokazi Jumuishi wa Kuboresha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji nchini (CAP) kwa kipindi cha miaka mitatu 2018/2019 – 2020/2021 (OWM, 2019).

Pia, utekelezaji wa Mpangokazi Jumuishi wa Kuboresha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji nchini (*Comprehensive Action Plan for Business Environment and Investment Climate Reforms in Tanzania - CAP)* utaiwezesha Tanzania kufikia lengo la nafasi ya tarakimu mbili kwenye taarifa ya wepesi wa kufanya biashara inayochapishwa na Benki ya Dunia kila mwaka. Mpangokazi huo unajumuisha hatua zinazotakiwa kuchukuliwa na wizara na taasisi za Serikali, muda wa utekelezaji, mfumo wa ufuatiliaji na tathmini na mkakati wa mawasiliano. Vilevile, Mpangokazi huo umejumuisha jitihada za Serikali za kuboresha mazingira ya biashara kupitia *Roadmap* iliyoidhinishwa na Serikali mwezi Julai, 2010; mapendekezo ya BRN ya mwaka 2014; na maboresho yanayopendekezwa kwenye *Blueprint* iliyoidhinishwa na Serikali mwezi Mei, 2018.

# 5.0. SEKTA YA ARDHI

## 5.1. UTANGULIZI

Ardhi ni moja ya sekta muhimu za kufanikisha malengo ya utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ya mwaka 2004. Sera ya Uwezeshaji inatambua kuwa umiliki wa Ardhi kwa wananchi una mchango mkubwa kufanikisha vipaumbele vya nchi na kuongeza ushiriki wa watanzania katika uwekezaji. Katika utekelezaji wa nguzo hii ya uwezeshaji katika kipindi cha mwaka 2017/18, Baraza limepokea taarifa ya utekelezaji ya uwezeshaji wananchi kiuchumi inayoonyesha juhudi mbalimbali zimeendelea kufanywa na Serikali kupitia sekta ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kama ifuatavyo:-

## 5.2. UWEZESHAJI WANANCHI

Serikali imeendelea kufanya jitihada mbalimbali za makusudi za uwezeshaji zenye lengo la kuongeza ushiriki wa Watanzania katika uwekezaji kupitia sekta ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Katika mwaka 2018/19, Serikali imefanya mambo ya msingi yafuatayo:-

a. Hati za Hakimiliki ya ardhi na Hati ya Hakimiliki ya Kimila zimewawezesha wamiliki wa ardhi kuzitumia hati hizo kama dhamana ya mikopo katika taasisi za fedha. Katika kipindi hiki, Hati za Hakimiliki **32,562** zimetolewa. Aidha, Hati za Hakimiliki za Kimila **88,840** zimetolewa kupitia Programu ya Kuwezesha Umilikishaji Ardhi inayotekelezwa katika wilaya ya Malinyi, Ulanga na Kilombero ambapo wamiliki wenye hati hizi wameweza kuzitumia kama dhamana na kukopa jumla ya shilingi **bilioni 1.3** kutoka katika Taasisi za fedha. Mikopo hii imewawezesha kuendesha miradi mbalimbali yenye kulenga katika kuboresha maisha yao.

b. Mfuko wa Mikopo ya Nyumba kwa Watumishi wa Serikali unaendelea kutoa mikopo kwa watumishi. Mikopo hii ni kwa ajili ya ujenzi, ununuzi au ukarabati wa nyumba ambazo watumishi hao huzitumia kwa ajili ya makazi au shughuli mbalimbali za kujiingizia kipato. Maombi yaliyopokelewa katika mwaka huu wa fedha ni shilingi bilioni **1.7** na marejesho ya mikopo ya nyuma yaliyokusanywa hadi tarehe 28 Februari 2019 ni shilingi **118,800,000**.

c. Kuendelea kuidhinisha taarifa za uthamini kwa ajili ya madhumuni mbalimbali kama vile kuwezesha wananchi kujipatia mikopo (*mortgage*) kutoka katika taasisi za fedha. Hadi mwezi Machi, 2019 taarifa za uthamini wa kawaida wa mali **7,223** zimeandaliwa na kuidhinishwa.

d. Wakala wa Taifa wa Utafiti wa Nyumba Bora na Vifaa vya Ujenzi imezalisha mashine za kutengeneza tofali za kupachika ambazo zimepunguza gharama za ujenzi. Mashine hizi zimegawiwa kwa vikundi mbalimbali vya vijana, ili waweze

kutengeneza matofali na kuyauza kwa wananchi na kuongeza kipato. Mashine **7** zimetolewa kwa kikundi kimoja cha Ukonga, Magereza na nyingine **43** zimetolewa kwa watu binafsi.

## 5.3. MAFANIKIO

### i. Ushiriki kwenye Miradi ya Kimkakati.

Ufuatiliaji umeendelea kufanyika na kubaini utekelezaji wa miradi ya kimkakati unashirikisha Wizara hususani katika masuala mtambuka yenye kuhitaji utaalam wa Wizara ama taasisi husika za Serikali. NEEC imebaini kuwa Wizara ya Ardhi haishiriki moja kwa moja ila imeweza kufanikisha mambo ya msingi yafuatayo.

a. Kushiriki katika uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi kwa ajili ya uendelezaji wa eneo la ukanda wa Reli ya Kisasa (Standard Gauge Railway – SGR) kuanzia Dar es Salaam hadi Isaka, Shinyanga na eneo la ukanda wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) kutoka Mtukula hadi Chongoleani, Tanga.

b. Kwa upande wa mradi wa Bomba la Mafuta, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Reli Tanzania (*Tanzania Railway Corporation - TRC*) inafanya uthamini katika njia ya Reli kutoka Mvomero mkoani Morogoro hadi Makutupora, Manyoni mkoani Singida yenye umbali wa **kilometa 333.081** kwa ajili ya ulipaji wa fidia kwa wananchi kupisha mradi.

c. Kushiriki pia katika upangaji, upimaji na uthamini kwa ajili ya utwaaji wa maeneo ya vipaumbele ambayo yanategemea kumilikishwa kwa Shirika la Maendeleo ya Petroli. Kuanza kutekelezwa kwa miradi hii kutawapatia fursa ya ajira wanavijiji wanaoishi jirani na maeneo ya mradi.

### ii. Ununuzi wa Huduma na Bidhaa

Hali halisi inaonyesha kuwa ununuzi wa huduma na bidhaa umeendelea kuzingatiwa kutoka katika kampuni za kitanzania kuanzia Julai, 2018 hadi kufikia Machi, 2019. Hali halisi ya utekelezaji inaonyesha mambo ya msingi yafuatayo yalifanyika:-

a. Shirika la Nyumba la Taifa lilichaguliwa kuwa mkandarasi wa jengo la Wizara katika kijiji cha Serikali katika eneo la Ihumwa, Dodoma. Katika mradi huu wanavijiji wanaoishi jirani na eneo la mradi walipata fursa ya ajira kwa kazi zisizohitaji utalaam. Pia, ujenzi wa majengo ya Wizara umetumia malighafi zinazozalishwa nchini na hivyo, kuongeza kasi ya ustawi wa wawekezaji wa ndani.

b. Kuendelea kupata huduma za ulinzi na usafi kutoka kwenye kampuni binafsi za wazawa ambazo ni kampuni ya *Suma JKT, Salu Security Services, Speed Security Services* na *Fulltime Security Services* ambazo zinatoa huduma ya ulinzi. Pia, Wizara imeendelea kupata huduma za usafi katika Ofisi zake kutoka kwa kampuni binafsi ya wazawa ya *Nansimo General Enterprises*.

c. Huduma mbalimbali za utoaji wa vifaa vya ofisi zinatolewa na kampuni za kitanzania zilizosajiliwa na Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini na hupatikana kwa ushindani baada ya zabuni kutangazwa. Kampuni mbalimbali za wazawa ambazo zilishinda zabuni hizo ni pamoja na *Action Garage, Leonard Automotive Garage, Nduvini Auto Works, Dubai Trading Company, Chef Asili Co Ltd, Firebrands Technologies, Bama Supplies and Services Ltd, Scott Networks Business Centre, Arfam Bakery, Silver General, Distributors Co. Ltd, Sac General Traders, TEMESA Regional Manager Dodoma, Ngoto Furniture, Supplies and Co. Ltd, Kanana Motors, M/S Outshining, Government Printers, Computer Online Tanzania Limited, Victory Bookshop* na *Mwanga Refrigeration and Aircondation* ambapo hadi sasa zinaendelea kutoa huduma katika Ofisi mbalimbali za Wizara.

d. Kushirikiana na Mamlaka za upangaji na kuwezesha kuingia mikataba na makampuni binafsi nchini ya upangaji na upimaji ardhi kwa ajili ya kupanga na kupima ardhi za Halmashauri na hatimaye ardhi humilikishwa kwa wananchi na taasisi mbalimbali. Uwezeshaji huu umekuwa na manufaa makubwa kwa nchi na kuwezesha ardhi kutumika kama dhamana ya kupata mikopo kutoka katika mabenki na taasisi za kifedha

### 5.4. MABORESHO YA SERA, SHERIA NA KANUNI

Taarifa ya utekelezaji inaonyesha mazingira wezeshi ambayo Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi imeyatengeneza ili kuwezesha Watanzania kushiriki kikamilifu katika shughuli za kiuchumi yametokana na mabadiliko ya sheria, kanuni, mikataba, kujenga uwezo kama ifuatavyo:-

i. Marekebisho ya Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995 yanayoendelea hivi sasa yanatoa fursa kwa Mtanzania yeyote kupata na kutumia ardhi bila kujali dini, jinsia au kabila.

ii. Sheria ya Ardhi (Sura 113) ilifanyiwa marekebisho kupitia Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali Na. 1 ya mwaka 2018 kwa lengo la kuhakikisha rasilimali ardhi inatumika kikamilifu kukuza uchumi wa nchi na hivyo kuwainua wananchi kiuchumi. Ilibainika kwamba, wawekezaji katika ardhi hususan katika mashamba makubwa walikuwa wanatumia ardhi kama dhamana kwa ajili ya kupata mikopo kutoka katika taasisi za fedha za ndani na nje ya nchi. Hali hii ilitokana na ukweli kwamba pamoja na Hati kuwa na masharti ya kuendeleza ardhi, bado Sheria ya

Ardhi Sura 113 haikuweka mfumo imara wa kudhibiti matumizi ya fedha hizo ili iweze kutumika katika uendelezaji wa ardhi au uwekezaji mwingine nchini. Kwa kuendeleza ardhi kulingana na masharti yaliyowekwa katika Hati, Watanzania wanapata fursa ya ajira katika miradi ya aina hii.

iii. Serikali kupitia Wizara imekamilisha utungaji wa Kanuni za Sheria ya Uthamini na Usajili wa Wathamini Namba 7 ya mwaka 2016. Kanuni hizi zimeanza kutumika tarehe 23 Machi 2018 kwa Tangazo la Serikali Namba 136 la tarehe 23 Machi 2018. Kanuni hizi zimewezesha kuongeza kasi ya utekelezaji wa sheria hasa eneo la udhibiti wa viwango vinavyotumika katika uthamini wa mali.

iv. Katika maadhimisho ya Siku ya Makazi Duniani yaliyofanyika tarehe 01 Oktoba 2018, Wizara kwa kushirikiana na taasisi za umma na binafsi ilitoa elimu kwa wananchi ya namna ya kurejelesha *(recycling)* taka na vyuma chakavu ili kujiongezea kipato.

v. Serikali kupitia Wizara inakamilisha maandalizi ya Mwongozo wa kuanzisha na kuendesha Vyama vya Ushirika wa Nyumba nchini, ambao utawawezesha wananchi wa kipato cha chini kumiliki nyumba za gharama nafuu, ambazo wanaweza kuzitumia kwa makazi pamoja na shughuli za biashara.

# 6.0. USHIRIKA

## 6.1. UTANGULIZI

Kwa muda mrefu upatikanaji wa takwimu sahihi za vyama vya ushirika umekuwa si wa uhakika katika Tanzania hadi ilipoanzishwa Tume ya Maendeleo ya Ushirika (TCDC) mwaka 2013. Mara baada ya kuanzishwa Tume ilifanya zoezi la uhakiki wa Takwimu za Vyama vya Ushirika nchini ili kupata takwimu sahihi za Vyama vya Ushirika. Kazi ya uhakiki ilikamilika mwaka 2018 ambapo takwimu halisi za vyama vya ushirika zilipatikana kama zinavyooneshwa hapa chini;

## 6.2. IDADI NA AINA YA VYAMA VYA USHIRIKA

Hadi kufikia **Februari 2019**, Tanzania Bara ilikuwa na vyama vya ushirika **11,331** ikilinganishwa na vyama **10,620** mwezi Februari 2018 sawa na ongezeko la vyama **711** (asilimia 6.3). Kati ya hivyo; AMCOS **3,719**; Ufugaji wa nyuki **20**; Walaji **36**; Uvuvi **687;** Miradi ya ubia **34**; Nyumba **19**; viwanda **30**; Umwagiliaji **25**; Ufugaji **181**; Madini **94**; Akiba na Mikopo **6,137**; Huduma **144**; Usafirishaji **16;** vyama vikuu **46**; vyama vya aina mbalimbali **24** na vyama vingine **119**. Takwimu hizi halisi zilizoainishwa katika jedwali hapa chini zimepatikana baada ya kumalizika kwa kazi ya uhakiki wa vyama vyote vya ushirika nchini. Taarifa ya uhakiki inaonesha vyama vingine vimeongezeka na vingine kupungua. Sababu kubwa ni vyama vingine havikuonekana wakati wa zoezi la uhakiki na vingine vilifutwa. Hata hiyo tathmini ya jumla inaoneshwa vyama vimeongezeka kwa asilimia 7.




*Waziri Mkuu akizindua* ***Ushirika Afya*** *kwa Wanachama wa Vyama vya Ushirika nchini. Uzinduzi huo ulifanyika Ushetu, Kahama – Shinyanga, Julai 16, 2018.*

## 6.3. HALI YA VYAMA VYA USHIRIKA

Hadi Februari 2019 Tume imebaini vyama hivi **11,331** vina jumla ya wanachama **3,998,193,** Kiasi cha mtaji uliopo ni Hisa za wanachama zenye thamani ya Shilingi **78,751,193,414,** Katika vyama vya Akiba na Mikopo (SACCOS), kiasi cha akiba kilichowekwa na wanachama ni Shilingi **538,413,737,576.** Katika kipindi hicho jumla ya mikopo iliyotolewa na vyama vya Akiba na Mikopo ni **Shilingi 1,299,661,801,996** ambapo jumla ya mikopo iliyorejeshwa ni Shilingi **809,328,103,267** na mikopo chechefu iliyopo ni Shilingi **25,527,250,227.** Aidha taarifa hii inaonesha ongezeko la wanachama 1,751,862 (78%) kutoka 2,246,331 Februari 2018 hadi wanachama 3,998,193 Februari 2019. Kwa ujumla katika kipindi hicho vyama vya ushirika vimeongezeka kwa idadi ya vyama, idadi ya wanachama, mtaji na mikopo iliyotolewa.

***Jedwali Na 2: Taarifa ya vyama vya ushirika hadi kufikia Februari 2019.***

| NA | AINA YA USHIRIKA | FEBRUARI 2018 | FEBRUARI 2019 | ONGEZEKO/PUNGUFU | % |
|---|---|---|---|---|---|
| **1** | AMCOS | 3,338 | 3,719 | 381 | 11 |
| **2** | SACCOS | 5,737 | 6,137 | 400 | 7 |
| **3** | HUDUMA | 157 | 144 | -13 | -8 |
| **4** | MADINI | 204 | 94 | -110 | -54 |
| **5** | MIFUGO | 207 | 181 | -26 | -13 |
| **6** | MULTPURPOSE | 52 | 24 | -28 | -54 |
| **7** | NYUKI | 56 | 20 | -36 | -64 |
| **8** | NYUMBA | 33 | 19 | -14 | -42 |
| **9** | UMWAGILIAJI | 78 | 25 | -53 | -68 |
| **10** | VYAMA VIKUU | 40 | 46 | 6 | 15 |
| **11** | USAFIRISAJI | 24 | 16 | -8 | -33 |
| **12** | UVUVI | 85 | 687 | 602 | 708 |
| **13** | VIWANDA | 118 | 30 | -88 | -75 |
| **14** | WALAJI | 132 | 36 | -96 | -73 |
| **15** | BENKI | 13 | | -13 | -100 |
| **16** | JOINT ENTERPRISE | 32 | 34 | 2 | 6 |
| **17** | VINGINE | 312 | 119 | -193 | -62 |
| JUMLA | | **10,620** | **11,331** | **711** | **7** |
| 1 | Wanachama | 2,246,331 | 3,998,193 | 1,751,862 | 78 |
| 2 | Hisa-SACCOS | | 78,751,193,414 | | |
| 3 | Akiba-SACCOS | | 538,413,737,576 | | |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 4 | Mikopo tolewa-SACCOS | | 1,299,661,801,996 | | |
| 5 | Mikopo rejeshwa-SACCOS | | 809,328,103,267 | | |
| 6 | Mikopo chechefu-SACCOS | | 25,527,250,227 | | |

*(Chanzo TCDC 2019)*

## 6.4. USIMAMIZI NA UHAMASISHAJI WA MAENDELEO YA USHIRIKA NCHINI

### 6.4.1. Usimamizi na uhamasishaji wa maendeleo ya ushirika

Tume ya Maendeleo ya Ushirika inasimamia maendeleo ya ushirika kwa kuzingatia vipao mbele vya kila mwaka wa fedha ambapo kwa mwaka wa fedha 2018/2019, Tume imetekeleza majukumu yake kwa;

### 6.4.2. Kuimarisha udhibiti na usimamizi wa vyama vya ushirika nchini

Hadi kufikia mwezi Februari 2019, Tume imefanya ukaguzi wa mara kwa kwa vyama vya ushirika 3,140 sawa na asilimia 54 ya lengo la kukagua vyama 5,830. Aidha, Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (COASCO) ilifanya ukaguzi wa nje kwa vyama vya ushirika 2,297 sawa na asilimia 57.4 ya lengo la kukagua vyama 4,000. Kati ya vyama vilivyokaguliwa na COASCO 4.62% vilipata hati inayoridhisha, 64.58% vilipata hati yenye shaka, 21.57% vilipata hati isiyoridhisha na 9.23% vilipata hati mbaya. Aidha, Tume imevisimamia vyama vya Ushirika katika;

i. Kuandaa na kuwasilisha Ofisi ya Mrajis wa Vyama vya Ushirika maombi ya kuidhinishiwa makisio ya mapato na matumizi kwa wakati yaani miezi miwili kabla ya kuanza msimu.
ii. Kufunga hesabu na kuziwasilisha kwa Mkaguzi wa nje (COASCO) ndani ya kipindi cha miezi mitatu baada ya kukamilisha msimu kwa mfano KTCU, NJORECU na Milambo
iii. Vyama vya ushirika 987 kufanya mikutano mikuu kwa mujibu wa Sheria
iv. Kuandaa kanuni mbalimbali kama vile kanuni za fedha, kanuni za utumishi na sera ya manunuzi mfano LATCU Ltd, KACU Ltd,
v. Kuhuisha masharti ya Vyama ili yaendane na Sheria ya Vyama vya Ushirika Na.6 ya mwaka 2013.
vi. Vyama vya upili kama vile MBIFACU Ltd, SONAMCU Ltd, RUNALI Ltd na WETCU Ltd kuajiri watendaji wenye sifa kama meneja Mkuu, wahasibu, wakaguzi wa ndani, n.k.

### 6.4.3. Kuratibu uhamasishaji wa maendeleo ya sekta ya ushirika, utafiti na mafunzo

**a) Kuhamasisha maendeleo ya sekta ya ushirika.**

Kwa upande wa sekta ya kilimo wakulima wamehamasishwa kujiunga pamoja ili kukusanya mazao yao na kupata soko la uhakika. Aidha, uhamasishaji umehusisha ufufuaji wa vyama sinzia. Vyama vya ushirika vilivyoanzishwa na kufufuliwa ni pamoja na vyama vya :-

i. **Michikichi:** mkoani Kigoma wakulima 2,752 wamehamasishwa ambapo vyama ushirika vya msingi vipatavyo 12 vimesajiliwa;
ii. **Pamba:** mikoa ya Simiyu, Geita, Mwanza, Singida, Shinyanga, Tabora, Mara, Kigoma na Dodoma ambapo vyama 1,469 vya msingi vimeamshwa;
iii. **Miwa:** mikoa ya Manyara, Kagera (Missenyi) pamoja na Morogoro (Mtibwa) ambapo wakulima wa zao hili wapo katika hatua za awali za uundaji wa vyama vya msingi vya ushirika;
iv. **Chai:** mikoa ya Mbeya wakulima 26,570 wamehamasishwa ambapo vyama 8 vya msingi vimeanzishwa na Tanga vyama 7 vya msingi vipo katika mchakato wa kuandikishwa;
v. **Kakao:** mikoa ya Mbeya vyama vya msingi 53, chama kikuu 1 vimeamshwa na vyama vya msingi 6 vimeanzishwa. Aidha, katika mkoa wa Morogoro uhamasishaji unaendelea;
vi. **Zabibu:** mkoani Dodoma vyama vya ushirika vya msingi 7 vinategemewa kuandikishwa;
vii. **Korosho:** mkoani Lindi vyama vya msingi 2 vimeanzishwa;
viii. **Kahawa:** mikoa ya Kilimanjaro, Arusha, Mbeya, Songwe, Kagera na Mara, vyama vyama 6 vimeamshwa ; na
ix. **Pareto:** mkoani Mbeya wakulima 971 wamehamasishwa ambapo vyama vya msingi 10 vinatarajiwa kuanzishwa.

**b) Utafiti na Mafunzo**

Tume imeendelea kufanya utafiti ili kuendeleza sekta ya ushirika nchini. Kufikia Februari 2019 tafiti 2 zimefanyika katika mkoa wa Dodoma. Utafiti wa kwanza; Tume ya Maendeleo ya Ushirika kwa kushirikiana na Tume ya Umwagiliaji imefanya utafiti wa awali kubaini matumizi ya maji ya mafuriko yanayopita bonde la Mtanana – Kibaigwa. Utafiti huo umebaini kuwa upo uwezekano wa kuvuna maji hayo na kuyatumia katika shughuli za kilimo cha umwagiliaji, ufugaji na uvuvi kupitia ushirika

Aidha, kwa upande wa mafunzo Tume imetoa mafunzo kwa wajumbe wa Bodi na Watendaji wakuu wa Vyama Vikuu 18 na miradi ya pamoja. Jumla ya viongozi wa bodi 408 wamepatiwa mafunzo mbalimbali yanayohusu usimamizi wa vyama vya ushirika nchini.

#### 6.4.4. Kuimarisha masoko, uwekezaji na uwezeshaji wananchi kiuchumi.

Katika jitihada za kujenga na kuimarisha uwezo wa kiuchumi katika vyama vya ushirika, Tume imeendelea kuvijengea uwezo vyama katika masoko na uwekezaji.

Hadi kufikia Februari 2019 Vyama vikuu vya ushirika vya mazao vya kahawa vya KDCU Ltd na KCU (1990) Ltd vimeunganishwa na mfumo wa soko la moja kwa moja na kuuza kahawa ya wakulima kwa bei ya ushindani ambapo gunia la kilo 60 limeuzwa kwa wastani wa Dola za Kimarekani 160.63 ikilinganishwa na bei ya mnada ya Dola za Kimarekani 84.97.

Wakulima wa Kakao wa mkoa wa Mbeya wamenufaika na utaratibu wa kuuza kakao kupitia vyama vya ushirika chini ya Mfumo wa Stakabadhi za Ghala ambapo kabla ya mfumo kakao ilikuwa ikiuzwa bei ya Shilingi 3,200 ikilinganishwa na Shilingi 5,011 baada ya mfumo. Aidha, AMCOS 9 zimepata soko la moja kwa moja katika nchi za Afrika Kusini, Japani na Uholanzi na kuuza kwa bei ya Shilingi 6,500 kwa kilo

### 6.5. MIPANGO YA BAADAYE

Mpango na Bajeti ya Tume ya Maendeleo ya Ushirika kwa mwaka 2019/2020 unalenga kutatua changamoto zinazoikabili Sekta ya ushirika. Mpango huu umeandaliwa kwa kuzingatia: Dira ya Maendeleo ya Taifa (2025), Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa miaka mitano, Mwongozo wa Mpango na Bajeti 2019/2020-2021/2022, Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2015-2020, Mpango Mkakati wa Tume na mapitio ya Bajeti ya mwaka 2018/2019.

Hivyo, maeneo ya kipaumbele yatakayotekelezwa ni kama ifuatavyo:

i. Kuimarisha udhibiti na usimamizi wa vyama vyama vya ushirika;

ii. Kuratibu uhamasishaji wa maendeleo ya sekta ya ushirika, utafiti na mafunzo;

iii. Kuimarisha masoko, uwekezaji na uwezeshaji wananchi kiuchumi kupitia ushirika

iv. Kuhuisha Sera ya maendeleo ya ushirika ya mwaka 2002 na kupitia Sheria za ushirika

v. Kujenga uwezo wa Tume kuhudumia watumishi wake na wadau

### 6.6. CHANGAMOTO

Changamoto zinazovikabili vyama vingi vya ushirika nchini ni pamoja na;

a) Ugumu wa upatikanaji wa takwimu sahihi unaotokana na utunzaji mbovu wa kumbukumbu za vyama.
b) Baadhi ya viongozi wa vyama kukosa elimu na ujuzi wa kutosha kusimamia vyama vya ushirika.

c) Migogoro kwa baadhi ya vyama baina ya viongozi na wananchama
d) Kukosekana kwa uaminifu na uadilifu kwa baadhi ya viongozi na wafanyakazi, hali inayopelekea upotevu wa mali za wanaushirika.
e) Marejesho duni ya mikopo kwa baadhi ya wakopaji ndani ya vyama vya ushirika
f) Ukosefu wa fedha za usimamizi wa vyama kwa maafisa ushirika katika mikoa husika.
g) Ukosefu wa masoko ya bidhaa zinazozalishwa na wanaushirika na hivyo kuchangia marejesho duni ya mikopo.

# 7.0. SOKO LA MITAJI NA HISA LA DAR ES SALAAM

## 7.1. UTANGULIZI

Miongoni mwa nguzo muhimu katika Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ni pamoja na uwepo wa Chombo au Taasisi za kusimamia masoko ya hisa na mitaji hapa nchini kutoka kwa wawekezaji wa ndani na nje ya Tanzania.

Soko la Hisa la Dar es salaam (DSE) limekuwa likifanya kazi hii tangu kuanzishwa mwaka 1996.Kazi za msingi za Taasisi hii ni pamoja na kuwezesha upatikanaji wa mitaji ili kutekeleza miradi mbalimbali ya Kiuchumi na kuwezesha uwekezaji ambapo jukumu hili hutekelezwa katika mazingira shirikishi na uwazi ili kutoa fursa kwa kila mhitaji.

Kwa kuzingatia ukweli kuwa kuna mahusiano kati ya ukuaji wa shughuli za Kiuchumi na maendeleo ya watu kwa upande mmoja na matumizi sahihi ya huduma za taasisi za kifedha, imekuwa ni jambo muhimu kwa DSE kubuni bidhaa na huduma za kifedha zenye malengo kama inavyoainishwa na Mpango wa Taifa wa Huduma za Kifedha Jumuishi yaani "National Financial Inclusion Framework 2018 – 2022".

Kampuni zilizoorodheshwa katika soko la Hisa hadi kufikia Mwezi Februari 2019 ni jumla ya kampuni 28; 21 zikiwa ni kampuni za ndani na saba (7) za nje ambazo zimeorodheshwa kwa utaratibu wa "cross-listing".

***Jedwali Na. 3: Orodha ya Kampuni za ndani na nje***

| Kampuni za ndani | |
|---|---|
| | |
| Tanga Cement | Kampuni ya Sigara (TCC) |
| NMB Bank | YETU Microfinance Bank |
| Swala Oil and Gas Tanzania PLC | Benki ya biashara (DCB) |
| Twiga Cement | CRDB Bank |
| Dar es salaam stock exchange | MUCOBA Bank PLC |
| TATEPA | Maendeleo Bank PLC |
| TCCIA Investment PLC | Swissport Tanzania PLC |
| Tanzania Breweries | National Investment Company Limited (NICOL) |
| Precision Air | Mwalimu Commercial Bank PLC |
| Vodacom Tanzania | Mkombozi Commercial Bank PLC |
| TOL Gas Limited | |
| | |

| Kampuni za nje | |
|---|---|
| | |
| Kenya Commercial Bank | East African Breweries |
| ACASIA | National Media Group |
| Uchumi Supermarket | Kenya Airways |
| Jubilee Holdings Limited | |
| | |

Katika kipindi cha mwaka jana 2018 kampuni za ndani zilikuwa 20 lakini mpaka sasa Kampuni moja imeongezeka na kufikia 21 huku za nje zikiwa 7. Vilevile hadi kufikia Desemba 2018, DSE ilikuwa imeorodhesha kampuni 28, ikiwa ni pungufu ya kampuni 4 kufikia malengo iliyojiwekea. Upungufu huo ulitokana na kutokamilishwa kwa taratibu kwa upande wa Kampuni za simu ambazo zinatakiwa na sheria inayosimamia sekta ya mawasiliano kuuza sehemu ya umiliki wake kwa umma na kujiorodhesha katika Soko la Hisa la Dar es Salaam.

Hadi kufikia Desemba 2018 DSE ilikuwa imepokea maombi ya kampuni za Tigo, Airtel na Halotel lakini bado hazijaweza kuorodheshwa kwenye soko la hisa kutokana na kutokamilika kwa baadhi ya taratibu.

### 7.2. HATIFUNGANI ZA SERIKALI

Kwa upande wa Hatifungani za Serikali (Government bonds), katika kipindi hiki, Serikali iliorodhesha hatifungani zenye thamani ya shilingi bilioni 1,451 Hii ni sawa na upungufu wa **asilimia 27** kulinganisha na hatifungani za Serikali **shilingi bilioni 1,989** zilizoorodhoshwa Mwaka 2017/18. Kwa ujumla, hatifungani za Serikali zilizoorodheshwa sokoni hadi Mwezi wa **Februari 2019 ni shilingi bilioni 9,196**. Hii ni sawa na ongezeko la **asilimia 4 ikilinganishwa na TZS 8,838** katika kipindi kama hiki mwaka 2018.

### 7.3. HATIFUNGANI ZA MAKAMPUNI BINAFASI (CORPORATE BONDS)

Kwa upande wa hatifungani za Makampuni binafsi (Corporate bonds),hadi kufikia Mwezi Februari 2019, hatifungani za Kampuni zenye thamani ya **shilingi bilioni140** zilikuwa zimeorodheshwa katika soko.

Kuhusu thamani ya hisa zilizopo sokoni (Total Market Capitalization) ilikuwa ni **shilingi bilioni 20,337. Kati ya hizi, jumla ya shilingi bilioni 9,272** ni kwa makapuni ya ndani.

### 7.4. DHAMANA

Uuzaji na ununuzi wa dhamana (hisa na hatifungani) ni jambo ambalo hufanywa kwa uwazi na huru hivyo kuwezesha utambuzi wa thamani ya uwekezaji kwa wawekezaji aina wa mbalimbali.

Kwa kipindi hiki hadi Mwezi Februari 2019, hisa zenye thamani ya shilingi **bilioni 98.49 ziliuzwa na kununuliwa**. Hii ni sawa na pungufu kwa asilimia 75 ikilinganishwa na hisa zenye thamani ya shilingi bilioni 395.62 zilizouzwa na kununuliwa katika kipindi kama hiki Mwaka 2018.

Kwa upande wa hatifungani, katika Mwaka 2018/19 hatifungani zenye thamani ya shilingi **bilioni 318.12** ziliuzwa na kununuliwa. Hili ni sawa na upungufu la asilimia 47 ikilinganishwa na hatifungani zenye thamani ya shilingi bilioni 595.16 zilizouzwa na kununuliwa katika kipindi kama hiki kwa Mwaka 2017/18.

### 7.5. IDADI YA WAWEKEZAJI

Hadi kufikia Februari 2019, DSE ilikuwa na jumla ya akaunti za uwekezaji **535,715**. Hii ni ongezeko **la asimilia 1.06 ikilinganishwa na idadi ya 530,182 katika Mwaka 2017/18**.

Kwa ujumla mwenendo wa soko kwa mwaka 2018/19 uliendelea kuwa wa kuridhisha kama ilivyokuwa katika mwaka 2017/18. Hali hii imechangiwa, pamoja na mambo mengine, mwenendo mzuri wa uchumi wa nchi na hali ya utulivu wa kisiasa ambavyo vimeendelea kuvutia wawekezaji kutoka na hivyo kuendelea kuwekeza katika makampuni yaliyoorodheshwa katika soko la DSE.

**a) Muundo na Usimamizi wa Uendeshaji**

Kufuatia kuanza kwa shughuli za Kampuni tanzu ya DSE, CSDR (Central Securities Depository and Registry Services) Mwezi Octoba 2017, kwa mwaka 2018 DSE ilifanya yafuatayo katika kuimarisha usimamizi wake na uendeshaji wa Soko:

i. Kuunda kwa Kamati za Bodi ya CSDR;
ii. Ilifanya tathmini ya uwezo na mapungufu kwa Watumishi waliopo katika kutekeleza Mpango Mkakati wa Miaka Mitano (2018 – 2022);
iii. Ilipitia tozo za soko ili kuona kama zinaendana na mahitaji;
iv. Iliendesha semina kwa Wajumbe wa Bodi ili kuwaongezea uwezo wa katika kutimiza majukumu yao.

**b) Hatifungani za Serikali za Mitaa (Municipal Bonds):**

i. Soko limeshiriki katika vikao kazi vilivyoandaliwa kwa pamoja na Wadau Wakuu wa mpango wa kuanzisha Hatifungani za Serikali za Mitaa (yaani UNCDF, TAMISEMI, Benki Kuu, CMSA na Wizara ya Wizara ya Fedha na Mipango);

ii. Ilitengeneza kanuni zitakazowezesha uorodheshwaji wa Hatifungani za Serikali za Mitaa;

iii. Ilishiriki katika kuandaa utaratibu wa kuwapata Washauri Mbalimbali wataowezesha uanzishwaji wa Hatifungani za Serikali za Mitaa

Lengo ni kupata Halmashauri moja ya Mfano itakayotoa Hatifungani za Serikali za Mitaa katika Mwaka 2019. Halmashauri ya Jiji la Mwanza inatarajiwa kuwa ya kwanza ya mfano.

**c) Kuongeza Ukwasi Sokoni:**

i. Kanuni za Uendeshaji ziliboreshwa kwa kuongeza uwazi zaidi kabla na baada ya mnada wa dhamana;

ii. Kanuni za uuzaji na ununuzi zinawataka Madalali kuweka oda mara tu waipatapo kwa Mwaji (Immediacy of order);

iii. DSE ilizishawishi Benki za Biashara kupata leseni za Uwakala katika soko la hatifungani (Bonds Market Dealership License) ambapo Benki mbili zilichukua leseni hizo.Benki za NMB na NBC zilichukua leseni hizo na kufikia idadi ya kuwa tano ambapo kabla zilizokuwepo ni CRDB, Stanbic Bank na Standard Chattered.

**d) Kuimarisha Miundo mbinu ya Mauzo ya Dhamana:**

i. DSE iliimarisha mfumo wa muundo wa hifadhi za "Data" yaani Data Centre Infrastructure"

ii. Ilitekeleza mradi wa kuweka mfumo wa kutoa huduma za "Registry Services"

iii. DSE ilijenga upya "Webserver Infrastructure and Hosting Diversification"

**e) Kuimalisha Muonekano wa Soko:**

DSE iliendelea na utaratibu wa kutoa taarifa za kila wiki kuhusu mwenendo wa soko ili kuleta hamasa na ushiriki kwa wawekekezaji wa ndani. Aidha, DSE iliendelea na juhudi ya kushirikiana na taasisi mbalimbali za kimataifa kama World Federation of Exchanges na United Nations Sustainable Stock Exchange

lengo likiwa ni kujenga uwezo na kuongeza wigo wa muonekano (profiling) kwa wawekezaji kimataifa.

**f) Uanachama wa Kudumu Katika Shirikisho la Masoko ya Hisa Duniani (World Federations of Exchanges)**

i. DSE ilianzisha mchakato wa kujiunga na Shirikisho la Masoko ya Hisa Duniani (World Federation of Exchanges- WFE) pamoja na kupata daraja (classification) kutoka moja ya taasisi za kimataifa zinazotoa "Classifications" hizo – ambapo Januari 2019 DSE imeweza kupata Uanachama wa Kudumu wa WFE na pia iko katika hatua za mbele kabisa kuwa "classified as Frontier Market Status";

ii. Kampuni Tanzu ya CSDR ilipata uanachama katika taasisi ya Kimataifa inayosimamia mambo ya hifadhi na uhamishaji dhamana ya Africa and Middle East Depository Association (AMEDA)

**g) Elimu kwa umma**:

i. Iliendelea na uendeshaji wa Shindano kuhusu uwekezaji kwa Wanafunzi waliopo vyuo vikuu – DSE Scholar Investment Challenge. Lengo la shindano hili ni kuleta uelewa na hamasa kuhusu uwekezaji kwa kada ya vijana wasomi ambao wanategemewa baadae kuwa watungaji wa Sera, waendeshaji wa shughuli za biashara (makampuni) au wajasiriamali nk.Katika kipindi cha kuanzia mwezi Juni mwaka 2018 mpaka sasa mpango huu umeweza kufikia wanafunzi 12000 wa vyuo vikuu vyote vya Tanzania.

ii. DSE iliendelea na kushirikiana na tasnia ya habari ikiwa ni nyenzo rahisi na madhubuti katika kufikisha elimu na hamasa ya uwekezaji kwa umma. DSE ilifanya hivyo kwa kutoa taarifa za kila wiki na pia kutoa machapisho na maandiko katika magazeti pamoja na kufanya vipindi vya radio na luninga.

Mpango huu unatekelewa kila Jumatatu katika vituo vya TBC Televisheni,Channel Ten,Clouds Televisheni wakati upande wa magazeti ni pamoja na Mwananchi,Daily News na The Guardian.

- DSE iliendesha mafunzo kwa wanachama wake kuhusu shughuli za uendeshaji soko.

## 7.6. MIPANGO NA MALENGO YA MWAKA 2019

| | MKAKATI | LENGO AU MALENGO |
|---|---|---|
| **1.** | Kukamilisha Marejeo ya Kanuni za Uendeshaji wa Soko | Kuwa na Kanuni ambazo zitaongeza tija na ufanisi wa uendeshaji wa shughuli za soko ikiwa ni pamoja na kukidhi mahitaji ya bidhaa na huduma mpya. |
| **2.** | Kuongeza ukwasi wasoko | Kufikia kiwango cha asilimia 5 katika uwiano wa mauzo ya hisa kwa ukubwa wa soko na pia asilimia 10 kwa mauzo ya hatifungani kwa thamani ya hatifungani zilizopo (outstanding bonds) |
| **3.** | Kushiriki kikamilifu katika uandaaji wa Sera zinazohusu au kugusa masuala ya masoko ya hisa. | Kuwa na sera sahihi na zenye kuleta tija kuhusu masuala ya uendeshaji wa masoko ya hisa |
| **4.** | Kujenga uwezo wa kampuni za kati kuweza kuvutia uwekezaji wa mitaji pamoja na mikopo kutoka kwa mabenki, hisa, hatifungani | Kuwa na kampuni nyingi ambazo zinavutia uwekezaji wa mitaji. |
| **5.** | Kuendelea kuimarisha muonekano wa soko la hisa kwa wawekezaji wa ndani na nje | Kuongeza ushiriki wa wawekezaji wa ndani na nje katika kuwe keza kupitia masoko ya hisa.. |
| **6.** | Kuendeleza juhudi za kupata Uanachama wa Kudumu katika Jumuiya ya Masoko ya Hisa Duniani (WFE) na Kupata "Classification ya Frontier Market Status | LengonikupataUanachama WFE 2019 na Frontier Market Status 2020 |

# 8.0. MIFUKO NA PROGRAMU ZA SERIKALI ZA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI




## 8.1. UTANGULIZI

Serikali imekuwa ikiwawezesha wananchi kujikwamua kiuchumi kwa kuwapatia mitaji kupitia mikopo yenye masharti nafuu, ruzuku ama Programu nyingine mbalimbali za Uwezeshaji. Uwezeshaji huu unatokana na utekelezaji wa Sera na Sheria ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ya mwaka 2004 pamoja na Sheria na Sera za sekta mbalimbali.

Serikali ilianzisha Mifuko na Programu za Uwezeshaji kutokana na changamoto mbalimbali zilizoonekana ikiwa ni pamoja na:-

i. Ufinyu wa vyanzo vya akiba kwa wananchi kutokana na kipato kidogo na kutokuwa na utamaduni wa kujiwekea akiba;

ii. Kuwepo kwa vikwazo vinavyosababisha benki kusita kutoa mikopo. Kwa mfano gharama kubwa za kuhudumia utoaji wa mikopo,ukosefu wa utambulisho rasmi, kutokuwa na taarifa muhimu za waombaji mikopo na ukosefu wa dhamana;
iii. kupanua wigo wa utoaji huduma za kifedha kwa makundi mbalimbali katika jamii yanayojishughulisha na shughuli za kiuchumi mijini na vijijini;
iv. Udhaifu unaowafanya wananchi wasikopesheke, kama vile ukosefu wa ujuzi wa kuandaa na kusimamia miradi inayokopesheka, ukosefu wa mtaji wa kuchangia uanzishaji wa miradi; na
v. Riba kubwa na tozo mbalimbali zinazotozwa na benki na taasisi za fedha kwenye mikopo.

Serikali ina jumla ya mifuko ya uwezeshaji 46 kati ya hiyo mfuko mmoja umefungwa, mfuko mmoja umeunganishwa na mfuko mwingine na mifuko minne iko katika hatua za kukusanya madeni.

Baraza la Uwezeshaji linafanya uratibu wa Mifuko na Programu kwa mujibu wa nguzo ya tatu (Upatikanaji wa Mitaji) ya Sera ya Taifa ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi 2004, aidha uratibu unaofanywa ni pamoja na :

i. Kutunza Daftari la Orodha ya Mifuko ya Uwezeshaji na kuhakikisha kuwa linafanya jitihada za kubaini mifuko mipya au ambayo haikuwa inafahamika hapo awali na kuiongeza katika Daftari;
ii. Kuweka uelewa kwa Umma juu ya uwepo wa Mifuko/Programu za Uwezeshaji na namna ya Umma itakavyonufaika na mifuko hiyo;
iii. Kuitisha vikao/mikutano na Taasisi za Mifuko/Programu;
iv. Kupokea taarifa za Mifuko, kuzipitia na kuandaa taarifa ya pamoja; na
v. Kufanya ufuatiliaji na tathmini ya huduma na matokeo ya Uwezeshaji.

Mifuko ya uwezeshaji wananchi kiuchumi imegawanyika katika makundi makuu manne ambayo ni Mifuko inayotoa mikopo moja kwa moja kwa walengwa, Mifuko inayotoa dhamana kwa kushirikiana na Taasisi za fedha, Mifuko inayotoa ruzuku na Programu za Uwezeshaji.

Walengwa wa mifuko na program za uwezeshaji wanaendana na madhumuni ya kuanzishwa kwa mifuko, walengwa hao kimakundi ni Wajasiriamali katika Vikundi au mtu mmoja mmoja (Vijana, Wanawake na Wenye Ulemavu), Wajasiriamali katika makampuni au Biashara za Ubia; na Asasi ndogondogo za Kifedha

## 8.2. MAKUNDI YA MIFUKO NA MATOKEO UTEKEZAJI WA SHUGHULI ZAKE

Utekelezaji wa shughuli za mifuko na program ni kama unavyoonekana chini:

## 8.3. MIFUKO INAYOTOA MIKOPO MOJA KWA MOJA KWA WALENGWA

Hili ni kundi linalohusisha mifuko inayotoa mikopo moja kwa moja kwa walengwa pasipo kuhusisha taasisi za fedha. Orodha ya mifuko katika kundi hili inaonekana katika jedwali lifuatalo:-

***Jedwali Na. 4: Mifuko inayotoa Mikopo Moja kwa Moja kwa Walengwa***

| **Mifuko inayotoa Mikopo Moja kwa Moja kwa Walengwa** | | | |
|---|---|---|---|
| i. | Mfuko wa Kutoa Mikopo kwa Wajasiriamali Wadogo (SELF Mcrofinance Fund) | viii. | Mfuko wa Maendeleo ya Vijana (Youth Development Fund –YDF); |
| ii. | Mfuko wa Mikopo ya Nyumba kwa Watumishi wa Serikali, | ix. | Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake (Women Development Fund –WDF); |
| iii. | Mfuko wa Kilimo Kwanza (Kilimo Kwanza Fund–KKCF); | x. | Mfuko wa Taifa wa Kuendeleza Wajasiriamali Wananchi (National Entrepreneurship Development Fund – NEDF); |
| iv. | Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu, | | |
| v. | Mfuko wa Mzunguko katika mikoa (SIDO RRF); | xi. | Mfuko wa Pembejeo wa Taifa (Agricultural Inputs Trust Fund –AGITF); |
| vi. | Mfuko wa Ufilisi wa Benki ya Nyumba (THB)- TIB Development; | xii. | Mfuko wa Kusaidia Kilimo cha Maua na Mbogamboga ; |
| vii. | Mfuko wa Japan wa Uagizaji bidhaa kutoka nje (Commodity Import Support) | xiii. | Mfuko wa Kiwanda cha Nyama |

### 8.3.1. Mfuko wa Maendeleo ya Vijana – (Youth Development Fund – YDF)

Mfuko ulianzishwa rasmi na Serikali mwaka 1993 chini ya Sheria ya Fedha (The Exchequer and Audit Ordinance, cap 439), namba 21 ya mwaka 1961 kifungu cha 17 ili kuwawezesha vijana kupata mitaji kwa njia ya mikopo yenye masharti.

Mfuko umefanikiwa kutoa mikopo ya Shilingi **5,434,641,000** zimetolewa kwa vikundi vya vijana 899 vyenye idadi ya vijana 5,404 katika Halmashauri 127 za Tanzania Bara.

### 8.3.2. Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake (Women Development Fund –WDF)

Mfuko ulianzishwa kwa Azimio la Bunge lililopitishwa Agosti, 1993 na kwa mujibu wa Kifungu Na.17 (1) cha Sheria ya "***Exchequer and Audit Ordinance (Cap.439)"*** ya mwaka 1961 kama ilivyorekebishwa na Sheria ya Fedha za Umma ya mwaka 2001 (Public Finance Act 2001) ili kuwainua kiuchumi wajasiriamali wanawake hususan masikini wenye umri wa miaka 18 na kuendelea na wasichana wenye umri chini ya miaka 18 wenye watoto.

Mfuko umefanikiwa kutoa mikopo yenye thamani ya shilingi 23,028,819,916 kwa vikundi 10,264 vyenye wanawake 811,692.

### 8.3.3. Mfuko wa Taifa wa Kuendeleza Wajasiriamali Wananchi (National Entrepreneurship Development Fund –NEDF)

Mfuko ulianzishwa mwaka 1994 kwa Azimio la Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili kutoa mikopo kwa wenye viwanda vidogo na wafanyabiashara wadogo Tanzania Bara, kwa lengo la kuondoa umaskini kwa kuanzisha na kuendeleza miradi yao katika sekta ya uzalishaji inayohusika na viwanda vidogo, kilimo na kusindika vyakula (matunda na mboga), ufugaji, uvuvi namadini, sekta ya biashara inayohusika na uuzaji wa vyakula na vinywaji, maduka ya bidhaa mchanganyiko na Sekta nyinginezo kama vile afya (maduka ya dawa baridi), huduma za uchapishaji, ujenzi, utalii na uchukuzi. Mfuko huu unaendeshwa na Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO) chini ya makubaliano maalumu na Serikali kupitia Wizara ya Viwanda

**Mafanikio ya mfuko**

i. Umetoa mikopo yenye thamani ya shs. Bilioni 71.87 kwa wananchi 90,862 ambapo thamani ya mikopo iliyotolewa kwa wanawake ni shs bn 33.292 sawa ana asilimia (46.3), wanaume ni shs bilioni 36.096 sawa na asilimia 50.2 na ubia ni shs. Bilioni. 2.84 sawa na asilimia 3.5;
ii. Jumla mikopo 47,029 yenye thamani ya Tshs 47,465,401,000 sawa na 66% ilitolewa kwa mikopo ya sekta ya uzalishaji inayojumuisha miradi ya Viwanda, Kilimo, Ufugaji, Uvuvi na Madini. Mikopo ya biashara 37,040 yenye thamani ya Sh. 18,752,729,000 sawa na 26.1% ilitolewa, ambapo kwa sekta nyinginezo kama afya n.k Mikopo 6,793 yenye thamani ya Sh. 5,651,802,000 sawa na 7.9% ilitolewa;
iii. Mfuko umekua kwa kiasi cha TSh 2.803 bilioni kutoka mtaji wa TSh 5.051 bilioni hadi TSh 7.854 bilioni kutokana na 50% ya riba ya mikopo inayoingizwa katika ukopeshaji. Mtaji wa Mfuko wa TSh 5.051 bilioni unajumuisha TSh 500 milioni zilizokelewa mwaka 1994 pamoja na nyongeza ya mtaji TSh 4.551 bilioni zilizopokelewa baadaye; na
iv. Umetengeneza Ajira zipatazo 184,542 kutokana na mikopo iliyotolewa;

### 8.3.4. Mfuko wa Pembejeo wa Taifa (Agricultural Inputs Trust Fund – AGITF)

Mfuko ulianzishwa mwaka 1994 kwa Sheria ya Bunge Na. 9 ya mwaka 1994 ili kutekeleza Sera ya Serikali kuhusu upatikanaji wa pembejeo za kilimo, mifugo na uvuvi kwa wakulima, wafugaji na wavuvi wadogo wadogo kwa wakati unaofaa na kwa bei nafuu.

Walengwa wa Mfuko wa Pembejeo ni Wakulima, Wafugaji na Wavuvi mmoja mmoja na vikundi (AMCOS, SACCOS nk.), Mawakala binafsi wanaosambaza pembejeo za kilimo, mifugo na uvuvi, Mashirika na Taasisi za Jamii, zinazojishughulisha na kilimo; na Benki za wananchi na Ushirika ambazo hutoa mikopo moja kwa moja kwa wakulima katika maeneo ambayo zipo kwa niaba ya Mfuko wa Pembejeo.

Mfuko umefanikiwa kutoa mikopo ya shilingi 82,097,446,770 ambayo imewasaidia wananchi kuongeza kipato na kupunguza umaskini. Mikopo hii imetolewa Tanzania Bara katika miradi 3589 (wanaume 2,871 (**80%)** na wanawake 718 (**20%)**. Mchanganuo wa miradi ni kama ifuatavyo:

***Jedwali Na. 5: Mchanganuo wa Mikopo iliyotolewa na aina ya mradi***

| Na | Aina ya mradi | Namba ya miradi | Thamani ya mradi |
|---|---|---|---|
| **1** | Mitambo ya mashambani | 1216 | 45,469,011,378 |
| **2** | Pembejeo za kilimo | 1780 | 31,354,183 |
| **3** | Matreketya madogo | 263 | 1,848,106,162 |
| **4** | Zana za kusindika na vifungashio | 9 | 243,772,000 |
| **5** | Zana unganishi (Farm Implements) | 1 | 59,000,000 |
| **6** | Miundombinu ya kilimo,mifugo na uvuvi | 42 | 2,019,839,751 |
| **7** | Ukarabati wa matrekta | 278 | 1,103,133,296 |
| | **Jumla kuu** | **3589** | **82,097,446,770** |

### 8.3.5. Mfuko wa Kutoa Mikopo kwa Wajasiriamali Wadogo (SELF Microfinance Fund)

Mfuko ulisajiliwa rasmi tarehe 04/09/2014 kwa Sheria ya Kampuni ya mwaka 2002 chini ya Udhamini wa Serikali '*Company Limited by Guarantee*' na kupata Hati ya Usajili namba 112091 kwa jina la *SELF Microfinance Fund (SELF MF)* ili kukuza na kuboresha upatikanaji wa huduma za kifedha kwa wananchi wenye kipato cha chini hususani waishio vijijini, na hivyo kuwapa fursa ya kushiriki katika shughuli za uzalishaji mali kwa lengo la kujiongezea kipato.

Walengwa wa Mfuko ni wajasiriamali wadogo kupitia Asasi ndogo na za Kati za kifedha. Asasi hizo ni Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo – (SACCOS), Benki za Wananchi (Community Banks); Mashirika yasiyo ya Kiserikali na Kampuni za fedha zinazotoa huduma za mikopo (Microfinance Companies).

**Mafanikio ya Mfuko**

i. Umetoa mikopo yenye thamani ya shlingi bilioni 128.7 katika mikoa 27 na wilaya 91 kwa jumla ya wajasiriamali 125,764 miongoni mwa wajasirmali hao wanawake ni 70,691 (56.2) na wanaume ni 55,073 (43.8);
ii. Umezifikia jumla ya asasi 490 kati ya hizo 281 zinatoka vijijini,79 zinatoka miji midogo na 130 zinatoka miji mikubwa;
iii. Umewajengea uwezo wajasiriamali 11,948, maafisa ushirika 518, viongozi watendaji wa asasi za kifedha 4,810; na
iv. Umetengeneza ajira kwa takribani watu wapatao 273,947 wakiwemo wajasiriamali waliojiajiri wenyewe na wale walioajiriwa katika biashara zilizofadhiliwa na mikopo ya Mfuko.

### 8.3.6. Mfuko wa Mikopo ya Nyumba kwa Watumishi wa Serikali

Serikali ilianzisha Mfuko wa Mikopo ya Nyumba kwa watumishi wake Kwa Waraka wa Utumishi wa Umma Na. 8 wa mwaka 1992 ili kuwawezesha watumishi wa ngazi zote wanaoishi mijini na vijijini kupata mkopo wa nyumba wenye masharti nafuu kwa ajili ya **kujenga, kukarabati au kununua nyumba**. Wanaostahili kukopa kutoka kwenye Mfuko huu ni watumishi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, raia wa Tanzania, walioajiriwa kwa masharti ya kudumu na kuthibitishwa kazini.

Mfuko umetoa jumla ya mikopo 1689 yenye thamani ya shilingi bilioni 9.16 kwa watumishi wa Serikali kati ya hao wanawake ni 661 na wanaume ni 1028;

### 8.3.7. Mfuko wa Kilimo Kwanza (Kilimo Kwanza Fund–KKCF)

Mfuko ulianzishwa mwaka 2009 chini ya Usimamizi wa Benki ya TIB ili kusaidia Serikali na wananchi hususani wanaoshughulika na masuala ya kilimo kufikia malengo na mikakati ya Serikali na dira ya maendeleo ya 2025 kwa lengo la kukuza uchumi wa nchi kutoka katika uzalisha mdogo na kuwa na uzalishaji mkubwa na wenye tija. Lengo ni kuwezesha Tanzania kuwa nchi ya viwanda kutokana na malighafi zinazotokana na kilimo na hivyo kusaidia mpango wa maendeleo ya sekta ya kilimo ***‘’Agricultural Sector Development Programme”*** (ASDP) ambao umekusudia kukuza kilimo cha biashara.

**Mafanikio ya mfuko**

i. Umekuwa kutoka shilingi bilioni 42 na kufikia shilingi bilioni 63.3 kutokana na marejesho yaliyotolewa kwa wakati;
ii. Umetoa mikopo ya matrekta 252, Power tillers 145, Mitambo ya umwagiliaji zaidi ya 15 (irrigation equipment) mashine za uvunaji zaidi ya 8 (combine harvesters), ujenzi wa maghala, magari ya kubeba mazao/nafaka; na
iii. Umekopesha miradi ipatayo 189 katika mikoa 23 wilaya 76 nchini kwenye miradi mbalimbali ya ufugaji, uvuvi, mazao ya biashara na chakula.

### 8.3.8. Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu

Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) ilianzishwa na Sheria ya HESLB (SURA 178) mwaka 2004 na kuanza rasmi utekelezaji wa majukumu yake mwezi Julai, 2005 Kuanzishwa kwa HESLB ni utekelezaji wa Sera ya Uchangiaji Gharama za Huduma za Kijamii iliyoanza kutekelezwa **mwaka 1992**.

**Mafanikio Kwa Kipindi Cha Kuanzia Julai-Desemba, 2018**

**i. Makusanyo ya mikopo**

a) Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) imekusanya jumla ya **TZS 94.01 bilioni** kutoka kwa wadaiwa wa mikopo ya elimu ya juu katika kipindi cha Julai – Desemba, 2018 na kuvuka lengo lake la kukusanya **TZS 71.4 bilioni** katika kipindi hicho. makusanyo hayo

yametoka kwa jumla ya wanufaika zaidi **198,659** ambao wamejiajiari au kuajiriwa katika sekta binafsi na umma.

b) Makusanyo haya ya **TZS 94.01 bilioni** ni sawa na ongezeko la **asilimia 8.7** ikilinganishwa na **TZS 85.88 bilioni** zilizokusanywa katika kipindi kama hicho mwaka uliopita yaani, Julai – Disemba, 2017

**ii. Wanufaika *waliobainika na kuanza kulipa kati ya Julai – Disemba 2018***
Wanufaika wapya zaidi ya **12,600** ambao walikua hawajaanza kurejesha mikopo yao na sasa wameanza na hivyo kufanya wateja wanaorejesha kufikia **198,656**

#### 8.3.9. Maelezo ya Mifuko mingine inayotoa Mikopo Moja kwa Moja

Mifuko mingine ya uwezeshaji katika kundi hili ni Kiwanda Cha Nyama –SAAFI, Mfuko wa Ufilisi wa Benki ya Nyumba (THB), Mfuko wa Kusaidia Kilimo cha Maua na Mbogamboga, Mfuko wa Japan wa Uagizaji Bidhaa Kutoka Nje (Commodity Importer Support) aidha mifuko hii kwa sasa inafanya ufuatiliaji wa madeni; Mfuko wa Rais wa Kujitegemea umefutwa na Serikali wakati Mfuko wa UTT Microfinance Fund umeunganishwa na SELF Microfinance Fund.

### 8.4. MIFUKO INAYOTOA DHAMANA

Iko jumla ya mifuko 10 inayojiendesha kwa kushirikiana na taasisi za fedha kwa njia ya kutoa dhamana. Orodha ya mifuko hiyo inaonekana katika jedwali lifuatalo:

***Jedwali Na. 6: Mifuko inayotoa Dhamana***

| MIFUKO INAYOTOA DHAMANA | | | |
|---|---|---|---|
| i. | Mfuko wa Kusaidia Sekta Binafsi ya Kilimo (Private Agricultural Sector Support Trust –PASS Trust); | vi. | Mfuko wa Dhamana za Mikopo kwa Wajasiriamli katika Sekta ya Kilimo (SIDO SME –CGS); |
| ii. | Mfuko wa Kudhamini Mikopo ya Mauzo Nje ya Nchi (Export Credit Guarantee Scheme –ECGS); | vii. | Mfuko wa Kupambana na Umasikini na Kuongeza Ajira (JK Fund); |
| iii. | Mfuko wa Uwezeshaji wa Mwananchi (Mwananchi Empowerment Fund –MEF); | viii. | Mfuko wa Nishati Jadiifu (TANZANIA Energy Development and Expansion- TEDAP); |
| iv. | Mfuko wa dhamana za mikopo kwa wakulima wadogowadogo (Smallholders' Credit Guarantee Scheme); | ix. | Mfuko wa Mikopo Midogo ya Nyumba (Housing Microfinance Fund); na |
| v. | Mfuko wa Kusaidia Makandarasi (Contractors Assistance Fund –CAF); | x. | Mfuko wa Dhamana za Mikopo kwa Wajasiriamali Wadogo na Wakati (SME-CGS). |

### 8.4.1. Mfuko wa Kusaidia Sekta Binafsi ya Kilimo (Private Agricultural Sector Support Trust –PASS Trust)

Ni chombo kilichoanzishwa Mwaka 2000 na kuanza utekelezaji kama mradi chini ya wizara ya Kilimo/Fedha ili kuchochea uwekezaji na kukuza kilimo cha biashara na sekta zinazohusika.

PASS Trusti inatoa huduma za maendeleo ya biashara kwa wateja kama Upembuzi yakinifu, Kuandaa Mipango ya Biashara, Kujenga utaalamu, Kuwaunganisha wakulima katika vikundi maalum kwa ajili ya kilimo cha mkataba, kusambaza pembejeo kwa mkopo, kufanya mazungumzo ya bei na kutoa ushauri, na Utafutaji na uunganishaji wa masoko

Walengwa wakuu wa Mfuko ni Watu binafsi wanao fanyabiashara za kilimo, ufugaji na uvuvi, Vikundi na Vyama vya Wakulima Wafugaji na Wavuvi vilivyosajiliwa; na Kampuni zinazo jishughulisha na miradi mbalimbali katika mnyororo wathamani wakilimo (Mazao, Mifugo na Uvuvi)

**Mafanikio ya Mfuko**

i. Umefanikiwa kudhamini miradi 20,355 yenye thamani ya shilingi bilioni 470.8 kwa walengwa 679,892 kati ya hao wanawake 286,714 na wanaume ni 393,178; na kutengeneza Ajira zipatazo 1,534,994;
ii. Mtaji umekuwa kutoka Shilingi za Kitanzania Bilioni 9.6 (2007) hadi kufikia Bilioni 81.4 kwa Desemba 2018;
iii. Unashirikiana na wadau mbalimbali kama vile WFP, SNV na AGRA kusaidia wakulima 7000 wa mazao ya mahindi na alizeti katika nyanda za juu kusini kwakuwapatia mafunzo na kuwaunganisha na taasisi za fedha kwa ajili ya kupata mikopo;
iv. Umeanzisha vituo viwili vya uatamizi (Incubator) kwakushirikiana na SUA (SUGECO) na TALIRI-Kongwa kupitia kituo chetu cha ubunifu wa biashara za kilimo (Agribusiness Innovation Centre – AIC);
v. Kupitia Kituo cha uatamizi PASS-AIC, Mfuko ulipokea maombi ya vijana 169 kutoka katika mikoa mbalimbali kujiungana vituo atamizi vya PASS kati ya hao vijana 102 waliweza kupatiwa mafunzo yakubadilisha fikra na mtazamo wao kuhusu kilimo biashara. Vijana wapatao 41 walichaguliwa kuingia kwenye mafunzo ya awali kwa vitendo kwenye vituo atamizi. Vijana wapatao 20 ndiyo waliofaulu kujiunga na vituo atamizi vya PASS wakiwemo Wasichana 9 na Wavulana 11; na
vi. Kwa kipindi cha kuanzia Januari 2018 hadi kufikia Desemba 2018, jumla ya mikopo yenye thamani ya shilingi za kitanzania Bilioni 191, 693,996,436 imedhaminiwa kupitia benki washirika wafuatao; CRDB, NMB, AMANA, MKOMBOZI, BOA, EQUITY, TADB, VISIONFUND, TPB BANK na ACCESS BANK.

### 8.4.2. Mfuko wa Kudhamini Mikopo ya Mauzo Nje ya Nchi (Export Credit Guarantee Scheme –ECGS) Na Mfuko wa Dhamana za Mikopo kwa Wajasiriamali Wadogo na Wakati (SME-CGS)

Mfuko wa ECGS unalenga wakopaji wenye miradi mikubwa yenye mahitaji ya mitaji ya kuanzia Shilingi milioni 501 na kuendelea. Kwa upande wa Mfuko wa SME-CGS, mfuko huu unalenga wajasiliamali wenye miradi midogo na ya kati yenye mahitaji ya mitaji ya kuanzia Shilingi milioni 5 hadi Shilingi milioni 500. Wakopaji wanaodhaminiwa ni wale wenye upungufu wa dhamana za kutosha kuweza kupata mkopo kwenye mabenki. Mifuko hii inasimamiwa na Benki Kuu ya Tanzania.

Mfumo wa uendeshwaji wa mifuko hii ni wa kutoa dhamana za mikopo kupitia taasisi za fedha zinazotoa mikopo kwenye sekta binafsi. Madhumini ya Mfuko wa ECGS ni kuhamasisha uzalishaji kwa ajili ya mauzo nje ya nchi ili kuchangia kukuza pato la Taifa. Halikadhalika, madhumuni ya Mfuko wa SME-CGS unalenga kukuza na kuendeleza miradi midogo na ya kati (SMEs) kwa kujenga mazingira ya kuwezesha wajasiriamali wenye miradi midogo na ya kati kupata mitaji kwa njia ya mikopo ili kuongeza mchango wao katika ukuzaji wa uchumi, kukuza ajira na kupunguza umaskini.

Utekelezaji wa Mifuko hii kisekta ni kama unavyoonekana hapa chini:

***Jedwali Na. 7: Utekelezaji wa mifuko kisekta***

| Na. | Sekta | Utekelezaji wa Mfuko wa ECGS | | | Utekelezaji wa Mfuko wa SME-CGS | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kiasi cha Mikopo | Kiasi cha Dhamana | % | Kiasi cha Mikopo | Kiasi cha Dhamana | % |
| **1.** | Kilimo | 1,654,907,413,754.01 | 1,260,003,702,734.99 | 93.3 | 4,800,075,230.00 | 2,316,491,491.00 | 45.0 |
| **2.** | Uzalishaji | 101,156,073,233.33 | 77,643,589,233.61 | 5.8 | 1,514,940,000.00 | 757,470,000.00 | 14.7 |
| **3.** | Ujenzi | | | | 1,485,000,000.00 | 725,000,000.00 | 14.1 |
| **4.** | Elimu | | | | 930,000,000.00 | 465,000,000.00 | 9.0 |
| **5.** | Utalii | | | | 874,160,000.00 | 420,830,000.00 | 8.2 |
| **6.** | Mawasilino | | | | 570,000,000.00 | 285,000,000.00 | 5.5 |
| **7.** | Huduma | | | | 130,800,000.00 | 65,400,000.00 | 1.3 |
| **8.** | Madini | 14,866,666,666.67 | 11,150,000,000.00 | 0.8 | 68,000,000.00 | 34,000,000.00 | 0.7 |
| **9.** | Afya | | | | 63,750,000.00 | 31,875,000.00 | 0.6 |
| **10.** | Uvuvi | 4,500,000,000.00 | 1,500,000,000.00 | 0.1 | 50,000,000.00 | 25,000,000.00 | 0.5 |
| **11.** | Usafirishaji | | | | 34,500,000.00 | 17,250,000.00 | 0.3 |
| **Jumla Kuu** | | **1,785,430,153,654.01** | **1,350,297,291,968.60** | **100** | **10,521,225,230.00** | **5,143,316,491.00** | **100** |

### 8.4.3. Mfuko wa Uwezeshaji wa Mwananchi (Mwananchi Empowerment Fund –MEF)

Kifungu 16 (1) cha Sheria ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Namba 16 ya mwaka 2004 kinaelekeza kuanzishwa kwa Mfuko wa Taifa wa Uwezeshaji wa Wananchi (MEF). Mfuko huu unaosimamiwa na Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC) unajiendesha katika mfumo wa kutoa dhamana za mikopo kwa walengwa kwa

kushirikiana na Taasisi mbalimbali za fedha, ambapo kwasasa unafanya kazi kwa kushirikiana na Benki ya TPB na UTT Microfinance.

**Mafanikio ya Mfuko**

i. Mfuko umefanikiwa kutoa dhamana za mikopo yenye thamani ya shilingi 13,409,583,413 kwa wajasiriamali 31,948 kati yao wanawake 20,832 na wanaume 11,116 na hali ya marejesho ya mikopo ni 93%

ii. Kwa mujibu wa utafiti (impact assessment) uliofanyika kwenye mikoa ya Lindi, Mtwara, Manyara, Rukwa na Singida unaonesha kwamba mpango huu ulikuwa na manufaa makubwa kwa wajasiriamali katika maeneo mbalimbali, mathalan;
   a) Wajasiriamali waliweza kupanua shughuli zao za kiuchumi;
   b) Mapato yao yaliongezeka;
   c) Baadhi ya wajasiriamali waliweza kujenga nyumba bora;
   d) Baadhi yao waliweza kulipa ada za shule kwa watoto na
   e) Wajasiriamali wengi katika mikoa ambako MEF inatekelezwa waliweza kupatiwa elimu ya ujasiriamali na kupewa mikopo yenye masharti nafuu.

### 8.4.4. Mfuko wa Dhamana za Mikopo kwa Wakulima Wadogowadogo (Smallholders' Credit Guarantee Scheme)

Mfuko huu unaosimamiwa na Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) unalenga kuhamasisha mabenki za kibiashara kuongeza mikopo yao kwa wakulima wadogo wadogo ambao wamesahaulika kwenye huduma rasmi za kibenki.

Mfuko umefanikiwa kuwezesha upatikanaji wa mikopo yenye thamani ya Shilingi 3,339,460,000 kupitia dhamana ya Shilingi 1,669,730,000 kwa wanufaika 871 wa kilimo cha mazao ya Miwa, Arizeti, na Mpunga katika Mikoa ya Morogoro, Iringa na Njombe;

### 8.4.5. Mfuko wa Kusaidia Makandarasi (Contractors Assistance Fund – CAF)

Bodi ya Usajili wa Makandarasi ilianzisha mfuko wa kusaidia Makandarasi (Contractors Assistance Fund – CAF) mwaka 2002 kwa lengo la kusaidia Makandarasi wazalendo kupata dhamana za zabuni na malipo ya awali. Bodi inashirikiana na Benki kutoa dhamana hizi. Walengwa wakuu wa mfuko huu ni Makandarasi wazalendo wa madaraja ya VII - IV kwa kazi za kawaida na daraja la III – II kwa kazi maalumu.

Mfuko umetoa dhamana ya shilingi 29,907,681,599 kwa Makampuni 1,612, Kati ya makampuni yaliyofaidika, makampuni 26 yanamilikiwa na kuongozwa na wanawake na 1,586 yanaongozwa na wanaume.

### 8.4.6. Mfuko wa Dhamana za Mikopo kwa Wajasiriamli katika Sekta ya Kilimo (SIDO SME –CGS)

Mfuko huu ulianzishwa kutokana na ruzuku ya Shilingi bilioni 1 iliyotolewa kutoka kwenye mfuko wa pamoja kati ya Serikali ya Tanzania na Japani (***Tanzania/Japan Food Aid Counterpart Fund***) chini ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika ili kuwawezesha Wajasiriamali Wadogo na wakati kupata mikopo kutoka Benki ya CRDB kwa udhamni wa mfuko kwa asilimia 50 kwa 50 ili waweze kuendeleza miradi yao ya Sekta ya uzalishaji wa mazao ya Kilimo (Agro Processing).

Walengwa wa mikopo ni Wajasiriamali Wadogo na wa Kati walioko kwenye sekta ya Uzalishaji wa Mazao ya Kilimo waliowahi kunufaika na huduma zinatolewa na SIDO kama vile Teknolojia, Mafunzo, Masoko na huduma za mikopo kupitia mfuko wa Kuendeleza Wajasiriamali (NEDF) na pia waliohudumiwa kupitia programu mbalimbali zinazotekelezwa na SIDO kama vile Kongano, MUVI, KAIZEN n.k.

**Mafanikio ya Mfuko**

i. Umefanikiwa kutoa Udhamini wa mikopo 33 yenye thamani ya Shilingi 1,048,000,000 kwenye mikoa ya Dar es salaam, Morogoro, Arusha, Kigoma, Mwanza, Singida, Mbeya, Iringa , Njombe, Tanga na Manyara

ii. Mikoa tisa (9) ya utekelezaji wa mfuko imeongezeka kutoka mikoa saba (7) ya awali na kuleta hamasa kwa Wajasiriamali walengwa.

iii. Mfuko umefanikiwa kutoa idadi ya ajira 132 kutokana na mikopo 33 yenye thamani ya Shilingi 1,048,000,000 ambapo wastani wa ajira ni 4 kwa kila kiwanda kidogo kilichofaidika na mkopo wa dhamana.

### 8.4.7. Mfuko wa Nishati Jadiifu (TANZANIA Energy Development and Expansion- TEDAP)

Mwaka 2010, Wakala wa Nishati Vijijini (REA) iliiteua TIB kusimamia kwa niaba yake mkopo wa Dola za Kimarekani milioni 23 kutoka Benki ya Dunia. Mnamo mwaka 2016 mkataba uliongezwa kwa miaka mingine mitatu (3) hadi 2019 ukiambatana na nyongeza ya mkopo kutoka Dola za Kimarekani milioni 23 hadi milioni 42 ambapo mkopo huo ni kwa ajili ya kuziwezesha benki za biashara kuweza kutoa mikopo kwa ajili ya uzalishaji wa nishati vijijini *(Refinancing*) na mikopo ya nishati asilia.

**Mafanikio ya Mfuko**

Tangu kuanzishwa kwa mfuko kumekuwa na mafanikio mengi ya kiuchumi na kijamii katika maeneo yenye miradi hii ya umeme kama ifuatavyo:

i. Kuongezeka kwa uzalishaji wa umeme (5.69 MW)

ii. Benki imefanikiwa kukusanya mikopo kiasi cha shilingi 8,043,538,720.20 kwa wakati.
iii. Kuongezeka kwa shughuli za uzalishaji kwa kutumia nishati inayopatikana katika maeneo ya miradi (ufugaji, usindikaji).
iv. Kuwezesha benki za biashara kushiriki katika kutoa mikopo kwa wananchi wanaozalisha umeme hususani vijijini.
v. Kuongezeka kwa ajira mfano uwepo wa kiwanda cha samaki Kamba kisiwa cha Mafia.
vi. Vilevile miradi hii (Ngombeni, Mwenga, Andoya na Darakuta) imetoa ajira kwa wananchi kwa ajili ya usimamizi wa mitambo, matengenezo nk)

### 8.4.8. Mfuko wa Mikopo Midogo ya Nyumba (Housing Microfinance Fund)

Serikali ilikasimu uendeshaji wa Mfuko huu kwa Benki Kuu kwa kupitia Mkataba wa Uwakala uliosainiwa mwaka 2010 ukiwa na madhumuni ya kuongeza ukwasi kwa taasisi za fedha zinazohudumia wananchi wa kipato cha chini ili ziweze kutoa mikopo ya ujenzi, ukarabati au ununuzi wa nyumba kwa gharama nafuu na masharti rahisi ya dhamana kwa lengo la kuwafikia watu wengi zaidi wa kipato cha chini ambao hawawezi kupata mikopo ya nyumba katika utaratibu wa kawaida kwenye benki na taasisi za fedha.

**Mafanikio ya Mfuko**

i. Mikopo yenye thamani ya Shilingi 17,870,000,000/= (sawa na dola za Marekani 8,089,950.79) imekwishatolewa kwa benki na taasisi za fedha kwa ajili ya kuwakopesha wananchi walengwa; na
ii. Jumla ya wananchi walengwa wanaokadiriwa kufikia 700 wamefaidika na mikopo hii.

### 8.4.9. Mifuko mingine inayotoa Dhamana

Mfuko mwingine uliokuwa unatoa dhamana kwa kushirikiana na taasisi kadhaa za kifedha ni wa mpango wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (Economic Empowerment Programme ama Mfuko wa JK) ulioanzishwa katika Mwaka wa fedha 2006/2007 kwa kutenga kiasi cha Shilingi bilioni 21.63.

Mfuko huu ulifanya kazi na Benki pamoja na taasisi za fedha 13 ambazo ni CRDB, NMB, Azania, Akiba, Tanzania Postal Bank, Kagera Farmers' Coop. Bank, Kilimanjaro Coop. Bank, Uchumi Commercial Bank, Mwanga Community Bank, Pride Tanzania, Presidential Trust Fund, SCCULT (1992) Ltd na Dunduliza Co. Ltd.

Mfuko wa Uwezeshaji Kiuchumi uliolenga wajasiriamali wadogo wadogo umesaidia vikundi mbalimbali kupata mikopo nafuu yenye thamani ya shilingi bilioni 50.35 zaidi kwa wananchi wapatao 77,431 kutoka Tanzania bara na Zanzibar.

## 8.5. MIFUKO INAYOTOA RUZUKU

Jumla ya mifiko inayotoa ruzuku ni 19, orodha yake inaonekana katika jedwali lifuatalo:

***Jedwali Na. 8: Mifuko inayotoa ruzuku***

| MIFUKO INAYOTOA RUZUKU | | | |
|---|---|---|---|
| i. | Mfuko wa Nishati Vijijini (Rural Energy Fund –REF); | ix. | Mfuko wa Misitu Tanzania (Tanzania Forest Fund –TaFF); |
| ii. | Bodi ya Mfuko wa Barabara; | x. | Mfuko wa Fidia ya Ardhi Tanzania; |
| iii. | SAGCOT-CTF; | xi. | Mfuko wa Maendeleo ya Maji Vijijini; |
| iv. | Mfuko wa Madini kwa wachimbaji wadogo nchini; | xii. | Mfuko wa kudhibiti Ukimwi; |
| | | xiii. | Mfuko wa Ubunifu Vijijini (RIF); |
| v. | Mfuko wa Mawasiliano kwa Umma (UCSAF); | xiv. | Mfuko wa Hifadhi za Milima ya Tao la Mashariki; |
| vi. | Mfuko wa Elimu Tanzania (Tanzania Education Fund –TEF); | xv. | Mfuko wa Hifadhi za Mazingira; |
| vii. | Mfuko wa Kuongeza Ujuzi na Stadi za Kazi (Skills Development Fund - SDF) | xvi. | Tozo ya Maendeleo ya Utalii (Tourism Development Levy - TDL); |
| viii. | Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (Tanzania Social Action Fund –TASAF; | xvii. | Mfuko wa Taifa wa Mambo ya Kale (The National Fund For Antiquities) |
| | | xviii. | Mfuko wa Sanaa na Utamaduni ; na |
| | | xix. | Mfuko wa Hifadhi za Wanyamapori. |

### 8.5.1. Mfuko wa Nishati Vijijini (Rural Energy Fund – REF)

Mfuko wa Nishati Vijijini unasimamiwa na Wakala wa Nishati Vijijini kwa niaba ya Bodi. Madhumuni ya Mfuko ni kuhakikisha wananchi wa vijijini wanapata huduma za nishati bora inayochangia ukuaji wa uchumi.

Walengwa wa Mfuko ni Makazi ya wananchi waishio Vijijini, Maeneo ya Biashara vijijini, Taasisi za Umma kama vile vituo vya Polisi, Shule za Msingi na Sekondari zilizopo vijijini, Pampu na Visima vya Maji vijijini, Shughuli za Uzalishaji Mali, Masamba ya Umwagiliaji.

**Mafanikio ya Mfuko**

i. Mfuko umefanikiwa kutoa mafunzo kwa watanzania 2,157 katika mikoa 20, kati ya washiriki hao wanawake ni 605 na wanaume 1,552;
ii. Mradi Kabambe wa Umeme Vijijini Awamu ya Pili (Rural Electrification under Turnkey Phase II) ulioanza Mwezi Oktoba 2013 n kutekelezwa kwenye Wilaya 133 katika Mikoa 25 ya Tanzania Bara. Miundombinu iliyojengwa chini ya mradi huu umefanikisha yafuatayo:
    a) Kukamilika kwa ujenzi wa vituo vya kuongeza nguvu ya umeme (Step-up Transformers) katika miji ya Kasulu, Kibondo, Kigoma, Mbinga, Ngara na Tunduru vilivyojengwa kuwezesha usambazaji wa umeme vijijini katika wilaya za Buhigwe, Kakonko, Uvinza, Nyasa, Ngara na Tunduru;

b) Kufikisha umeme katika Makao Makuu ya Wilaya za Buhigwe, Busega, Chemba, Itilima, Kakonko, Kalambo, Kyerwa, Mkalama, Mlele, Momba, Nanyumbu, Nyasa na Uvinza;
c) Ujenzi wa miundombinu ya usafirishaji umeme kwa msongo wa kati (kilovolti 11 na 33), Ufungaji wa transformers kwa ajili ya usambazaji umeme, Ujenzi wa miundombinu ya usambazaji (kilovolti 0.4)na umekamilika kwa asilimia 98.5; na
d) Idadi ya wateja waliokwisha unganishwa na huduma ya umeme ni 158,061 sawa na asilimia 63.2 ya matarajio ya kuunga wateja wa awali 255,000.

### 8.5.2. Bodi ya Mfuko wa Barabara (RFB)

Bunge la Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania lilipitisha Sheria ya Tozo za Barabara ya mwaka 19981 (Roads Tolls Act, 1998) iliyoanzisha Mfuko na Bodi yake. Sheria hiyo ilipitiwa na kuboreshwa na sasa inaitwa Sheria ya Barabara na Tozo za Mafuta (Roads and Fuels Tolls Act, CAP 220).

Bodi imepewa mamlaka ya kusimamia Mfuko wa Barabara kwa Kuhakikisha ukusanyaji madhubuti wa fedha za mfuko,Ugawaji thabiti wa fedha kwa watekelezaji, na Kufuatilia matumizi ya fedha hizo ili kuhakikisha kwamba thamani ya pesa imefikiwa katika utekelezaji.

**Mafanikio ya mfuko**

i. Kuongezeka kwa makusanyo toka TZS 40bn mwaka 2000 hadi kufikia TZS 870bn mwaka 2018;
ii. Kuongezeka kwa uwajibikaji katika kusimamia matunzo ya mtandao wa Barabara;
iii. Kuongezeka kwa ubora wa mtandao wa Barabara;
iv. Kuimarika zaidi kwa matumizi ya tehama kwenye mifumo ya kazi na usimamizi wa kifedha; na
v. Kuongezeka kwa ufanisi zaidi katika usimamiaji wa matunzo ya Barabara kupitia Wakala wa Barabara (Implementing agencies i.e. TANROADS,TARURA, MoWTC na TAMISEMI).

### 8.5.3. SAGCOT-CTF

Mfuko Kichocheo wa SAGCOT yaani SAGCOT Catalytic Trust Fund (SCTF) ulianzishwa kwa ushirikiano wa Serikali na Sekta binafsi (wakulima, wabia wa maendeleo, na majukwaa mbalimbali ya Kilimo). Lengo kuu la mfuko ni kuchochea uwekezaji wa sekta binafsi katika kilimo kama soko kuu la mazao ya wakulima wadogo na kuwekeza katika kutatua changamoto za kilimo biashara. Mfuko wa SCTF umeanza kufanya kazi rasmi Mwezi Mei, mwaka 2011 baada ya kusajiliwa chini ya Sheria ya Mifuko (Trustee Incorporation Act, Cap 318 R.E 2002).

**Mafanikio ya Mfuko**

i. Katika mwaka wa Fedha 2018/19 mfuko umefadhili ujenzi wa ghala kuhifadhia mpunga katika kijiji cha Mwakanga, Kata ya Ubaruku, Wilaya ya Mbalari. Ujenzi wa ghala hili umelenga kuwawezesha wakulima waliopo kwenye Skimu ya Umwagiliaji ya Mwendamtitu kuhifadhi mpunga wao baada ya mavuno na hivyo kuweza kuendana na mahitaji ya soko kwa ujazo pamoja na kupata bei nzuri. Ghala lina uwezo wa kuhifadhi Tani 7,500 za mpunga na limeanza kutumiwa na wakulima ambao tayari wameunganishwa na soko linalotolewa na kampuni ya kusindika mpunga ya Mtenda Kyela Rice Supply Limited; na

ii. Kwa kushirikiana na Chuo kikuu cha Nelson Mandela African Institute of Science and Technology (NM-AIST) chini ya mradi wa CREATES, mfuko umetoa ufadhili kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa kukusanya takwimu za wakulima pamoja na shughuli zao za kilimo (farmers electronic monitoring system) ili kutoa majawabu ya msingi kwa wakulima pamoja na wadau wengine kuhusu maeneo yanayohitaji utafiti na kutoa takwimu sahihi. Mfuko utatumia uwezo wa mifumo ya kompyuta (super computer) pamoja na ujuzi wa wataalamu waliopo Chuo kikuu cha Nelson Mandela ili kutoa uchambuzi wa takwimu za kilimo zilizokusanywa chini ya mfumo huu kwa kuoanisha uhusiano wa vipengele ndani ya takwimu hizo (attributed relationships among data). Wakulima walioingizwa katika mfumo huu kwa sasa ni wakulima 1,500 waliounganishwa na soko la Mtenda Kyela Rice Supply Ltd, Wafugaji 400 waliounganishwa na soko la ASAS Dairies Ltd na Wafugaji 700 waliounganishwa na soko la Njombe Milk Factory Ltd. Kupitia utambuzi wa wakulima hawa kama wanufaika wa moja kwa moja wa mfuko, itakuwa rahisi kuweka mpango mzuri wa urejeshwaji wa fedha za mfuko kupitia masoko ya wanufaika.

### 8.5.4. Mfuko wa Mawasiliano kwa Umma (UCSAF)

Mfuko ulianzishwa kwa Sheria namba 11 ya mwaka 2006 sura ya 422 ya Sheria za Tanzania ili kuleta msukumo na ushiriki wa watoa huduma za mawasiliano katika kukuza na kusukuma maendeleo ya kijamii na uchumi kwa kutumia mawasiliano hususani katika maeneo ya vijijini na maeneo ambayo hayana mvuto wa kibiashara.

**Mafanikio ya Mfuko**

i. Umefikisha mawasiliano kwa kata 518, zenye vijiji 1,939 ambapo wananchi zaidi ya milioni 3.1 wamenufaika, jumla ya dola za Kimarekani 41.5 milioni zimetumika kukamilisha miradi hiyo;
ii. Umetoa mafunzo mbalimbali ya TEHAMA kwa walimu 309 wa shule za msingi na sekondari kutoka katika kila mkoa;
iii. Kwa kushirikiana na kampuni ya Star Media, Mfuko umewezesha wananchi 2,500 kuunganishwa na matangazo ya televisheni ya kidigitali;
iv. Umetoa ruzuku ya ving'amuzi 2,500 katika mikoa ya Songwe, Geita, Simiyu, Njombe na Katavi; na

v. Kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, Mfuko umefikisha vifaa vya TEHAMA na kuunganisha mtandao wa intaneti katika shule 300;

### 8.5.5. Mfuko wa Elimu Tanzania (Tanzania Education Fund –TEF) na Mfuko wa Kuongeza Ujuzi na Stadi za Kazi (SDF)

Mfuko wa Elimu Tanzania umeanzishwa kwa Sheria Namba 8 ya mwaka 2001, ili kusaidia juhudi za Serikali katika kuwezesha maendeleo ya Elimu katika ngazi zote kwa Tanzania Bara na Elimu ya Juu kwa Zanzibar.

**Mafanikio ya Mfuko**

i. Ukarabati wa Shule Kongwe 17 za sekondari, ujenzi wa nyumba za walimu 570 katika shule 99 zilizo kwenye maeneo magumu kufikika, ujenzi wa mabweni 40 kwenye shule za sekondari, Mikopo kwa ajili ya ujenzi wa Hosteli za Watoto wa kike kwenye vyuo vikuu 3;
ii. Kupitia Mfuko wa Kukuza ujuzi (SDF), TEA imetiliana saini na taasisi 15 kati ya 16 na kuidhinisha utoaji fedha kwenye taasisi hizo ambazo zimefuzu mchakato wa kupata fedha kwa ajili ya kutoa mafunzo ya kuongeza ujuzi kwenye sekta ya kilimo. Hadi kufikia Desemba, 2018 jumla ya shilingi **876,327,462.43** zilikwishatolewa kwa taasisi 11 kati ya 16 zilizofuzu mchakato;
iii. Miradi inayotekelezwa na Mfuko wa Elimu ambayo ilianza utekelezaji katika kipindi husika imetengeneza ajira mpya **215**; na
iv. Jumla ya wanafunzi na walimu **1,946** walinufaika moja kwa moja na miradi iliyopitishwa katika mwaka wa fedha 2018/19.

### 8.5.6. Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (Tanzania Social Action Fund – TASAF)

Mfuko ulianzishwa na Serikali Mwaka 2000 kama moja ya mikakati ya kupambana na umaskini kwa kutumia dhana ya ushirikishwaji jamii. Utekelezaji wa Mfuko umekuwa ukifanyika kwa awamu tangu ulipoanzishwa ambapo kwa sasa Awamu inayotekelezwa ni ya tatu (Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini).

Madhumuni ya Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini ni kuendeleza mafanikio yaliyopatikana katika Awamu mbili zilizotangulia ili kuwezesha kaya maskini kuongeza kipato na fursa pamoja na kuinua kiwango cha matumizi yao. Walengwa wa Mpango ni kaya maskini zinazokadiriwa kuwa karibu milioni 6.8, yaani wastani wa asilimia 15 ya Watanzania wote.

**Mafanikio ya Mpango**

i. Mfuko umehawilisha ruzuku ya Shilingi 43,000,818,840 katika mzunguko wake wa 30 kwa jumla ya kaya za walengwa 1,003,858, zenye idadi ya watu wapatao 5,222,309 kwa Halmashauri 161. Ruzuku hiyo imesaidia kaya kukidhi mahitaji ya msingi, kama kununua chakula cha familia, nguo, kupata huduma za afya na mahitaji ya shule kwa watoto wanaosoma shule za msingi na Sekondari n.k.;

ii. Jumla ya shilingi 232,000,000 zilitumika kuunda vikundi 11,769 vyenye wanachama 151,821 (Wanawake 112,962 Wanaume 38,859) katika Halmashauri 57 za Tanzania Bara na Zanzibar (Unguja na Pemba);

iii. Kupitia mpango wa Kutoa Ajira za Muda kwa Kaya Maskini uliogharimu shilingi 6,957,184,900 ulifanikisha kutengeneza Ajira kwa walengwa 258,096 (Wanaume 123,886 na Wanawake 134,210) ambao walipata fursa ya kufanya kazi za mikono kwenye miradi 1,124 katika Halmashauri 19 miradi ya Jamii;

iv. Halmashauri ndani ya Mkoa wa Arusha na Njombe zimeendelea kutekeleza Miradi 23 katika Sekta Umwagiliaji, Maji na Ujenzi iliyogharimu kiasi cha shilingi 401,301,780.06. Miradi hii iko chini ya Mpango wa OPEC III inayofadhiliwa na Mfuko wa Maendeleo wa nchi zinazozalisha Mafuta kwa wingi Duniani (OPEC);

v. Kuongezeka uandikishaji katika Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF) katika kaya za Walengwa kwa asilimia 21.7 ukilinganisha na kaya zisizo za Walengwa; na

vi. Walengwa kupata ujuzi kupitia ushiriki wao katika utekelezaji wa miradi ya ajira ya muda, kwa mfano ujenzi wa barabara, makinga maji, hifadhi ya vyanzo vya maji n.k.

### 8.5.7. Mfuko wa Misitu Tanzania (Tanzania Forest Fund –TaFF)

Mfuko wa Misitu Tanzania umeanzishwa kisheria (chini ya Sheria ya Misitu Sura ya 323 ya mwaka 2002) kwa lengo la kukabiliana na changamoto ya uhaba wa fedha za kuwezesha usimamizi wa rasilimali ya misitu na kuimarisha utekelezaji wa Sera na Sheria ya Misitu. Walengwa wa Mfuko ni Watu binafsi; Vikundi vya Jamii; asasi zisizo za kiserikali; Jumuiya/Taasisi za Kidini; Asasi/Taasisi za Mafunzo; Taasisi za Utafiti; Wizara, Idara, na Wakala za Serikali; Mamlaka za Serikali za Mitaa na wadau wengine wanaojihusisha na uhifadhi, usimamizi na uendelezaji wa rasilimali misitu katika Mikoa ya Tanzania Bara.

**Mafanikio ya mfuko**

i. Umetoa ruzuku ya jumla ya **shilingi 6,215,743,987** kwa miradi 514 ambapo miradi 244 ni ya kuongeza kipato cha jamii zinazoishi pembezoni mwa misitu, miradi 235 ni ya uhifadhi, uendelezaji na usimamizi wa misitu na miradi 35 ni ya utafiti katika misitu. Miradi hiyo ni ya upandaji miti, ufugaji nyuki na samaki, nishati mbadala, viwanda vidogo vya kuchakata asali, kutenga misitu ya jamii na ya utafiti;
ii. Mfuko umefadhili wanafunzi **68** Katika fani za misitu na nyuki katika ngazi ya Astashahada na Stashahada;

iii. Mfuko umewezesha ujenzi wa **majengo 5** ya ofisi na barabara zenye urefu wa kilometa **100** katika mashamba ya miti ya ya kupandwa ya Biharamulo (Wilaya ya Chato), Iyondo Nsimwa (Wilaya ya Ileje), Mpepo (Wilaya ya Mbinga), Buhigwe (Wilaya ya Buhigwe) & Magotwe na Pagale (Wilaya ya Morogoro), yaliyopo chini ya Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS);
iv. Mfuko uliwezesha vifaa (gari nane na Pikipiki 14) vya doria kwa TFS makao makuu na kanda zake zote saba pamoja na kuiwezesha TFS kufanya doria katika maeneo mbalilimbali ili kukabiliana na uvunaji haramu wa mazao ya misitu pamoja na wasafirishaji wa mazao ya misitu; na
v. Mfuko umeinunulia TAFORI magari moja katika vitendea kazi kwa Taasisi ya hiyo ya Utafiti wa Misitu Tanzania.

#### 8.5.8. Mfuko wa Fidia ya Ardhi Tanzania

Mfuko wa Fidia ya Ardhi (*The Land Compensation Fund*) ni chombo cha kisheria kinachosimamia masuala ya malipo ya fidia anayolipwa mmiliki ambaye ardhi na maendelezo yake yametwaliwa.

**Mafanikio ya Mfuko**

Tangu kufunguliwa kwa ofisi za Mfuko wa Fidia, watumishi wameweza kutekeleza majukumu yao ya kazi chini ya Mfuko kama ifuatavyo:-

i. **Kuwasiliana na Wadau (Taasisi mbalimbali) hamsini na tisa (59) -** Taasisi hizi zinatarajiwa kuwasilisha taarifa katika Mfuko wa Fidia kuhusu maeneo wanayokusudia kuyatwaa kwa ajili ya shughuli mbalimbali za maendeleo;

ii. **Kuandaa rasimu ya Mwongozo wa Ulipaji wa Fidia -** Mwongozo huu mara baada ya kuidhinishwa unatarajiwa kusambazwa katika Halmashauri zote nchini; na

iii. **Kuandaa muundo wa uendeshaji wa Mfuko wa fidia (*OperationalManual*) -** Muundo huu unaainisha kada mbalimbali zitakazokuwepo ndani ya Mfuko wa Fidia pamoja na majukumu yake.

#### 8.5.9. Mfuko wa Hifadhi za Wanyamapori (TWPF)

Mfuko wa Kuhifadhi Wanyamapori Tanzania ulianzishwa kwa Sheria ya Bunge Na.21 ya mwaka 1978 baada ya marekebisho ya kifungu cha 69 cha Sheria ya Kuhifadhi Wanyamapori Na.12 ya mwaka 1974 ili kupambana na ujangili na biashara haramu za wanyamapori.

**Mafanikio ya Mfuko**

i. Kikosi Kazi cha Taifa cha Kupambana na ujangili kinachofadhiliwa na mfuko kimefanikiwa kukamata watuhumiwa wa ujangili 958, silaha 328, risasii 3,608 na meno ya tembo mazima 191 na vipande 333;

ii. Kupungua kwa ujangili wa tembo kwa zaidi ya 60% .Matukio ya kukamatwa kwa meno ya tembo Kimataifa (*International Seizure*) imeshuka kutoka matukio**107** (2013), **46** (2015), **1** (2018) ;
iii. TZS 2,265,800,000 zimelipwa kama kifuta machozi/Jasho kwa wananchi walioathirika na wanyamapori wakali na waharibifu (2014/15 – 2017/18);
iv. Ushiriki wa wananchi katika uhifadhi wa wanyamapori kwa kutenga maeneo yao ya vijiji kwa ajili ya uhifadhi umeongezeka. Jumla ya Jumuiya 38 za kuhifadhi wanyamapori zimeazishwa na kati ya hizo 22 zimeshatangazwa katika Gazeti la Serikali; na
v. Tsh 2,074,978,915,000 zimetumika kuchangia miradi ya huduma za jamii (Elimu, Afya, Maji, umeme) kwenye vijiji vilivyo karibu na Mapori ya Akiba.

#### 8.5.10. Mfuko wa Hifadhi za Milima ya Tao la Mashariki

Ni Mfuko wa Udhamini (Trust Fund) ulioanzishwa mwezi Juni 2001 nchini Tanzania chini ya Sheria ya Ujumuisho wa Wadhamini (Trustees' Incorporation Act) kama ilivyorejelewa mwaka 2002 (Cap. 318 R. E. 2002 ) Madhumuni ya mfuko ni kushughulikia haja ya kuwa na mkakati endelevu wa vyanzo vya fedha vya uhakika na vya kudumu kwa ajili ya kuhifadhi bioanuwai ya misitu iliyomo katika Milima ya Tao la Mashariki nchini Tanzania, kupunguza umaskini wa jamii zinazoishi kandokando ya milima hii muhimu pamoja na kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabia nchi.

Tangu kuanzishwa kwake EAMCEF imefadhili miradi ya upandaji miti zaidi ya milioni 14 katika hekta zaidi ya elfu kumi na saba (Ha.17,000) kwenye maeneo mbalimbali ya Milima ya Tao la Mashariki. Miradi mingine ni pamoja na ufugaji wa mbuzi wa maziwa zaidi ya 450, Ng'ombe wa maziwa zaidi ya 70, kuku zaidi ya 10,000, nguruwe zaidi ya 500, ufugaji nyuki zaidi ya mizinga ya kisasa 1,000, majiko banifu zaidi ya 10,000, uwekaji na uimarishaji wa mipaka ya misitu ya hifadhi zaidi ya kilometa 1,500 nk katika vijiji 244.

#### 8.5.11. Mfuko wa Taifa wa Mambo ya Kale (The National Fund For Antiquities)

Mfuko wa Taifa wa Mambo ya Kale (The National Fund for Antiquities) ulianzishwa kwa sheria ya Mambo ya Kale Na.22 ya mwaka 1979, kifungu kidogo cha 19B. Kwa mujibu wa sheria hii, malengo ya mfuko ni kuwezesha shughuli za utafiti, uhifadhi na uendelezaji wa malikale.

Katika kipindi cha Julai hadi Septemba 2018, Mfuko wa Taifa wa Mambo ya Kale umetekeleza kazi zifuatazo:-

i. Kuboresha mandhari ya kituo cha Kimondo cha Mbozi. Maboresho yanayofanyika ni kuweka mabomba ya kutolea maji; kujenga ukuta mfupi eneo la choo; na kujenga ukuta kwenye kingo ili kuzuia mmomonyoko wa

udongo.Aidha, Mfuko umegharamia ukarabati wa Kituo cha Taarifa na Kumbukumbu katika Kituo cha Michoro ya Miambani, Kolo Kondoa;

ii. Kugharamia vituo 16 vya Mambo ya Kale kupata huduma mbalimbali kama vile; maji, umeme, usafi, simu, samani za ofisi na vitendea kazi; na

iii. Uchambuzi wa Mikusanyo ya utafiti wa Mambo ya Kale iliyopo katika Kijiji cha Makumbusho, Dar es Salaam.

#### 8.5.12. Tozo ya Maendeleo ya Utalii (Tourism Development Levy - TDL)

Tozo ya Maendeleo ya Utalii (TDL) imeanzishwa kwa Sheria ya Utalii Na.29 ya mwaka 2008, kifungu kidogo cha 59 (2). Kanuni za TDL zilianza kutumika kwa Tangazo la Gazeti la Serikali Na.352 la tarehe 01 Oktoba, 2013.

**Mafanikio ya mfuko**

i. Kuwezesha kazi ya mapitio ya Sera ya Taifa ya Utalii na kutafsiriwa katika lugha ya Kiswahili, hatua inayoendelea ni kuandaa Mkakati wa utekelezaji wa Sera hiyo;

ii. Kuwezesha kubaini vivutio vipya vya utalii na maeneo yenye fursa za uwekezaji kwa ajili ya shughuli za utalii nchini;

iii. Kuwezesha wataalamu kufanya utafiti wa watalii walioondoka nchini na taarifa mbalimbali zikiwemo za mapato yatokanayo na biashara za utalii;

iv. Kuwezesha utoaji mafunzo ya ukarimu na utalii kwa wanafunzi;

v. Kuwezesha ukarabati na matengenezo ya Chuo cha Taifa cha Utalii;

vi. Kuwezesha kufanya mapitio ya Mpango Mkakati wa Chuo, Mkataba wa Huduma kwa Mteja na kuandaa daftari la vihatarishi;

vii. Kuwawezesha wanafunzi kwenda katika ziara za mafunzo katika Hoteli na vivutio vya utalii; na

viii. Kuwezesha ufuatiliaji wa wanafunzi wanaofanya mafunzo kwa vitendo kwenye Hoteli na Kampuni za Utalii Tanzania Bara na Zanzibar.

#### 8.5.13. Mifuko Mingine Inayotoa Ruzuku

Mifuko mingine inayotoa ruzuku ni Mfuko wa Ubunifu Vijijini, Mfuko wa kudhibiti UKIMWI, Mfuko wa Utamaduni Tanzania (Tanzania Culture Trust Fund), Mfuko wa Wachimbaji wadogo wa Madini na Mfuko wa Kuwasidia walemavu.

### 8.6. PROGRAMU ZA UWEZESHAJI

Programu za uwezeshaji kiuchumi zilianzishwa kwa ajili ya kuweka mazingira wezeshi ya kuwaandaa wananchi ili waweze kushiriki kikamilifu katika shughuli mbalimbali za kiuchumi, aidha Baraza linaratibu Programu nne ambapo orodha yake inaonekana katika jedwali lifuatalo:

***Jedwali Na. 9: Programu za Uwezeshaji Kiuchumi***

| PROGRAMU ZA UWEZESHAJI KIUCHUMI | | | |
|---|---|---|---|
| i. | Mfuko wa Kuendeleza Sekta Binafsi za Fedha Tanzania (Financial Sector Depening Trust- FSDT); | iii. | Mpango wa Kurasimisha Rasilimali za Wanyonge Tanzania (MKURABITA); na |
| ii. | Programu ya miundombinu ya masoko na Huduma za kifedha Vijijini (MIVARF); na | iv. | UTT AMIS. |

### 8.6.1. Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za wanyonge Tanzania (MKURABITA)

MKURABITA ilianzishwa na Serikali ya Jamhuri ya Tanzania mwezi Novemba, 2004 kwa Tamko la Rais wa Serikali ya Awamu ya Tatu, Mh. Benjamin William Mkapa Mpanho huu ni sehemu ya jitihada kubwa za Serikali ya Tanzania katika kuhakikisha kuwepo kwa mfumo wa usawa na manufaa ya kiuchumi na kijamii kwa wananchi walio wengi. Aidha, ni sehemu ya utekelezaji wa sera za uwezeshaji wananchi kiuchumi.

**Mafanikio ya Mpango**

**a) Mafanikio kwa wananchi**

(i) Wamiliki **526** wenye Hatimiliki za kimila wametumia hati kama dhamana na kupata mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni **4.99.** Aidha, vyama vitano (5) vya wakulima vimedhamini wakulima kupata mikopo ya thamani ya shilingi milioni **625.9**;

(ii) Wamiliki **93** waliorasimisha viwanja vyao mjini wametumia hati miliki kupata mikopo ya thamani ya shilingi bilioni **3**; na

(iii) Wafanyabiashara 2,300 wamepata mikopo ya thamani ya shilingi bilioni **1.1** kwa ajili ya kuongeza mitaji wa biashara;

**b) Mafanikio kwa Taifa**

(i) Wananchi kupata uelewa na kukubali kuchangia gharama za urasimishaji ambapo jumla ya **Shilingi 151,694,364** zimechangwa na wananchi na kutumika kugharamia urasimishaji katika maeneo mengine;

(ii) Baadhi ya Halmashauri za Wilaya zilizojengewa uwezo kuanza kutekeleza zenyewe urasimishaji katika maeneo yao na kufanya urasimishaji kuwa endelevu. Halmashauri za wilaya 24 zimetekeleza urasimishaji ambapo jumla ya mashamba 18,394 yamepimwa katika vijiji 224 na kutoa hati za Hakimiliki za Kimila 13,034.

### 8.6.2. Programu ya Miundo Mbinu ya Masoko na Huduma za Kifedha Vijijini (MIVARF)

Programu hii ambayo ilianzishwa kwa tangazo la Serikali (GN) na kuzinduliwa rasmi tarehe 27 Oktoba 2011 ikilenga kuchangia katika kufanikisha malengo mkakati ya

kukuza uchumi na kupunguza umaskini Tanzania Bara na Tanzania Visiwani yaani MKUKUTA na MKUZA katika sekta ya kilimo. Utekelezaji wa Programu hii kitaifa unasimamiwa na Kamati ya Uendeshaji (Programme Steering Committee – PSC) na Ofisi ya Uratibu wa Programu.

Walengwa wa Programu ni Wakulima wadogo wadogo wakiwemo wafugaji, wavuvi na wafanya kazi za mikono (artisans), Wajasiriamali wadogo wadogo vijijini pamoja na wafanyabiashara vijijini, Asasi ndogo ndogo za kifedha zinazotoa huduma vijijini na Vyama vya Msingi vya Ushirika/asasi za vijijini zinazojishughulisha na usindikaji wa mazao na masoko ya mazao vijijini.

**Mafanikio ya Programu**

**a) Miundombinu ya Masoko**

i. Ukarabati wa barabara zenye urefu wa Km 1078.6 umekamilika ambapo kwa Zanzibar (Unguja 68 na Pemba 80km).

ii. Ujenzi wa maghala 28 (tani 1000 kila moja) kati ya 29 na ukarabati wa Maghala yote 6 yaliyopangwa

iii. Ujenzi wa masoko 15 kati ya 16 yaliyopangwa umekamilika na moja lililobaki lilikuwa katika hatua za mwisho za kukamilika,

**b) Kuongeza Thamani Mazao**

Shughuli za msingi zilizofanywa katika kipengele hiki ni pamoja na:

i. Mafunzo ya kuwajengea uwezo wazalishaji yanaendelea katika kipengele cha PEML. Aidha, zaidi ya walengwa 26,694 (75% wanawake) wamejengewa uwezo katika uongezaji thamani mazao;

ii. Vituo kumi na tatu (13) vya kutoa mafunzo ya utunzaji mazo baada ya mavuno (Post Harvest Training Centers – PHTCs) vimeshakarabatiwa; na

iii. Utoaji wa ruzuku za mashine/mitambo ya usindikaji mazao ili kuongeza thamani: - Jumla ya vikundi 36 vimefanikiwa kupata ruzuku za asilimia 75% za kununua mitambo/mashine za kuongeza thamani ya mazao.

**c) Kuwajengea uwezo wazalishaji na kuwaunganisha na masoko**

Jumla ya Halmshauri 62 za Tanzania bara na wilaya 10 za Zanzibar zinashiriki utekelezaji wa kipengele hiki. Aidha mpaka kufikia Machi 2018 jumla ya vikundi 2,408 vyenye wanachama 83,988 (45% wanawake) vya wazalishaji wadogo, wasindikaji na vikundi vya masoko vimewezeshwa.

**d) Huduma za kifedha vijijini**

Programu imeweza kuzifikishia huduma za kifedha wananchi zaidi ya milioni mbili waishio vijijini. Jumla ya wananchi 4,048,913 (57% wanawake) wamefikiwa na huduma za kifedha kupitia asasi mbalimbali za kifedha zilizo rasmi na zisizo rasmi zinazofanya kazi na Programu. Asasi hizi zimeweza kukusanya akiba zenye thamani ya shilingi bilioni 16 na kutoa mikopo yenye thamani ya shilingi trilioni 6.6. Aidha,

Programu kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB) imeanzisha mifuko miwili kwa ajili ya dhamana kwa wakulima wadogo wadogo (Smallholder Covered Guarantee Scheme) wenye dola za kimarekani milioni kumi (US$ 10M) na ubunifu (Innovation Fund) wenye dola za kimarekani milioni moja (US$1M).

### 8.6.3. UTT AMIS

Historia ya UTT ilianza mwaka 1997 pale Serikali, kupitia Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilipopitisha Sheria ya Ubinafsishaji ya Mwaka 1997 (Privatisation Act (No. 7) of 1997). Chini ya sheria hii, Dhamana ya Ubinafsishaji (Privatisation Trust (PT)) iliundwa rasmi tarehe 15 Juni 1998. Malengo ya Programu ni Kuanzisha na kusimamia Mifuko ya uwekezaji wa Pamoja (CIS); Kutoa huduma za ushauri wa masuala ya uwekezaji; Kutoa huduma za usimamizi wa mifuko ya Pensheni, na Taasisi za Fedha; na Kutoa huduma za usimamizi wa mitaji binafsi.

**Mafanikio ya Programu**

i. Imefanikiwa kukusanya amana/fedha kutoka kwa wateja/wananchi jumla Tshs 282.00 Bilioni hadi tarehe 31 Disemba 2018 akuwafikia wananchi 139,478 nchini Tanzania
ii. Kwa mwaka ulioishia Juni 2018, taasisi ya UTT AMIS imekuwa na utendaji mzuri na umeiwezesha kulipa gawio la shilingi milioni 500 Serikalini.
iii. Mfuko wa Umoja tangu uanzishwe Mwaka 2005 hadi Mwezi Disemba 2018, ukubwa wa Mfuko umenakiri ongezeko la TZS 110.81 Bilioni na kufikia TZS 218.81 Bilioni na thamani ya kipande kwa muda wote tangu Mfuko uanzishwe imeongezeka kwa zaidi ya asilimia 400 kutoka TZS 100.00 Mwaka 2005 hadi TZS 570.17

iv. Wananchi wawekezaji walilipwa shilingi bilioni 2 kama faida ya uwezekaji kupitia mfuko wa Wekeza sambamba na hilo thamani ya kipande cha mfuko wa Wekeza maisha kwa kipindi chote tangu Mwaka 2007 hadi Disemba 2018 iliongezeka hadi TZS 377.69 ikilinganishwa na TZS 100.00 ya mwaka 2007.

v. Mfuko wa watoto umefunga Mwezi Disemba 2018 na ukubwa wa TZS 3.15 Bilioni ikilinganishwa na TZS 0.72 Bilioni tangu kuanzishwa kwake mwaka 2008. Aidha, kwa kipindi hichohicho thamani ya kipande imeongezeka kwa TZS 232.00 hadi kufikia TZS 332.00.

vi. Imefanikiwa kuchangia mapato ya serikali zaidi ya shilingi bilioni 21 tangu mwaka 2006 hadi Desemba, 2018

### 8.6.4. Mfuko Wa Kuendeleza Sekta Ya Fedha Tanzania (Financial Sector Deepening Trust (FSDT))

FSDT ilianzishwa mwaka 2004 na kuanza kazi rasmi mwaka 2005. FSDT imesajiliwa chini ya Sheria ya Muunganisho wa Wadhamini Sura 318. Madhumuni ya Programi ni pamoja na

i. Kuona mazingira ya sera, sheria na taratibu za uendeshaji wa masoko ya fedha na huduma zake unaimarika ili kuharakisha upatikanaji na utumiaji wa huduma za kifedha nchini;
ii. Kuona miundo mbinu ya usambazaji wa huduma za kifedha inakua, inaimarika na kuwa karibu na watu au biashara ili zitumike kuleta manufaa mapana;
iii. Kupanua upatikanaji na kuboresha bidhaa na huduma za kifedha mahususi kwa wajasiliamali na biashara zao; na
iv. Kupanua upatikanaji na kuboresha bidhaa na huduma zinazowalenga watu wa kipato cha chini na kaya maskini hasa waishio vijijini.

**Mafanikio ya FSDT**

i. FSDT imeshirikiana vizuri na serikali pamoja na wadau wengine katika mchakato wa kuandaa na kutunga sheria ya mifumo ya malipo nchini pamoja na kanuni zake (NPS Act, Licensing rules and regulations) na kutengeneza Mpango wa Elimu ya Fedha kwa wananchi (Financial Education Framework);
ii. Imesaidia kuhamasisha matumizi ya kitambulisho cha Taifa na kupunguza vikwazo vya upatikanaji wa huduma za kifedha;
iii. FSDT imetoa mawazo na fedha katika utengenezaji wa Sera mpya ya Huduma Ndogo za Kifedha (National Microfinance Policy 2017) iliyozinduliwa mwezi Octoba 2017;
iv. Ushirikiano baina ya wadau huu umewezesha kupatikana kwa Mkakati wa Pili wa Huduma Jumuishi za kifedha nchini (yaani National Financial Inclusion Framework 2018-2022).

## 9.0. VIKUNDI VYA KIFEDHA VYA KIJAMII



### 9.1. UTANGULIZI

Mfumo wa vikundi vya kuweka akiba na kukopa (vikundi vya kifedha vya kijamii) ulianzishwa kwa mara ya kwanza mwaka 1994 na Shirika la Care Internatinal nchini Niger. Mfumo huo kwa Kihausa unaitwa *Mata Masu Dubara* (kwa Kiswahili Wanawake katika Harakati za Maendeleo). Shirika la Care Internatinal lilianzisha Mfumo huo nchini Tanzania katika miaka ya 2000 na kuendelea kusambazwa nchini kupitia mashirika mbalimbali ya kimataifa na ya Kitanzania. Hapa nchini vikundi hivyo vinaitwa kwa majina mbalimbali kama vile VICOBA, VSLA, ROSCAs, VITOVU, SILC, ASCAs, Benki Imani, Benki Jamii, JOSACA, COCOBA, n.k. Sababu za kuanzishwa kwa vikundi hivyo ni kutokana na wananchi walio wengi, hasa wa kipato cha chini kupata shughuli mbadala za kiuchumi, kuweka akiba na kuwakutanisha ili kutumia mkusanyiko wao kuinua uchumi wao. Sababu nyingine ni kutumia mfumo huo kukusanya mapato yao na kuweka akiba baada ya kuonekana kwamba hawana sifa za kukopeshwa na benki za biashara. Hivyo, mfumo huo unawapa wananchi chanzo mbadala cha mitaji kwa ajili ya kuanzisha na kuendeleza shughuli za kiuchumi.

Hivi ni vikundi vya watu kati ya 15 hadi 30 ambavyo huundwa na wanajamii wa eneo husika (kitongoji au kijiji) kwa lengo la kujikwamua kiuchumi. Vikundi hivi vinaendesha shughuli za kifedha kwa wanavikundi kujiwekea akiba na kukopeshana kwa ajili ya kuendesha miradi ya kiuchumi na kutatua matatizo ya kijamii kama afya na elimu. Pia vikundi hivi vimekuwa chachu ya kuleta hamasa ya kimaendeleo katika jamii husika. Baadhi ya sifa za vikundi hivyo ni:

a) Huanzishwa na wanajamii kwa hiari baada ya kuhamasishwa na wataalam kutoka mashirika mbalimbali.

b) Hupewa mafunzo ya msingi ya uendeshaji wa vikundi hususan mafunzo ya usimamizi wa vikundi, mafunzo ya ujasiriamali, biashara na usimamizi wa fedha.

c) Huanzisha mfuko wa pamoja kwa kila mwanachama kuwekeza kwa mtindo wa kununua hisa kwa kiwango kinachokubalika na wanakikundi wote.

d) Hukubaliana namna ya kuendesha vikundi kwa kuwa na sheria ndogo/katiba ya kikundi

e) Huendeshwa kwa demokrasia na kwa uwazi

Hadi sasa vikundi hivyo vinaendelea kushamiri kwa kasi nchini kwa kuwezeshwa na taasisi mbalimbali. Kwa mujibu wa matokeo ya utafiti wa kitaifa wa mwaka 2017 unaolenga kutoa uelewa mpana kuhusu hali ya huduma za kifedha nchini (FinScope Tanzania 2017) upatikanaji wa huduma za

kifedha kupitia vikundi vya kifedha vya kijamii uliongezeka kutoka asilimia 12 ya watazania wenye umri wa miaka 16 na zaidi (mwaka 2013) hadi asilimia 16 (mwaka 2017). Hali hii inamaanisha kuwa hadi mwaka 2017 watu zaidi ya 4,450,000 walikuwa wanapata mitaji kwa ajili ya kuendesha shughuli zao za kiuchumi kupitia vikundi vya kifedha vya kijamii ikilinganishwa na watu 2,900,000 mwaka 2013.



Hata hivyo, pamoja na matokeo mazuri ya kuongeza huduma za kifedha kwa wananchi kupitia mifumo hiyo kumekuwepo na changamoto kadhaa ikiwemo baadhi ya taasisi kuviibia vikundi fedha zao kwa njia ya hila, kuwatoza ada kubwa kwa huduma wanazopewa, taasisi kufanya kazi kwenye Mikoa na Halmashauri kinyemela bila kupata kibali kutoka kwa mamlaka husika wala kutoa taarifa za kazi wanazofanya katika maeneo hayo. Kutokana na hali hiyo kumekuwa hakuna takwimu sahihi za taasisi zinazofanya kazi ya uhamasishaji, uanzishaji na uendelezaji wa vikundi vya kifedha vya kijamii wala takwimu sahihi za vikundi vyenyewe.

### 9.2. UHAKIKI WA TAASISI NA VIKUNDI

Ili kukabiliana na changamoto ya ukosefu wa taarifa za taasisi zinazowezesha uanzishwaji wa vikundi vya kifedha vya kijamii, Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais-TAMISEMI, Shirikisho la VICOBA Tanzania (VICOBA FETA), *Tanzania Informal Microfinance Association of Practitioners (TIMAP)*, *Inter-Religious VICOBA (IR-VICOBA),* Viongozi wa Mikoa na Halmashauri za Mamlaka za Serikali za Mitaa walifanya uhakiki (inventory) wa taasisi zinazowezesha uanzishwaji wa vikundi vya kifedha vya kijamii (Community Financial Groups (CFGs) Promoters) nchini. Lengo la zoezi hilo lilikuwa ni kuthibitisha uwepo wa taasisi hizo, mahali zinapofanya kazi, kujua vikundi vyao kwa majina, idadi ya vikundi, idadi ya wanavikundi, majina na mawasiliano ya viongozi wa taasisi na viongozi wa vikundi pamoja na mchango wao katika kuongeza huduma jumuishi za kifedha nchini. Pia kuweka utaratibu wa kudhibiti utendaji wa taasisi hizo ambazo baadhi yake wamekuwa wakifanya vitendo vinavyoleta athari katika jamii (utapeli wa fedha za wananchi), kufanya kazi katika Mikoa na Halmashauri bila kupata kibali kutoka kwa mamlaka husika na kutotoa taarifa za kazi zao katika maeneo husika.

Zoezi hili lilianza kwa Baraza kuomba takwimu za taasisi zinazofanya kazi ya kuanzisha na kuendeleza vikundi vya kifedha kutoka kwenye Halmashauri za Majiji, Manispaa, Miji na Wilaya. Majina ya taasisi 721 yalipokelewa kutoka kwenye Halmashauri 158 kati ya 185.

Baada ya kupokea takwimu hizo timu za wataalam kutoka Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, Ofisi ya Rais-TAMISEMI, VICOBA-FETA, TIMAP na IR VICOBA

zilienda kufanya mikutano ya Kikanda/Kimkoa kuhakiki uwepo wa taasisi hizo pamoja na vikundi. Mikutano hiyo ilifanyika katika mwezi Novemba na Desemba 2018. Kanda na mikoa husika ni kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali namba 10** hapa chini.

***Jedwali Na. 10: Kanda na mikoa iliyohusika katika uhakiki wa taasisi zinazowezesha uanzishaji wa vikundi vya kifedha vya kijamii***

| Na | Kanda | Mikoa |
|---|---|---|
| 1 | Kaskazini Magharibi | Kagera, Geita, Mwanza |
| 2 | Kanda ya Kaskazini | Arusha, Kilimanjaro, Tanga na Manyara |
| 3 | Kanda ya Kati | Morogoro, Singida, Iringa, Dodoma |
| 4 | Kanda ya Magharibi | Rukwa, Katavi, Kigoma, Tabora |
| 5 | Kanda ya Mashariki | Dar, Pwani, Lindi, Mtwara |
| 6 | Kanda ya Ziwa | Mara, Simiyu, Shinyanga |
| 7 | Kanda ya Nyanda za juu Kusini | Ruvuma, Mbeya, Songwe, Njombe |

Mikutano ilifanyika katika makao makuu ya Mikoa na kuongozwa na Makatibu Tawala wa Mikoa. Washiriki wa mikutano hiyo ni pamoja na viongozi wa taasisi (promoters) na waratibu wa uwezeshaji wa mikoa na Halmashauri. Katika mikutano hiyo viongozi au wawakilishi wa taasisi zinazowezesha uanzishwaji wa vikundi vya kifedha vya kijamii waliwasilisha taarifa kuhusu vikundi vyao zikionesha jina la kikundi, mahali kilipo, jina na namba za simu za viongozi wa kikundi, idadi ya wanakikundi (wanawake na wanaume), kiasi cha mtaji wa kikundi, idadi na thamani ya mikopo iliyotolewa kwa wanavikundi.

### 9.3. MATOKEO YA UHAKIKI

Matokeo ya uhakiki wa taasisi hizo yanaonesha kuwa kati ya taasisi 721 ni taasisi 272 (37.73%) tu zilizoweza kuhudhuria kwenye mikutano hiyo na kuweza kuwasilisha taarifa za vikundi vyake. Kwa ujumla taasisi hizo kwa pamoja zina jumla ya vikundi 17,326 vyenye jumla ya wanavikundi 442,756 ambapo kati yao wanawake ni 233,946 na wanaume ni 131,031. Jumla ya kiasi cha mtaji wa vikundi hivyo kilikuwa shilingi 88,156,066,474 na jumla ya mikopo iliyokuwa imetolewa ni 198,667 yenye thamani ya shilingi 88,858,965,939. Hali ya taasisi na vikundi hivyo kwa mikoa imeoneshwa kwa undani kwenye **Jedwali namba 11** hapa chini


***Jedwali Na. 11: Hali ya taasisi na vikundi kimikoa***

| Na | Mkoa | Taasisi | vikundi | Idadi ya wanavikundi | | | Mtaji | Mikopo | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | ke | me | jumla | | Idadi | thamani |
| 1 | Arusha | 7 | 535 | 8,847 | 3,331 | 12,178 | 6,134,958,513 | 2,281 | 11,569,544,233 |
| 2 | Dar es Salaam | 31 | 864 | 3,145 | 2,385 | 5,530 | 1,306,091,960 | 844 | 2,820,594,088 |
| 3 | Dodoma | 9 | 550 | 7,388 | 3,955 | 12,076 | 4,066,830,953 | - | 2,969,274,100 |
| 4 | Geita | 9 | 928 | 13,429 | 6,745 | 20,907 | 4,230,415,588 | 14,112 | 5,803,870,140 |
| 5 | Iringa | 16 | 1,097 | 17,067 | 6,097 | 26,167 | 3,701,919,822 | 8,510 | 2,726,496,939 |
| 6 | Kagera | 29 | 1,834 | 36,212 | 46,661 | 82,873 | 8,932,327,790 | 16,069 | 6,714,837,554 |
| 7 | Katavi | 2 | 9 | - | - | 339 | 103,302,070 | 2,073 | 278,524,878 |
| 8 | Kigoma | 1 | 38 | - | - | - | - | - | 117,653,000 |
| 9 | Kilimanjaro | 17 | 925 | 17,252 | 7,859 | 25,420 | 8,364,022,198 | 12,204 | 7,576,781,200 |
| 10 | Lindi | 1 | 62 | 747 | 234 | 981 | 61,636,340 | - | - |
| 11 | Manyara | 9 | 292 | 7,778 | 2,161 | 9,939 | 6,050,910,352 | 49,379 | 8,138,201,216 |
| 12 | Mara | 6 | 75 | 1512 | 709 | 2235 | 411,136,070 | | 411136070 |
| 13 | Mbeya | 18 | 2,028 | 26,806 | 3,147 | 56,743 | 18,343,185,366 | 44,216 | 17,099,280,250 |
| 14 | Morogoro | 24 | 1,371 | 21,330 | 8,213 | 31,738 | 7,850,458,980 | 11,506 | 4,610,284,642 |
| 15 | Mtwara | 1 | 9 | 232 | 214 | 446 | 56,961,000 | | 39,139,000 |
| 16 | Mwanza | 16 | 1,553 | 17,182 | 19,005 | 42,802 | 703,122,747 | 10,217 | 3,380,173,366 |
| 17 | Njombe | 6 | 357 | 5372 | 1846 | 7003 | 917,222,245 | 1,855 | 638,526,800 |
| 18 | Pwani | 6 | 112 | 1599 | 575 | 2237 | 778,479,450 | - | 854,622,500 |
| 19 | Rukwa | 13 | 241 | 888 | 348 | 4434 | 381,106,450 | 2,508 | 223,796,300 |
| 20 | Ruvuma | 8 | 1018 | 17424 | 4791 | 22215 | 1,254,489,871 | 5,271 | 1,027,358,444 |
| 21 | Shinyanga | 6 | 1229 | 1861 | 860 | 28905 | 1,089,484,000 | - | 1,341,549,600 |
| 22 | Simiyu | 3 | 559 | 7542 | 3828 | 8591 | 930,190,650 | - | 748,949,050 |


| Na | Mkoa | Taasisi | vikundi | Idadi ya wanavikundi | | | Mtaji | Mikopo | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | **ke** | **me** | **jumla** | | **Idadi** | **thamani** |
| **23** | Singida | 15 | 585 | 9791 | 3046 | 12747 | 3,275,046,874 | 7,409 | 1,626,866,270 |
| **24** | Songwe | 7 | 597 | 3193 | 1972 | 15625 | 5,665,288,820 | 7,520 | 5,009,167,588 |
| **25** | Tabora | 5 | 279 | 2587 | 1666 | 4504 | 457,425,472 | 1,447 | 387,945,800 |
| **26** | Tanga | 7 | 179 | 4762 | 1383 | 6121 | 3,090,052,893 | 1,246 | 2,744,392,911 |
| | **JUMLA KUU** | **272** | **17,326** | **233,946** | **131,031** | **442,756** | **88,156,066,474** | **198,667** | **88,858,965,939** |

**Taarifa hizi pia zinaelezewa kwenye mchoro namba Na.6 Hapa chini**


***Mchoro Na. 6: Idadi ya Taasisi kwa Mkoa***




**Mchoro Na. 7: Idadi ya Vikundi kwa Mkoa**





**Mchoro Na. 8: Jumla ya wanavikundi kwa mkoa**




***Mchoro Na. 9: Jumla wanavikundi kijinsia***





***Mchoro Na. 10: Uwiano wa wanavikundi kijinsia***




***Mchoro Na. 11: Mitaji ya vikundi kwa mkoa (bilioni)***



***Mchoro Na. 12: Thamani ya Mikopo iliyotolewa (bilioni)***




## 9.4. HATUA ZA MABORESHO

Kama matokeo ya uhakiki yanavyoonesha kati ya taasisi 721 ambazo zinahusika na uanzishwaji wa vikundi vya kifedha vya kijamii zilizowasilishwa kwa Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kutoka kwenye Halmashauri ni taasisi 272 tu zilizoweza kuwasilisha taarifa zao kwenye mikutano ya uhakiki iliyofanyika mikoani. Kiasi hiki ni kidogo ikilinganishwa na idadi ya majina ya taasisi zilizowasilishwa kwa Baraza. Ili kupata uhakika zaidi taarifa hii ilitumwa kwa Makatibu Tawala wa Mikoa na Wakurugenzi wa Halmashauri ili waipitie na kuona kama taasisi zote zinazojihusisha na vikundi vya kifedha vya kijamii katika maeneo yao zimejumuishwa. Baada ya kufanya ulinganifu wa taarifa hii na hali halisi kwenye mikoa na Halmashauri Makatibu Tawala wa Mikoa watatuma taarifa kwa Baraza ili kuweza kuboresha takwimu hizi.

## 9.5. SERA YA TAIFA YA HUDUMA NDOGO ZA FEDHA YA MWAKA 2017

Sera ya Taifa ya Huduma Ndogo za Kifedha ya mwaka 2017 inavitambua vikundi vya kifedha vya kijamii kama njia mojawapo muhimu katika kuongeza huduma jumuishi za kifedha, hasa kwa wananchi wenye vipato vidogo mijini na vijijini. Aidha, Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha ya mwaka 2018 imeipa Benki Kuu ya Tanzania mamlaka ya kusimamia watoa huduma wote katika sekta ndogo ya fedha vikiwemo vikundi vya kifedha vya kijamii. Hata hivyo, Benki kuu ina uhuru wa kuteua taasisi ambazo zitasimamia baadhi ya makundi kwa niaba yake. Katika Sheria hiyo watoa huduma ndogo za kifedha wamegawanyika katika makundi (tiers) manne kama ifuatavyo:

i. Tasisi za fedha zinazopokea amana kama vile benki za biashara. Taasisi hizi zitasimamiwa na Benki Kuu ya Tanzania kama inavyotakiwa na Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006;
ii. Taasisi zisizopokea amana kama vile mtu mmoja mmoja au Kampuni za kukopesha. Pia usimamizi wa kundi hili utafanywa na Benki Kuu ya Tanzania;
iii. Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo (Savings and Credit Cooperative Societies-SACCOS). Kundi hili litasimamamiwa na Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania kwa niaba ya Benki Kuu ya Tanzania; na
iv. Vikundi vya Kifedha vya Kijamii. Kundi linaweza kusimamiwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa niaba ya Benki Kuu ya Tanzania.

Kwa mujibu wa Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha ya mwaka 2018, Benki Kuu ya Tanzania itashirikiana na Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kuhamasisha uanzishaji na uendelezaji wa vikundi vya kifedha vya kijamii (kundi la nne). Shughuli zitakazofanyika ili kufikia lengo hilo ni pamoja na:

i. Kutoa elimu ya fedha kwa watoa huduma katika kundi hilo;
ii. Kufuatilia na kutoa msaada unaohitajika kwa lengo la kusaidia watoa huduma kutoa huduma bora;
iii. Kulinda haki na stahiki za watoa huduma na wapokeaji wa huduma hizo katika kundi hilo;
iv. Kusaidia kuboresha uwezo wa watoa huduma katika kundi hili kupitia Programu mbalimmbali za Serikali; na
v. Kuchukua hatua au kufanya shughuli yoyote kwa lengo la kukuza na kuwawezesha watoa huduma kutoa huduma bora kwa kundi hili

Benki Kuu ya Tanzania iko katika hatua za kuandaa kanuni za utekelezaji wa Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha ya mwaka 2018. Mojawapo ya kanuni hizo ni za kusimamia vikundi vya kifedha vya kijamii. Taarifa ya uhakiki (inventory) wa taasisi zinazowezesha uanzishwaji wa vikundi vya kifedha vya kijamii nchini itaweza kusaidia Benki Kuu ya Tanzania na Mamlaka nyingine kupata picha ya hali ilivyo kwenye vikundi vya kifedha vya kijamii na kuweza kuandaa kanuni nzuri za kusimamia sekta hii ndogo ya fedha. Aidha, taarifa hii itaweza pia kusaidia Ofisi ya Rais-TAMISEMI, Mikoa na Halmashauri pamoja na Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kuhamasisha uanzishwaji na uendelezaji wa vikundi vya kifedha vya kijamii, kuweza kufahamu hali halisi ya taasisi zinazosaidia kuanzisha vikundi hivyo na kuweka utaratibu mzuri wa kufanya nazo kazi.

# 10.0. USHIRIKI WA WATANZANIA KATIKA UWEKEZAJI NA MIRADI YA KIMKAKATI

## 10.1. UTANGULIZI

Tanzania kama nchi zingine zilizobarikiwa na mali asili imekuwa ikiweka mazingira yanayowezesha watanzania kushiriki kikamilifu katika uchumi wa nchi. Kuanzia mwaka 2015 hadi 2018 Sera na Sheria katika sekta ya uziduaji zimefanyiwa marekebisho na Kanuni zilitengenezwa ili kuhakikisha watanzania wanapata fursa za ajira, kutoa huduma, kuuza bidhaa, kujenga uwezo na uhaulishaji wa teknolojia katika mnyororo mzima wa thamani katika sekta hiyo. Aidha, miradi mbalimbali inayotekelezwa katika sekta mbalimbali ikiwemo sekta za ujenzi na uchukuzi suala la ushiriki wa wananchi na kampuni za kitanzania limekuwa likizingatiwa.

Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi katika kutekeleza jukumu lake la kuratibu na kufuatilia uwezeshaji wa wananchi kiuchumi kupitia ushirikishwaji wa wananchi katika uwekezaji na miradi ya kimkakati ilitengeza Mwongozo wa Kitaifa wa Ushiriki wa Wananchi katika Uwekezaji. Mwongozo huu pamoja na mambo mengine umetengeneza mwongozo wa mfumo wa kupima ushiriki wa wananchi katika uwekezaji ambao ulisambazwa kwa taasisi mbalimbali zinazotekeleza miradi ya kimkakati. Baraza limepokea taarifa kutoka kwenye miradi ya ujenzi ya Ubungo Interchange, Daraja jipya la Selander, Ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Julius Nyerere-Terminal III, Mradi wa Reli ya Standard Guage na taarifa kutoka kwenye kampuni mbalimbali kwenye sekta ndogo ya gesi.

Taarifa hii inajumuisha taarifa za utekelezaji wa ushiriki wa wananchi katika miradi ya kimkakati, mabadiliko ya sheria, miongozo iliyotengenezwa, taarifa za kanzidata za watoa huduma kwenye sekta ya mafuta na gesi (mkondo wa kati na chini) na kanzi data ya nguvu kazi katika kipindi cha Julai 2018 hadi Machi 2019.

## 10.2. UTEKELEZAJI WA MIRADI YA KIMKAKATI

Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi limekuwa likiratibu utekelezaji wa ushiriki wa watanzania katika miradi ya kimkakati iliyopo katika sekta za ujenzi, usafirishaji na uziduaji kwa kipindi cha mwezi Julai hadi Desemba 2018. Miradi hiyo imeainishwa hapa chini:-

### 10.2.1. MRADI WA UBUNGO INTERCHANGE

Mradi huu ni wa ujenzi wa barabara za kupishana (interchange roads) katika makutano ya barabara za Morogoro, Sam Nujoma na Mandela. Mradi huu upo chini ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano na unatekelezwa na Wakala wa Barabara

Tanzania(TANROADS). Mkandarasi katika nradi huu ni Civil Engineering Construction Corporation. Ushiriki wa watanzania katika mradi huu ni kama ifuatavyo:-

(a) **Ajira**

Mradi huu katika kipindi hiki umetoa ajira kwa watu 502. Wageni wameajiriwa kwenye nafasi za ujuzi wa juu na wa kati. Hata hivyo asilimia kubwa ya watanzania wameajiriwa kwenye nafasi za ujuzi wa kati na kwa 100% kwa nafasi za wasio na ujuzi kama ilivyoaininshwa kwenye jedwali hapo chini:

***Jedwali Na. 12: Aina ya Ujuzi wa Watanzania na Wageni katika mradi Ubungo Interchange***

| Aina ya Ujuzi | Watanzania | | Wageni | |
|---|---|---|---|---|
| | Wananume | Wanawake | Wananume | Wanawake |
| Ujuzi wa Juu | 21 | 5 | 28 | 2 |
| Ujuzi wa Kati | 182 | 4 | 23 | 0 |
| Wasio na Ujuzi | 225 | 12 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **428** | **21** | **51** | **2** |

### 10.2.2. MRADI WA UJENZI WA DARAJA JIPYA LA SELANDER

Mradi huu ni wa ujenzi wa daraja kutoka Sea View mpaka Coco Beach. Daraja litakuwa na urefu wa km 6.23 na unalenga kupunguza msongamano kwenye barabara ya Ally Hassan Mwinyi. Huu mradi bado upo katika hatu a za awali na upo chini ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano na unasimamiwa na TANROADS. Mkandarasi wa mradi huu ni GS Engineering and Construction Cooperation kutoka Korea ya Kusini. Ushiriki wa watanzania katika mradi huu ni kama ifuatavyo:-

(a) **Ajira**

Katika kipindi cha Julai mpaka Desemba 2018 watu 42 walikuwa wameajiriwa kwenye mradi huu ambapo wageni wameajiriwa kwenye nafasi za ujuzi wa juu tu. Nafasi za ujuzi wa kati na wa chini watanzania wameajiriwa kwa 100% kama ilivyoainishwa hapa chini**.**

***Jedwali Na. 13: Aina ya Ujuzi wa Watanzania na Wageni katika mradi Daraja jipya la Selander***

| Aina ya Ujuzi | Watanzania | | Wageni | |
|---|---|---|---|---|
| | Wanaume | Wanawake | Wanaume | Wanawake |
| Ujuzi wa Juu | 18 | 4 | 9 | 0 |
| Ujuzi wa kati | 7 | 0 | 0 | 0 |
| Wasio na Ujuzi | 2 | 2 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **27** | **6** | **9** | **0** |

### 10.2.3. MRADI WA UJENZI WA UWANJA WA KIMATAIFA WA NDEGE WA JULIUS NYERERE-TERMINAL III



Ujenzi wa Uwanja wa Kimataifa wa Julius Nyerere-Terminal III ni mradi unaotekelezwa na TANROADS pamoja na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (TAA). Mkandarasi katika mradi huu ni BAM International kutoka Netherlands. Ushiriki wa watanzania katika mradi huu ni kama ifuatavyo:-

**(a) Ajira**

Katika mradi huu jumla ya watu 1,056.walipata ajira. Wageni walipata kazi kwenye nafasi za ujuzi wa juu tu na watanzania walipata kazi kwenye nafasi za ujuzi wa kati na wa chini kwa 100% kama ilivoainishwa hapa chini:

***Jedwali Na. 14: Aina ya Ujuzi wa Watanzania na Wageni***

| Aina ya Ujuzi | Watanzania | | Wageni | |
|---|---|---|---|---|
| | Wanaume | Wanawake | Wanaume | Wanawake |
| Ujuzi wa Juu | 40 | 11 | 57 | 2 |
| Ujuzi wa kati | 582 | 48 | 0 | 0 |
| Wasio na Ujuzi | 268 | 48 | 0 | 0 |

**(a) Ununuzi**

Katika miradi hii mitatu ya ujenzi wa Ubungo interchange, Daraja jipya la Selander na Uwanja wa Kimataifa wa Julius Nyerere-Terminal III bidhaa ambazo zinapatikana Tanzania zilinunuliwa Tanzania kama sementi. Hata hivyo kuna bidhaa ambazo zilinunuliwa nje ya

nchi kutokana na bidhaa zilizopo hapa nchini kutokidhi viwango vinavyotakiwa kama Chuma.

**(c ) Mafunzo**

Mafunzo mbalimbali yalitolewa kwa wafanyakazi wa TANROADS kuhusu ujenzi na utunzaji wa barabara na masuala mengine ya kiutendaji.

### 10.2.4. MRADI WA UJENZI WA BARABARA TABORA-KOGA-MPANDA

Serikali ya Tanzania kupitia TANROADS inatekeleza mradi wa kuboresha barabara ya Tabora-Koga-Mpanda yenye urefu wa km 321 kwa kiwango cha bitumen. Ili kukamilisha kwa wakati ujenzi wa barabara hii ujenzi umegawanyika katika sehemu tatu. Sehemu hizi ni Usesula-Komanga (km 108), Komanga-Kasinde (km 105) na Kasinde-Mpanda (km 105). Ushiriki wa watanzania katika mradi huu ni kama ifuatavyo:-

#### I. SEHEMU YA 1-USESULA-KOMANGA

**a) Ajira**

Jumla ya watu walioajiriwa katika mradi huu ni watu 355.Ajira za Ujuzi wa Juu Watanzania wameajiriwa 11.5% wakati Wageni wameajiriwa 88.5%. Ajira za Ujuzi wa kati na wa chini watanzania wameajiriwa 100%. Hivyo watanzania walipata fursa za ajira 91.3% wakati wageni walipata ajira 8.7%.

**b) Ununuzi**

Bidhaa zote ambazo zinapatikana hapa nchini zilinunuliwa Tanzania kwa mfano mifuko ya sementi, mafuta ya magari, mchanga, kokoto, na vifaa vingine. Bidhaa chache mfano bitumen na vyuma vya daraja vimenunuliwa kutoka nje kutokana na kutouwepo kwabidhaa zenye kiwango cha ubora unaohitajika hapa nchini.



**c) Mafunzo**

Mafunzo ya Usalama sehemu ya kazi yalitolewa kwa wafanyakazi 2 wenye ujuzi wa juu. Mafunzo ya  Ushirikishaji na mawasiliano na jamii yalitolewa kwa watu 2,520 ambapo

watu 2,301 walikuwa na ujuzi wa juu, 159 walikuwa na ujuzi wa kati na 60 walikuwa na ujuzi wa chini.

**d) Uwajibikaji kwa Jamii**

Mkandarasi amejenga mabwawa matatu (3) yenye thamani ya sh. Milioni 6kwa ajili ya umwagiliaji kwa wakulima wadogo na kwa ajili ya maji ya kunywa ya mifugo kwenye vijiji viwili Sikonge. Aidha, mkandarasi aliboresha barabara za kijiji cha Chabutwakwa thamani yash. Milioni 2 na kuwezesha kusafisha kiwanja wa ajili ya ujenzi wa hospitali ya wilaya ya Sikonge.

## II. SEHEMU YA 2- KOMANGA-KASINDE (KM108)

**a) Ajira**

Katika ujenzi wa sehemu hii watu 263 walipata ajira. Kwa nafasi za ujuzi wa juu watanzania 7 (30.4%) walipata ajira ukilinganisha na wageni 16 (69.6%) waliopata kazi kwenye nafasi za ujuzi wa juu.  Wafanyakazi wenye ujuzi wa kati na wa chini wote walikuwa watanzania. Kwahiyo watanzania walioajiriwa kwenye ujenzi wa sehemu hii ni 93.9% na wageni 6.1%.

**b) Ununuzi**

Bidhaa na huduma zilizopatikana hapa nchini ambazo zilikidhi viwango vinavyohitajika kwenye mradi zilitumika kama sementi, kokoto, mafuta, mchanga na *earth materials*. Aidha thamani ya bidhaa na huduma kutoka ndani ya Tanzania ni sh. Milioni 47, 750.6 wakati bidhaa na huduma kutoka nje vina thamani ya sh. milioni 1,097.4.

**c) Mafunzo**

Mafunzo yaliyotolewa ni ya Usalama maeneo ya kazi kwa wafanyakazi 2 wenye ujuzi wa juu na wafanyakazi 4 wenye ujuzi wa chini. Mafunzo ya Usalama wa Moto na Uokoaji kwa wafanyakazi 2 wenye ujuzi wa juu na 58 wenye ujuzi wa chini.

**d) Uwajibikaji kwa Jamii**

Mkandarasi alijenga mabwawa 2 kwa ajili ya umwagiliaji na maji ya kunywesha mifugo katika vijiji vya Kamsisi na Inyonga wilaya ya Mlele vyenye thamani ya sh. Million 15 na kisima cha maji kijiji cha Utende wilaya ya Mlele chenye thamani yash. Milioni 23. Mkandarasi pia alijenga jengo la utawala la shule ya sekondari ya Nsekwa katika kata ya Nsekwa. Aidha, mafunzo ya kujenga uelewa wa ugonjwa wa UKIMWI na namna ya kujikinga yalitolewa kwa wafanyakazi na jamii inayozunguka eneo la mradi.

## III. SEHEMU YA 3 KASINDE-MPANDA (KM105)

### a) Ajira

Jumla ya watu 342 walipata ajira kwenye ujenzi wa kipande hichi. Watanzania wenye ujuzi wa juu waliajiriwa 73.4% ukilinganisha na wageni wenye ujuzi wa juu waliokuwa 29.6%. Kwa wafanyakazi wenye ujuzi wa kat watanzania walikuwa 85.5% na wageni 14.6%. Kwenye nafasi za wafanyakazi wenye ujuzi wa chini watanzania waliajiriwa kwa 100%. Hivyo ajira kwa sehemu ya 3 ya ujenzi watanzania waliajiriwa kwa 93.6% na wageni 6.4%.

### b) Ununuzi

Bidhaa na huduma zinazopatikana Tanzania zilinunuliwa hapa Tanzania ambapo bidhaa na huduma zenye thamani ya Dola za Kimarekani 700,000 zilinunuliwa kutoka Tanzania na bidhaa na huduma zenye thamani ya dola za kimarekani 100,000 zilinunuliwa kutoka nje ya Tanzania.

### c) Mafunzo

Mafunzo yaliyotolewa ni ya Usalama maeneo ya kazi kwa wafanyakazi 97 wenye ujuzi wa juu na wafanyakazi 19 wenye ujuzi wa kati. Mafunzo ya Usalama wa Moto na Uokoaji kwa wafanyakazi 15 wenye ujuzi wa chini.

### d) Uwajibikaji kwa Jamii

Mkandarasi alifanya ukarabati wa madarasa katika kijiji cha Isanjandugu, wilaya ya Nsimbo mkoa wa Katavi kwa thamani inayokadiriwa kuwa milioni 15.

## 10.2.5. MRADI WA UJENZI WA RELI KWA KIWANGO CHA STANDARD GAUGE



Ujenzi wa reli ya Standard Gauge kutoka bandari ya Dar es Salaam mpaka mikoa ya kati na ya magharibi ya Tanzania unaendelea. Reli hii inalenga kuwezesha usafirashaji mkubwa na wa haraka wa abiria na mizigo. Mradi unatekelezwa na Shirika la Reli Tanzania (TRC). Mkandarasi wa mradi huu ni Yapi Merkezi kutoka Uturuki. Ushiriki wa watanzania katika mradi huu ni kama ifuatavyo:-

a) **Ajira**

Jumla ya watu 3,785 walipata ajira katika mradi huu. Wageni wameajiriwa katika nafasi za ujuzi wa juu na wa kati na watanzania wasio na ujuzi wameajiriwa kwa asilimia 100 kama ilivyoainishwa hapa chini.

***Jedwali Na. 15: Aina ya Ujuzi wa Watanzania na Wageni katika Ujenzi wa Mradi wa Reli ya Kati***

| Aina ya Ujuzi | Watanzania | | | | Wageni | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Me | Ke | Walemavu-Me | Walemavu-Ke | Me | Ke |
| Ujuzi wa juu | 2,292 | 36 | | | 124 | 8 |
| Ujuzi wa Kati | 461 | 24 | | | 127 | 0 |
| Wasio na Ujuzi | 566 | 147 | | | 0 | 0 |
| **Jumla** | **3,319** | **207** | **12** | **3** | **251** | **8** |

b) **Mafunzo**

Katika kipindi husika mafunzo ya ujumla ya masuala ya reli na uendeshaji wa reli ya Standard Gauge yalitolewa kwa watumishi 124 mkoani Dar es Salaam.

c) **Uwajibikaji kwa Jamii**

Mradi huu umetoa huduma kwa jamii kwenye maeneo ya elimu, afya, mazingira, ujenzi wa miundo mbinu hasa barabara na kituo cha afya pamoja na kusaidia yatima na watu waliokutwa na majanga mf. MV Nyerere. Maeneo yaliyonufaika na huduma hizo ni mkoa wa Pwani (Kisarawe na Kibaha), Mwanza, Dar es Salaam ( Temeke, Kinondoni na Ilala)

### 10.2.6. MRADI WA TRANSPORT INTERMODEL RAILWAY

Mradi huu unatekelezwa na Shirika la Reli Tanzania. Katika mradi huu ushiriki wa watanzania ulikuwa kama ifuatavyo:

**(a) Ajira**

Mradi huu umetoa ajira 1281 hadi Desemba 2018. Wageni wameajiriwa kwenye nafasi za ujuzi wa juu tu. Watanzania wameajiriwa kwa 100% kwenye nafasi za ujuzi wa kati na wa chini kama ilivyoainishwa hapa chini.

***Jedwali Na. 16: Aina ya Ujuzi wa Watanzania na Wageni katika Ujenzi wa Mradi wa Transport Intermodel Railway***

| Aina ya Ujuzi | Watanzania | | Wageni | |
|---|---|---|---|---|
| | **Wananume** | **Wanawake** | **Wanaume** | **Wanawake** |
| **Wenye Ujuzi wa Juu** | 233 | 0 | 152 | 0 |
| **Ujuzi wa Kati** | 85 | 0 | 0 | 0 |
| **Wasio na Ujuzi** | 811 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **1,129** | **0** | **152** | **0** |

**(b) Ununuzi wa Bidhaa na Huduma**

Kwenye mradi huu bidhaa za kitanzania zilizonunuliwa ni Mifuko ya sementi, nondo, rip rap, kokoto, *ballast, riversand*, matofali, *admixture of concrete,chemical anchor, grouting agent* na mafuta ya petroli na diesel.

Huduma zilizotumika katika mradi huu ni 16 ambapo kati ya hizo 1 ilitolewa na kampuni kutoka nje na 3 zilitolewa na kampuni za nje zilizoingia ubia na kampuni za ndani. Huduma zilizobaki zilitolewa na watanzania.

## 10.3. SEKTA NDOGO YA MAFUTA NA GESI

Sekta hii ina miradi ambayo ipo kwenye mkondo wa juu na ambazo zipo kwenye mkondo wa kati na chini.Katika sekta ndogo ya mafuta na gesi taarifa za Ushiriki wa watanzania zilikuwa kama zifuatazo:-

### 10.3.1. MRADI WA SONGAS

Songas ni kampuni inayotengeneza umeme kwa kutumia gesi kutoka kisiwa cha Songosongo kusini mwa Tanzania. Gesi inachakatwa katika kisiwa hicho na kusafirishwa kwa bomba lenye urefu wa km 225 mpaka Dar es Salaam ambapo inatumika kuzalisha umeme kwenye mitambo ya Songas Ubungo. Ushiriki wa watanzania katika mradi huu ni kama ifuatavyo:-



a) **Ajira**

Mpaka kufikia Desemba 2018, Songas ilikuwa na wafanyakazi 71 ambapo watanzania walikuwa 68 na wageni 3 ambao wako kwenye nafasi za uongozi tu.

Songas inamtumia Pan African (PAET) kama mkandarasi anayendesha mitambo ya kuchakata gesi Songosongo kwa niaba ya Songas. PAET ina wafanyakazi 52 ambapo watanzania wapo 41 na mgeni 1 pamoja na wafanyakazi wa muda mfupi 10 wakitanzania.

b) **Mafunzo kwa Vitendo**

Songas wanatoa mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi kwenye nafasi mbalimbali.Katika mwaka 2018, Songas ilichukua wanfunzi wa vitendo 12 ambapo 2 wamepata ajira za kudumu.

c) **Mafunzo**

Kampuni hii imekuwa ikitoa mafunzo ya ndani na nje ya nchi kwa wafanyakazi ambapo katika kipindi husika wafanyakazi 12 walipelekwa kwenye mafunzo ya shahada na shahada ya uzamivu Wafanyakazi wengine pia waipewa mafunzo ya kiutendaji.

#### 10.3.2. MRADI WA BOMBA LA MAFUTA GHAFI (EAST AFRICA CRUDE OIL PIPELINE)

Mradi huu ni wa ujenzi wa bomba la kusafirisha mafuta ghafi lenye urefu wa km 1,443 kutokaa Hoima, Uganda mpaka Chongoleani, Tanga, Tanzania upo katika hatua za majadiliano kati ya Serikali ya Tanzania na mwekezaji. Katika kipindi hiki cha taarifa masuala yafuatayo yalifanyika:-

i. Total East Africa Midstream B.V iliingia mkataba na Deloitte Consulting Limited ili kufanya tafiti bainifu wa bidhaa zinazozalishwa na huduma zinazotolewa na kampuni za kitanzania. Lengo la utafiti huu ni kuwawezesha kufahamu uwezo na mapungufu ya bidhaa na huduma za kitanzania na kuainisha hatua ambazo watachukua ili kuweza kuboresha maeneo yenye upungufu kulingana na mahitaji yao.

ii. EACOP walifanya Kongamano la Ushiriki wa Watanzania katika mradi huo (National Content Development Workshop) tarehe 6 Februari, 2019. Lengo la Kongamano hili lilikuwa ni kuonyesha fursa mbalimbali ambazo zitakuwepo wakati wa ujenzi wa mradi huu ikiwemo bidhaa, huduma pamoja na nguvu kazi itakayohitajika. Aidha, Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC) pamoja na Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji (EWURA) zilifanya mawasilisho kuhusu mipango na mikakati ya Serikali katika kuhakikisha watanzania wanashiriki katika mradi huu.

iii. NEEC kwa kushirikiana na wadau mbalimbali kama TCCIA, EWURA, TPDC na TaESA walifanya kongamano kuhusu mradi wa EACOP mkoani Tanga tarehe 2 Machi, 2019. Kongamano hili lilikuwa na lengo la kuwajengea uwezo viongozi wa mkoa, taasisi za Serikali pamoja na sekta binafsi kuhusu Sera na Sheria za *local content*, hatua za mradi, fursa zitakazokuwepo kwenye mradi pamoja na kuweka mikakati ya mkoa kuhakikisha wananchi wa mkoa wa Tanga wanashiriki katika mradi huu.

### 10.3.3. MAUREL ET PROM

Kampuni hii ina jumla ya wafanyakazi wa kudumu 93 ambapo watanzania wapo 84 na wageni 9. Katika kipindi cha Januari hadi Desemba 2018 ajira zilitolewa kwa nafasi za Menejimenti 2 kwa watanzania na 1 kwa wageni. Nafasi za wataalam (Technicians) watanzania 21 na wahandisi 23 watanzania na 6 wageni.Kwenye fani zingine kama fedha, sheria, local content na Uwajibikaji kwa jamii watu 40 ambao wote ni watanzania.

a) **Mafunzo**

Katika kipindi husika mafunzo mbalimbli yalitolewa kwa wafanyakazi ambapo jumla ya watu 14 walipewa mafunzo na wote ni wafanyakazi watanzania. Mafunzo hayo yameainishwa hapo chini:

***Jedwali Na. 17: Aina ya mafunzo yaliyotolewa na kampuni ya* MAUREL ET PROM**

| Na. | Aina ya Mafunzo | Watanzania | Wageni |
|---|---|---|---|
| **1.** | Production Superintendent Certification | 1 | 0 |
| **2.** | Masuala ya Mahesabu na Ukaguzi | 1 | 0 |
| **3.** | Mfumo wa habari | 2 | 0 |
| **4.** | Mafunzo ya viwango maeneo ya kazi na utekelezaji wa sheria za ajira | 2 | 0 |
| **5.** | Mafunzo ya mikatabaya wafanyakazi | 2 | 0 |
| **6.** | Kozi ya Kompyuta | 1 | 0 |
| **7.** | Kozi ya Usafirishaji | 1 | 0 |
| **8.** | Kozi ya Kiingereza | 1 | 0 |
| **9.** | Uendeshaji wa magari makubwa | 2 | 0 |
| **10.** | Mafunzo ya uchukuzi | 1 | 0 |
| | **JUMLA** | **14** | **0** |

## 10.4. KANZI DATA YA WATOA HUDUMA SEKTA YA MAFUTA NA GESI NA YA NGUVU KAZI

### I. Kanzi Data ya Watoa Huduma sekta ya Mafuta na Gesi

Kanzi Data ya watoa Huduma kwenye sekta ya Mafuta na Gesi (Mkondo wa Kati na wa Chini) ulitengenezwa na Mamlaka ya Kudhibiti Nishati na Maji (EWURA) mwaka 2018. Mwezi Agosti, 2018 watoa huduma waliosajiliwa walikuwa 170. Hadi kufikia mwezi Februari 2019 watoa huduma walikuwa wamesajiliwa na EWURA. Lengo la Kanzi Data hii ni kuwatambua watoa huduma kwenye sekta ya mafuta na gesi pia kuwaunganisha watoa huduma na wawekezaji na wakandarasi. Jedwali hapo chini inaonyesha aina ya watoa huduma waliosajiliwa na idadi yao.

***Jedwali Na. 18: Kanzi data ya watoa huduma sekta ya mafuta na gesi***

| S/N | SEKTA | IDADI YA KAMPUNI |
|---|---|---|
| 1. | Kilimo, Uvuvi na Misitu | 4 |
| 2. | Uzalishaji | 8 |
| 3. | Huduma ya Umeme na Vifaa vya Umeme | 25 |
| 4. | Ujenzi | 64 |
| 5. | Biashara za Jumla, rejareja, huduma ya vifaa vya spare, na Fundi magari | 8 |
| 6. | Huduma za Uchukuzi na Uhifadhi | 50 |
| 7. | Huduma za malazi na chakula | 11 |
| 8. | Huduma za Afya | 2 |
| 9. | Mawasiliano, TEKNOHAMA na Mifumo ya Ulinzi | 18 |
| 10. | Huduma ya Fedha na Bima | 7 |
| 11. | Huduma ya Nyumba na Viwanja | 5 |
| 12. | Professional, Scientific and Technical Services | 65 |
| 13. | Huduma za Sheria | 30 |
| 14. | Huduma za Utawala na support service | 18 |
| 15. | Ujengaji Uwezo na Huduma za Ajira | 3 |
| 16. | Huduma za Ulinzi | 16 |

### II. Kanzi Data ya Nguvu Kazi

Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajirana Watu Wenye Ulemavu) wametengeneza Kanzi Data ya Nguvu Kazi. Lengo la Kanzi Data hii ni kuweza kufahamu nguvu kazi iliyopo kwenye fani mbalimbali, kujua uwezo na mapungufu yaliyopo kwa nguvu kazi ya kitanzania na kuunganisha nguvu kazi hii na fursa za ajira kwenye miradi na kazi mbalimbali zinazopatikana hapa nchini. Kanzi Data hiyo ina jumla ya watu waliosajiliwa 16,677 kama ilivyoainishwa hapa chini:-

***Jedwali Na. 19: Kanzi data ya nguvu kazi***

| Na | TAALUMA | Me | Ke | JUMLA |
|---|---|---|---|---|
| 1. | CRAFTING | 654 | 42 | 696 |
| 2. | HOISTING & LIFTING | 28 | 0 | 28 |
| 3. | DRIVERS | 2823 | 0 | 2823 |
| 4. | ELECTRICAL ENGINEER | 1404 | 77 | 1481 |
| 5. | MECHANICAL ENGINEER | 1463 | 45 | 1508 |
| 6. | WELDING | 413 | 10 | 423 |
| 7. | MACHINE OPERATOR | 486 | 5 | 491 |
| 8. | CIVIL ENGINEER | 902 | 103 | 1005 |
| 9. | GEO SCIENCES | 696 | 116 | 812 |
| 10. | PETROLEUM ENGINEER | 300 | 44 | 344 |
| 11. | CHEMICAL ENGINEER | 155 | 26 | 181 |
| 12. | NON-TECHNICAL | 5196 | 1689 | 6885 |
| JUMLA | | **14518** | **2159** | **16677** |

# 11.0. SERA, SHERIA NA MIONGOZO

## 11.1. UTANGULIZI

Katika kipindi cha taarifa hii hamna Sera au Sheria mpya iliyotungwa ya masuala ya *local content*. Hata hivyo kulikuwa na marekebiso kwenye Kanuni za Ushiriki wa Watanzania katika sekta ya Madini na pia Miongozo iliyotengenezwa kama ilivyoainishwa hapa chini:-

### I. *The Mining (Local Content) (Amendments) Regulations, 2019*

Wizara ya Madini ilitoa Kanuni hizi tarehe 8 Februari, 2019. Kanuni hizi zimefanya mabadiliko yafuatayo:-

a) Tafsiri ya kampuni ya kitanzania imebadilishwa kumaanisha kampuni iliyosajiliwa chini ya Sheria za Kampuni (Companies Act No. 12 RE. 2002) na yenye hisa zisizopungua 20% zinazomilikiwa na watanzania na wafanyakazi kwenye nafasi za juu za uongozi si chini ya 81% na wafanayakazi wakitanzania 100% kwa nafasi ambazo si za uongozi na nafasi nyingine. Mabadiliko haya yamepunguza kiwango cha hisa za watanzania kwenye kampuni ya kitanzania kutoka hisa si chini ya 51% kama ilivyokuwa kwenye Kanuni za mwaka 2018 hadi hisa si chini ya 20%.

b) Kanuni hizi zimetaka wadau kwenye sekta ya madini kuwa na akaunti na benki za kitanzania ambazo watanzania wanashikilia si chini ya hisa za 20% kwenye benki hiyo.

c) Kanuni hizi zinampa mamlaka Waziri wa Madini kwa kushauriana na Tume ya Madini kutoa maelekezo ya kiwango cha chini cha utekelezaji wa *local content* ambazo ni mbadala kwa zile zilizoainishwa kwenye Jedwali la Kwanza la Kanuni.

### II. *The Mining Commission (Guideline for Submission of Local Content Plan) 2018*

Mwongozo huu unawataka wawekezaji katika sekta ya madini kukiri kwenye sehemu ya II ya Mwongozo huo kuwa watatoa kipaumbele cha kwanza kwa bidhaa na huduma za kitanzania na ajira na mafunzo kwa watanzania. Mwongozo huo pia umetoa formati kwa wawekezaji katika kuandaa mipango ya masuala yafuatayo:-

a) Ajira na Mafunzo
b) Uhaulishaji wa Teknolojia
c) Bima
d) Huduma za benki na taasisi za kibenki
e) Huduma za Sheria
f) Utafiti na Maendeleo

g) Mfumo wa taarifa na Teknohama
h) Kazi za Ujenzi, Bidhaa na Vifaa n.k.

***III. Mwongozo wa Kitaifa wa Ushiriki wa Wananchi katika Uwekezaji, 2019***

Mwongozo huu umetengenezwa na Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kwa lengo la kutoa mwongozo wa jinsi ya kuongeza ushiriki wa watanzania katika miradi na uwekezaji kwenye sekta mbalimbali za kiuchumi pamoja na masuala yafuatayo:-

a) Kuweka mfumo wa uratibu wa masuala ya *local content*;
b) Kuelezea kazi za kamati mbalimbali za *Local Content;*
c) Kuelezea wajibu wa wadau mbalimbali katika kutekeleza masuala ya *local content,*
d) Kutoa mwongozo wa kutengeneza taarifa za *local content* kwenye miradi mbalimbali.

## 11.2. CHANGAMOTO

1. Suala la ununuzi wa bidhaa na huduma kutoka kwa watanzania au kampuni za kitanzania pamoja na uhaulishaji wa teknolojia havifanyiwi ufuatiliaji vizuri kwenye baadhi ya miradi. Kutokufanya ufuatiliaji wa makini kwenye suala la ununuzi itapelekea Baraza na wadau wengine kutofahamu uwezo na changamoto za kampuni za kitanzania kushiriki kwenye miradi mbalimbali pamoja na thamani inayobaki nchini kutokana na kutumia bidhaa na huduma za kitanzania;
2. Kanzi Data ya nguvu kazi haipo kwenye mfumo wa kielektroniki ili kuwawezesha watu kujisajili kirahisi na waajiri kuunganishwa na waajiriwa kirahisi;
3. Sekta binafsi bado wana mwamko mdogo kujisajili kwenye Kanzi Data ya watoa huduma kwenye sekta ya mafuta na gesi na hivyo kuwa changamoto kwa wawekezaji na wakandarasi kupata watoa huduma wa kutosha wakitanzania kwenye sekta ndogo ya mafuta na gesi; na
4. Wafanyakazi katika idara au vitengo vya *local content* kwenye taasisi mbalimbali ni wachache na kazi hii ni kubwa inayohitaji ufuatiliaji wa hali ya juu.

## 11.3. MAPENDEKEZO

1. Miradi yote ya kimkakati ifuatilie masuala ya ushiriki wa watanzania katika miradi hiyo kikamilifu hasa kwenye masuala ya ununuzi, uhaulishaji wa

teknolojia na uwajibikaji kwa jamii ambavyo vimeonekana kutokufuatiliwa vizuri;

2. Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi litoe mafunzo kuhusu Mwongozo wa Local Content na maeneo ya muhimu ya kupima ushiriki wa wananchi kwenye miradi ya kimkakati;
3. Kanzi Data ya nguvu Kazi iwekwe kwenye mfumo wa kielektroniki ili kurahisiha usajili na uunganishaji wa mwajiri na mwajiriwa;
4. EWURA, NEEC, Sekta binafsi na Asasi za Kiraia ziwahamasishe wafanyabiashara wakitanzania kujisajili kwenye kanzi data ya watoa huduma iliyopo EWURA na kuchnagamkia fursa kwenye sekta ya mafuta na gesi;
5. Idara au vitengo vya *Local Content* viongezewe nguvu kazi na watumishi wajengewe uwezo wa kutosha ili waweze kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa masuala ya *local content* kwa ufanisi.

## 12.0.UJASIRIAMALI




## 12.1. UTANGULIZI

Ujasiriamali ni mojawapo ya nguzo tisa za Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ambayo inalenga kuinua viwango vya elimu na ujuzi ili kukuza ubunifu wa kufanya biashara na shughuli za uzalishaji nchini kwa umakini na ushindani wa hali ya juu. Sera imetoa mwongozo wa kuandaa mikakati inayolenga kuwajengea wananchi uwezo wa kujiamini, kuthubutu na ubunifu wa uzalishaji mali ili kukuza vipato vyao na kujitegemea kiuchumi. Baraza la Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kupitia utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na mwongozo wake linaendelea kuratibu maendeleo ya ujasiriamali nchini kwa kushirikiana na wadau mbalimbali kama vile Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia; Wizara ya Viwanda na Biashara pamoja na Taasisi ya Sekta Binafsi (TPSF). Katika kipindi cha kuanzia Julai, 2018 mpaka Machi, 2019, mambo yafuatayo ya uratibu wa ujasiriamali nchini yametekelezwa:

## 12.2. KAMATI YA TAIFA YA MAENDELEO YA UJASIRIAMALI

Ili kuendelea kuimarisha uratibu wa maendeleo ya ujasiriamali nchini, serikali iliunda Kamati ya Kitaifa ya Maendeleo ya Ujasiriamali (*National Entrepreneurship Development Committee*). Kamati hii inajumuisha wataalam kutoka sekta ya umma, wanataaluma na sekta binafsi kwa lengo la kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Ujasiriamali nchini (*Inclusive National Entrepreneurship Strategy*) kama ilivyoanishwa kwenye Mwongozo wa Ufundishaji Elimu ya Ujasiriamali yaani *National Entrepreneurship Training Framework*. Kazi kubwa ya wajumbe wa kamati hii ni kuishauri serikali kupitia Baraza njia bora ya kuimarisha ujasiriamali nchini kwa kuibua fursa za uwezeshaji zinazokidhi mahitaji ya wananchi katika mazingira yaliyopo. Pia, kamati hii inashauri uratibu nzuri wa ujasiriamali nchini kwa kuhamasisha ushirikiano kutoka kwa wadau mbalimbali wakati wa utekelezaji wa majukumu yao na kuondoa vikwazo vinavyosababisha mazingira ya biashara kuwa magumu kwa wajasiriamali nchini.




Katika kutekeleza majukumu yake, Kamati ya Taifa ya Maendeleo Ujasiriamali nchini (NEDC) imebaini kuwa biashara nyingi za wajasiriamali zinakufa haraka kutokana na kukosa mipango madhubuti ya kuhimili ushindani katika masoko, usimamizi sahihi wa rasilimali watu na rasilimali fedha, kukosa ubunifu, kutojiunga na mitandao sahihi ya biashara, pia mitaji midogo. Kamati imeshauri kuendeleza na kuanzisha vituo vya malezi ya biashara kwa wajasiriamali (*Incubators*) ili kuwapatia mafunzo na mwongozo sahihi wa kusimamia uanzishwaji na uendelezaji wa biashara zao kama vile SIDO, VETA, TECC, COSTECH, DTBi pamoja na vituo maalum vilivyoanzishwa katika taasisi za Elimu ya Juu na Vyuo Vikuu.

### 12.3. MATUMIZI YA TEKNOLOJIA NA UBUNIFU KATIKA BIASHARA




Kamati ya Taifa ya Maendeleo ya Ujasiriamali nchini (NEDC) imebaini kuwa matumizi ya teknolojia katika kuzalisha na kutafuta masoko kwa wafanyabiashara wengi yamekuwa madogo sana, hivyo imechangia kudumaa kwa biashara zilizo nyingi hatimaye kufa mapema kwa kukosa nguvu ya ushindani kimasoko mathalani vifaa vinavyotumika katika uzalishaji kuwa na uwezo mdogo hivyo kutokidhi mahitaji ya wateja kwa wakati, ufungashaji mbovu, matumizi madogo ya TEHAMA pia kutokuwa na mpangilio wa masoko unaoeleweka. Katika ubunifu na ufumbuzi mbalimbali wa kiteknolojia unaendelea kutoka ndani na nje ya nchi, Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kama mshirika wa Maonesho ya Ubunifu na Teknolojia Kusini mwa Jangwa la Sahara yanayoendeshwa na Sahara Ventures Limited linahamasisha wajasiriamali wa Kitanzania kutumia fursa hii kujifunza mifano bora ya matumizi ya teknolojia katika biashara kutoka kwa mataifa mengine ili kuongeza ubunifu wa kukabiliana na utandawazi unaongeza ushindani wa biashara nchini.

### 12.4. KUPANUA WIGO WA MITAJI KWA WAFANYABIASHARA NA WAJASIRIAMALI NCHINI

Pamoja na kushuka kwa riba za mikopo ya biashara za mabenki kutoka wastani wa asilimia 22% hadi 18% kwa mwaka, bado mazingira ya mikopo ya biashara kwa wajasiriamali hayajawa rafiki kutokana na masharti mengine. Biashara nyingi za wajasiriamali zinaendeshwa kwa kutegemea faida inayotokana na mzunguko wa biashara au fedha za uwezeshaji ambazo hukoma baada ya muda fulani ambapo kwa upande mwingine baadhi ya makampuni yaliyojiimarisha vizuri ndio wananufaika na mikopo ya biashara kutoka taasisi za fedha. Ili kuleta ufumbuzi mbadala kuhusu upatikanaji wa Mitaji kwa wajasiriamali na makampuni madogo, Kamati ya Taifa ya Maendeleo ya Ujasiriamali nchini kupitia Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi iliunda timu ya wataalam wa soko la fedha na mitaji kuandaa mpango wa kuwasaidia wajasiriamali Wadogo na wa Kati kupata mitaji ya kuendeleza na kukuza biashara zao kupitia vyanzo mbalimbali kama vile *Angel Investors Networks*, *Venture Capital* na *Private Equity*.

## 12.5. HALI YA UTEKELEZAJI WA MKAKATI WA TAIFA WA UJASIRIAMALI

Katika jitihada za makusudi zinazochukuliwa na serikali kuboresha mazingira ya biashara kwa wazalishaji, wafanyabiashara na wajasiriamali nchini bado kumekuwa na changamoto mbalimbali zinazokwamisha maendeleo ya biashara ndogo na za kati nchini. Hivyo, serikali kwa kushirikiana na Shirika la Umoja na Maendeleo ya Biashara la Umoja wa Mataifa (UNCTAD), Wizara ya Viwanda na Biashara pamoja na Taasisi ya Sekta Binafsi iliandaa Mkakati wa Taifa wa Ujasiriamali ambao umejikita kuleta ufumbuzi katika maeneo matano yaliyotafitiwa ambayo ni i) Kuboresha Mazingira ya Biashara ii) Kuimarisha Ujuzi na Elimu ya Ujasiriamali iii) Kuwezesha Matumizi ya Teknolojia na Ubunifu iv) Kuboresha Upatikanaji wa Mitaji na v) Kuimarisha Uhamasishaji na Matumizi ya Mitandao ya Kibiashara.




Pamoja na mambo mengi mazuri ya kuendeleza ujasiriamali nchini yaliyoainishwa kwenye mkakati huo, utekelezaji wake unafanywa na wadau mbalimbali kutoka wizara na taasisi zake, pamoja na sekta binafsi ambapo Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ndiye Mratibu wa utekelezaji wa mkakati huo.


## 12.6. UBORESHAJI WA MAZINGIRA YA BIASHARA

Katika utekelezaji wa Andiko la Kuimarisha Mazingira ya Biashara Tanzania (Blue Print), serikali imeanza kuchukua hatua ya kutatua changamoto za kiusimamizi na udhibiti zilizolalamikiwa na wafanyabiashara walio wengi hususan kuwepo kwa tozo nyingi za biashara, urasimu wa kupata vibali na leseni mbalimbali za biashara, miundombinu duni katika maeneo yaliyotengwa kibiashara pamoja na muingiliano wa majukumu ya uthibiti kwa baadhi ya taasisi za serikali. Serikali kupitia taasisi zake imeendelea kufanya mikutano na wadau mbalimbali kwa lengo la kupatia ufumbuzi kero za wajasiriamali kuanzia ngazi ya Taifa hadi Wilaya kupitia mabaraza ya biashara, majukwaa na makongamano, pia kuchukua hatua ya kuunganisha baadhi ya taasisi zenye majukumu yanayofanana. Mahali pengine taasisi za usimamizi kama Mamlaka ya Mapato Tanzania imekuwa ikitoa miongozo ya tozo mbalimbali za kodi kila unapoanza mwaka mpya wa fedha na kutoa matangazo ya kukamilisha malipo hata kwa kuongeza muda wa ziada.

Pia, Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi katika uboreshaji wa mazingira ya biashara nchini kupitia uratibu wa shughuli za uwezeshaji wananchi kiuchumi katika Mikoa na Serikali za Mitaa linaratibu uanzishwaji wa vituo vya uwezeshaji kwa lengo la kusogeza huduma karibu na wananchi kwa Mfano Kituo cha Uwezeshaji Kahama ambapo taasisi na mamlaka za udhibiti zaidi ya 22 zimepewa Ofisi ndani ya eneo moja kwa ajili ya kuwahudumia wananchi wa Kahama na Kanda ya Ziwa kwa ujumla.

## 12.7. KUIMARISHA UJUZI NA ELIMU YA UJASIRIAMALI

Utekelezaji wa Mwongozo wa Taifa wa Ufundishaji wa Elimu ya Ujasiriamali umefanikiwa kwa kiwango kikubwa katika mfumo rasmi wa elimu nchini. Kuanzia shule za msingi, vyuo vya ufundi mpaka vyuo vikuu vimefanikiwa kuhuisha elimu ya ujasiriamali katika mitaala yao. Aidha program tofauti za kukuza ujuzi katika sekta isiyo rasmi zimeanzishwa kwa ajili ya kujengea uwezo wananchi, wahitimu wa vyuo mbalimbali na wajasiriamali mmojammoja kwa mfano *National Skills Development Program* kupitia mradi mpya wa Kukuza Stadi za Kazi na Ujuzi wa Kisekta ulianza kutekelezwa kuanzia mwaka 2018, Uanzishwaji wa Kiongozi cha Kitaifa cha Mafunzo ya Ujasiriamali katika Mfumo Usio Rasmi, Programu ya Elimu ya Ujasiriamali kwa Mtandao (*www.tadiye.or.tz*), Programu za mashindano ya ujasiriamali kwa vijana mfano *Young Graduate Entrepreneurship*, Kijana Jiajiri, *Biashara Forum*, *Social Innovation Challenge* na kadhalika. Programu hizi pamoja na nyingine zimechangia kukuza ujuzi na elimu ya ujasiriamali kupitia mafunzo maalum ya biashara, ujasiriamali, malezi na mitaji yanayotolewa kwa walengwa husika.




## 12.8. KUWEZESHA MATUMIZI YA TEKNOLOJIA NA UBUNIFU

Ili kuwezesha matumizi ya Teknolojia na Ubunifu kwa wananchi, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imetoa mwongozo wa kuanzisha vituo atamizi vya ubunifu nchini ambapo utekelezaji wake umeanza mapema katika vyuo vya elimu ya juu kama vile Chuo cha Teknolojia Dar es Salaam, Chuo cha Kilimo Sokoine, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Chuo cha Mtakatifu Joseph Dar es Salaam. Mwongozo wa uanzishwaji wa vituo hivi unaenda sambamba na kutambua vituo vilivyonzishwa kwa muda mrefu ili kuweza kuainisha mahitaji halisi ya wajasiriamali katika vituo hivyo (**www.innovate.co.tz**).

Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi limekuwa likishirikiana na Kampuni ya Ubunifu katika Teknolojia (*Sahara Ventures Ltd*) kutambua mchango wa wajasiriamali nchini katika kukuza tasnia ya ubunifu, kutoa nafasi ya kuwasilisha mada ya ubunifu kwa mapana yake wakati wa Kongamano la Nne la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi pamoja na kushirikiana na wadau wengine kuimarisha uratibu wa vituo vya ubunifu kwa kuanzisha taasisi mwamvuli.

Aidha, Tume ya Sayansi kwa kushirikiana na Mfuko wa Ubunifu na Maendeleo ya Teknolojia (*HDIF*) imekuwa ikiendesha mashindano ya ubunifu kila mwaka pia kutoa ruzuku kwa mawazo bora ya biashara zinazohusu ubunifu na matumizi ya teknolojia nchini.



Kwa upande mwingine, Baraza limekuwa likihamasisha wabunifu mbalimbali nchini kutumia ujuzi wao kuanzisha viwanda vidogo vinavyotumia malighafi za ndani kuzalisha bidhaa na kutengeneza ajira kwa wananchi. Kupitia mbunifu na mnufaika wa Mfuko wa Uwezeshaji Mwananchi wa Baraza (MEF) **Bw. George Buchafwe** wa Star Natural Product amefanikiwa kuanzisha **viwanda 7** vilivyotoa **ajira 100** za moja kwa moja na **ajira 1,600** zisizokuwa za moja kwa moja katika mikoa ya Simiyu, Iringa, Mara, Mbeya na Dar-es-salaam kwa kushirikiana na viongozi wa Mikoa na Halmashauri. Uanzishwaji wa viwanda hivi kwa sehemu kubwa umetumia mapato ya ndani ya fedha za halmashauri za uwezeshaji kwa vijana, wanawake na wenye ulemavu, mikopo ya Benki pamoja na wahisani. Hadi kufikia Aprili, 2019 Star Natural Products Ltd ilikuwa imefungua viwanda vifuatavyo:-

***Jedwali Na. 20: Viwanda vilivyofunguliwa na Star Narual Products kufikia Aprili, 2019.***

| Na. | JINA LA MKOA | HALMASHAURI HUSIKA | AINA YA KIWANDA | MTAJI WA KIWANDA | CHANZO CHA FEDHA/MTAJI | AJIRA ZA MOJA KWA MOJA | AJIRA NYINGINE | JUMLA YA AJIRA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | SIMIYU | MASWA | Sabuni za Mche | 18,000,000 | Mapato ya Ndani 10% | 16 | 120 | 136 |
| | | BUSEGA | Sabuni za Mche | 35,000,000 | Mapato ya Ndani 10% | 10 | 240 | 250 |
| | | ITILIMA | Sabuni za Mche na Maji | 83,000,000 | Mapato ya Ndani 10% | 20 | 360 | 380 |
| 2 | IRINGA | MJI WA MAFINGA | Sabuni ya Mche na Maji | 70,000,000 | Mapato ya Ndani 10% | 19 | 360 | 379 |
| 3 | DAR ES SALAAM | KINONDONI | Sabuni ya Mche | 18,000,000 | Mkopo wa Benki | 10 | 120 | 130 |
| 4 | MARA | MUSOMA | Sabuni ya Mche | 19,000,000 | Mkopo wa Benki | 7 | 120 | 127 |
| 5 | MBEYA | IPINDA KYELA | Mashine ya kukamua mawese | 20,000,000 | Land O'Lakes, USAID | 18 | 180 | 260 |
| | **Jumla Kuu** | **7** | | **263,000,000** | | **100** | **1,500** | **1,600** |

### 12.9. KUBORESHA UPATIKANAJI WA MITAJI

Serikali ya Awamu ya tano inaendelea kuchukua jitihada za makusudi kutunga sheria na kutoa miongozo mbalimbali kulinda maslahi ya waweka akiba na wakopaji wa fedha nchini kupitia taasisi za fedha kama vile kutungwa kwa Sheria ya Taasisi Ndogo za Fedha yaani Microfinance Act 2018, Utoaji wa Vitambulisho vya Taifa, Upimaji wa maeneo na utoaji wa Hati Miliki za Kimila kwa wananchi wanaoishi katika maeneo yasiyopimwa ambavyo vyote vinaongeza fursa ya kukopesheka kwa wananchi walio wengi. Aidha mafunzo yanayoendelea ya kujengea uwezo watoa huduma za ushauri na uendelezaji biashara nchini kupitia Kiongozi cha Kitaifa cha Mafunzo ya Ujasiriamali kwa Sekta isiyo rasmi yanaongeza tija kwa wajasiriamali kuandaa Maandiko ya Biashara yanayotekelezeka.

Pia, ongezeko la utoaji wa huduma za fedha na uwakala kupitia mitandao ya simu za mkononi umewezesha wananchi wengi kufikiwa na huduma za fedha katika maeneo yasiyo na mabenki na kupata mikopo kwa masharti nafuu kupitia mitandao husika ya simu kama vile M-PAWA, M-KOBA, AIRTEL Fursa, na kadhalika.

### 12.10. KUIMARISHA UHAMASISHAJI NA MATUMIZI YA MITANDAO YA KIBIASHARA

Mahali pengi, jumuia za kijasiriamali na mitandao ya biashara zimeonesha kuwa na mafanikio makubwa sana katika kukuza maendeleo ya biashara kwa wanachama wake hata kwa wajasiriamali wengine walio nje na jumuia hizo. Katika kuongeza hamasa kwa wananchi kujiunga katika vyama vya ushirika, jumuia na mitandao ya kibiashara kwa lengo la kuwa na mahusiano endelevu ya kupashana habari na taarifa za kibiashara, serikali kupitia taasisi zake imefanya mikutano, makongamano na maonesho mbalimbali ya kuwakutanisha wadau pamoja kushirikishana uzoefu na kujadili changamoto za mazingira ya biashara ili kujenga mahusiano ya kimkakati. Uhamasishaji huo umefanyika kwa njia ngingi ikiwemo Mifuko ya Uwezeshaji ya serikali, Programu za Uwezeshaji na Vikundi vya Kiuchumi yaliyofanyika katika Kanda ya Kusini Nyanda za Juu Mwezi Oktoba, 2018 kwa lengo la kuhamsisha ukuzaji wa masoko kwa wajasiriamali na ushirikiano, makongamano na mabaraza ya biashara na uwekezaji ya mikoa na wilaya. Aidha, Maadhimisho ya Wiki ya Ujasiriamali 2018, Maonesho ya Biashara (Sabasaba), Maonesho ya Kilimo (Nanenane), pamoja na mikutano ya wadau wa sekta mbalimbali na majukwaa ya wanawake kwa pamoja vinajenga mahusiano na ushirikiano endelevu kwa wananchi.

### 12.11. MAENDELEO YA BIASHARA YA SEKTA NDOGO NA KATI

Takwimu mbalimbali zinaonesha kuwa biashara nyingi zinazoanzishwa ndani ya mwaka hufa kutokana na changamoto mbalimbali ikiwemo elimu ndogo ya ujasiriamali, ukosefu wa kumbukumbu muhimu za hesabu za biashara, kuanzishwa bila kutafitiwa, mitaji midogo, ukosefu wa masoko na mitandao imara ya biashara. Ili kujifunza ukweli wa jambo hili Taasisi ya Uimarishaji wa Sekta ya Fedha nchini (FSDT) ilifanya utafiti wa Watoa Huduma za Uendelezaji wa Biashara na Ushauri nchini kwa lengo la kuanisha mahitaji na mapungufu ya huduma za uendelezaji wa biashara yaani *Business*

*Development Services* na kutoa mapendekezo kwa serikali kuhusu uimarishaji na uratibu wa Watoa Huduma za Uendelezaji wa Biashara na Ushauri nchini.

Utafiti huo ulibaini kuwa wafanyabiashara wengi hawana ushirikiano wa ndani unaowawezesha kutatua changamoto zinazotegemeana wao kwa wao, pia biashara nyingi zimeanzishwa bila kutafitiwa hivyo hazikupata ushauri wa kibiashara. Kwa upande mwingine utafiti huo umeonesha kuwa wafanyabishara na wajasiriamali wengi hawana elimu inayojitosheleza ya biashara na ujasiriamali kutokana na utitiri wa walimu wa biashara na ujasiriamali usiokidhi viwango wanaotumia sekta isiyo rasmi kama chanzo cha kipato kwao, pia hutumia miongozo ya ufundishaji isiyo na viwango.

Katika kufanyia kazi mapendekezo ya utafiti huo ili kuimarisha uratibu wa Watoa Huduma za Uendelezaji wa Biashara na Ushauri nchini, Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kwa kushirikiana na Taasisi ya Uimarishaji wa Sekta ya Fedha nchini (FSDT) pamoja na Watoa Huduma za Uendelezaji wa Biashara na Ushauri limeandaa Kiongozi cha Kitaifa cha Mafunzo ya Ujasiriamali katika Mfumo Usio Rasmi kwa lengo la kutatua changamoto zilizobainishwa katika utafiti huo.

### 12.4.1. Utambuzi wa wafanyabiashara wadogo kwa vitambulisho

Serikali ya Awamu ya Tano, kupitia utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi 2015-2020 iliazimia kurasimisha wafanyabiashara wadogo ili waweze kutambulika kisheria na kupata leseni za biashara. Tarehe 10 Disemba, 2018 Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Joseph Pombe Magufuli alizindua vitambulisho vya biashara **670,000** kwenye mkutano wake na watendaji wa Mamlaka ya Mapato Tanzania na kuvigawa kwa kila Mkoa kwa lengo wa kuondoa kero na malalamiko ya wafanyabiashara wadogo wenye mtaji pungufu ya Shilingi milioni Nne ambao kwa muda mrefu wamekuwa wakisumbuliwa katika biashara zao kutokana na kutotambuliwa kisheria na mahali pengine wamekuwa wakitozwa kodi tofauti na maagizo.

Kufikia Aprili, 2019 vitambulisho **1,850,000** viligawiwa katika mamlaka za Mikoa na Serikali za Mitaa Tanzania Bara ambapo wajasiriamali **1,022,721** wametambuliwa tayari. Utambuzi huu unaongeza tija ya urasimishaji wa biashara nchini kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania pamoja na Halmashauri za Majiji/Manispaa/Wilaya na Miji kupitia utoaji wa Namba za Utambulisho wa Mlipa Kodi na leseni za biashara.

### 12.4.2. Taarifa za biashara na elimu za ujasiriamali nchini



Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi limekuwa likishirikiana na wadau mbalimbali kuweka mazingira rahisi ya upatikanaji wa taarifa za biashara na elimu ya ujasiriamali bure kwa lengo la kuwaunganisha wahitaji, huduma na watoa huduma mbalimbali. Vituo na tovuti za huduma za biashara na ujasiriamali vimeanzishwa katika taasisi mbalimbali za serikali pamoja na sekta binafsi kama vile Kanzidata ya Watoa

Huduma za Uendelezaji Biashara na Ushauri nchini kutoka Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC), Masoko ya bidhaa mbalimbali ndani na nje ya nchi na Kliniki ya Biashara kutoka TANTRADE, Taarifa za maeneo ya Uwekezaji kutoka TIC, Taarifa na Tafiti zinazohusu ujasiriamali nchini kutoka TPSF.

#### 12.4.3. Kanzidata ya Watoa Huduma za Uendelezaji Biashara na Ujasiriamali Nchini

Kwa miaka mingi huduma za ushauri wa kuendeleza biashara Kubwa, Ndogo na za Kati yaani "*Business Development Services*" imekuwa haifahamiki vizuri kwa wafanyabiashara, wajasiriamali na baadhi taasisi za sekta binafsi. Katika Sekta isiyo rasmi, kumekuwa na utitiri wa watoa huduma za biashara kama walimu wa ujasiriamali wasio na viwango. Walimu hao wanatoa huduma zisizokidhi mahitaji ya wajasiriamali kwa kutumia mitaala yao binafsi isiyokidhi viwango vya kitaifa vya ufundishaji wa elimu ya ujasiriamali. Ili kuimarisha uratibu wa utoaji wa huduma za biashara na ushauri nchini kutoka kwa wadau mbalimbali, Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kwa kushirikiana na Jukwaa la Watoa Huduma za Ushauri na Uendelezaji wa Biashara nchini yaani *Tanzania Forum for Business Development Service Providers* limeandaa kanzidata maalum kwa ajili ya kuwatambua watoa huduma hizo. Hadi kufikia mwezi Machi, 2019, watoa huduma **97** wamejisajili kwenye kanzidata hiyo na watoa huduma hao kutoka mikoa yote Tanzania Bara wameshiriki kutoa mapendekezo ya kuboresha Kiongozi cha Kitaifa cha Mafunzo ya Ujasiriamali katika Mfumo Usio Rasmi yaliyofanyika kikanda mwezi Oktoba – Novemba, 2018 katika mikoa ya Morogoro, Mbeya, Mwanza na Dar es Salaam. Hivyo, ni matumaini ya Baraza kuona kuwa kanzidata hii inatumika kama kiunganishi cha kuimarisha uratibu kati ya watoa huduma mbalimbali na wajasiriamali kupitia utekelezaji wa Kiongozi cha mafunzo kilichoaandaliwa.

#### 12.4.4. Lango la Taarifa za Ujasiriamali (Information Portal)

Katika kurahisisha upatikanaji wa taarifa za masoko na bei, upatikanaji wa fedha, watoa huduma mbalimbali, jinsi ya kuendesha biashara, jinsi ya kuanzisha biashara na nyinginezo, Taasisi ya Sekta Binafsi (*TPSF*) kwa kushirikiana na Taasisi ya Uimarishaji wa Sekta ya Fedha nchini (*FSDT*) imeanzisha mfumo wa taarifa kwa wajasiriamali (***Information Portal***) kwa lengo la kuhakikisha kuwa wajasiriamali wanapata taarifa sahihi zitakazowawezesha kuboresha biashara zao. Kuanzishwa kwa lango hili la taarifa kwa wafanyabiashara na wajasiriamali nchini kunaongeza kasi ya upashanaji wa habari na kupunguza gharama za mawasiliano kwa wahitaji wa taarifa mbalimbali kuhusu biashara, usafirishaji, uchukuzi na mawasiliano. Lango hilo linapatikana kwa lugha ya Kiingereza na Kiswahili kupitia https://entrepreneurs.or.tz na **wajasiriamalitz.or.tz**

#### 12.4.5. Maktaba ya Mtandaoni

Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kupitia uratibu wa tafiti mbalimbali nchini, limebaini kuwa kumekuwa na tafiti nyingi ambazo zimefanywa na serikali, wahisani, vyuo na mashirika binafsi zilizohifadhiwa kwenye Ofisi husika. Hali hii

inasababisha serikali na mashirika binafsi kutumia pesa nyingi kurudia kufanya tafiti zile zile ambazo zimeshafanyika tayari. Ili kupunguza marudio ya kazi za utafiti katika mzingira ya biashara pamoja na mambo mengine, wadau wa shughuli za utafiti kupitia Baraza walishauri kuratibu kazi za utafiti kwa kuanzisha maktaba za mtandaoni ambapo Taasisi ya Sekta Binafsi kwa kushirikiana na BEST Dialogue imeanzisha maktaba ya mtandaoni kwa lengo la kuwawezesha wafanyabiashara, wawekezaji na wajasiriamali kuweza kupata taarifa za matokeo ya tafiti mbali mbali zinazoendelea kufanyika nchini kuhusu mazingira ya biashara. **Maktaba hiyo hadi sasa ina taarifa zaidi ya elfu tatu (3,000) ambazo zimeandaliwa muhtasari kuwawezesha wananchi wa kawaida kuelewa kwa urahisi.** Maktaba hiyo inapatikana kupitia **http://businessinsightz.org/** au tovuti ya Baraza **www.neec.go.tz**

### 12.4.6. Mabaraza ya Ujuzi ya Kisekta

Katika kuinua viwango vya elimu na ujuzi kwa wananchi kupitia Mkakati wa Taifa wa Kuendeleza ujuzi, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kushirikiana Taasisi ya Sekta Binafsi na imeandaa Mradi wa Kukuza Stadi za Kazi na Ujuzi (*Education and Skills for Productive Jobs*). Mradi huo unalenga kuanzishwa kwa Mabaraza ya Ujuzi ya Kisekta ambapo sekta sita zimepewa kipaumbele za Kilimo, Utalii, TEHAMA, Ujenzi, Uchukuzi na Nishati utakaohitimishwa kwa kuanzisha Baraza la Taifa la Ujuzi nchini.

Uanzishwaji wa mabaraza haya unatokana na changamoto kubwa ya waajiri walio wengi kukosa rasilimali watu yenye ujuzi unaohitajika kutekeleza majukumu yao kwa viwango vinavyokusudiwa (*Approved of competence and Certification*). Ukosefu wa rasilimali watu wenye ujuzi wa aina hiyo unasababisha kuongezeka kwa gharama za uendeshaji wa biashara na waajiri hulazimika kutafuta wataalamu wenye ujuzi stahiki kutoka nje ya nchi au kutumia fedha nyingi katika kugharamia mafunzo kwa watumishi katika sehemu za kazi. Utekelezaji wa Mradi huo umeanza rasmi mwezi Februari, 2019 kwa kuwajengea uelewa wa pamoja wadau mbali mbali kupitia warsha na makongamano ambapo awamu ya pili ya mradi huo inahusisha kuajiri watumishi wa mabaraza ya kisekta, kutenga ofisi kwa ajili ya watumishi wa mabaraza, ununuzi wa vifaa na vitendea kazi mbalimbali vya ofisi pia kuunda na kuteua wajumbe wa mabaraza hayo.

### 12.4.7. Masuala mtambuka ya uboreshaji wa mazingira ya biashara kwa wajasiriamali

Serikali inaendelea kuchukua hatua za kimkakati kuboresha mazingira ya biashara kwa wajasiriamali na makampuni ya biashara nchini kwa kuondoa vikwazo mbalimbali. Jitihada hizo ni pamoja na kutekeleza kwa vitendo Andiko la Maboresho ya Sheria ili Kuimarisha Mazingira ya Biashara *(Blueprint for Regulatory Reforms to Improve the Business Environment)* ikiwemo utoaji wa leseni za biashara, usajili wa majina ya biashara kwa kutumia mtandao na huduma nyingine kutoka Wakala wa Usajili wa Biashara (*BRELA*), upatikanaji wa taarifa za maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya uwekezaji

(*Special Economic Zones*) kutoka Kituo cha Uwekezaji Tanzania (*TIC*) na EPZA, pia kupitia Miongozo ya Uwekezaji kwa kila Mkoa (*Investment Guides*).

### 12.4.8. Vikwazo katika Urasimishaji wa Biashara nchini

Mkakati wa Taifa wa Ujasiriamali umeainisha baadhi ya changamoto zinazosababisha mazingira ya biashara nchini kuwa magumu kiasi cha kuwafanya wajasiriamali na baadhi ya makampuni yanayoanzishwa kuona kuwa gharama za kufanya biashara ziko juu yaani "*High Cost of Doing Business"*. Changamoto hizi zinapunguza kasi ya urasimishaji wa biashara. Maeneo hayo ni kama ifuatavyo;-

| Na | KIKWAZO | HATUA ZA KUCHUKULIWA |
|---|---|---|
| 1 | Kukosekana kwa uratibu mahsusi wa kuchambua gharama za kuanzisha biashara | - Kulinganisha gharama na muda unaotumika kuanzisha biashara rasmi katika Serikali za Mitaa;<br>- Kuanzisha utaratibu wa kisheria wa kuchambua kwa mapana athari za mabadiliko ya sera na sheria kwa biashara kabla hazijapitishwa; na<br>- Kushawishi upande wa serikali kutekeleza maazimio yanayotokana na majadiliano na sekta binafsi kupitia majukwaa pamoja na mabaraza ya biashara ya Wilaya, Mkoa, Sekta na Taifa. |
| 2 | Mchakato mrefu na gharama kubwa za kuandikisha biashara, kupata leseni na vibali husika | - Kuboresha na kurahisisha taratibu za kuandikisha, kutoa leseni na kulipa kodi ikiwemo matumizi ya mtandao;<br>- Kutekeleza kwa ukamilifu na umakini Andiko la Maboresho ya Sheria ili Kuimarisha Mazingira ya Biashara *(Blueprint for Regulatory Reforms to Improve the Business Environment)* ; na<br>- Kuanzisha vituo vya huduma (One Stop-Service Centres) kwenye Serikali za Mitaa, kuweka taratibu za uandikishaji na utoaji wa leseni pamoja. |
| 3 | Kutofautiana taratibu na kukosekana uwazi na miongozo ya ulipaji kodi | - Kuondoa utaratibu wa kuanza kulipa kodi ya mapato kabla ya kuanza biashara;<br>- Kuanzisha utaratibu wa kusuluhisha migogoro ya kibiashara ambao unaweza kutumiwa na biashara ndogo na za kati; na<br>- Kuanzisha utaraibu wa kutoa elimu ya hati miliki na utatuzi wa migogoro ya kibiashara kwa njia ya usuluhishi. |
| 4 | Kutokuwepo utaratibu wa kisheria na kanuni unaotekelezeka kuzitambua biashara ndogo (Zaidi ya asilimia 90 ya biashara ndogo haziwezi kurasimishika kwa utaratibu wa kawaida | - Kuanzisha utaratibu wa kutoa elimu ya kuandikisha, kupata leseni na kutimiza masharti mengine ya kisheria ya kuendesha biashara kwa kutumia mtandao;<br>- Kuanzisha sera au utaratibu maalum wa kutoa vivutio kwa biashara kurasimishwa;<br>- Kuanzisha mfumo maalum wa kisheria kwa ajili ya kurasimisha biashara ambazo hazijafikia kiwango cha kupata leseni ya kawaida kwa mfano Vitambulisho; na<br>- Kuimarisha madawati ya uwezeshaji ya Kisekta, Mikoa na Serikali za Mitaa kuwapa elimu na kuwajengea uwezo wajasiriamali wadogo |


## 12.12. MCHANGO WA PROGRAM YA FURSA KWA WAJASIRIAMALI NCHINI

Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi limekuwa likishirikiana na wadau mbalimbali katika kuandaa na kubuni program zenye kuelimisha na kuhamasisha utekelezaji wa shughuli za uwezeshaji nchini kupitia mijadala, kampeni au makongamano maalum ya kijasiriamali kwa wananchi ikiwemo Program ya Fursa ya Clouds Media. Kupitia **Program ya Fursa 2018**, wajasiriamali wadogo zaidi ya **3,337** wamepatiwa elimu ya ujasiriamali moja kwa moja katika Mikoa ya **Morogoro**, **Iringa, Mtwara, Tanga, Mwanza, Arusha, Dodoma** na **Dar es Salaam** na wengine maelfu wamefikiwa mubashara kupitia Luninga, Redio na Mitandao ya Kijamii. Elimu hiyo ilijikita katika eneo la kuanzisha wazo bora la biashara, kutafuta masoko, usimamizi wa biashara, upatikaji wa mitaji na urasimishaji kwa kutumia vitabulisho vya biashara ndogo na leseni za biashara kupitia Ofisi za Halmashauri za Majiji/Manispaa/Miji na Wilaya.

### 12.4.1. Wanufaika wa Programu ya Fursa 2018

Katika wanufaika wa elimu ya ujasiriamali wa moja kwa moja kwa mwaka 2018 wajasiriamali **1,756** (52.47%) ni wanaume na wajasiriamali **1,586** (47.52%) ni wanawake. Mara nyingi Programu hii imekuwa ikilenga wajasiriamali vijana wenye umri kuanzia miaka 18 hadi miaka 35, lakini imeonekana kupendwa wa watu wa rika zote bila kujali umri wao kama inavyoonesha kwenye jedwali hapo chini

***Mchoro Na. 13: Mahudhurio katika Asilimia***




Zaidi ya asilimia **74** ya wajasiriamali waliofikiwa na program hii wana mitaji midogo sana na hawana biashara endelevu wakati asilimia **11.6** wana mitaji chini ya Milioni tano (5M) na asilimia **13.7** wana mitaji kati ya Milioni 5 mpaka Milioni 15.

### 12.4.2. Elimu za wanufaika wa Programu ya Fursa kwa Mwaka 2018

Kati ya wajasiriamali 3,337, wanufaika **2,906** sawa na asilimia **87.08** walitaja kiwango cha Elimu walizofikia. Wajasiriamali **799** (27.5%) walikuwa na Elimu ya Shule ya Msingi, wajasiriamali **738** (25.4%) walikuwa na Elimu ya Sekondari, wajasiriamali

**1,279** (43.9%) walikuwa na Elimu ya Chuo Kikuu, wajasiriamali **90** (3.1%) walikuwa na Elimu za Mifumo mingine na wajasiriamali **435** (13%) hawakutaja kiwango cha Elimu zao.

Kutokana na mchanaganuo wa kimaudhui katika utekelezaji wa program, zaidi ya wajasiriamali **520** wamejiajiri kwenye sekta ya kilimo, wajasiriamali **1,780** wamejiajiri katika biashara Ndogo na za Kati, wajasiriamali **365** ni waajiriwa, wajasiriamali **169** walikuwa na shughuli mchanganyiko wakati washiriki **356** hawakuwa na ajira wala biashara yeyote.

## 13.0.UBUNIFU NCHINI



### 13.1. UTANGULIZI

Mara nyingi ubunifu hutafsiriwa kama matumizi ya njia bora kutatua changamoto mpya, changamoto ambazo tayari zipo lakini hazijapatiwa ufumbuzi bado, au changamoto zilizopo kwenye soko au jamii kwa kipindi fulani. Dhana hiyo hukamilika pale ambapo bidhaa, huduma, teknolojia au njia nyingine yoyote inayoweza kutatua changamoto husika katika jamii haipatikani kirahisi.

Ubunifu unapatikana katika sekta zote ambazo zinamuhusisha binadamu na shughuli za maendeleo. Kutokana na mabadiliko ya sayansi na teknolojia, vijana wengi wamekuwa wakijitokeza na kutumia uwezo na ubunifu wa teknolojia kutafuta suluhisho la changamoto zilizopo katika jamii inayowazunguka, lengo ikiwa kujipatia kipato na kujiajiri. Nchini Tanzania tasnia ya ubunifu imekua ikikua kwa kasi kufuatia ya atamizi za ubunifu, sekta ya umma na sekta binafsi kujiunga kwa pamoja katika kuwezesha Ujasiriamali, Teknolojia na Ubunifu.

Kwenye ripoti ya Benki ya Dunia ya Mwaka 2017 ya tathmini ya ubunifu katika sayansi na teknolojia ijulikanayo kama 'Dar es Salaam ecosystem tech startup 2017' benki hiyo inasema Tanzania kuna fursa kemkem za kukuza uchumi wa taifa na kuimarisha kipato cha wananchi kwa ujumla endapo kutakuwa na mazingira rafiki kuufanikisha.

Utafiti huo uliowashirikisha wajasiriamali 221 wa jijini Dar es Salaam kati ya Julai na Septemba 2016 unaonyesha kuwa kampuni 12 za wabubifu huanzishwa kila mwaka kuanzia mwaka 2009 na nyingi ni ndogo zinazoajiri wafanyakazi wanne kila moja. Tofauti ya maendeleo kati ya nchi zinazoendelea na mataifa makubwa kiuchumi unatokana na matunizi ya teknolojia mpya inayoongeza tija katika uzalishaji ambayo pekee huchangia tofauti hiyo kati ya asilimia 70 mpaka 80.

Wabunifu katika teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) wanaelezwa kuwa muhimu katika kubuni teknolojia itakayoendana na mazingira pamoja na ufahamu wa watumiaji na kuziba pengo lililopo la maendeleo katika kuondokana na umaskini, kutengeneza ajira na kuchochea ukuaji wa uchumi wa viwanda. Dunia hivi sasa iko katika hatua ya nne ya mapinduzi ya viwanda yanayochagizwa na matumizi ya teknolojia ya dijitali. Tanzania kama sehemu ya Dunia haikwepi mapinduzi hayo na tayari matumizi ya teknolojia ya dijitali inatumika hapa nchini.

Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi katika kuratibu na kuwezesha ushiriki mpana wa watanzania kumiliki sehemu kubwa ya uchumi wao, linaguswa na mchango chanya wa tasnia ya ubunifu hasa uliojikita katika matumizi ya teknolojia na kushiriki katika kuratibu juhudi hizo.

## 13.2. MNYORORO WA THAMANI KATIKA UBUNIFU

Ubunifu unajumuisha makundi mbali mbali katika jamii ili kuweza kufikia malengo yake hasa kuwa na ubunifu endelevu na tija kwa mahitaji mapana ya kijamii.

### 13.2.1. Wadau muhimu katika tasnia ya ubunifu ni kama ifuatavyo;

(i) **Atamizi**

Inahusisha atamizi zinazosaidia mawazo ya mapya ya biashara, biashara change kupitia mafunzo, malezi na mitaji.

(ii) **Taasisi na Mashirika ya utoaji wa mitaji na ruzuku**

Hujumuisha Taasisi na Mashirika ya Umma na Binafsi yanayojihusisha na utoaji wa mitaji kama mikopo pamoja na ruzuku. Taasisi hizi ni pamoja na wadau wa maendeleo, mifuko ya uwezeshaji, wawekezaji na taasisi za fedha.

(iii) **Taasisi za Elimu**

Inajumuisha Taasisi za Elimu ya Juu nchini kama vile vyuo vikuu, vyuo vya ufundi na utafiti. Vyuo vikuu nchini kama vile Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Kikuu kishishiriki cha Iringa, Chuo Kikuu cha Dodoma na Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Mbeya, Chuo cha Nelson Mandela Arusha ni sehemu ya taasisi za elimu zilizoazisha atamizi za ubunifu.

(iv) **Wadau wa Maendeleo**

Wadau mbali mbali wa maendeleo nchini kama vile VSO ni sehemu ya washiriki katika kuanzisha atamizi za ubunifu katika programu zao mbali mbali hapa nchini.

(v) **Sekta ya Umma (Sera, Sheria na Kanuni)**

Sekta ya Umma kupitia Wizara, Idara na Taasisi zake mbali mbali zinahusika katika kuandaa sheria, sera, kanuni na miongozo mbali mbali katika kuendeleza tasnia ya ubunifu hapa nchini. Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) ndio taasisi kiongozi katika usimamizi wa tasnia ya ubunifu wa teknolojia hapa nchini.

(vi) **Makongamano, Warsha na mikutano mbali mbali**

Katika kuhamasisha tasnia ya ubunifu nchini kuwepo kwa makongamano, warsha na mikutano mbali mbali ni fursa muhimu ya kukutanisha wabunifu na wawekezaji kupitia uonyeshaji na uwasilishaji wa kazi zao. Pia ni fursa ya kukutanisha wadau mbali mbali katika kujadiliana kwa pamoja namna ya kupeleka mbele tasnia ya ubunifu wa teknolojia. Kumekuwa kukifanyika makongamano ya ubunifu wa teknolojia kama vile ‘’Sahara Sparks, kila mwaka chini ya uratibu wa COSTECH na HDIF pamoja kutokana na kuthamini ubunifu wa teknolojia, kila mwaka huandaliwa ‘Wiki Ya Ubunifu’ ambayo huwakutanisha wadau mbalimbali wa maendeleo kujadili hatua zilizopigwa katika kuendeleza

ubunifu nchini na maeneo yanayohitaji msukumo wa kipekee wa matumizi ya teknolojia na mikutano mbali mbali. Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi linafurahi kuwa mdau kutoka sekta ya umma katika kuwezesha kongamano la Sahara Sparks 2018 lililofanyika jijini Dar es Salaam lililoleta pamoja wadau na atamizi za ubunifu kupitia teknolojia kutoka nchi mbali mbali barani Afrika kupitia mwamvuli wa umoja wa atamizi za ubunifu wa teknolojia Afrika.

(vii) **Utafiti na Maendeleo**
Utafiti ni nguzo muhimu katika kuchochea maendeleo ya ubunifu kupitia teknolojia. Taasisi mbali mbali za utafiti nchini kama vile CARMATEC, SIDO, TIRDO na DIT zinajihusisha na utafiti unaochochea maendeleo ya ubunifu hapa nchini.

(viii) **Biashara zinazoanza (startups)**
Biashara changa ni sehemu ya wadau muhimu katika kukuza ubunifu wa teknolojia. Atamizi za ubunifu nchini zimekuwa zikilea biashara change kupitia mafunzo, malezi na kuunganishwa na mitaji ili ziweze kukua zaidi.

(ix) **Sekta Binafsi (Ushirikiano, Utaalamu na Uwekezaji)**
Sekta binafsi ni mdau muhimu katika kutoa ushirikiano, utalaamu na uwekezaji katika tasnia ya ubunifu wa teknolojia nchini. Makampuni ya mawasiliano ya simu kama vile Tigo, Airtel na Vodacom wameonyesha nia ya kushirikiana na tasnia ya ubunifu wa teknolojia hapa nchini na hivyo kutoa chachu ya kukua kwa sekta hiyo.

(x) **Utamaduni**
Utamaduni wa kupenda na kutumia bidhaa na huduma zinazotokana na ubunifu wa teknolojia ni nguzo muhimu ya uendelevu wa tasnia ya ubunifu wa teknolojia nchini. Mikakati mbali mbali ya kuelimisha na kuhamsisha watanzania kupenda na kutumia bidhaa na huduma zitokanazo na ubunifu wa teknolojia ni endelevu.

### 13.3. ATAMIZI ZA UBUNIFU NCHINI

Tume ya Sayansi na Teknolojia Nchini (COSTECH) kwa kushirikiana na Taasisi ya Ubunifu na Maendeleo (HDIF) walifanya tathimini ya atamizi za ubunifu nchini mwaka 2018 ili kuweza kubaini uwepo, malengo, mgawanyo wake hapa nchini na changamoto zinazozikabili. Kupitia utafiti huo ulibainisha uwepo wa atamizi za ubunifu zaidi ya 40 nchini ambazo zimeenea katika miji mbali mbali nchini huku jiji la Dar es Salaam likiwa na zaidi ya nusu ya atamizi zote za ubunifu nchini. Kutokana na utafiti huo ilionekana kuwa atamizi hizi pamoja na kutofautiana katika uendeshaji, makundi wanayolenga, huduma na mpango wa kibiashara zinaweza kupangwa katika makundi matatu kama ifuatavyo;

a) Kundi linalohusisha atamizi za zinazoendeshwa kitaalamu zikiwa na bajeti, Bodi teknolojia, mkazo katika sekta fulani na watumishi wa kudumu.

b) Atamizi ambazo zipo katika mfumo usio rasmi zinazoendeshwa na jamii ambazo zimejikita katika ujuzi, ajira, maendeleo ya watu na zikiwa na watumishi wa kujitolea.

c) Atamizi zinazoendeswa na taasisi za elimu ya juu nchini kama vyuo vikuu na taasisi za umma kama COSTECH au ambazo zimeanzishwa na wadau wa maendeleo kama sehemu ya miradi na hazina ulazima wa kuwa na watumishi wa kudumu.

d) Kupitia utafiti huo mgawanyo wa aina za uanzishwaji wa atamizi ulikuwa kama ifuatavyo;

    i. Sekta isiyo rasmi (asilimia 4)


    ii. Mradi (asilimia 35)

    iii. Asasi zisizokuwa za kiserikali (asilimia 48) na

    iv. Kampuni (asilimia 13)

Sehemu kubwa ya atamizi hizi zinalenga makundi maalumu kama vile vijana, wasichana, wana sanaa, biashara za teknolojia, kampuni za kilimo biashara na kampuni za vijana zinazokua na vijana ndio kundi kubwa zaidi.

***Mchoro Na. 14: Atamizi za Ubunifu Tanzania***




**Chanzo: Ripoti ya Tathimini ya Ubunifu Tanzania (HDIF Report 2013-2018)**

### 13.3.1. Tathimini ya atamizi za tasnia ya ubinifu nchini


***Jedwali Na. 21: Tathimini ya atamizi za tasnia ya ubunifu nchini***

| S/N | ATAMIZI | MKOA | IDADI |
|---|---|---|---|
| 1. | Elimu Lab Sengerema, EQWIP Hubs, VSO International T-LED | Mwanza | 3 |
| 2. | UDOM | Dodoma | 1 |
| 3. | Mbeya Living Lab, Mbeya University of Science and Technology | Mbeya | 2 |
| 4. | RLabs, Kiota Hub, VSO International T-LED, Mkwawa Arts | Iringa | 4 |
| 5. | VSO International T-LED | Mtwara | 1 |
| 6. | VSO International T-LED | Lindi | 1 |
| 7. | Twende, Kakute, NM-AIST,Carmatec, Obuntu Hub, Vision for Youth | Arusha | 6 |
| 8. | Anza, Kili Hub | Kilimanjaro | 2 |
| 9. | Biashara Lab TAYOA, Nafasi Arts Space, Ndoto | Dar es Salaam | 20 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | Hub, Buni Hub, Smart lab, Niwezeshe Lab,UDCTI, UDIEC, DTBI, EQWIP Hubs,Energy Change Lab, She Codes for Change, Tarebi/IMED, dlab, Jenga Hub, Sahara Accelerator, Hub 255, Seedspace,AMCET Hub, Safe Space Co. | | |
| | **JUMLA** | | **40** |

Mikoa 9 tuu kati ya 26 ndiyo ambayo tayari atamizi za ubunifu 40 zimeanza ambapo mkoa wa Dar es Salaamu ukioongoza kwa kuwa na atamizi 20 sawa na asilimia 50 ya atamizi zote. Mikoa yenye atamizi za ubunifu ni Mwanza (3), Mbeya (2), Dodoma (1), Lindi (1), Mtwara (1), Iringa (4), Arusha (6), Kilimajaro (2) na Dar es Salaam (20).

***Mchoro Na. 15: Mikoa 9 ambayo atamizi zimeanza***



### 13.3.2. Atamizi za Kisekta - Sekta ya Umma


***Jedwali Na. 22: Atamizi za kisekta – Sekta ya Umma***

| S/N | ATAMIZI | SEKTA | IDADI |
|---|---|---|---|
| **1.** | Mbeya University of Science and Technology | Umma | 1 |
| **2.** | UDCTI | Umma | 1 |
| **3.** | Nelson Mandela Institute of Science and Technology | Umma | 1 |
| **4.** | UDOM | Umma | 1 |
| **5.** | Buni Hub | Umma | 1 |
| **6.** | DTBI | Umma | 1 |
| **7.** | Camartec | Umma | 1 |
| | **Jumla** | | **7** |

### 13.3.3. Atamizi za Kisekta - Sekta Binafsi

Kutokana na mchanganuo hapo juu tuna jumla ya atamizi 40 ambazo 7 ni zinasimamiwa na taasisi za sekta ya umma. Atamizi **33** zilizobakia zinasimamiwa au kuanzishwa na sekta binafsi inayojumuisha pia mashirika ya kimataifa.

***Mchoro Na. 16: Mgawanyiko wa Atamizi za Sekta ya Umma na Binafsi***




### 13.3.4. Atamizi za Kimfumo

Pamoja na kuwepo kwa atamizi katika mikoa zinazosimamiwa na sekta za umma na binafsi, lengo kubwa la atamizi hizi ni kutengeneza majawabu wa changamoto mbali mbali za kimfumo kama vile elimu, afya, kilimo, huduma za fedha, manunuzi ya biashara nk.


## Tathimini ya Atamizi Kimfumo

***Jedwali Na. 23: Atamizi za Kimfumo***

| s/n | Atamizi | Afya | Kilimo | Elimu | Fedha | Nyingine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Elim Lab Sengerema | | | √ | | |
| 2 | Carmatec | | √ | | | √ |
| 3 | Buni Hub | | | √ | √ | √ |
| 4 | UDOM | | | √ | | √ |
| 5 | UDCTI | | √ | √ | √ | √ |
| 6 | DTBI | √ | √ | √ | √ | √ |
| 7 | Mbeya University of Science and Technology | √ | √ | √ | | √ |
| 8 | Twende | | | | | √ |
| 9 | Nelson Mandela Institute of Science and Technology | | √ | | | √ |
| 11 | Vision for Youth | | | √ | | √ |
| 12 | Obuntu Hub | | | √ | | √ |
| 13 | Kakute | | | | | √ |
| 14 | Ndoto Hub | | | √ | | √ |
| 15 | Sahara Accelerator | √ | √ | √ | √ | √ |
| 16 | Anza | | | √ | √ | √ |
| 17 | Kili Hub | | | √ | √ | √ |
| 18 | Biashara Lab Tayoa | | | | √ | √ |
| 19 | Nafasi Arts Space | | | | | √ |
| 20 | Smart lab | | √ | √ | √ | √ |
| 21 | Niwezeshe Lab | | | √ | √ | √ |
| 22 | EQWIP Hubs | | | √ | | √ |
| 23 | UDIEC | | √ | √ | √ | √ |
| 25 | Energy Change Lab | | | | | |
| 26 | She Codes for Change | | | √ | √ | √ |
| 27 | Dlab | | | | | √ |
| 28 | Tarebi/IMED | | | | | √ |
| 29 | Jenga Hub | | | | √ | √ |
| 30 | Hub 255 | | | √ | √ | √ |
| 31 | Seedspace | √ | √ | √ | √ | √ |
| 32 | AMCET Hub | √ | √ | √ | √ | √ |
| 33 | SafeSpace Co. | √ | √ | √ | √ | √ |
| 34 | VSO International T-LED | | | | | √ |
| 35 | Kiota Hub | | | | √ | √ |
| 36 | Mkwawa Arts | | √ | √ | | √ |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **37** | Rlabs | | | | | √ |
| **38** | Mbeya Living Lab | | √ | √ | √ | √ |
| **39** | TIRDO | | √ | √ | √ | √ |
| | **Total** | **6** | **14** | **24** | **19** | **35** |

***Mchoro Na. 17: Atamizi za Kimfumo***




Atamizi zimeonekana kujikita katika kutengeneza majawabu katika mifumo ya kiuchumi na kijamii kama vile Afya (6%), Kilimo (14%), Elimu (25%), Fedha (19%) na mifumo mingine (36%). Mifumo Mingine kama vile biashara, manunuzi, masoko, imekuwa inaongoza kwa kuwa na ushiriki mkubwa wa 36% ikifuatiwa na elimu 25% na fedha 19%. Kumeanza kuwa na mwitikio katika na ushiriki mzuri wa atamizi kutengeneza mifumo ya kusaidia tija katika sekta ya kilimo kwa asilimia 19. Bado mwitikio wa ushiriki wa tamizi za ubunifu ni mdogo katika sekta ya afya kwa asilimia 4.

**Chanzo**: Ripoti ya Tathimini ya Ubunifu Tanzania

### 13.4. CHANGAMOTO KATIKA TASNIA YA UBUNIFU NCHINI

Tasnia ya ubunifu wa teknolojia nchini pamoja na mafanikio yaliyopatikana bado inakabiliwa na changamoto mahususi zinazochelewesha ukuaji wake mpana kwa sehemu kubwa ya uchumi wetu. Kwa mujibu wa tafiti mbali mbali zilizofanyika kutathimini hali ya tasnia ya sekta ya ubunifu wa teknolojia nchini, changamoto zifuatazo ziliainishwa;

a) **Uendelevu**
Uendelevu wa atamizi nyingi za ubunifu wa teknolojia bado ni kikwazo kikubwa katika ukuaji wake katika kufikia malengo tarajiwa. Atamizi za ubunifu wa

teknolojia nchini hazijaweza kuwa na mipango endelevu inayoziwezesha kuwa endelevu na kudumu katika vipindi vyote vya mzunguko wa biashara.

b) **Ushirikiano**
Ushirikiano miongoni mwa atamizi ni hafifu kutokana na kila mmoja kufanya mambo yake bila kushirikiana na wadau wengine katika soko na kupelekea kuwa na marudio na matokeo hafifu ya ubunifu.

c) **Upatikanaji wa Mitaji**
Upatikanaji wa mitaji kwa ajili ya kuendeleza mawazo bora ya ubunifu ni changamoto kutokana na ukosefu wa utayari wa wadau utoaji mitaji, ruzuku na mikopo kwa atamizi za ubunifu wa teknolojia. Bado taasisi za fedha nchini hazijatoa kipaumbele kwa kuwa na bidhaa za mitaji zinazoendana na mahitaji ya atamizi za ubunifu wa teknolojia. Pia kukosekana kwa wawekezaji wa kitaasisi (Venture Capitalists) na mtu mmoja mmoja (Angel Investor) kuwekeza katika mawazo ya ubunifu hapa nchini.

d) **Ujuzi**
Changamoto ya ujuzi wa kibashara, uendelezaji wa atamizi na teknolojia bado ni kikwazo katika ukuaji wa tasnia ya ubunifu wa teknolojia hapa nchini. Juhudi kubwa inahitajika kupitia mfumo wa elimu nchini kuboresha mafunzo ya ujuzi na ujasiriamali miongoni mwa vijana walioko katika mfumo wetu wa elimu katika ngazi mbali mbali.

e) **Tafiti**
Bado tasnia ya ubunifu wa teknolojia inakabiliwa na ukosefu wa tafiti za kutosha ili kuchochea ukuaji wake. Teknolojia ni moja ya tasnia zinazokua na kubadilika kwa kasi kutokana na tafiti za mara kwa mara.

f) **Sera na Miongozo**
Sera, Sheria na Miongozo mbali mbali bado haijaakisi mahitaji ya tasnia ya ubunifu wa teknolojia ili kuchochea ukuaji wake. Mfano usajili wa biashara changa za ubunifu unapata changamoto kutokana na taratibu zilizopo kutokidhi uhalisia wake.

g) **Ushiriki finyu wa Sekta Binafsi**
Ushiriki wa sekta binafsi katika kuwekeza, kutoa utalaamu na kushirikiana na tasnia ya ubunifu wa teknolojia bado ni mdogo sana kulingana na mahitaji.

h) **Mtizamo**
Elimu ya uhamasishaji kuhusu umuhimu wa tasnia ya ubunifu wa teknolojia bado unahitajika sana ili kuchochea ushiriki mpana wa wadau mbali na wananchi katika kukuza na uendelevu wa sekta hii.

i) **Teknolojia**
Uwekezaji katika miundo mbinu ya teknolojia ni eneo muhimu katika kukuza na kuendeleza sekta ya tasnia ya ubunifu wa teknolojia hapa nchini.

j) **Mazingira kuchochea ukuaji**
Kuwepo kwa maziringira wezeshi ya kisera na kisheria katika kuchochea ukuaji wa sekta hii ni jambo muhimu sana hasa kwa kuwa na sera na sheria wezeshi za kukuza tasnia ya ubunifu wa teknolojia nchini.

k) **Miundombinu**
Uboreshaji wa miundo mbinu kama vile nishati ya uhakika, barabara, maeneo ya kufanyia shughuli za atamizi na mawasiliano ya kiteknolojia ni eneo muhimu linalohitaji kuwekewa mkazo kuiwezesha kushamiri kwa tasnia ya ubunifu wa teknolojia nchini.

l) **Upatikanaji wa Taarifa**
Upatikanaji wa taarifa kwa urahisi kuhusiana na tasnia hii ya ubunifu bado unahitaji kuboreshwa ili sehemu kubwa ya jamii iweze kuhusishwa na kushiriki kwa upana zaidi.

### 13.5. MAPENDEKEZO

Ili kuwa na uendelevu wa tasnia ya ubunifu wa teknolojia nchini, ni muhimu kutekeleza yafuatayo;

a) **Ushirikiano**
Kuimarisha ushirikiano kati ya wadau wa mnyororo wa ubunifu hapa nchini hasa kuwa na ushirikiano wa karibu kati ya atamizi mbali mbali zinazojihusisha na masuala ya ubunifu wa teknolojia hapa nchini. Kuwa na umoja rasmi wa atamizi za ubunifu wa teknolojia ni hatua muhimu ya kuboresha ushirikiano.

b) **Uendelevu**
Ni muhimu atamizi za ubunifu zikawa na mipango thabiti itakayowezesha kuwa endelevu.

c) **Mitaji**
Ni wakati mwafaka sasa kwa wawekezaji mbali mbali kutoka sekta ya umma na binafsi kuwezesha kimitaji atamizi za ubunifu wa teknolojia. Mifuko ya Uwezeshaji kuwezesha mitaji, kuwepo kwa wawekezaji wa kitaasisi (venture capitalists), angel investors na utoaji ruzuku kuchochea ukuaji wa biashara changa za ubunifu. Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi linapendekeza kuanzishwa kwa '*'National Venture Capital Fund*'' ambao utakuwa unawekeza kimitaji katika biashara changa na za kati katika tasnia ya ubunifu wa teknolojia

ili kuziwezesha kukua na kuchangia kwa kasi katika utengenezaji wa ajira na ukuaji wa uchumi.

d) **Ujuzi**
Maboresho ya mfumo wa elimu nchini kwa kuhuisha utoaji wa mafunzo unaozingatia masuala ya ujasiriamali, ubunifu na teknolojia kuanzia ngazi ya msingi, ufundi hadi elimu ya juu. Kutumika kwa Mwongozo wa Ufundishaji Ujasiriamali (NETF) kutawezesha kufikia malengo hayo.

e) **Utafiti**
Kuwekeza katika utafiti unaochochea ubunifu wa teknolojia katika kutafuta majawabu ya changamoto mbali mbali za huduma kijamii katika sekta mbali mbali kama vile afya, elimu, maji, teknolojia nk ni muhimu sana.

f) **Sera na Sheria**
Kuwa na sera rafiki na wezeshi katika kulea na kukuza biashara changa na za kati katika tasnia ya ubunifu wa teknolojia hapa nchini.

g) **Ushiriki mpana zaidi wa sekta binafsi.**
Sekta binafsi ishiriki zaidi katika kuwezesha tasnia ya ubunifu katika masuala ya utaalmu, uwekezaji na ushirikiano wenye tija na faida kwa pande zote.

# 14.0.UWEZESHAJI KWA VIJANA

## 14.1. UTANGULIZI

Takwimu za Sensa ya watu na makazi iliyofanyika mwaka **2012** inaonesha kuwa idadi ya vijana nchini inafikia jumla ya **15, 115, 987** ambayo ni sawa na asilimia **34.6** ya idadi ya wananchi wote wapatao **43, 625, 354** ambapo vijana wa kiume ni **7,096,862** na vijana wa kike **8,019,125.**

Sera ya Taifa ya Vijana inatafsiri vijana kuwa ni wenye umri wa kuanzia miaka **15-35** ambao wanawakilisha kundi kubwa la nguvu kazi nchini.

Kutokana na maendeleo ya kiuchumi na kijamii nchini ambapo serikali imewekeza nguvu kubwa katika kuwapatia vijana elimu kuanzia ngazi ya msingi mpaka vyuo vikuu bado kuna changamoto ya ukosefu wa ajira rasmi katika nyanja za Serikali na Sekta binafsi.

Serikali kupitia Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC) kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo nchini linaratibu programu mbalimbali za vijana kwa lengo la kuwawezesha kujiajiri,kutengeneza ajira kwa wengine na kuwaunganisha na fursa za mikopo yenye masharti nafuu ili kuanzisha miradi ya uzalishajimali. Miongoni mwa kazi zilizoratibiwa na kutekelezwa na Serikali ni kama zifuatazo.


### 14.1.1. Programu ya ujasiriamali kwa vijana wa elimu ya juu

Programu hii ya vijana waliomaliza elimu ya juu au ambao bado wanasoma vyuoni inatekelezwa na Baraza kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa maendeleo kutoka sekta binafsi na umma hufanyika kila mwaka tangu ilipoanzishwa mara ya kwanza katika mwaka wa fedha wa 2013/2014.

Programu hii hutoa mafunzo ya wiki nane (8) ya ujasirimali na biashara yanayojumuisha pia mafunzo ya vitendo.Vijana huandaa michanganuo ya biashara na kushindanishwa kisha mawazo bora hupewa zawadi za mbegu
Mtaji ili kuendeleza mawazo yaliyowasilishwa.

Kabla ya kufikia mwaka wa fedha wa 2018/2019 Program hii ilikuwa imefikia jumla ya vijana 134 waliopewa mafunzo ambapo kati yao vijana 30 wameunganishwa na mitaji kupitia mbegu mtaji na mikopo kutoka taasisi za fedha nchini.
Novemba 2018, Baraza kwa kushirikiana na Ubalozi wa Uholanzi liliendesha program ya mafunzo kwa vijana 50 ambapo kati yao vijana watatu walipewa mbegu mtaji.

Mshindi wa kwanza anayejishughulisha na ufugaji wa mbuzi alipewa milioni 10, mshindi wa pili anayezalisha manukato na vipodozi kwa kutumia malighafi za ndani alipewa milioni 7 na mshindi wa tatu anayetengeneza dawa za kilimo kupitia ufugaji wa sungura alipewa milioni 5.




*Washindi watatu wa shindano la Kliniki ya Ujasiriamali kwa vijana wa elimu ya juu wakiwa kwenye picha ya pamoja baada ya kupewa mbegu mtaji na Baraza la Uwezeshaji kwa kushirikiana na Ubalozi wa Uholanzi.*

### 14.1.2. Programu ya Vijana waendesha BODA BODA

Mpango huu ulianzishwa na Baraza la Taifa la Uwezeshaji katika mwaka wa fedha wa 2015/2016 ukiwa na lengo la kushawishi vijana kuanzisha vyama vya kuweka na kukopa SACCOSS ili kujenga tabia ya kuweka na kukopa.

Lengo ni kuwa na SACCOSS ya Boda Boda kila Mkoa nchini na kudhamini mikopo ya Boda Boda kupitia Mifuko ya Uwezeshaji.Mpaka sasa SACCOSS 16 za Boda Boda zimeanzishwa katika mikoa ya Dar es salaam,Kigoma, Rukwa, Mara, Arusha, Mbeya, Ruvuma, Tanga na Geita.

Mbali na kutoa ajira kwa namba kubwa ya vijana lakini kumekuwepo na changamoto nyingi za ajali za mara kwa mara ambapo hadi kufika Desemba mwaka 2018 kulikuwa na jumla ya ajali 306,610 ambazo zimesababisha vifo ni 6,529 na majeruhi ni 31,928.

Kutokana na changamoto hiyo, Baraza la Uwezeshaji lilikutana na Chama cha Wafanyakazi wa Usafirishaji kwa njia ya barabara (TAROTWU) kilichosajiliwa mwaka 2013 kujadili na kukubaliana kufanyakazi na wadau wengine ili kukabiliana na tatizo la ajali kwa kuweka mazingira mazuri ya uendeshaji wa aina hiyo ya usafiri.

TAROTWU hadi kufikia Desemba 2018 ilifanikisha kupata wawakilishi katika Mikoa 13 ya Tanzania Bara ambayo ni Arusha, Dar es salaam, Dodoma, Iringa, Mbeya, Morogoro, Mtwara, Mwanza, Lindi,Shinyanga, Tanga,Ruvuma na Pwani.Ambapo jumla ya wanachama waliofikiwa ni 3,284.

#### 14.1.3. Kijana Jiajiri

Ni program ya Vijana wenye umri wa miaka 18-35.Inatekelezwa na Taasisi ya Ushindani na Ujasirimali nchini (TECC) ambayo imeanzishwa kwa ushirikiano kati ya Baraza, Taasisi ya Sekta Binafsi na Tume ya Sayansi na Teknolojia Nchini. Programu hii imejikita katika mafunzo ya wiki 6, mpango wa malezi na kuunganishwa na mitaji katika taasisi za fedha na mifuko ya uwezeshaji nchini.

Programu hii imefanyika kwa majaribio katika mikoa ya Lindi, Mtwara, Dar es Salaam, Morogoro na Pwani.Udhamini wa program hii umefanywa na makampuni ya uchimbaji Gesi nchini, Taasisi ya Kimataifa ya Vijana ya Biashara (YBI,) Benki ya Barclays na Mastercard Foundation.

Katika awamu ya majaribio vijana waliopata mafunzo kwa Mikoa kama ifuatavyo; Dar es Salaam 60, Mtwara, 61, Lindi 61. Waliopatiwa Malezi; Mtwara 53, Lindi 42 na Dar es Salaam 56.Walezi walikuwa 23 na waliounganishwa na fursa za mitaji walikuwa vijana 48.

Hadi kufikia Desemba 2018 program ilikuwa imepanga kufikia vijana 950 ambapo maombi yaliyopokelewa yalikuwa 680 wahudhuriaji wa mafunzo walifikia idadi ya 430 ambapo vijana 97 waliopata mikopo kutoka kwenye mifuko ya uwezeshaji na kuendeleza mawazo yao.

Sambamba na hilo kuna jumla ya vijana 80 ambao walipewa mafunzo ya kusimamia mawazo ya biashara za vijana wengine ili kusaidia kukua.

Matokeo ya program nzima yamesaidia kuanzishwa kwa kampuni mpya 85 hizo ni nje ya kampuni 215 ambazo tayari zilikuwa zimeanzishwa.Vilevile program imesaidia kurasimisha biashara 100 katika maeneo ya majaribio.



Jonson Boaz kutoka Mtwara kijana mnufaika na program ya Kijana Jiajiri ambaye alijiunga tangu mwaka 2015.

**Mambo mengine yaliyotekelezwa katika Program hii ni pamoja na;**

a) Kuajiri vijana wataalamu katika masuala ya uchambuzi wa maombi ya kushiriki kwenye program za mafunzo ya ujasiriamali ambapo jumla ya vijana 38 kati ya 40 walichukuliwa.
b) Kutoa mafunzo kwa jamii za walezi kuhusiana na changamoto ambazo zinawakumba vijana kwenye ujasiriamali.Zoezi hili liliwafikia washiriki 69 ambapo asilimia 58% walikuwa wanawake.
c) Kuendesha mafunzo ya ujasiriamali kwa vijana waliochaguliwa ambapo jumla ya vijana 36 walishiriki.Asilimia 34 walikuwa tayari wana biashara zao.
d) Katika mafunzo hayo vijana 5 walianzisha kampuni mpya na 14 zilikuwa na uelekeo wa kukua.
e) Mafunzo kwa walezi wa mawazo ya vijana (mentors) yalifanyika kwa washiriki 24 ambapo 46% walikuwa wanawake.

### 14.1.4. JIANDALIE AJIRA (''VIA'')

Hii ni programu mwendelezo wa Kijana Jiajiri ya kuendeleza Vijana inayoratibiwa na Taasisi ya Ushindani na Uendelezaji Ujasiriamali (TECC) iliyojikita katika kuwaandalia vijana ajira.Utekelezaji wa program hii unashirikisha Mamlaka za Serikali za Mitaa na Watoa Huduma za Uendelezaji Biashara chini ya Udhamini wa Taasisi ya Kimataifa ya Vijana (IYF).

Programu hii imejikita katika Mafunzo ya Stadi za Biashara na za Kazi. TECC inashirikiana na IYF katika kutoa mafunzo ya wakufunzi kwa Mamlaka ya Serikali za Mitaa na SIDO kwa ajili ya kuwafundisha vijana katika maeneo mbalimbali nchini.

Programu hii inafanyika katika mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma na Mtwara.Vijana 304 waliomba kujiunga na programu hii na wakufunzi 20 wamepatiwa mafunzo ambapo wakufunzi hawa wametoka SIDO na Mamlaka ya Serikali za Mitaa katika Mikoa husika.

Vijana 195 walifaulu kujiunga na program kutoka mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma na Mtwara na wamepatiwa mafunzo ya elimu ya ujasiriamali wa usimamizi wa biashara.Kati yao ni vijana 108 walioweza kuhudhuria mafunzo.

TECC imeweza kutoa semina za ufahamu kuhusu program hii kwa taasisi washirika wa program hii 26. Taasisi washiriki ni SIDO, NEEC, TCCIA, Watoa huduma za uendelezaji biashara, IYF na Watumishi wa TECC.

#### 14.1.5. Programu za Uwezeshaji Vijana kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi Vijana Ajira na Watu wenye Ulemavu

Tangu mwaka 1997 baada ya kupitishwa kwa sera ya ajira Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeendelea kubuni mifumo ya kisheria, mazingira wezeshi ya kisera na programu kwa lengo la kutengeneza namba kubwa ya ajira kwa vijana.Miongoni mwa mambo yaliyofanyika hadi kufika hivi sasa ni kama ifuatavyo

i. **Mfuko wa Taifa wa Vijana (YDF)**.

Hii ni moja kati ya njia ambazo zimebuniwa na Serikali katika kuwezesha mitaji kwa vijana ambao wanashughulika na uzalishaji mali.Mfuko huu ulianzishwa katika mwaka wa fedha wa 1993/94 ukilenga vijana wa kuanzia miaka 15 hadi 35 ambao wanakadiriwa kufikia idadi ya milioni 16.Fedha inayotumika katika mfuko huu kwa asilimia 100 inategemea bajeti ya Serikali ambavyo ni vyanzo vya ndani.

Katika kipindi cha kuanzia mwaka 2013 hadi sasa Mfuko huu umefanikiwa kunufaisha vikundi **899** vyenye jumla ya wanachama **6293** na kufadhili miradi yenye thamani ya shilingi **5,434,641000**.

ii. **Kutenga maeneo ya Vijana**.

Katika kufanikisha uwezeshaji kwa vijana nchini, Ofisi ya Waziri Mkuu imeendelea kuratibu utengaji wa maeneo ya vijana kufanyia kazi za uzalishaji mali ili kukuza vipato vyao.

Serikali kupitia mamlaka ya Serikali za mitaa ilianzisha mpango wa kutenga maeneo mwaka 2016 na kuzitaka halmashauri zote 185 kutekeleza.Mpaka hivi sasa jumla ya ekari **217.886.36** zimetengwa kwa matumizi ya vijana.Hiyo ni tofauti na mwaka wa fedha wa 2016/2017 ambapo kulikuwa na ekari **84.037 zilizotengwa.**

#### 14.1.6. Halmashauri kutenga mafungu ya vijana

Serikali kupitia halmashauri zake imendelea na mpango wa kutenga mafungu ya fedha kwa ajili ya kukopesha vijana wazalishaji mali.Katika mwaka wa fedha wa

**2016/17 zilitengwa Shilingi 5,164,698,256 ambazo ni sawa na asilimia tano ya mapato yote kwenye ngazi za halmashauri. Mgawanyo huo ni kwa vikundi 3,918** vya vijana.Hivi sasa Halmashauri zinapaswa kutenga asilimia 4 kwa vijana,asilimia 4 kwa wanawake na asilimia 2 kwa watu wanaoishi na ulemavu.

#### 14.1.7. Uwezeshaji vijana kupitia vituo vya ubunifu

Serikali imeanisha vituo vya malezi ya vijana wenye mawazo ya ubunifu na kuwaunganisha na fursa za mitaji baada ya mawazo yao kuonesha dalili za kukua katika kipindi cha malezi.Miongoni mwa vituo hivyo kwa Taifa zima ni pamoja na COSTECH, DATA LAB, VETA na vyuo vingine vya ufundi.

#### 14.1.8. Uwezeshaji wa vijana kupitia uanzishwaji wa Makampuni

Mpango huu unashawishi vijana kuanzisha makampuni binafsi ambayo yanaweza kutengeneza ajira kwao na kwa vijana wengine.Baada ya kufungua makampuni hayo wanaunganishwa na taasisi za kifedha kama Mabeki na mifuko ya Serikali kupata mikopo.

#### 14.1.9. Uwezeshaji kupitia mafunzo ya ujuzi

Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu imeendelea na program za kukuza ujuzi kwa vijana na kurasimisha ujuzi uliopatikana kwa mfumo usio rasmi kupitia mashirikiano na taasisi mbalimbali za Umma na sekta binafsi.

Katika moja ya njia zilizotumika kufanikisha ujuzi ni Serikali kuingia mikataba ya kutoa mafunzo kupitia miradi ya fundi stadi kwa Vijana unaotekelezwa kupitia chuo cha ufundi stadi DONBOSCO kwa ufadhili wa Ofisi ya Waziri.

Katika kurasimisha ujuzi uliopatikana kwa mfumo usio rasmi OWM-KVAU imeingia mkataba na VETA wa kurasimisha ujuzi wa vijana katika fani za ujenzi, uashi na useremala.

### 14.2. MCHANGO WA ASASI ZA KIRAIA KWA VIJANA

Pamoja na mchango wa Serikali katika kusaidia vijana kujikwamua Kiuchumi, Mashirka yasiyokuwa ya Kiserikali yamekuwa na mchango mkubwa katika kuunga mkono jitihaha za uwezeshaji kupitia program za mafunzo na kujengeana uwezo baina ya vijana kwa vijana na kusaidia kubuni miradi ya uzalishajimali ili kuboresha vipato vyao.

Tanzania Youth Coalition ni mtandao unaounganisha mashirika yasiyo ya kiserikali zaidi ya 120 na vikundi 249 vya ujasiriamali kwa lengo la kujengeana uwezo kupitia mijadala ya kubadilishana mawazo na kupeana mafunzo.

Mtandao huu kwa kiasi kikubwa unalenga masuala ya Afya na usawa wa kijinsia kwa vijana, Demokrasia na uongozi kwa vijana,uhusiano wa Kimataifa ili kujengeana uwezo

katika mambo ya Kiuchumi na kubadilishana mawazo kwa shabaha ya kuchochea maendeleo.

Mpaka kufika Desemba 2018, Mtandao huu umeweza kufikia jumla ya vituo 107 vya vijana vilivyopo kwenye Mikoa ya Tanzania Bara ikiwemo Morogoro, Dar es salaam, Mara, Pwani, Njombe, Singida, Tabora, Kagera, Kilimanjaro, Arusha, Tanga na Mwanza kwa lengo la kutoa elimu juu ya umuhimu wa kujengeana uwezo kupitia njia ya mabadilishano ya kufanya kazi kwa kujitolea (Exchange Program) ambayo imekuwa ikifanyika kati ya Tanzania na Ujerumani.

Katika kipindi cha Agosti 2 mpaka 4 mwaka 2018 jijini Dar es salaam TYC ilikutanisha wadau wa vijana kutoka katika taasisi 17 zinazoshughulika na sanaa, michezo na burudani kujadiliana kuhusu umuhimu wa mpango wa mabadilishano ya vijana kati ya Tanzania na Ujerumani kwa lengo la kujifunza kupitia kazi za kujitolea.

Kongamano lililenga kukutanisha wadau kutoka Ujerumani na Tanzania kwa lengo la kupata njia nzuri itakayonufaisha namba kubwa ya vijana kupitia mpango wa mabadilishano na kazi za kujitolea.

Januari 16 hadi 17 mwaka 2019 mjini Dodoma TYC ilikutanisha wadau 58 kutoka katika Taasisi binafsi na Umma ambazo zimetoa nafasi kwa vijana kujifunza kazi kwa njia ya vitendo na kushirikishana uzoefu juu ya kupata njia bora za kuendeleza mfumo huo.

Mkutano huo ambao ulihudhuriwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Mheshimiwa Jensita Mhagama ulitoa nafasi kwa vijana wanaofanya kazi za kujitolea kushirikisha uzoefu wao.

# 15.0. UWEZESHAJI WA WANAWAKE KIUCHUMI

## 15.1. UTANGULIZI

Baraza la uwezeshaji wananchi kiuchumi linasimamia utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kwa kuwaongoza watanzania kwenye uchumi imara kwa kuhakikisha mazingira mazuri ya biashara na uchumi shirikishi. Utekelezaji wa shughuli zake unafanya kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali ikiwemo Tawala za Mikoa na Serikali za mitaa.

Katika kufikia malengo ya maendeleo endelevu ya kiuchumi, Wanawake bado wamekuwa nyuma katika kupata fursa za kutosha za kiuchumi hapa nchini na hata duniani kote. Takribani asilimia 60 ya wanawake wa kitanzania bado wanaishi katika umaskini uliokithiri. Wanawake wanaendelea kubeba mzigo mzito kutokana na kutokuwa na Usawa katika fursa, uwezo wa kupata mitaji, ajira na hata elimu.

Uwezeshaji wa wanawake kiuchumi ni muhimu kwani unasaidia kuondoa umaskini katika jamii kwani mchango wa mwanamke katika familia ni muhimu ili kuleta uhakika wa kuishi kwa mwanamke mwenyewe, wanaume, wasichana na wavulana. Pia ni muhimu katika kuleta usawa katika jamii. Usawa wa kijinsia hauwezi kufikiwa kama wanawake wataendelea kuwa na haki finyu za kiuchumi, kutomiliki mali na kutopata fursa za kiuchumi kama wanaume.

Lengo mojawapo la Baraza ni Kuwezesha Wanawake Kiuchumi ili kupunguza au uondoa pengo kubwa ambalo limejengeka na pia kuongeza ushiriki wa wanawake katika uchumi. Uwezeshaji wa Wanawake Kiuchumi ni muhimu kwa kuhakikisha malengo ya 50/50 ya dunia kufikia mwaka 2030.

## 15.2. UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA UWEZESHAJI WANAWAKE KIUCHUMI

Serikali imeendelea kujikita katika kuwezesha wanawake kuinuka kiuchumi kwa kutekeleza program mbalimbali kupitia Wizara, halmashauri, mabaraza mbalimbali na taasisi za Serikali. Serikali kupitia SIDO imeendelea kuratibu mfuko wa wafanyabiashara wananchi NEDF na kufanikiwa kutoa jumla ya mikopo yenye thamani ya Shilingi **Bilioni 1.74** ambapo mikopo **520** yenye thamani ya Shilingi **milioni 788** kwa wanawake.

Kwa kuzingatia tatizo la upatikanani wa maji vijijini ambalo limekuwa likiwakabili hasa wanawake kwa kuwa ndio walezi wakuu wa familia na hata kusababisha wasichana kukosa muda wa kujipambanua kielimu kutokana na kupoteza muda mrefu kusaka maji kwa ajili ya jamii. Serikali kupitia sera ya Taifa ya Maji ya Mwaka 2002 imetelekeza kwa kujenga miradi ya maji sehemu mbalimbali nchini. Hadi Februari 2019, jumla ya **miradi 65** ya maji vijijini ilikamilishwa ambapo wananchi **milioni 25.36** waishio vijijini wamenufaika na kufanya hali ya upatikanaji wa maji vijijini kuongezeka kutoka **58.7%** julai 2018 na kufikia **64.8%** Februari 2019. Hii inawapa wanawake na wasichana

kutumia muda wao kufanya majukumu mengine ya kiuchumi na vilevile vijana wa kike kupata muda wa kujiendeleza kielimu.

Wanawake ni zaidi ya asilimia 50 ya wananchi wote nchini Tanzania na asilimia kubwa wapo katika ajira au mfumo wa biashara usio rasmi wakijihusisha na kubuni bidhaa mbalimbali na biashara katika vikundi au mtu mmoja mmoja hivyo kufanya idadi kubwa ya wanawake kuwa wajasiriamali. Kwa kutambua umuhimu na mchango wa wajasiriamali wadogo nchini katika kuchagia pato la Taifa na kukuza Uchumi, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alitoa vitambulisho 670,000 kwa ajili ya wajasiriamali wadogo ili viweze kuwapa nafasi huru ya kufanya biashara zao na kufikia malengo yao kimaisha na kuweza kuwa na mitaji mikubwa ya kuwawezesha kuanza kulipa kodi. Hadi kufikia 10 machi 2019, jumla ya vitambulisho **496,221** sawa na **asilimia 74** vimegawiwa kwa wajasiriamali na hii imepawa wanawake nafasi ya kuweza kufanya biashara zao katika maeneo mbalimbali nchini na kuweza kujipatia kipato.

Halmashauri mbalimbali kwa kushirikiana na wadau wa uwezeshaji nchini zimefanikiwa kutoa mafunzo kwa vijana na wanawake katika nyanja mbalimbali za maendeleo. Vitengo mbalimbali ya halmashauri kama vitengo vya biashara vimefanya kazi ya uhamasishaji wa urasimishaji wa biashara na utunzaji wa kumbukumbu za biashara. Pia miradi mbalimbali imeanzishwa kupitia vikundi vyao vya kijasiriamali na kusaidia kupata mikopo kwenye vikundi kupitia mifuko mbalimbali ya kifedha.

Halmashauri ya wilaya ya kilolo, kwa kushirikiana na mdau wa IOP (Ilula Orphanage Program) pamoja na SIDO wamefanikiwa kuwajengea uwezo wanavikundi wa Vicoba kwa kuwapa ujuzi wa kutengeneza dawa za wadudu wa mashambani, mbolea za asili za maji na za kuvundika ambazo ndizo wanatumia katika bustani zao na mashamba yao hadi sasa pia wamepata ujuzi wa kusindika nyanya na kutengeneza Juisi za nyanya pamoja mvinyo wa asili. Wanachama 477 walionufaika ambapo 385 ni wanawake

Wadau mbalimbali wa Asasi za Kiraia wameendelea kushirikiana na Serikali kuleta matokeo chanya ya utekelezaji wa uwezeshaji wa wanawake kiuchumi nchini ili kuwanyanyua wanawake kutoka katika hali ya kuwa tegemezi, kuanza kujitegemea na kukua kiuchumi. Zimefanikiwa kutoa mafunzo na taarifa mbalimbali kupitia madarasa na makongamano mbalimbali ambayo yamekuwa na mafanikio makubwa.


Taasisi ya Girl of Fire Foundation kupitia program yake ya Mwanamke Tajiri Project imefanikiwa kufikia wanawake zaid ya **2,000** na kuwapa mafunzo ya ujasiriamali kukuza biashara zao, kujenga tabia ya uwekezaji kama njia ya kukua kiuchumi. Pia imezindua programu kwa ajili ya vijana wa kike waliopo vyuoni na waliomaliza ili kuwajengea kujiamini na kujitambua malengo yao katika maisha na jinsi gani wanaweza kujiajiri, wanafunzi zaidi ya **200** kutoka vyuo mbalimbali Dar es Salaam wamefanikiwa kupata mafunzo haya.

Vilevile Taasisi ya Purple Planet kupitia program yake endelevu ya mafunzo na ushauri inayojulikana kama MWANAMKE SAHIHI imefanikiwa kufikia wanawake zaidi ya **3000** na kupitia makongamano na semina mbalimbali katika mikoa ya Pwani, Morogoro, Tanga, Mwanza, Dodoma na Kilimanjaro wamefanikiwa kufikia wanawake **6000**. Wamefanikiwa kutoa malkia wa nguvu watatu kwa mwaka 2019 katika vipengele vya Kilimo Biashara na Biashara za Rejareja na kusaidia kuanzishwa kwa taasisi zingine za kijamii. Juhudi zao zimeleta mabadiliko katika maisha ya wanawake wengi na kuvumbua vipaji mbalimbali, kujiajiri na pia kuepuka unyanyasaji wa kijinsia.

### 15.3. MAREKEBISHO YA SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA YA MWAKA 2018

Serikali imefanya marekebisho ya Sheria ya Fedha za serikali za Mitaa, sura 290 kifungu cha 37A ya Mwaka 2018 ambayo imeelekeza kwamba mikopo yote inayotoka na asilimia 10 ya mapato ya ndani ya Halmashauri sasa inatolewa bila riba kuanzia Julai, 2018. Hadi kufikia Februari 2019, Jumla ya **shilingi bilioni 13.2** kati ya **shilingi bilioni 54.08** sawa na asilimia 24.4 zimetolewa kama mkopo kwa vikundi **5,628** kati ya vikundi **28,028** vya wanawake, Vijana na watu wenye ulemavu. Kati ya fedha hizo **Shilingi bilioni 8.04** zimetolewa kwa vikundi **3,835** vya wanawake ambayo ni sawa na **asilimia 68** ya vikundi vyote.

Marekebisho haya yamewapa nafasi kubwa wanawake kupata kipato bila masharti magumu kupitia mikopo hii na kuweza kuanzisha miradi na kuendeleza miradi yao kwa maendeleo yao binafsi, familia, jamii na taifa kwa ujumla.




### 15.4. USHIRIKI WA WAJASIRIAMALI WANAWAKE KATIKA MANUNUZI YA SERIKALI

Serikali kwa kutambua umuhimu wa makundi maalum na mchango wake katika maendeleo ya nchi, ilifanya mabadiliko katika sheria ya manunuzi ya umma na kuelekeza asilimia 30 ya manunuzi ya Umma kutengwa kwa ajili ya wajasiriamali walio kwenye makundi maalum wakiwemo wanawake.

Ushirikishwaji wa wanawake katika manunuzi ya Umma ni muhimu katika ustawi wa jamii na kukuza uchumi wa nchi. Kwa kuzingatia haya, Serikali imeendelea kufanya

jitihada mbalimbali za kuhakikisha kuwa mazingira rafiki yanakuwepo na kuwawezesha wanawake kushiriki katika zabuni za Umma. Baraza la Uwezeshaji wananchi kiuchumi kwa kushirikiana na PPRA wameandaa mwongozo mahsusi unaolenga kuongeza ushirikishwaji wa makundi maalum ya kijamii wakiwapo wanawake katika zabuni za Umma na tayari muongozo umeshirikishwa kwa wanunzi wote wa serikali na kuanza kuutekeleza vile vile mafunzo mbalimbali yanafanyika ili kuwajengea uwezo wanawake wa kuweza kushiriki kikamilifu katika fursa hii.

### 15.5. HITIMISHO

Uwezeshaji wa wanawake kiuchumi ni jambo la msingi kwani linaleta usawa kati ya wanaume na wanawake. Jitihada hizi za uwezeshaji zinasababisha kupungua kwa unyanyasaji na udhaifu wa wanawake na vile vile kusaidia kuwezesha wanawake kushiriki vema na kunufaika na manufaa ya fursa za kiuchumi na kujenga mafanikio kwa ajili yao binafsi, familia, jamii na nchi kwa ujumla

# 16.0. MANUNUZI YA UMMA

## 16.1. UTANGULIZI

Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC) limefanya jitihada kubwa kwa kushirikiana na Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma (PPRA) kwa karibu sana ili kuwawezesha Watanzania wengi kushiriki kikamilifu katika manunuzi ya umma. Aidha, Baraza na Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma (PPRA) walisaini makubaliano ya utekelezaji wa kuwashirikisha Watanzania wengi zaidi katika manunuzi ya umma ikiwa ni sambamba na kuunga mkono juhudi za dhati za serikali za kuongeza ushiriki wa makampuni ya wazawa na Watanzania wenye kipato cha chini katika mchakato wa manunuzi ya umma.




## 16.2. MWONGOZO WA USHIRIKI WA MAKUNDI MAALUM KATIKA MANUNUZI YA UMMA

Ushiriki wa Vijana, Wanawake, Wazee na Watu wenye Ulemavu kama makundi maalum ya kijamii katika manunuzi ya umma umeonekana kuwa na mchango mkubwa katika ukuaji wa uchumi wa nchi endapo utasimamiwa vizuri. Baada ya kuona umuhimu wa ushiriki wa makundi maalum katika manunuzi ya umma, Mamlaka ya Ununuzi wa Umma kupitia Sheria yake ya manunuzi ya Umma ya mwaka 2011 na marekebisho yake ya mwaka 2016 ilitoa upendeleo kwa makundi maalum katika jamii.

Aidha, Baraza kama chombo cha juu cha Serikali kinachosimamia na kutathmini utekelezaji wa mambo mbalimbali yanayolenga kuwawezesha Wananchi kiuchumi yakiwemo makundi maalum ya kijamii linatambua utekelezaji huu wa Mamlaka kutayarisha na kuandaa mwongozo utakaosimamia na kutoa fursa za upendeleo kwa makundi maalum ya kijamii ili waweze kushiriki kikamilifu katika manunuzi ya umma kama utekelezaji wa Makubaliano.

Kutokana na marekebisho ya sheria hii, Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma ilitayarisha Mwongozo wa kuyawezesha makundi maalum katika jamii (Wanawake, Vijana, Wazee na Watu wenye Ulemavu) kushiriki kikamilifu katika shughuli mbalimbali za manunuzi ya umma. Aidha, Mwongozo umezielekeza taasisi zote za umma zinazofanya manunuzi kuhakikisha zinatenga asilimia thelasini (30%) ya manunuzi ya umma kwa makundi maalum katika jamii ili kutanua wigo na kuongeza fursa za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi. Vilevile Mwongozo umeainisha mgawanyo wa manunuzi ya umma kwa kada zote za makundi maalum ya kijamii kama ifuatavyo;

Vijana asilimia kumi (10%), Wanawake asilimia tano (5%), Wazee asilimia tano (5%) na Watu wenye Ulemavu asilimia (10%) ya Manunuzi ya Umma.

## 16.3. MADHUMUNI NA MALENGO YA MWONGOZO

### 16.3.1. Lengo Kuu

Lengo kuu la mwongozo ni kusimamia taasisi za umma na makundi maalum juu ya utekelezaji wa Sheria ya Manunuzi ya Umma na Kanuni zake ili kuongeza Ushiriki wa makundi maalum katika manunuzi ya Umma.

### 16.3.2. Malengo Maalum Ya Mwongozo

a) Kutoa uelewa na kurahisisha taratibu zinazoongoza mipango ya kutoa upendeleo kwa makundi maalum ya kijamii.

b) Kusaidia makundi maalum kuandaa, kupanga na kuwasilisha mipango ya zabuni zitakozokuwa zimekidhi matakwa ya zabuni husika kama yalivyoainishwa kwenye makabrasha ya zabuni

c) Kuhamasisha taasisi za umma kuzingatia mpango wa mahitaji na upendeleo uliowekwa kwenye sheria ya manunuzi ya umma

d) Kuhamasisha na kuwezesha kujenga uwezo wa Vikundi maalum juu ya Ununuzi wa Umma

e) Kuweka wazi majukumu ya wahusika katika mipango hii ya upendeleo kwa Vikundi maalum.

## 16.4. UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA UWEZESHAJI KWENYE MANUNUZI YA UMMA

### 16.4.1. Uendelezaji wa nyenzo au vigezo vya kutathmini utekelezaji

Mamlaka ya Ununuzi wa Umma imeandaa nyenzo au vigezo maalum vitakavyotumika kutathmini utekelezaji wa utolewaji wa Zabuni za Serikali kwa kuzingatia vipaumbele kwa kampuni za ndani na makundi maalum (Vijana, Wanawake, Wazee na Watu wenye Ulemavu) katika shughuli za ununuzi wa umma.

### 16.4.2. Kujenga uwezo watanzania

Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma (PPRA) kwa kushirikiana na Baraza pamoja na Chemba ya Wafanyabiashara Wanawake (TWCC) waliandaa Warsha ambayo ililenga kuwajengea uwezo Wanawake Wajasiriamali hapa nchini juu ya ushiriki wao katika shughuli za manunuzi ya umma, Warsha hiyo ilihudhuriwa na Wanawake 34. Utaratibu huu uliwekwa mahsusi ili kufanikisha utekelezaji wa programu mbalimbali za

kuwajengea uwezo Wanawake, Vijana, Wazee na Watu wenye Ulemavu ili waweze kushiriki kikamilifu katika shughuli mbalimbali za manunuzi ya umma.

#### 16.4.3. Mipango ya PPRA

Mamlaka itatoa taarifa kamili kuhusu ushiriki wa watanzania katika Manunuzi ya Umma mara baada ya kukamilisha tathmini baada ya mwaka wa fedha 2018/19 kumalizika. Aidha, taasisi 5 za juu ambazo zimezingatia mahitaji katika kufanya manunuzi kutoka kwa makampuni ya ndani na makundi maalum ya kijamii zitatambuliwa rasmi na Mamlaka.

### 16.5. MFUMO WA MANUNUZI KWA NJIA YA MTANDAO "TANePS"

Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (*PPRA*), imeanza majaribio ya mfumo kamili wa manunuzi ya umma kwa njia ya mtandao. Hii ni kufuatia kukamilika kwa utayarishaji wa mfumo huo ulioanza zaidi ya mwaka mmoja uliopita. Mfumo huu, unaojulikana kwa jina la *TANePS* – yaani "*Tanzania National e-Procurement System*", na kupatikana kwenye anwani ya *www.taneps.go.tz*, unao uwezo wa kuwezesha hatua mbalilmbali za manunuzi kufanyika, kuanzia utayarishaji wa mpango wa manunuzi hadi usimamizi wa mikataba.

Katika hatua ya kwanza mambo yafuatayo yatatekelezwa:

a) Mamlaka imefanya majaribio ya mfumo wa *TANePS* kwa awamu kwa mujibu wa Kanuni ya 342(1); kwenye taasisi 100 za umma kwenye manunuzi ya bidhaa na huduma mtambuka, madawa na vifaa tiba.
b) Mafunzo kwa taasisi za majaribio yamefanyika, Mamlaka imeendelea kutoa mafunzo na semina mbalimbali kuhusu mfumo na taarifa zaidi zinapatikana kwenye tovuti ya mfumo ambayo ni *www.taneps.go.tz*, tovuti ya mamlaka PPRA ambayo ni *www.ppra.go.tz* na Jarida la manunuzi la kila wiki.

c) Mfumo ulikuwa wazi kuanzia Machi, 2018 kwa wafanyabiashara kuanza kujisajili, hususani wale wenye kuhusika na manunuzi chini ya mikataba ya muda (***framework agreements***). Aidha, kabla ya kujisajili Mamlaka iliweka utaratibu kwa Wazabuni kuangalia miongozo (***Training Video na Manuals***) ili kuweza kujua mahitaji ya usajili na uwezo wa mfumo wenyewe.

d) Mamlaka iliendesha zoezi la kuwasajili wazabuni katika mfumo wa Ununuzi wa umma kwa njia ya mtandao ***Tanzania National Electronic Procurement System*** (*TANePS*) zoezi hili lilifanyika mkoani Dar es Salaam. Pia mzabuni anaweza kujisajili moja kwa moja kwenye tovuti ya mfumo kupitia *www.taneps.go.tz*

## 17.0.UWEZESHAJI KATIKA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA




## UTANGULIZI

### 17.1. MKAKATI WA TAIFA WA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI

Katika utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ya mwaka 2004, Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi liliandaa Mkakati wa Taifa wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na mwongozo wake ili kuongoza utekelezaji wa sera kwa vitendo kupitia wadau wengi. Utekelezaji wa mkakati huo unafanywa na wizara na taasisi zake, Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa katika ngazi zote, Sekta Binafsi pamoja na wadau wa Maendeleo ambapo kilele cha utekelezaji wa shughuli za uwezeshaji ni **Kongamano la Kitaifa la kila Mwaka la Uwezeshaji**.

Utekelezaji wa shughuli mbalimbali za uwezeshaji kutoka kwa wadau unaratibiwa na kamati sita za kitaalam za kisekta ambazo ni **i) Kamati ya Mifuko ya Uwezeshaji na Dhamana, ii) Kamati ya Vikundi vya Kiuchumi, iii) Kamati ya Uratibu wa Uwezeshaji Sekta ya Umma, iv) Kamati ya Ushiriki wa Watanzania kwenye Uwekezaji v) Kamati ya Taifa ya Ujasiriamali** na **vi) Kamati ya Utafiti**. Aidha, utekelezaji wa shughuli hizo kuanzia ngazi ya taifa hadi kwenye familia unafanyika kupitia mifumo ya kiutendaji iliyopo katika wizara, taasisi na mamlaka mbalimbali za serikali kupitia madawati ya uwezeshaji yanayoratibiwa na maafisa mbalimbali wa serikali kama Waratibu wa Uwezeshaji yaani "*Empowerment Coordinators*".




Katika kipindi cha kuanzia Julai, 2018 mpaka Machi, 2019, mambo yafuatayo ya uratibu wa shughuli za uwezeshaji katika Mikoa na Halmashauri nchini yametekelezwa:

### 17.2. PROGRAMU ZA UWEZESHAJI NA UBUNIFU

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imekuwa ikichukua hatua za makusudi kubuni na kuanzisha program mbalimbali za uwezeshaji wananchi kiuchumi kupitia wizara na taasisi zake. Utekelezaji wa program hizo hufanywa na taasisi husika kwa kufuata taratibu na miongozo iliyopo ambapo Baraza huratibu taarifa za utekelezaji wa program hizo.

Kupitia OR-TAMISEMI, Mwongozo wa utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi katika **ukurasa wa 21 hadi 26 umefafanua majukumu ya kamati** zenye dhamana ya kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa shughuli za uwezeshaji wananchi katika **Mikoa, Halmashauri, Kata na Vijiji/Mitaa**. Mojawapo ya majukumu hayo ni kubuni program za uwezeshaji na kutenga fedha za utekelezaji wa program hizo.




Kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2018/2019, Mikoa na Halmashauri zimetenga jumla ya shilingi **54,084,460,371.23** ya mapato yake ya ndani kwa ajili ya uwezeshaji wa makundi maalum. Hadi kufikia mwezi Machi, 2019 kiasi cha shilingi **7,401,034,836** zimetolewa kwa Vijana, shilingi **11,474,211,371** kwa Wanawake na shilingi **2,102,654,045** kwa Watu wenye ulemavu ambapo kwa asilimia **38.7** zimenufaisha zaidi ya vikundi **8,000** vya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu. Miongoni mwa wanufaika hao ni vikundi **2,361** vya vijana, **5,057** vya wanawake na **582** vya watu wenye ulemavu kama inavyoonesha kwenye jedwali hapo chini.

***Jedwali Na. 24: Wanufaika (Makundi Maalum) wa program za uwezeshaji kimkoa***

| Na. | Jina la Mkoa | Makisio 10% 2018/2019 | Fedha zilizotolewa Hadi kufika Februari, 2019 | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Wanawake | Vijana | Wenye Ulemavu | Jumla Kuu |
| 1 | Katavi | 785,906,062 | 108,600,000 | 83,555,750 | 21,000,000 | 213,155,750 |
| 2 | Simiyu | 1,353,820,755 | 89,019,802 | 50,694,651 | 56,573,255 | 196,287,708 |
| 3 | Njombe | 1,000,188,111 | 273,454,000 | 303,224,000 | 62,027,000 | 638,705,000 |
| 4 | Geita | 1,271,195,150 | 345,051,244 | 265,150,533 | 72,350,178 | 682,551,955 |
| 5 | Arusha | 2,536,292,396 | 1,417,880,000 | 1,677,250,000 | 481,500,000 | 3,576,630,000 |
| 6 | Pwani | 2,523,371,397 | 413,556,280 | 354,936,952 | 112,019,883 | 880,513,114 |
| 7 | Dodoma | 3,572,751,688 | 1,230,930,000 | 572,430,000 | 49,930,000 | 1,853,290,000 |
| 8 | Iringa | 1,534,158,920 | 291,862,750 | 218,862,750 | 42,901,375 | 553,626,875 |
| 9 | Kigoma | 909,903,845 | 95,400,000 | 29,300,000 | 2,409,000 | 127,109,000 |
| 10 | Kilimanjaro | 1,382,499,683 | 733,624,000 | 180,500,000 | 12,000,000 | 926,124,000 |
| 11 | Lindi | 1,352,535,338 | 202,580,000 | 425,900,000 | 70,680,000 | 699,160,000 |
| 12 | Mara | 1,463,185,355 | 238,200,000 | 196,160,000 | 51,900,000 | 486,260,000 |
| 13 | Mbeya | 2,340,574,781 | 417,239,000 | 31,541,000 | 364,900,000 | 813,680,000 |
| 14 | Songwe | 767,437,482 | 149,400,000 | 153,000,000 | 23,000,000 | 325,400,000 |
| 15 | Morogoro | 2,686,948,588 | 368,418,774 | 227,779,774 | 86,464,004 | 682,662,552 |
| 16 | Mtwara | 1,876,916,552 | 54,300,000 | 100,004,000 | 24,226,000 | 178,530,000 |


| Na. | Jina la Mkoa | Makisio 10% 2018/2019 | Fedha zilizotolewa Hadi kufika Februari, 2019 | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | **Wanawake** | **Vijana** | **Wenye Ulemavu** | **Jumla Kuu** |
| **17** | Mwanza | 3,162,752,338 | 495,302,224 | 330,802,224 | 107,301,112 | 933,405,560 |
| **18** | Ruvuma | 1,007,420,198 | 162,121,808 | 150,903,400 | 66,382,000 | 379,407,208 |
| **19** | Shinyanga | 1,534,471,585 | 329,000,000 | 238,211,000 | 24,333,200 | 591,544,200 |
| **20** | Singida | 1,067,238,924 | 100,400,000 | 77,000,000 | 17,000,000 | 194,400,000 |
| **21** | Tabora | 1,875,373,871 | 346,552,129 | 279,102,129 | 45,563,564 | 671,217,822 |
| **22** | Tanga | 2,497,116,878 | 437,600,000 | 205,260,000 | 43,600,000 | 686,460,000 |
| **23** | Kagera | 1,364,878,888 | 334,415,070 | 215,220,726 | 88,471,449 | 638,107,244 |
| **24** | Dar Es Salaam | 12,331,746,683 | 2,487,604,267 | 841,237,471 | 89,000,000 | 3,417,841,738 |
| **25** | Rukwa | 679,922,382 | 137,578,000 | 70,697,000 | 7,500,000 | 215,775,000 |
| **26** | Manyara | 1,205,852,522 | 214,122,024 | 122,311,477 | 79,622,024 | 416,055,526 |
| | **Jumla Kuu** | **54,084,460,371** | **11,474,211,371** | **7,401,034,836** | **2,102,654,045** | **20,977,900,252** |

(*Chanzo: OR-TAMISEMI*)

Katika fedha zilizotengwa kwa ajili ya uwezeshaji wa Vijana, Wanawake na Watu Wenye Ulemavu Mikoa ya **Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Kilimanjaro, Pwani** na **Mwanza** imetoa fedha nyingi kama inavyoonekana katika jedwali hapo chini. Aidha Mkoa wa **Arusha** umevuka malengo kwa kutoa Shilingi **3,576,630,000** sawa na asilimia **141** ya Shilingi **2,536,292,396** katika fedha zilizotengwa kutoka vyanzo vya ndani vya mapato.


jedwali hilo hapo juu linaweza kuelezwa vizuri zaidi kwa mchoro hapa chini.

***Mchoro Na. 18: Fedha zilizotolewa Hadi kufika Februari, 2019***




Mpaka Machi, 2019 takwimu za matokeo ya shughuli za uwezeshaji wa makundi maalum kutoka katika fedha zilizotolewa shillingi **20,977,900,252** zinaonesha kuwa wanawake wamenufaika kwa zaidi ya **asilimia 54, asilimia 36** kwa vijana na **asimilia 10** kwa watu wenye ulemavu.

***Mchoro Na. 19: Matokeo ya Uwezeshaji wa Makundi Maalum 2018/2019 kwa asilimia***



### 17.3. VIWANDA NA UWEKEZAJI

Katika kuhakikisha kuwa Sera ya Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ya mwaka 2004 inatekelezwa kwa vitendo, Baraza linatekeleza kwa vitendo jitihada za serikali ya Awamu ya Tano za **ujenzi wa viwanda na kukuza uchumi nchini** ili kuongeza uzalishaji, ajira kwa wananchi, pia kupunguza umasikini. Katika mwaka wa fedha 2017/2018 mpaka 2018/2019, Mikoa na Halmashauri zote nchini kwa kushirikiana na Shirika la Miradi ya Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) wametengeneza miongozo ya uwekezaji katika maeneo yao yaani ***"Regional Investment Guides"*** ambayo imeanisha fursa na maeneo ya kimkakati ya uwekezaji kwa kila Mkoa. Katika utekelezaji wa agizo la Serikali la kuanzisha viwanda 100 kwa kila Mkoa, Jumla ya viwanda **4,876** vimeanzishwa katika mamlaka za Mikoa na Halmashauri nchini na kuzalisha ajira **35,796** sambamba na kutenga hekari **1,098,922.29** kuwezesha shughuli za kiuchumi. Katika viwanda vilivyojengwa, Viwanda vikubwa ni **108**, viwanda vya kati **236** na viwanda vidogo **4,532.**

Aidha, mamlaka za Mikoa na Halmashauri nchini zinaendelea kuweka mazingira rafiki kwa wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kwa kuimarisha ushirikiano baina ya sekta binafsi na serikali ili kuongeza tija ya uwekezaji katika maeneo yao, pia kuhamasisha uwekaji wa miundombinu wezeshi katika maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya shughuli za ujenzi wa viwanda, biashara, kilimo, ufugaji, umwagiliaji na kadhalika.

***Jedwali Na. 25: Jedwali la Viwanda Vilivyoanzishwa kufikia Disemba, 2018***


| **Na** | **Jina la Mkoa** | **Viwanda Vilivyoanzishwa Hadi Disemba, 2018** | | | | | **Maeneo yaliyotengwa** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | **Vikubwa** | **Kati** | **Vidogo** | **Jumla** | **Ajira** | **Ukubwa (Hekari)** |
| **1** | ARUSHA | 6 | 10 | 105 | 121 | 1,973 | 216,259 |
| **2** | DAR ES SALAAM | 46 | 12 | 425 | 483 | 7,182 | 3,556 |
| **3** | DODOMA | 1 | 1 | 196 | 198 | 778 | 16,571 |
| **4** | GEITA | 1 | 57 | 41 | 99 | 1,316 | 1,249 |
| **5** | IRINGA | 4 | 9 | 157 | 170 | 1,262 | 8,003 |
| **6** | KAGERA | 1 | 11 | 119 | 131 | 785 | 145,000 |
| **7** | KATAVI | - | 5 | 50 | 55 | 306 | 127,789 |
| **8** | KIGOMA | - | 1 | 219 | 220 | 1,843 | 3,170 |
| **9** | KILIMANJAR0 | 3 | 6 | 99 | 108 | 887 | 13,383 |
| **10** | LINDI | 7 | 2 | 571 | 580 | 3,355 | 210,028 |
| **11** | MANYARA | 2 | 2 | 99 | 103 | 840 | 3,341 |

| Na | Jina la Mkoa | Viwanda Vilivyoanzishwa Hadi Disemba, 2018 | | | | | Maeneo yaliyotengwa |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Vikubwa | Kati | Vidogo | Jumla | Ajira | Ukubwa (Hekari) |
| **12** | MARA | - | 12 | 433 | 445 | 616 | 10,163 |
| **13** | MBEYA | - | 40 | 167 | 207 | 1,417 | 5,650 |
| **14** | MOROGORO | - | - | 204 | 204 | 736 | 31,697 |
| **15** | MTWARA | 1 | 2 | 92 | 95 | 1,101 | 13,507 |
| **16** | MWANZA | 7 | 19 | 88 | 114 | 921 | 10,928 |
| **17** | NJOMBE | 2 | 3 | 144 | 149 | 2,097 | 25,820 |
| **18** | PWANI | 8 | 21 | 241 | 279 | 2,877 | 22,937 |
| **19** | RUKWA | 1 | 1 | 103 | 105 | 576 | 2,187 |
| **20** | SHINYANGA | 1 | 5 | 99 | 105 | 352 | 15,951 |
| **21** | SIMIYU | 7 | 3 | 106 | 116 | 775 | 3,670 |
| **22** | SINGIDA | 2 | 2 | 183 | 187 | 1,515 | 14,548 |
| **23** | SONGWE | - | 7 | 218 | 225 | 764 | 12,931 |
| **24** | RUVUMA | - | 2 | 108 | 110 | 283 | 13,816 |
| **25** | TABORA | 3 | 3 | 172 | 178 | 1,534 | 7,868 |
| **26** | TANGA | 5 | 1 | 93 | 99 | 705 | 158,901 |
| Jumla Kuu | | **108** | **236** | **4,532** | **4,876** | **35,796** | **1,098,922.29** |


(***Chanzo: OR-TAMISEMI***)

Utekelezaji wa viwanda 100 kwa kila Mkoa unaonesha kuwa Mikoa ya **Dar es Salaam, Lindi, Mara, Pwani** ikifuatiwa na **Morogoro, Mbeya, kigoma, Iringa, Singida na Songwe** imeanzisha viwanda vingi zaidi ya viwanda **150** kwa kila Mkoa wakati Mikoa ya **Arusha, Dar es Salaam, Geita, Iringa, Kigoma, Lindi, Mbeya, Mtwara, Njombe, Pwani, Singida na Tabora** imezalisha ajira zaidi ya **1000** kwa kila Mkoa kama inavyoonekana kwenye jedwali hapo chini.


***Mchoro Na. 20: Viwanda vilivoanzishwa hadi Disemba 2018***




***Mchoro Na. 21: Jedwali la viwanda na ajira zilizotengenezwa***



***Mchoro Na. 22: Maeneo yaliyotengwa***




## 17.4. URASIMISHAJI WA BIASHARA NDOGO KWA VITAMBULISHO

Katika kukuza kiwango cha ukuaji wa uchumi nchini na kuleta chachu ya maendeleo imara kwa wananchi, Mikoa na Halmashauri zimekuwa zikishiriki kikamilifu kutekeleza miongozo mbalimbali ya kuondoa vikwazo vya uanzishwaji na ukuaji wa biashara kwa kuweka utaratibu au kutunga sheria ndogondogo zinazowaongoza wafanyabiashara, wajasiriamali, na watoa huduma mbalimbali katika maeneo yao kama vile utoaji wa leseni za biashara; maeneo ya biashara, minada na maonesho; usafi; vibali vya afya; miundombinu na kadhalika. Viongozi wa Mikoa kwa kushirikiana na Jumuia za wafanyabiashara pamoja na Asasi za Kiraia wamekuwa wakiendesha majadiliano ya pamoja kutatua kero za wafanyabishara na wajasiriamali wadogo ambao kwa idadi ni wengi na biashara zao zilizo nyingi sio rasmi kutokana na ukosefu wa ujuzi sahihi wa elimu ya biashara ndani yao inayosababisha kufanya biashara kimazoea na kwa kuigana.

Katika uratibu wa shughuli za uwezeshaji kwa kuweka mazingira rafiki ya ukuaji wa kiuchumi kama ilivyotamkwa kwenye Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa Mhe. Rais, Dkt. John Joseph Pombe Magufuli imetoa vitambulisho vya wafanyabiashara wadogo na wajasiriamali kwa viongozi wote wa Mikoa 26 Tanzania Bara katika awamu mbili tofauti ili kuongeza tija ya urasimishaji wa biashara ndogo na kuwaondolea kero zinazokinzana na maagizo ya uboreshaji wa mazingira ya biashara katika maeneo yao.

Kufikia tarehe **30 Aprili, 2019** wajasiriamali wadogo **1,022,721** wametambuliwa kwa kupewa vitambulisho sawa na asilimia **55.28** ya vitambulisho **1,850,000** vilivyogawiwa kwa kila Mkoa. Jumla ya **shilingi 20,454,420,000/-** zimekusanywa kama ada ya kulipia vitambulisho hivyo na kufanya wepesi wa urasimishaji wa biashara kupitia Halmashauri za Majiji/Manispaa/Miji na Wilaya kuwa rahisi.


Kasi ya utoaji wa vitambulisho kwa wajasiriamali imekuwa ikiendelea vizuri katika Mikoa ya **Dar es Salaam, Tabora, Pwani, Kilimanjaro, Kagera, Tanga na Shinyanga** ikifuatiwa na Mikoa ya **Geita, Mwanza, Manyara, Mbeya, Morogoro, Ruvuma,** na **Simiyu**

***Jedwali Na. 26: Mgawanyo wa Vitambulisho vya wajasiriamali wadogo kwa kila Mkoa kufikia Aprili, 2019.***


| Na | Jina la Mkoa | Jumla ya Vitambulisho | Vilivyotolewa | Na | Jina la Mkoa | Jumla ya Vitambulisho | Vilivyotolewa |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **1** | Mwanza | 80,000 | 50,377 | 14 | Dodoma | 75,000 | 30,300 |
| **2** | Mtwara | 65,000 | 30,193 | 15 | Arusha | 125,000 | 42,435 |
| **3** | Kigoma | 60,000 | 26,154 | 16 | Dar es Salaam | 175,000 | 166,676 |
| **4** | Lindi | 65,000 | 21,893 | 17 | Mbeya | 105,000 | 61,852 |
| **5** | Ruvuma | 60,000 | 34,487 | 18 | Njombe | 60,000 | 6,682 |
| **6** | Rukwa | 55,000 | 13,768 | 19 | Kilimanjaro | 65,000 | 50,598 |
| **7** | Iringa | 60,000 | 18,446 | 20 | Kagera | 60,000 | 43,240 |
| **8** | Morogoro | 65,000 | 38,013 | 21 | Mara | 65,000 | 25,401 |
| **9** | Pwani | 60,000 | 46,597 | 22 | Simiyu | 60,000 | 34,090 |
| **10** | Shinyanga | 60,000 | 42,354 | 23 | Manyara | 60,000 | 37,128 |
| **11** | Katavi | 60,000 | 3,370 | 24 | Singida | 65,000 | 28,028 |
| **12** | Tanga | 60,000 | 43,249 | 25 | Songwe | 60,000 | 26,137 |
| **13** | Tabora | 65,000 | 61,477 | 26 | Geita | 60,000 | 39,776 |
| **Jumla Kuu** | | | | | | **1,850,000** | **1,022,721** |

(*Chanzo: Ofisi za Wakuu wa Mikoa*)

***Mchoro Na. 23: Vitambulisho vilivyotolewa kwa wajasiriamali kwa kila Mkoa***




***Mchoro Na. 24: Mchoro wa vitambulisho vilivyopokelewa na mikoa na vilivyotolewa***



## 17.5. MIKUTANO YA BIASHARA NA MAONESHO YA WAZI

Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ya mwaka 2004 katika nguzo ya saba inasisitiza kuwa masoko yote yanayotokana na uzalishaji wa ndani na nje ya nchi yanakabiliwa na ushindani mkali unaotokana na mabadiliko ya mfumo wa ulaji na utandawazi. Mara nyingi bidhaa zinazozalishwa nchini zinashindwa kupata masoko ndani na nje ya nchi kwa sababu mbalimbali ikiwemo ukosefu wa mitandao hai ya biashara kupitia mikutano ya pamoja ya kibiashara na maonesho ya wazi ambayo hupanua wigo wa masoko na kuchochea ushirikiano *(Business linkages and Networking)*. Kupitia Wizara ya Viwanda na Biashara, Wizara ya Kilimo, Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TANTRADE) na Baraza la Taifa la Biashara Tanzania (TNBC), Mikoa na Halmashauri zimekuwa zikiwakutanisha pamoja wananchi, wazalishaji viwandani, wakulima, wafanyabiashara na wawekezaji kupitia maonesho mbalimbali kama vie Saba Saba, Nane Nane, Viwanda, Mabaraza ya biashara pamoja Majukwaa ya wanawake. Mikutano hii ya biashara pamoja na maonesho imewezesha makundi tofauti ya wanaozalishaji wa bidhaa mbalimbali kukutana na mamlaka za usimamizi na udhibiti kupata elimu sahihi ya viwango vya ubora wa bidhaa, usalama, ufungashaji na upatikanaji wa mitaji ili kuhimili ushindani wa soko na kukidhi matakwa ya walaji walio wengi.

Mojawapo ya mambo ya kujifunza yaliyofanyika katika Mikoa na Halmashauri kwa mwaka wa fedha 2018/2019 ni kama ifuatavyo;-

***Jedwali Na. 27: Mambo ya kujifunza yaliyofanyika katika Mikoa na Halmashauri kwa Mwaka 2018/19.***

| Na | Tukio | Mratibu | Mahali/ Muda | Mikoa Husika | Walengwa | Maudhui |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **1** | Maonesho ya Mifuko na Programu za Uwezeshaji | NEEC | Mbeya<br>Oktoba 19 - 23, 2018 | Mbeya, Songwe, Ruvuma, Rukwa, Njombe, Iringa | Wananchi, Vikundi vya kifedha vya kijamii, mifuko ya uwezeshaji, asasi za kiraia, taasisi za fedha | Kutangaza na kupanua wigo wa huduma za mifuko na program za uwezeshaji kwa wananchi wa mikoa ya Kusini Nyanda za Juu |
| **2** | Maonesho ya Bidhaa za Viwanda vya Tanzania | TANTRADE | Dar es Salaam Disemba 5 – 9, 2019 | Dar es Salaam, Pwani, Morogoro | Wazalishaji wa bidhaa za viwanda, makampuni, taasisi na wananchi | Kupanua wigo wa masoko ya bidhaa zinazozalishwa ndani ya nchi |
| **3** | Maonesho ya Viwanda | SIDO | Simiyu August 23- | Simiyu, Mwanza, | Wajasiriamali wadogo na wa | Kuchochea maendeleo ya |

| Na | Tukio | Mratibu | Mahali/ Muda | Mikoa Husika | Walengwa | Maudhui |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Vidogo | | 28, 2018 | Mara, Shinyanga , Geita, Kagera | kati, makampuni, mamlaka za usimamizi na udhibiti | viwanda katika Mikoa ya kanda ya Ziwa |
| **4** | Maonesho ya wachimbaji madini Geita | TANTRA DE | Geita 24-30 Septemba, 2019 | Mikoa ya Kanda ya Ziwa | Wachimbaji na wadau wa madini nchini | Kushirikisha fursa za uwekezaji katika madini na teknolijia za uchimbaji |
| **5** | Mkutano wa wadau wa madini | Wizara ya Madini | Dar es Salaam 22-23 Januari, 2019 | Machimbo ya madini | Wadau wa biashara ya madini | Kutatua changamoto ya masoko, uchimbaji na uchakataji wa madini |
| **6** | Maonesho ya Saba Saba | TANTRA DE | Dar es Salaam 28 June, 2018 hadi 13 Julai, 2018 | Mikoa yote Tanzania Bara na Visiwani | Wananchi, Makampuni ya biashara, wazalishaji wa bidhaa mbalimbali, wajasiriamali, serikali na taasisi zake | Kufanya maonesho ya biashara kimataifa na kupanua wigo wa masoko ya bidhaa mbalimbali nchini |
| **7** | Maonesho ya Nane Nane | Wizara ya Kilimo | Simiyu 1 Agosti, 2018 hadi 8 Agosti, 2018 | Mikoa ya Kanda ya Ziwa | Wakulima, wazalishaji wa bidhaa mbalimbali za kilimo, serikali na wadau wote wa sekta ya kilimo | Kufanya maonesho ya bidhaa za kilimo kitaifa na kupanua wigo wa masoko ya bidhaa kilimo nchini kupitia wadau wake |

(***Chanzo: MDAs***)

# 18.0. MAMBO YA KUJIFUNZA KUTOKA MIKOANI (BEST PRACTICES)



## 18.1. MKOA WA TANGA (Utatuzi wa changamoto ya Masoko na Uchakataji wa Muhogo Wilaya ya Handeni)



Wilaya ya Handeni ni moja ya maeneo yanayozalisha muhogo kwa uwingi nchini. Katika mwaka wa fedha 2017/2018, Wilaya ya Handeni ilikuwa imefanikiwa kuhamasisha wakulima kuzalisha **tani 1,603,232** za muhogo kwa ajili ya soko la ndani na nje ya nchi. Pamoja na jitihada hizo wakulima walikabiliwa na changamoto ya upungufu wa mashine za uchakataji na ukaushaji wa muhogo, elimu ndogo ya mnyororo wa thamani wa zao la muhogo na upungufu wa maghala ya kuhifadhia muhogo ili kukidhi viwango na mahitaji ya soko la nje ya nchi.

Katika kutatua changamoto za wakulima hao kupitia vikundi, Halmashauri ya Wilaya ya Handeni ilitafuta mwekezaji **Kampuni ya Dar Canton** anayenunua muhogo mbichi na kuuchakata kutoka kwa wakulima. Kampuni hiyo **imejenga mashine 10** zenye uwezo wa kuchakata **tani 15** kwa siku. Katika kipindi cha kuanzia Oktoba, 2018 hadi Machi, 2019 kampuni imefanikiwa kuchakata **tani 204.314** wakati mnunuzi mwingine yaani Kampuni ya Taepz and Epoch Agriculture Development imenunua tani **54.575** za muhogo mkavu.

Aidha, Halmashauri inaendelea na jitihada za kutatua changamoto za wakulima kwa kuwajengea uwezo kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Kilimo (SUA) kupitia utekelezaji wa mradi wa **TAP II katika Kata ya Kabuku** kwenye shamba lenye ukubwa wa **ekari 20**. Hadi kufikia Machi, 2019 kituo hicho kimefanikiwa kuchakata **tani 6.3** za muhogo mkavu.

Kwa upande mwingine, Halmashauri inatumia ubunifu wa kipekee kuviwezesha vikundi vilivyojiimarisha vizuri kupitia fedha za mapato ya ndani yaani asilimia 10 za vijana, wanawake na watu wenye ulemavu kwa kununulia mashine za

kuchakata na kukausha muhogo. Jumla ya **Shilingi 28,909,100** zimetolewa kwa kikundi cha wanawake cha JIPE MOYO kwa ajili ya ununuzi wa mashine ya kusindika na kuchakata muhogo ambacho kitakuwa na uwezo wa kuchakata **tani 8.4** kwa siku.

## 18.2. MKOA WA GEITA (Soko la Madini)




Katika kuvutia uwekezaji unaotokana na uchimbaji wa madini, Mkoa wa Geita ulitenga eneo kwa ajili ya kufanikisha ujenzi wa Soko la Dhahabu nchini. Hadi kufikia mwezi Februari, 2019, ujenzi wa soko hilo ulikuwa umekamilika ambapo **tarehe 17 Machi, 2019**, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim M. Majaliwa alizindua soko hilo. Soko hilo lina jumla ya **vyumba 15** na kila chumba kinatumiwa na mfanyabiashara mkubwa mmoja wa madini. Kwa upande mwingine eneo la soko limejumuisha Ofisi za benki ambazo ni NMB, CRDB na Azania, Ofisi ya Tume ya Madini, Ofisi ya Uhamiaji na Ofisi ya Halmashauri ya Mji kwa lengo la kusogeza huduma karibu na wananchi wengi hususan, wafanyabiashara na wajasiriamali wadogo, wa kati na wakubwa. Ujenzi wa soko hili unaenda sambamba na ujenzi wa soko la wajasiriamali wengine ambao bado haujakamilika unaogharimu jumla ya shilingi **1.9 Bilioni**.

Pia kuna vituo mbalimbali vya madini vinavyotarajiwa kufunguliwa kwenye maeneo yanayozalisha Dhahabu kwa kila Halmashauri, vituo hivyo ni kwaajili ya kurahisisha biashara ya Dhahabu kwa wachimbaji wadogo waliopo kwenye

Halmashauri kabla ya kufikishwa kwenye soko kuu la Dhahabu lililopo Geita Mjini. Jumla ya **vituo kumi** (10) vinatarajiwa kufunguliwa kwenye Halmashauri zote za Mkoa wa Geita.

### 18.3. MKOA WA KIGOMA (Utekelezaji wa Mradi wa LIC na KJP)

Mkoa wa Kigoma unatekeleza mwongozo wake wa Uwekezaji yaani *Kigoma Region Investment Guide* kwa vitendo kupitia wadau. Mojawapo ya jitihada hizo ni Mradi wa Kuboresha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji (Local Investment Climate) unaofadhiliwa na nchi ya Denimark na Program ya Uwezeshaji Pamoja (Kigoma Joint Program) unaotekelezwa na Mashirika ya Umoja wa Mataifa. Miradi hii imeanza kuonesha mafanikio kwa wananchi, Kwa mfano Mradi wa Kigoma Joint Program (KJP) umesaidia **kujenga Masoko ya Mipakani katika Wilaya za Kibondo na Kakonko** pamoja na kusaidia **miradi ya wajasiriamali** kwa Wilaya za Kigoma (Petro & Sons Ltd), Kibondo (BRIMA) na Uvinza (Miradi ya Umwagiliaji).

Aidha, kupitia mipango ya Uwekezaji Mkoani Kigoma imesaidia Wilaya ya Buhigwe kupokea fedha za Mkopo wa masharti nafuu kiasi cha **Shilingi Bilioni 589.26** kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (**AfDB**). Fedha hizo zimepangwa kutumika katika ujenzi wa barabara ya kiwango cha lami kutoka Kabingo halmashauri ya Kakonko hadi Manyovu halmashauri ya Kasulu yenye umbali wa **kilometa 260**.

Kwa upande mwingine, Mashirika ya UNDP na ILO yamewezesha Halmashauri kwa kutoa ajira za muda mfupi (mkataba) kwa vijana ambao wamepewa mafunzo kwa ajili ya kufundisha vikundi vya wajasiriamali vijana na akina mama katika Halmashauri za **Wilaya na Mji wa Kasulu, Kibondo na Kakonko**. Wajasiriamali hao wamepatiwa vitendea kazi ambavyo ni Pikipiki (12), Kompyuta (12), Printer 12, Projectors 12, Projector screen 12 na posho ya kujikimu kwa kila mwezi.

Pia kupitia utekelezaji wa Mradi wa Kuboresha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji Mkoa wa Kigoma umeweza kuendesha kampeni ya kuhamasisha wananchi kushiriki katika shughuli mbalimbali za kiuchumi kupitia Mabaraza ya biashara kwa kila wilaya pamoja na Majukwaa ya wanawake.

### 18.4. MKOA WA SIMIYU (Uvutiaji wa Biashara na Uwekezaji)




Katika kuhakikisha kuwa mwongozo wa uwekezaji wa Mkoa unatekelezeka kwa vitendo, Mkoa wa Simiyu kwa kushirikiana na Halmashauri zake umetenga maeneo ya kimkakati kuvutia uwekezaji na ujenzi wa viwanda kwa mfano **Eneo la Maonesho ya wazi Nyakabindi, Ujenzi wa Kiwanda cha Chaki – Maswa na Kiwanda cha maziwa – Meatu**. Kupitia utekelezaji wa kauli mbiu ya Mkoa, "*Wilaya Moja; Kiwanda Kimoja*" Mkoa wa Simiyu umefanikisha ujenzi wa Kiwanda cha chaki na vifungashio wilayani Maswa, Kiwanda cha Maziwa na Chumvi wilayani Meatu, Kiwanda cha Sabuni wilayani Itilima, Kiwanda cha Ushonaji Mji wa Bariadi, Kiwanda cha Nyanya wilayani Busega na Kiwanda cha Alizeti, Vifaa Tiba na Bohari ya Madawa wilayani Bariadi.

Aidha, Halmashauri ya Wilaya ya Maswa ilipokea fedha shilingi **4,099,982,784** kati ya **shilingi 8,200,000,000** zilizoidhinishwa na kutolewa na Serikali katika mpango wa Bajeti ya mwaka 2018/2019 kwa ajili ya kupanua ujenzi wa kiwanda cha chaki, sambamba na **shilingi bilioni 4.8** kukamilisha ujenzi wa Kiwanda cha kusindika maziwa wilayani Meatu.

Pamoja na jitihada za ujenzi wa viwanda, Mkoa wa Simiyu umewezesha kufanyika kwa **Maonesho ya Kitaifa ya Nane Nane** yaliyofanyika kuanzia tarehe 1 Agosti, 2018 hadi tarehe 8 Agosti, 2018 na kuhudhuriwa na washiriki zaidi ya **10,000** katika Viwanja vya Nyakabindi. Pia **Maonesho ya Viwanda Vidogo Kitaifa** yaliyoandaliwa na SIDO kati ya tarehe 23.10.2018 hadi 28.10.2018 ambapo **wajasiriamali 8,000** walishiriki maonesho hayo.

## 18.5. MKOA WA MBEYA (Uanzishaji wa Mtandao wa Biashara na Nchi Jirani)

Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mbeya kwa kushirikiana na Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TanTrade) pamoja na Taasisi ya Biashara na Uwekezaji ya Malawi (MITC) iliandaa Kongamano la Kimataifa la biashara na kuvutia uwekezaji kati ya Tanzania na nchi ya Malawi. Kongamano hilo lilifanyika tarehe 26 – 27 Julai, 2018 Jijini Mbeya ambapo wawekezaji na wafanyabishara 747 walishiriki kutoka Tanzania na Malawi. Mgeni rasmi katika kongamano hilo alikuwa *Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan.* Kongamano hilo lililenga kuimarisha uhusiano katika maeneo yafuatayo;-

a. Kuimarisha ushirikiano wa kibiashara na uwekezaji kati ya nchi ya Tanzania na Malawi.
b. Kubuni, kuanzisha na kuendeleza miradi yenye kusababisha matokeo ya haraka katika sekta za viwanda, usafirishaji, utalii, uvuvi, kilimo, madini, elimu, afya, benki, mawasiliano, TEHAMA na biashara kwa ujumla.
c. Kupanua wigo wa masoko, biashara na uwekezaji kati ya Tanzania na Malawi hususan, kupitia Mkoa wa Mbeya ambao umepakana na nchi ya Malawi.
d. Kujenga uelewa wa pamoja katika kupanga, kutekeleza na kufuatilia mipango, mikakati ya maendeleo ya kiuchumi, kisiasa na kijamii.




*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan akipata maelezo kutoka kwa Mhandisi Paulo Sango alipolitembelea banda la Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kabla ya ufunguzi wa Kongamano la Biashara*

*na Uwekezaji kati ya Tanzania na Malawi kwenye ukumbi wa Royal Tughimbe mkoani Mbeya tarehe 26, Julai 2018.*

### 18.6. MKOA WA SHINYANGA (Kutenga eneo kwa ajili ya Kituo cha Uwezeshaji)

Mkoa wa Shinyanga kupitia Halmashauri ya Mji wa Kahama ilitenga eneo la ukubwa wa **ekari 500** na kuligawa kwa wajasiriamali, pia kuwapatia hati miliki kwa ajili ya kuendesha shughuli za kiuchumi. Katika eneo la Bukondamoyo kumetengwa eneo la ekari 500 kwa ajili ya ujenzi wa Viwanda vidogovidogo vya Wajasiriamali hasa vijana na wanawake. Katika eneo hilo viwanja 623 vimepimwa na kugawanywa kwa Wajasiriamli ili waweze kuvitumia kwa shughuli za Ujasiriamali ikiwemo kuweka mashine za kupasua mbao, Useremala, Kuchomea vifaa mbalimbali (Welders) na kufanya biashara ndogondogo.

Aidha, katika eneo hilo Wajasiriamali 1,021 (wengi wao wakuwa ni wanawake) walipewa viwanja kulingana na shughuli wanazofanya. Sambamba na hilo, Halmashauri imetenga eneo la ekari 15,000 kwa jili ya kilimo cha Biashara ambapo eneo hilo limekwisha pimwa na kufanyiwa utafiti kwa ajili ya maandalizi ya kilimo.

Mkoa ulishirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu kulitumia eneo hilo kwa kuanzisha Kituo maalum cha Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ili kuhamasisha utekelezaji wa shughuli za uwezeshaji kwa wananchi. Kituo hicho kilifunguliwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mhe. Jenista J. Mhagama (Mb) tarehe 18.11.2018

Walengwa wa kituo hiki ni Wajasiriamali wote wakiwemo wadogo, wa kati na wakubwa wakiwa mmoja mmoja, vikundi ama makampuni yaliyoko katika sekta zote za kiuchumi; wananchi wote; na Taasisi na Asasi zote zikiwemo za binafsi na za Serikali. **Lengo kuu la kituo ni kusaidia upatikanaji wa huduma mbalimbali za kiuchumi ambapo mjasiriamali atapata huduma zote muhimu kituoni hapo. Miongoni mwa huduma zinazotolewa ni pamoja na:** urasimishaji wa biashara, ushauri wa kibiashara; elimu na mafunzo ya ujasiriamali; upatikanaji wa mitaji na masoko; teknolojia na ufundi; hifadhi ya mazingira, hifadhi za jamii na afya; na uanzishwaji wa vikundi vya kifedha vya kijamii na Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo (SACCOS) n.k.

#### 18.7.1. Taasisi zinazotoa huduma katika Kituo

Taasisi zinazotoa huduma katika Kituo cha Uwezeshaji Kiuchumi cha Kahama ili kufanikisha malengo ya kituo ni Baraza la Taifa la Uwezeshaji (NEEC), Mfuko wa Maendeleo ya Vijana (YDF), Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake (WDF), Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA), Mfuko wa Rais wa Kujitegemea (PTF), Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO) , Mfuko wa Pembejeo wa Taifa (AGITF), SELF Microfinance Fund, Mpango Wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za wanyonge Tanzania (MKURABITA), Mfuko wa Taifa wa Hifadhi

za Jamii (NSSF), Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), Mamlaka ya Uendelezaji wa Biashara (TANTRADE), Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA), Shirika la Viwango la Tanzania (TBS), GSI Tanzania Limited, Chemba ya Biashara, Viwanda na Kilimo Tanzania (TCCIA), Benki ya Taifa ya Biashara (NBC (T) LTD), Taasisi ya VICOBA vya kidini (IR-VICOBA), Shirikisho la VICOBA Tanzania (VICOBA FETA), Tanzania Informal Microfinance Association of Practioners (TIMAP) na Chuo kikuu huria cha Tanzania (OUT).

#### 18.7.2. Utekelezaji wa Taasisi zinazotoa Huduma katika Kituo

### I. SHIRIKA LA KUHUDUMIA VIWANDA VIDOGO (SIDO)

Shirika la kuhudumia viwanda vidogo (SIDO) lilianzishwa kwa mujibu wa sheria ya Bunge Na. 28 ya mwaka 1973 kupanga, kuratibu, kuendeleza na kutoa huduma mbalimbali kwa viwanda/biashara ndogo na za kati. Lengo la shirika ni kuchangia katika kuondoa umaskini na kukuza maendeleo ya viwanda/ biashara, hivyo basi kuchangia katika maendeleo ya kiuchumi kupitia utoaji wa huduma ziendeshwazo kwa mhitaji ambazo zinaleta ajira na kipato kwa mtumiaji wa huduma.

Walengwa wa SIDO ni Viwanda/biashara ndogo na kati, Wajasiriamali binafsi pamoja na vikundi vya Wajasiriamali chipukizi (wenye mawazo, wanaoanza na waliokwisha anza biashara), Mashirika/Taasisi zinazo saidia wajasiriamali, Mashirika yasiyo ya kiserikali yanayojishughulisha (NGOs)

**a). Kutoa huduma ya ushauri wa biashara.**

i. Jumla ya Wajasiriamali 298 wamepata huduma ya ushauri wa biashara kwa kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka Jan-Marchi, 2019.
ii. Wajasiriamali 02 (Msindikaji wa maziwa na siagi ya karanga) wamesaidiwa kupata vifungashio, ku-design lebo pamoja na kuwaunganisha na wanaouza chachu (cultures) ya maziwa.
iii. Wajasiriamali 02 (01Ke na 01 Me) wamesaidiwa kusajili Brela jina la Biashara na kupata vyeti rasmi vya usajili (Reg. No. 453295- Cotella Food Products na Reg. Na. 451543 -Matoboki Nice Food Products)
iv. Mjasiriamali mmoja ameelekezwa na kusaidiwa kutengeneza mpango biashara yake kwaajili ya kuombea mkopo.
v. Wajasiriamali 03 wameunganishwa na taasisi nyingine SELF, TCCIA na GS1 baada ya kuhitaji huduma zinazowahusu.
vi. Mjasiriamali 01 tayari ameunganishwa na TBS baada ya kuhudumiwa na SIDO (Rachanya Africa EAST paints).

**b). Mafunzo:**

Jumla ya wajasiriamali 94 wamepata Mafunzo kama ifuatavyo;

i. Mafunzo ya Utengenezaji Sabuni (16) -Kata Kagongwa
ii. Mafunzo ya Usindikaji wa vyakula (3) -Kata Kagongwa
iii. Huduma za SIDO na TBS (59) –Ukumbi wa Mkurugenzi Kahama

iv. Menejimenti ya Biashara (6) – SIDO/NEEC Kahama

**c). Huduma ya Fedha**

i. Jumla ya Wajasiriamali 108 waliulizia na kutaka kujua taratibu zinazohusiana na huduma ya fedha hususani mikopo inayotolewa na SIDO.

ii. Kati yao Jumla ya Wajasiriamali 31 (14Ke 17Me) waliomba mikopo yenye thamani ya shs. 109,300,000/= kwa awamu 3 tofauti.

iii. *Waliopata Mkopo.* Hadi sasa ni Wajasiriamali 6 (60%) (04Ke na 02Me) kutoka awamu ya kwanza ya waombaji 10, tayari wamepata mikopo yao yenye thamani ya Tshs. 17mil. Waliobakia hawakukidhi vigezo vya mkopo na wamepewa taarifa.

iv. *Awamu ya pili*. Jumla ya waombaji ni 9 (05Ke 04Me) tayari barua zao zimepokelewa na kujadiliwa, 3 wamekosa vigezo na tayari wamepewa taarifa, waliobakia 6 tayari wametembelewa miradi yao na kupewa fomu za kujaza.

v. *Awamu ya tatu.* Waombaji wako 12 (04Ke 08Me). Maombi yao yamepokelewa na yanafanyiwa kazi.

## II. ASASI BINAFSI YA KUSAIDIA SEKTA YA KILIMO (PASS)

Asasi binafsi ya Kusaidia Sekta ya Kilimo (PASS) ni chombo kilichoanzishwa kama mradi mwaka 2000 ili kuhamasisha uwekezaji na ukuaji wa kilimo cha biashara na sekta zinazohusika kwa njia ya kuunganisha upatikanaji wa fedha nchini Tanzania. PASS hutoa huduma za maendeleo ya kilimo cha biashara na huduma za kifedha kwa wajasiriamali wadogo na wa kati kwa njia ya kuwaunganisha na taasisi za fedha.

**Mafanikio ya Taasisi**

i. Ofisi imepokea wateja 58 (Ke 9 na Me 49) kutoka maeneo ya Mhungula, Nyihogo, Nyahanga, Nyasubi, Nyakato, Shunu, Kagongwa, Bukondamoyo, Malunga, Mondo, Msalala, na Ushetu;

ii. Imefanikiwa kutoa elimu ya huduma kwa wateja 32 katika makundi yafuatayo:

***Jedwali Na. 28: Walengwa wa elimu ya huduma kwa wateja***

| Na | Walengwa | Idadi |
|---|---|---|
| 1 | Wauza pembejeo | 24 |
| 2 | Wachakata mazao | 07 |
| 3 | Wasindika mafuta | 01 |
| | **Jumla** | **32** |

iii. Ofisi imefanikiwa kutembelewa na wajumbe kutoka Ubalozi wa Denmark ili kuona shughuli zinazofanywa na PASS katika Kituo cha Kahama;
iv. Imefanikiwa kufanya vikao na Taasisi za fedha za NBC, BOA, NMB, CRDB, Benki ya ACCESS, AZANIA, BENKI YA POSTA kwa ajili ya kuhamasisha matumizi ya dhamana yao.

## III. TANZANIA CHAMBER OF COMMERCE, INDUSTRY AND AGRICULTURE (TCCIA)

Ni Taasisi isiyo ya Kiserikali iliyoanzishwa mwaka 1988, kwa lengo la kushirikiana na Serikali kuleta ufanisi katika sekta binafsi. TCCIA ni kiungo kati ya Sekta ya Umma na sekta Binafsi. Wajibu wa TCCIA ni Kuandaa Mabaraza ya Biashara kuanzia ngazi ya Wilaya, Mkoa na Taifa, majadiliano, ushawishi na utetezi kwa Sekta binafsi (Dialogue, Advocacy & Lobbing), kutoa vyeti vya Uasili (Certificate of Origin), urasimishaji biashara, kutafuta ubia wa kibiashara, ushauri wa kibiashara, mafunzo ya ujasiriamali na VICOBA. kuandaa Maonyesho ya kibiashara na ziara za kibiashara.

Walengwa wa TCCIA ni Viwanda/biashara ndogo na kati, Wajasiriamali binafsi, pamoja na vikundi vya Wajasiriamali chipukizi (wenye mawazo, wanaoanza na waliokwisha anza biashara), Mashirika/Taasisi zinazo saidia wajasiriamali, Mashirika yasiyo ya kiserikali (NGOs),wafanyabiashara wote, wakulima na wafugaji.

### Mafaniko ya Taasisi

i. Imefanikiwa kutembelewa na wateja 230 (Ke: 81 na Me:149) ambapo wateja hao wametokea maeneo ya Kahama Mji, Msalala, Ushetu, Tinde na Ngara;
ii. Imeendesha mafunzo kwa wajasiriamali 780 katika maeneo ya umuhimu wa makongano, taratibu za urasimishaji biashara na masoko ndani na nje ya nchi,aidha mafunzo hayo yalifanyikia katika Ukumbi wa Kakola, Kahama Gold Hotel na Halmashauri;
iii. Imefanikiwa kusaidia urasimashaji wa biashara za wajasiriamali kuanzia katika hatua ya upatikanaji wa majina ya biashara/Kampuni hadi leseni ya Viwanda: majina ya Biashara yaliyofunguliwa ni Kahama Cotton & Oil Mill, Quality Food Processors, Janeth Spice, Mkasiwa Company Limited, Leseni ya uuzaji mifugo ndani ya nchi, na KAL Holding Company LTD.

## IV. SELF MICROFINANCE FUND

Mfuko wa SELF unatoa mikopo ya jumla kwa asasi ndogo na za kati za fedha kama vile mashirika yasiyo ya kiserikali (NGOs), SACCOs na kampuni za fedha zinazotoa huduma za mikopo pamoja na benki ili ziweze kutoa mikopo kwa jamii ambayo haijafikiwa na huduma rasmi za kifedha. Pia taasisi hii inatoa milopo kwa wahusika katika mnyororo wa kuongeza thamani mazao ya kibiashara kwa kuwapatia

mitaji,vifaa/mashine za uzalishaji pamoja na mikopo ya uwezeshaji wa miradi ya kilimo.Wajasiriamali wote wanaoangukia kundi hili la wadau wetu huitwa SMEs.

Ofisi hii ni ya kimkakati yenye dhumuni la kuhudumia wadau wote waliopo kanda ya ziwa ambao wapo karibu na mji huu wa kahama kijiografia.Pamoja na shughuli nyingine ofisi hii ina jukumu la kuhakikisha inatoa huduma za kiwango cha juu katika utoaji wa mikopoa kwa wahitaji ambao ni pamoja na vikundi,makampuni na watu binafsi.

**Mafanikio ya Taasisi**

i. Ofisi imefanikiwa kutembelewa na wananchi 104 ambapo miongoni mwao wanawake ni 27 na wanaume ni 97 katika maeneo yafuatayo:

***Jedwali Na. 29: Wananchi waliotembelea Ofisi za Self Microfinance***

| Na | Eneo | Me | Ke | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Halmashauri | 55 | 22 | 77 |
| 2 | Msalala | 4 | 2 | 6 |
| 3 | Ushetu | 5 | 3 | 8 |
| 4 | Mbogwe | 8 | 0 | 8 |
| 5 | Kwingineko | 5 | 0 | 5 |
| | Jumla | 77 | 27 | 104 |

ii. Umetoa mkopo wa shilingi Milioni kumi (Tshs.10,000,000/=) kwa Mjasiriamali Mwanamke anayejishughurisha na uchakataji wa mahindi na kuzalisha unga wa sembe;

iii. Kiasi cha shilingi milioni mia sita (Tshs.600,000,000/=) kimeombwa na wateja ambapo maombi hayo yako katika hatua mbalimbali za kufanyiwa tathmini kabla ya kupatiwa mikopo hiyo, miongoni mwa waombaji hao wawili ni wanaume na mmoja ni mwanamke.

iv. Taasisi imefanikiwa kuwatembelea wateja wafuatao:

***Jedwali Na. 30: Wateja waliotembelewa na Ofisi za Self Microfinance***

| | | |
|---|---|---|
| 1 | Dorfin Trading company Ltd. | i. Wanajishughulisha na uchakataji mpunga(warehousing)<br>ii. Uwezo wa kuhifadhi;jazoTani 10,000<br>iii. Maombi ya mkopo: Sh.Milioni 400<br>iv. Hatua:Ombi linashughulikiwa |
| 2 | Masabone Company Ltd | i. Wanajishughulisha na uchakataji mahindi na uhifadhi mpunga(warehousing)<br>ii. Uwezo wa kuzalisha ni tani 5 kwa siku<br>iii. Maombi ya mkopo: Sh.Milioni150<br>iv. Hatua:Ombi linashughulikiwa |

| | | |
|---|---|---|
| 3 | Halima Shija Vicent-KIWANGO SUPER SEMBE | i. Anajishughulisha na uchakataji mahindi (Posho mill)<br>ii. Uwezo wa kuzalisha ni tani 1moja kwa siku<br>iii. Maombi ya mkopo: Sh.Milioni35<br>iv. Hatua:Kapatiwa shilingi milioni 10 |
| 4 | Richard Israel Kirenga | i. Anajishughulisha na uhifadhi mpunga<br>ii. Uwezo wa ghala ni tani 200<br>iii. Maombi ya mkopo: Sh.Milioni200<br>iv. Hatua:Ombi linashughulikiwa |
| 5 | Frank Venance Baratelanya-SAYUNI POSHO MILL | i. Anajishughulisha na uchakataji mahindi (Posho mill)<br>ii. Uwezo wa kuzalisha ni tani 1moja kwa siku<br>iii. Maombi ya mkopo: Sh.Milioni15<br>iv. Hatua:Anapungukiwa baadhi ya nyaraka.Anashughulikia zikamilike |
| 6 | Asha Msangi | i. Anashughulika na uchakataji wa mazao ikiwa ni pamoja na mpungana mahindi na uhifadhi ghalani Uwezo wa kuhifadhi ni tani 6,000 kwa msimu<br>ii. Maombi ya mkopo: Hajaamua bado<br>iii. Hatua:Bado |
| 7 | Buzwagi Vegetable Oil Co.Ltd | i. Wanajishughulisha na uzalishaji wa mafuta kutokan na alizeti<br>ii. Uwezo wa kuzaliaha ni lita 20,000<br>iii. Maombi ya mkopo: Sh.Milioni100<br>iv. Hatua:Ameahirisha maombi kwa mwaka huu. |
| | Jonas Busiga Kurwa-SEGESE | i. Anajishughulisha na uhifadhi mpunga<br>ii. Uwezo wa ghala ni tani 150<br>iii. Maombi ya mkopo: Bado<br>iv. Hatua:Bado.kaahidi msimu ujao |
| | James Kanoni-MBOGWE | i. Anajishughulisha na uhifadhi mpunga<br>ii. Uwezo wa ghala ni tani 400<br>iii. Maombi ya mkopo: Bado<br>iv. Hatua:Bado |
| | Faida Lutege | i. Anajishughulisha na uuzaji wa pembejeo<br>ii. Uwezo wa biashara ni mifuko 2000 kwa mwaka<br>iii. Maombi ya mkopo: Bado<br>iv. Hatua:Anatarajiwa msimu wa kilimo kuanzia Agasti |

### v. MKURABITA

Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA) ni kati ya Programu za Serikali, zenye ofisi katika Kituo cha Uwezeshaji Kiuchumi cha Kahama. Lengo la Mpango huu katika kituo ni kuwawezesha wamiliki wa rasilimali ardhi na biashara kushiriki katika uchumi rasmi unaosimamiwa na utawala wa sheria. Hii ni pamoja na kuzitumia mali zao zilizokwisha rasimishwa kama dhamana, katika kupata mikopo na fursa zinginezo zilizoko katika uchumi wa soko. Walengwa wa

MKURABITA ni wananchi wa mijini na vijijini, wanaomiliki rasilimali nje ya mfumo unaotambulika kisheria na wanaoendesha biashara bila kukidhi matakwa ya kisheria.

**Mafanikio ya Taasisi**

i. Ofisi imepokea maombi matano ya wajasiriamali wenye lengo la kuhitaji kurasimisha maeneo yao. Kati ya wananchi walioomba kurasimisha maeneo yao, kuna mwanamke mmoja na wanaume wanne;
ii. Mkurugenzi wa Halmashauri ametoa wataalamu wa Mipango Miji na Upimaji ili kutembelea mashamba matano ya wajasiriamali waliotuma maombi, kuanza maandalizi ya urasimishaji wa maeneo hayo ambapo upimaji wa mashamba matatu umefanyika na mashamba mawili yako katika hatua za awali za upangaji;
iii. Kwa kuwa wajasiriamali hawa wanajishughulisha na biashara ya kunenepesha ng'ombe na mbuzi, mazungumzo ya awali yamefanyika na Mfuko wa PASS, ili pindi watakaporasimisha maeneo yao na kupewa Hati miliki, wasaidiwe katika kuunganishwa na vyombo vya fedha.

## VI. GSI Tanzania

GS1 ni taasisi isiyojiendesha kwa faida yaani Non Profitable Agency iliyozinduliwa rasmi na Makamu wa Rais wa awamu ya nne Dr.Mohamed Gharibu Bilal mnamo mwaka 2011. GSI ni taasisi pekee yenye mamlaka ya kutoza *barcode*.

Taasisi hii imefanikiwa kutoa huduma kwa wateja watano(5) na kutoa elimu kwa wadau wasiopungua ishirini na tano(25) aidha wateja hao walikuwa wanajishughulisha na ujasiriamali wa bidhaa za sabuni na *chia seeds.*

## VII. MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA (TRA)

Mamlaka ya Mapato Tanzania ilianzishwa kwa Sheria ya Bunge Na.11 ya mwaka 1995, na ilianza kufanya kazi tarehe 1 Julai 1996.TRA ina jukumu la kusimamia kwa uadilifu kodi mbalimbali za Serikali Kuu.

**Mafanikio ya Taasisi**

i. Imetembelewa na wateja 95 waliohitaji huduma za Vibali vya Leseni,Usajili na kutaka ufafanuzi juu ya malalamiko kuhusu masuala ya kodi; na
ii. Kumekuwa na ongezeko la Kodi kutoka kwa wajasirimali wadogo kwa kiwango cha asilimia 25.

## VIII. BENKI YA NBC TANZANIA

Benki ya Taifa ya Biashara ni Benki ya zamani kuliko zote nchini Tanzania ikiwa na uzoefu wa zaidi ya miongo mitano. Benki hii inatoa huduma mbalimbali kwa wateja wa rejareja, biashara,mashirika na misaada ya uwekezaji, bidhaa na huduma za usimamizi mzuri wa fedha.

**Mafanikio ya Taasisi**

i. Ofisi imefanikiwa kutembelewa na wateja 92 miongoni mwao ni Wanawake 63 na wanaume 29;
ii. Imefungua akaunti binafsi 15 kwa wajasiriamli wa Zongomela; na
iii. Imefungua akaunti mbili za Vikundi vya wajasiriamali wa Zongomela

## IX. MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI (VETA)

VETA ni Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi iliyoanzishwa kwa Sheria ya Bunge Na. 1 ya 1994 na kupewa majukumu ya kuratibu, kusimamia, kutoa na kugharamia elimu na mafunzo ya ufundi stadi nchini. VETA inamiliki vyuo 28 Tanzania Bara, kati ya vyuo hivyo VETA Shinyanga ni moja wapo.

**Mafanikio ya Taasisi**

i. Imefanikiwa kutembelewa na wananchi 116 (Wanawake 15 na wanaume 101) kutoka maeneo ya Shinyanga, Nyihogo, Nyahanga, Kagongwa, Igunda,Nyakato, Dodoma, Muhungula, Kilago – Ushetu, Mpera, Bukoba, na Zongomela; na
ii. Baada ya kituo kuanza VETA kwa kupitia ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Kahama Mji,Idara ya Maendeleo ya Jamii, imeanza kutoa mafunzo ya muda mfupi katika fani zifuatazo:-

***Jedwali Na. 31: Mafunzo yaliyotolewa na VETA***

| NA | AINA YA KOZI | IDADI YA WANAFUNZI | | MUDA | MAHALI |
|---|---|---|---|---|---|
| | | KE | ME | | |
| **1** | ALUMINIUM | 2 | 3 | MIEZI 6 | MWANVA FDC |
| **2** | USHONAJI | 10 | 0 | MIEZI 6 | MWANVA FDC |
| **3** | PSV | | 01 | SIKU 10 | VETA SHY |
| **4** | UDEREVA | | 01 | WIKI 5 | VETA SHY |
| **5** | UCHOMELEAJI | | 5 | MIEZI 6 | MWANVA FDC |
| **6** | SALOON | 5 | | MIEZI 6 | MWANVA FDC |
| **7** | MAPAMBO | 4 | 1 | MIEZI 6 | MWANVA FDC |
| **8** | UMEME | 4 | 6 | MIEZI 6 | MWANVA FDC |
| **9** | UFUNDI BOMBA | 4 | | MIEZI 6 | MWANVA FDC |

## X. CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA (OUT)

Chuo kikuu huria cha Tanzania kilianzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Bunge Na. 17 ya mwaka 1992 kuratibu, na kutoa elimu kwa njia ya huria, masafa na kimtandao. Mfumo wa utoaji elimu unamwezesha mwanafunzi kusoma huku pia akiwa anajishughulisha na shughuli zingine za kujipatia kipato.

Walengwa wa Chuo hiki ni wafanyakazi wa serikalini na taasisi binafsi,wahitimu wa elimu ya kidato cha nne na kidato cha sita, wahitimu wa elimu ya ngazi ya cheti, stashahada, astashhada na shahada.

Chuo kimekua kichocheo muhimu cha kutekeleza Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kupitia njia zifuatazo:

i. Kuhamasisha wanafunzi kujihusisha na shughuli mbalimbali za kiuchumi kama vile za ujasiriamali kwa kupitia maarifa wanayoyapata kwenye programu wanazosomea;
ii. Kuwafanyia tathimini kwenye elimu ya vitendo ili kuwajengea uwezo na maarifa;
iii. Kuwatangazia na kuwahabarisha wanafunzi wote kuhusu uwepo wa baraza la uwezeshaji kiuchumi Kahama na fursa zilizopo;
iv. Kuendelea kudahili wanafunzi wapya katika programu mbalimbali zinazotolewa na Chuo;
v. Kuwatembelea wafanyakazi mbalimbali wa ofisi za serikali na taasisi binafsi na kuwapa ushauri kuhusu kujiendeleza kielimu ili waweze kuongeza ufanisi wa kazi kwenye taasisi zao;
vi. Kahama

**Mafanikio ya Chuo kwenye Kituo cha Uwezeshaji cha Kahama**

i. Kina idadi ya wanafunzi 130 katika ngazi na fani mbalimbali za masomo;
ii. Idadi ya waombaji wapya ni 35 ambao wanasubiri kuchaguliwa na kuhakikiwa na TCU pamoja na NACTE;
iii. Kimedahili mwanafunzi wa kwanza wa PHD kwa mwaka wa masomo 2018/2019;
iv. Kimeendesha mitihani kwa awamu tofauti tofauti ambapo awamu ya kwanza ya mitihani ilifanyika mwezi Julai, 2018, awamu ya pili ilikua Septemba,2018 na mwaka huu 2019 awamu ya kwanza ilifanyika mwezi Februari, 2019 na awamu inayofuata itafanyika Mei,2019;
v. Kimefanikiwa kuendesha mafunzo ya ana kwa ana kwa wanafunzi wa ***foundation programme*** kuanzia tarehe 8 – 12 Machi, 2019.